**25 MEI, 2022**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 25 Mei, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Almasi Maige. Katibu, tuendelee.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali kwa siku ya leo tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 258

### Ujenzi wa Daraja la Mto Nduruma-Arumeru

**MHE. ZAYTUN S. SWAI** aliuliza:-

Je, ni lini Daraja la Mto Nduruma litakalounganisha Kata za Mlangarini, Nduruma na Bwawani Wilayani Arumeru litajengwa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaytun Seif Swai Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga Shilingi Milioni 70 kwa ajili ya ujenzi wa daraja la mawe katika Mto Nduruma ili kuunganisha Kata za Mlangarini, Nduruma na Bwawani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TARURA* itaendelea kuboresha miundombinu ya barabara hii ili kuboresha mawasiliano ya Kata za Mlangarini, Nduruma na Bwawani

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini pia kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Arumeru, naishukuru Serikali kwa kutenga kiasi hiki cha fedha Milioni 70 kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, je, ni lini ujenzi wa daraja hili utaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Wilaya ya Ngorongoro, kuna mto, unaitwa Mto Yuhe, mto huu ni hatari sana hasa kipindi cha mvua kwa kuwa watoto wetu wanashindwa kwenda shule upande wa pili vilevile akina Mama wajawazito wanashindwa kwenda kujifungua upande wa pili.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa kujenga daraja hili ili kunusuru Maisha ya wananchi hawa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali madogo mawili ya Mheshimiwa Zaytun Seif Swai, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kumuahidi Mheshimiwa Mbunge ni kwamba daraja hili litajengwa katika mwaka fedha unaonza na tutalipa kipaumbele kuhakikisha kwamba linakuwa ni moja ya madaraja ambayo yatajengwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, katika Halmashauri ya Ngorongoro ambako kuna daraja la Nyuki ambalo na lenyewe linahitaji kujengwa, ninamuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatafuta fedha na tutatuma wataalam wetu waende wakafanye tathmini ili na daraja hilo tulitafutie fedha ili liweze kujengwa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga Mbunge wa Kalenga, aulize swali lake.

Na. 259

**Shule ya Sekondari Kalenga kuwa ya kidato cha tano na sita**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi Shule ya Sekondari Kalenga iliyopo Kata ya Ulanda kuwa ya kidato cha tano na sita?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maelekezo ya Serikali ni kuwa na Shule ya Kidato cha Tano na Kidato cha Sita katika kila Tarafa zikiwemo Tarafa zilizoko katika Jimbo la Kalenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatafuta fedha katika mwaka 2022/2023 za ujenzi wa bweni la kulalia wanafunzi ili kukamilisha vigezo vya kupandishwa hadhi ya kuwa na Kidato cha Tano na Kidato cha Sita.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Serikali kwa majibu mazuri, ingawa shule hii ya Kalenga tayari imeshatimizi vigezo. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Kata nyingine ya Sekondari ya Isimila ambayo ina Kidato cha Tano na Kidato cha Sita, hii ina wasichana na wavulana. Mwaka 1999 aliyekuwa Rais wakati huo Mheshimiwa Hayati Mkapa alipita pale na akaahidi kujenga ukuta ili kuwalinda wanafunzi pale lakini mpaka leo haujakamilika.

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, tunafahamu kule Marekani wameanzisha kitu kina Ben Carson Reading Clubs, huyu mwana sayansi Ben Carson alipata maarifa yake kwa kusoma kwenye maktaba.

Je, Serikali ni lini sasa itajenga Maktaba kwenye shule za Kata zote katika Jimbo la Kalenga.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ambayo ilitolewa ya ujenzi wa ukuta katika shule ya sekondari Isimila bado ipo na sisi niseme tu kwamba katika mipango yetu tumeiweka, kikubwa ambacho tunatafuta sasa hivi kwa sababu tuna mipango mingi sana ya kutafuta fedha, tutakapopata fedha kwa ajili ya kujenga maana yake tutaanza haraka iwezekanavyo. Lengo la Serikali kwa sasa ni kuhakikisha shule zote nchini zinapata maktaba zikiwemo hizo za Kalenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kikubwa tu ambacho tunabanwa sasa hivi ni bajeti lakini tunaendelea kutafuta fedha na ninaamini chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan tunaweza tukalifikia hili kama tulivyofanikiwa kwenye madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea bado na TAMISEMI, Mheshimiwa Ally Yahya Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Butondo.

Na. 260

**Hitaji la ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kijiji cha Mikuwa Kata ya Mnanje – Nanyumbu**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO K.n.y MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga Kituo cha Afya katika Kijiji cha Mikuwa Kata ya Mnanje Wilayani Nanyumbu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepeleka fedha Shilingi Milioni 250 kwenye Kata ya Mnanje kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya ambapo Kijiji cha Mikuwa ni miongoni mwa vijiji vilivyomo kwenye Kata hiyo. Majengo yanayojengwa kwenye Kituo hicho ni jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD),* Jengo la maabara na kichomea taka. Majengo hayo yapo katika hatua ya umaliziaji ukiacha kichomea taka ambacho ujenzi wake ndiyo umeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais – TAMISEMI tayari imekwisha wasilisha maombi Wizara ya Fedha na Mipango ya Shilingi Milioni 250 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa wodi ya wazazi, chumba cha upasuaji na jengo la kufulia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niipongeze Serikali kwa jitihada kubwa ilizozifanya kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi hawa wa

Kata ya Mnanje, Wilayani Nanyumbu, wanapata ukombozi kwa kupata hii *consent* ambayo itaweza kupunguza pakubwa sana adha na changamoto katika Kata hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize swali maswali mawili ya nyongeza. Je, Serikali iko tayari kufanya jitihada za haraka kuleta hizi Milioni 250 ili kukamilisha ujenzi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali itakuwa tayari kuleta watumishi wa kutosha ikiwa ni pamoja na vifaatiba ili kituo hiki kiweze kuanza kufanyakazi haraka na kwa wakati?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Boniphace Butondo, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia tu kwamba hizi fedha Milioni 250, kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha huu Kata zote, maeneo yote ambayo tulipeleka fedha nusu, yatakuwa yamefikiwa ikiwemo katika Jimbo la Nanyumbu la Mheshimiwa Mhata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, mara baada ya kukamilika moja ya lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba tunanunua vifaatiba pamoja na kupeleka watumishi katika vituo vyote ambavyo Serikali imeanzisha, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Waziri Mkuu alipotembelea Kata ya Jangalu kwenye Kijiji cha Itolwa aliahidi kujengwa kituo cha afya. Naomba kujua ni lini sasa kituo hicho kitajengwa maana sasa ni miaka minne, ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya Serikali kwanza ilikuwa ni kuhakikisha tunamaliza ujenzi katika Tarafa zote, lakini lengo la pili, ni kuhakikisha zile Kata ambazo hazifikiwa na zenyewe tunazijengea vituo vya afya. Kwa hiyo, hayo ndiyo malengo ya Serikali. Tatu, ahadi zote za Viongozi ambazo zimetolewa ziko katika mpango wetu tutahakikisha kabisa kwamba zinafikiwa ikiwemo katika Jimbo la Chemba, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Yahya Mhata nimekuona.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aweke kumbukumbu sawa ni Jimbo la Nanyumbu, naona maelekezo yako mengi yanazungumza Jimbo la Nanyamba, ni Jimbo la Nanyumbu, liko Mkoani Mtwara na Jimbo la Nanyamba pia liko Mkoani Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la nyongeza kumekuwa na ucheleweshaji wa fedha hasa kwenye hii miradi ambayo wananchi wanaiibua. Sasa katika Jimbo langu nina maboma zaidi ya Kumi ambayo mpaka sasa hivi hayajapata fedha.

Je, Serikali ina kauli gani juu yama boma hayo?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya lengo la Serikali ambalo hata kwenye bajeti tumepitisha, kila mwaka tumekuwa tukitenga fedha kwa ajili ya umaliziaji wa maboma ambayo yameanzishwa huko chini na wananchi pamoja na Serikali zetu kule chini. Kwa hiyo, tumekuwa tukitenga labda kwa kiwango fulani. Sasa hatuwezi kuyamaliza yote kwa wakati mmoja ila kwa wakati. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Mhata kwamba hata katika Jimbo la Nanyumbu, tutafanya hivyo katika mwaka wa fedha unaokuja kuongeza baadhi ya maboma ili tuhakikishe yanakamilika yote kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, niliona umesimama.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Serikali inajenga hospitali pale Ukerewe ambayo ikikamilika itakuwa na hadhi ya Mkoa na ikikamilika itakuwa inahudumia *cases* kubwa za rufaa. Sasa nataka kuiuliza Serikali haioni umuhimu sasa kuimarisha kituo cha afya cha Nakatungulu ambacho kitasaidia kuhudumia wagonjwa magonjwa ya kawaida na kikikamilika kitahudumia Kata zaidi ya Sita kwenye eneo la Mjini pale?

**MWENYEKITI:** Majibu swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tumekuwa tukiboresha vituo vya afya ambavyo vimekuwa na idadi kubwa ya watu na zile ambazo zinahudumia Kata nyingi ikiwemo katika hii Kata ya Nakatundu ambayo Mheshimiwa Mbunge ameainisha. Kwa hiyo, bado iko katika mipango yetu na sisi tutaendelea kuziboresha kuhakikisha tunapeleka huduma za afya karibu na watu.

**MWENYEKITI:** Tunamalizia na Mheshimiwa Juliana Shonza.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kufahamu ni lini Serikali itatujengea kituo cha afya katika Kata ya Vwawa ili kupunguza msongamano katika Hospitali ya Wilaya ya Mbozi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juliana Shonza, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Songwe, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ilikuwa ni kuhakikisha kwamba Tarafa zote zinapata vituo vya afya, hilo eneo ambalo analianisha ndiyo Makao Makuu ya Mkoa ambako tunayo hospitali ya Mkoa ambayo tumeipandisha hadhi kutoka hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, baada ya kumaliza hizo *process* zote ambazo tunazo sasa hivi, maana yake ndiyo tutafuatia hiyo hatua ambayo Mheshimiwa Mbunge anaainisha, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Swali la mwisho kwa TAMISEMI, linatoka kwa Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu.

Na. 261

**Asilimia 50 ya wanafunzi wanaojiunga na kidato cha tano kutoka ndani ya Halmashauri**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, ni nini mpango wa Serikali kufanya asilimia 50 ya wanafunzi wanaojiunga na Kidato cha Tano katika shule za Kata watoke ndani ya Halmashauri?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya Mbunge wa Jimbo la Meatu, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali kuchanganya wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali ili kujenga Utaifa, kuchanganya wanafunzi kunasaidia msawazo wa nafasi zilizopo

ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa wanafunzi wote waliofaulu wanapata nafasi ya kujiunga Kidato cha Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutumia wanafunzi asilimia 50 kujiunga na Shule za Sekondari kutasababisha baadhi yao kukosa nafasi kwa kuwa siyo kila mchepuo unapatikana kwenye shule zilizopo katika Halmashauri husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Elimu bila malipo imeweza kuibua vijana wenye vipaji kutoka familia zenye mazingira magumu. Mfano, Bariadi mwaka juzi alitokea kijana aliyepata 'A' zote katika masomo yake. Wanafunzi hao wamekuwa wakipangwa shule maalum au shule zilizo mbali zaidi na kushindwa kumudu gharama za kusafiri na zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani wa kuwabaini wanafunzi wa aina hii ili waweze kuwasaidia na kutimiza ndoto zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tumekuwa tukiomba mabweni kwa ajili ya shule zetu za Kata na zinapokamilika shule hizi zinakuwa za Kitaifa. Je, Serikali haioni haja ya kuona kuwa na *catchment area* kama vile katika Mkoa au Wilaya kuwe na shule ya bweni ili tuweze kuwanusuru vijana wanaokatisha masomo kwa kutembea umbali mrefu. Kwa mfano, mwanafunzi anayetokea Lukale kilomita 40 kwenda Bukundi na kurudi kilomita 40? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti,

ahsante sana. Naomba kujibu maswali mawili madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie kwamba wanafunzi wote wenye vipaji Serikali inawazingatia, na inapotokea wanafunzi waliofanya vizuri kama huyo na bahati mbaya anakuwa ameenda katika maeneo ambayo hakustahili, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumefungua dirisha, mnatuletea hayo maombi na tunaweza tukafanya mabadiliko mengine. Kwa hiyo, hilo liko wazi na liko ndani ya uwezo wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ujenzi wa shule za bweni katika ngazi ya mkoa kwa kuzingatia hayo; umbali, mahitaji na vipaji, ndiyo maana kwa mwaka huu wa fedha na mwaka 2021, Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan ameamua kujenga Shule za Kimkoa kwa wasichana. Mwaka 2021 tumeshapeleka fedha shule 10 na mwaka huu vile vile tumetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule nyingine 10 za kimkoa ambazo zitapokea wasichana wenye vipaji katika mikoa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba lengo la Serikali litafikiwa na tunafanya hivyo kupunguza umbali pamoja na kuongeza tija ya elimu katika maeneo husika, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde kwa majibu mafupi ya maswali ya Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, tutaanza na Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini.

Na. 262

**Kuendelea na masomo kwa vijana wanaopata daraja la nne na sifuri**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuwaendeleza vijana wanaomaliza kidato cha nne na kupata daraja la nne au sifuri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Costantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa fursa kwa vijana wote hata wale waliomaliza darasa la saba kujiunga na vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi stadi na vyuo vya maendeleo ya wananchi vilivyo karibu na maeneo wanayoishi kwa lengo la kujiendeleza katika ujuzi na stadi mbalimbali za maisha. Vile vile vijana hao wanaweza kurudia mitihani yao kama watahiniwa wa kujitegemea iwapo wanahitaji kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu) inatekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi kwa kuwapatia vijana mafunzo ya uanagenzi na utambuzi wa ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Makamo.

**MHE. MICHAEL C. MAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru Serikali kwa kunipatia majibu kwenye swali hili la msingi, lakini nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kutokana na uwekezaji mkubwa wa Serikali kwenye maeneo mbalimbali ya nchi hii kujenga Shule za Kata, kunakopelekea watoto wengi kumaliza Kidato cha Nne kwa alama hizo za Daraja la Nne au Sifuri na kwa vyuo hivyo vinavyotajwa na Serikali ni taasisi za Umma ambavyo vimejengwa kwa malengo ya kutoa elimu hizo kwa vijana wetu:-

Je, Serikali haioni sasa ipo haja ya kuwapangia moja kwa moja kwenye vyuo hivyo badala ya wao kuamua wenyewe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tubebe ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu utaratibu huu sasa haupo wa kuwapangia moja kwa moja wale waliopata *division four* na *zero* au wale waliofeli darasa la saba. Kwa vile umetoa ushauri huo, acha tuuchukue kama Serikali twende tukaufanyie kazi, tufanye tathmini ya kina kama iwapo jambo hili linawezekana, basi tutaliingiza kwenye mipango yetu kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond, nimekuona.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ili mwanafunzi afikie kupata *division zero au four* ni

pamoja na ufatiiaji hafifu wa masomo yake. Wazazi wanatakiwa wahudhurie mikutano ya shule wanapoitwa nakadhalika: Ni lini sasa Serikali italeta Muswada hapa Bungeni kuhakikisha kwamba tunatunga sheria ya wazazi kufatilia masomo ya watoto wao mashuleni? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo fupi la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu ni suala ambalo linahusu pande karibu tatu; upande wa kwanza ni wanafunzi yeye mwenyewe, upande wa pili ni wa wazazi kama Mheshimiwa Mbunge alivyoshauri na upande wa tatu ni wa walimu au Serikali kwa ujumla. Kwa vile amezungumza hapa suala la kuleta Muswada Bungeni wa kuangalia namna gani tunaweza kuwabana wazazi ili waweze kufuatilia maendeleo ya watoto wao katika elimu, naomba tuubebe ushauri huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tunafahamu kwamba katika shule zetu kunakuwa na Kamati mbalimbali za kufuatilia maendeleo ya shule pamoja na wanafunzi kwa ujumla. Kwa hiyo, nadhani Kamati zile sasa zinatekeleza wajibu huu, lakini kwa vile ni wazo au ushauri ambao ameutoa, acha tuuchukue kama Serikali twende tukafanye tathmini, halafu kama tukiona kama kuna umuhimu wa kuleta Muswada huo, tuweze kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu ya Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa  Mussa nilikuona.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mimi nataka kujua tu, Serikali imeweka mkakati gani wa kuondokana na hili daraja sifuri? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mussa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyozungumza katika swali lililopita, suala la ufuatiliaji au suala la elimu ni lazima pande zote ziweze kushiriki, kwa maana ya mwanafunzi mwenyewe, ni lazima atengeneze mkakati wa namna gani anaweza kujifunza na kuhakikisha kwamba anafaulu kwenye masomo yake. Pia kuna sehemu ya walimu na vilevile kuna sehemu ya wazazi. Kwa hiyo, sisi kama Serikali jukumu letu kubwa ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na miundombinu wezeshi ya kumwezesha mwanafunzi kuweza kusoma na kupata elimu yake sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile lazima tupeleke walimu wa kutosha kuhakikisha kwamba masomo yote yanafundishwa kwa vipindi vyote kwa wakati, kwa maana ya kutekeleza mtaala wetu kwa wakati na sehemu inayobaki ni ya mwanafunzi yeye mwenyewe kujitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kama Serikali mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba tunakwenda kutengeneza *facilities* za kuwezesha wanafunzi wetu kufanya masomo yao vizuri, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, nimekuona.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba mtihani wa mwisho wa Kidato cha Nne mwanafunzi anapofanya wakati mwingine anaweza akawa amechanganyikiwa: Kwa nini sasa Wizara isiangalie matokeo yake ya nyuma ijumlishe na yale ya mwisho ili tuweze kumuhukumu kuendelea na maisha yake ya baadaye?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la fupi la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mtihani wetu wa mwisho wa *Form Four* siyo una-*contribute* au unaosababisha kuwa na matokeo ya mwisho. Mtihani wetu wa mwisho wa *Form Four* una maeneo mawili; asilimia 30 inakuwa kwenye maendeleo yake ya elimu, tunaita *continuous assessment.* Kwa hiyo, asilimia 30 ya zile alama *(marks)* zinatoka kwenye maendeleo yake yale ambayo ameyafanya kwa kipindi chote cha miaka minne; na asilimia 70 ndiyo ambayo inazingatiwa au inakuwa *contributed* na ule mtihani wake wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, iwapo amefanya vizuri kwenye maendeleo yake kutoka *Form One* mpaka *Form Four,* ile asilimia 30 ina maana itambeba na ule mtihani wa mwisho unachangia kwenye asilimia 70 tu ya mitihani yake. Kwa hiyo, hilo kama Serikali tumeshalizingatia na ndivyo inavyofanyika mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Madini, Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, sasa aulize swali lake.

Na. 263

**Kuwawezesha wachimbaji wadogo – Mbogwe**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawawezesha wachimbaji wadogo kwa kuwapatia mikopo katika Wilaya ya Mbogwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimimiwa Waziri wa Madini, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Jimbo la Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo mwanzo Serikali ilikuwa na utaratibu wa kuwapatia mikopo wachimbaji wadogo kwa lengo la kuwaongezea mitaji ili kuwafanya wafanye shughuli zao kwa tija. Baadaye tathmini ilifanyika na ilionesha upotevu wa fedha hizo. Kufuatia tathmini hiyo, Serikali inaendelea kuangalia namna bora ya kuwapatia mikopo wachimbaji wadogo nchini wakiwemo wa Wilaya ya Mbogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hiyo, Serikali kupitia Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* limeingia makubaliano *(MoU)* na Benki za *CRDB, NMB* na *KCB* kwa ajili ya kuwapatia mikopo wachimbaji wadogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo kwa wawekezaji, wanakuja na leseni sehemu ambapo wanachimba wachimbaji wadogo, wakifika na leseni wanawafukuza bila kuwalipa fidia wamiliki wenye maeneo (ardhi): Sasa nataka kujua, nini kauli ya Serikali kuhusu hawa waliomiliki ardhi yao kwa muda mrefu wanafukuzwa pasipo kupewa malipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili: Wachimbajii wadogo wamekuwa na kilio kikubwa cha tozo kwenye mifuko ya mawe: Ni lini Serikali itawapunguzia tozo ya mawe kwenye maduara pale wanapochimba ili kusudi nao waweze kufaidika na kazi zao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimimiwa Waziri wa Madini.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maganga, Mbunge machachari wa Jimbo la Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ieleweke kwamba uchimbaji wa madini, ili mtu aweze kuchimba ni lazima awe na leseni ya uchimbaji madini. Kabla hatujatoa leseni kwenye eneo lolote, timu yetu ya wataalam lazima ikague maeneo hayo kujiridhisha nani yupo? Anafanya kazi gani? Kama hawajaomba maeneo hayo, mara nyingi huwa tunawakumbusha kuomba. Inapotokea anatokea mtu amepewa leseni kwa kawaida, na hata Mbogwe tumefanya hivyo; wale waliopewa leseni lazima waingie makubaliano na wenyeji ili kusionekane kuna upunjaji wa namna yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu tozo za mifuko, jambo hili ni jambo ambalo linawezekana kufanyiwa kazi kama tu aina ya uchimbaji unaofanyika utakuwa wa nia ya kuchimba, kuchakata na kuzalisha dhahabu. Ila, kama wachimbaji wenyewe wataamua kugawana mawe, na ni uchimbaji usiokuwa rasmi kwenye rashi, wajue kwamba na Serikali lazima iwe na sehemu ya mgao kwenye migao hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq na Mheshimiwa Esther Bulaya nimewaona.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Wanawake wengi sasa hivi wameanza kujiingiza katika biashara ya madini: Nini mkakati wa Serikali katika kuendeleza wanawake hawa kwa kuwapatia mikopo na kuwahamasisha wanawake wengi zaidi waweze kushiriki katika biashara ya madini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimimiwa Waziri wa Madini, majibu ya swali hilo zuri la wanawake.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Toufiq kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikubali kwamba katika watu ambao wamechangamkia fursa ya uchimbaji madini, kundi kubwa la wakina mama wameingia kwenye uchimbaji madini. Mahali ambako wanawake wanachimba, tuna uzoefu, ni watu waaminifu, wanaolipa kodi kwa wakati, hawahitaji kusimamiwa na Polisi; na hata mirabaha ambayo tumewapa kusimamia, wao wameonesha bila shaka yoyote kwamba ni watu wanaoweza kujisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi Serikali tunaangalia utaratibu bora zaidi wa kuwapatia wachimbaji mikopo wakiwemo na wanawake. Tunachohitaji ni muda wa kufanya *study*. Kwa sababu kinachowekwa kama dhamana ya kuchukulia mkopo, tungetamani iwe hiyo leseni yenyewe ambayo mchimbaji anapewa. Kwa hiyo, tunalikamilisha ili tufanye kwa namna ambayo hatutakosea kama tulivyowahi kukosea huko nyuma, kuwapatia watu mikopo na baadaye watu hao wakapotea na fedha zenyewe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Bulaya, halafu Mheshimiwa Hussein Amar.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri anajua Bunda kuna wachimbaji Kamkenga na Kinyambwiga naye amefika. Sasa sisi kule wachimbaji wetu wanataka watengenezewe mazingira bora ya uchimbaji, kwa sababu hali iliyoko pale siyo nzuri, na siyo kuwahamisha: Ni lini sasa mtawapatia mikopo wachimbaji wa Kinyambwiga na Gwishigwamara ili waweze kununua mashine ya kisasa na waweze kuchimba kama wachimbaji wengine kwenye maeneo mengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimimiwa Waziri wa Madini, majibu ya swali hilo zuri la wanawake.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikubali kwamba Kinyambwiga na maeneo mengine aliyoyataja ni maeneo ambayo kwenye Wilaya ya Bunda ndiyo yanatupatia mapato mengi sana. Wachimbaji wa kule wanafanya kazi nzuri ya kuchimba. Pamoja na kwamba kuna changamoto kidogo za ki-*management,* katika eneo lile wako watu ambao wana mashamba, wako watu wenye leseni, tunakamilisha ule mgogoro ili uchimbaji uendelee kufanyika kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo, ni kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi, ni lazima tukubali Waheshimiwa Wabunge kwamba, kumpatia mtu fedha ni lazima kuwe na utaratibu ambao uta-*guarantee* fedha hiyo kuweza kurudi na kuwakopesha watu wengine. Tusingependa kutoa mikopo ambayo mwisho wa siku fedha hizi zitapotea na aliyepewa pesa haonekani na pesa hazionekani na tunashindwa kuwakopesha wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeomba Waheshimiwa Wabunge watupe muda, *study* hii inaendelea na Mheshimiwa Rais mwenyewe analijua jambo hili na ametupa maelekezo mahususi ya kuangalia namna bora ya kulifanyia kazi ili wachimbaji wetu waweze kupata tija.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hussein Amar swali la mwisho kwa Wizara ya Madini.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema kuna uchimbaji wa wachimbaji wadogo kwenye maeneo ya leseni, na kuna wachimbaji ambao wanachimba kwenye eneo la rashi; lakini wachimbaji hao wadogo wanatumia fedha na gharama kubwa kutoa ile mifuko ndani ya ardhi. Unakuta anatoa mifuko 100, lakini wasimamizi wa kwenye rashi wanachukua asilimia 40:

Kwa kuwa wao husimamia tu: Serikali inatoa kauli gani ili kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo, ipunguze hiyo mifuko 40? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimimiwa Waziri wa Madini, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati njema Mheshimiwa Amar ni mchimbaji mzoefu na anajua sekta hii. Tulikotoka ilikuwa mchimbaji mdogo anachimba anatoa mawe, msimamizi au miaka ile walikuwa wanaitwa ma-*digger,* yeye peke yake anachukua asilimia 70. Serikali tulitoa mwongozo maalum wa usimamizi wa *rash* na tukasema hivi, katika uchimbaji wowote unaofanyika mahali popote kwenye maeneo yasiyokuwa rasmi, mgawanyo utakuwa kama ifuatavyo: asilimia 15 itakwenda kwa mwenye shamba, asilimia 15 itakwenda kwa msimamizi, na msimamizi fedha hiyo atakayoipata itatumika kwa ajili ya kujenga miundombinu kama vile vyoo na huduma mbalimbali maeneo ya uchimbaji huo. Asilimia 70 yote inayobaki ni kwa ajili ya mchimbaji ambaye yuko kwenye shimo anayetumia nguvu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaratibu ni huo na mwongozo upo. Kama kuna mahali unakiukwa, tuwasiliane Mheshimiwa Mbunge ili tuchukue hatua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Madini kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Anatropia Rwehikila Theonest, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 264

**Barabara ya Karagwe – Nkwenda – Murongo**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST** aliuliza:-

Je, ni lini barabara inayotoka Karagwe kupitia Nkwenda hadi Murongo itatengenezwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY KASEKENYA MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Kyerwa hadi Chonyonyo (Kilometa 50) zimetangazwa na kufunguliwa tarehe 10 Mei, 2022. Kwa sehemu iliyobaki, Serikali ipo kwenye hatua ya manunuzi ya kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hiyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Waziri amenijibu mchakato. Najua na ninatambua taratibu kwamba lazima hiyo michakato ifanyike. Sasa swali langu linabaki, ni lini? Kwa sababu natambua mtatangaza zabuni na Serikali inafuata utaratibu na *schedule;* kwa hiyo, nataka kujua ni lini? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili: Wilaya ya Kyerwa, *TANROADS* ina mtandao mdogo wa barabara ya Kyerwa na *TARURA* wana mzigo mkubwa ikiwepo na madaraja: Je, Serikali haioni ni wakati muhimu wa kutanua mtandao wa barabara kuunganisha Kata ya Nkwenda - Songambele pamoja na Karagwe na Rwanda kwa upande wa Kusini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo ya nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY KASEKENYA MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, huu tena siyo mchakato, tumetaja tarehe 10 mwezi huu wa Tano, zabuni imefunguliwa. Ukishafungua zabuni, maana yake tayari unaanza kujenga utakapokuwa umempitisha Mkandarasi baada ya kufanya *evaluation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, zipo taratibu ambazo zinafuatwa ili barabara zipandishwe kutoka hadhi ya kuhudumiwa na *TARURA* na kuhudumiwa na *TANROADS.* Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba viko vikao ambavyo vinapitia, zinaletwa kwenye Wizara, Wizara inaenda kufanya tathmini na kuona hizi barabara zinakidhi vigezo halafu zinapandishwa kutoka *TARURA* kuja *TANROADS?* Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mheshimiwa Anthony Mwantona nimewaona.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali

lini itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Kibada, Kisarawe II mpaka Tundi- Songani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu ya swali hilo fupi la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY KASEKENYA MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Mariam Kisangi Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti iliyopitisha jana barabara hiyo inajengwa kwa kiwango cha lami na iko kwenye manunuzi na tutajenga kilomita 41 kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anthony nilikutaja na Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. ANTHONY A. MWANTONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini barabara inayoanzia KK Kata ya Kimo ikipitia Ikwenjola, Ikuti, Ibungu mpaka Kafwafwa ambayo iko kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi itajengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu ya swali hilo fupi la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY KASEKENYA MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwantona Mbunge wa Rungwe Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Kimo, Kafwafwa, Luswiswi, Katengele hadi Ibunge kwenye bajeti ya mwaka huu tunaokwenda kuitekeleza imepangwa ifanyiwe upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa na maandalizi ya

kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami baada ya kukamilisha hizo taratibu za awali, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, kwa kipindi kirefu kumekuwa na mchakato wa upanuzi wa barabara ya *New Bagamoyo Road* na *Old Baganoyo Road* kwa ajili ya kuondoa foleni Mkoa wa Dar es Salaam. Na kwenye *New Bagamoyo Road* hususan kutoka Tegeta Kibaoni kwenda mpaka Daraja la Bagamoyo. Na kwa *Old Bagamoyo Road* kutoka Morocco mpaka Afrikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka nijue ni lini mchakato huu utaanza kwa sababu imekuwa kwenye mipango muda mrefu na utekelezaji umekuwa finyu. Ni lini barabara hizi mbili zitapanuliwa *New Bagamoyo Road* kwenye eneo ambalo nimekutajia na *Old Bagamoyo Road* katika Ukanda wa Morocco Daraja la Mlalakua mpaka Afrikana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY KASEKENYA MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Halima Mdee Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mpango kabambe wa kupunguza misongamano kwenye miji na ikiwepo Mji wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, katika bajeti tunazoenda nazo barabara hizi zimeainishwa kwamba itakuwa ni barabara ambazo zitapewa kipaumbele ili kujengwa kwa barabara nne ama sita ili kupunguza msongamano. Kwa hiyo, nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zipo zinaendelea na fedha itakapopatikana basi hiyo kazi itaanza mara moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata swali la mwisho la nyongeza kwa wizara hiyo.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Ni lini Serikali itapasua na kumalizia barabara inayotoka Mtowisa, Ngongo mpaka Kristo Mfalme Sumbawanga DC? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu ya swali hilo fupi la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY KASEKENYA MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata Mbunge wa Viti Maalum Rukwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja pia ni ahadi ya viongozi wa kitaifa. Naomba nimwakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatafuta fedha ili kuweza kuipasua hii barabara inayoanzia Mtowisa kama ambavyo viongozi waliahidi kufanya hivyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante na nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na uchukuzi kwa majibu hayo ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi sasa ni swali la Mheshimiwa Maulid Ali Mohamed Mbunge wa Kiembe Samaki.

Na. 265

**Kukarabati Kituo cha Polisi Mazizini- Kiembe Samaki**

**MHE. MAULID ALI MOHAMED** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakifanyia ukarabati Kituo cha polisi Mazizini pamoja na kukarabati nyumba za Askari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimwa Maulid Ali Mohamed Mbunge wa Kiembe samaki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya tathmini ya uchakavu wa kituo na nyumba za makazi za askari polisi Mazizini na kubaini kuwa kiasi cha fedha shilingi 64,484,700 zinahitajika kugharamia ubadilishaji paa, dari, mfumo wa umeme, maji safi, maji taka na kupaka rangi. Ukarabati huo utafanyika kulingana na mpango wa ukarabati kutegemea na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maulid Ali Mohamed.

**MHE. MAULID ALI MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kumpa ushauri mmoja. Kituo hiki ni kituo chetu cha Wilaya na bahati mbaya sana kipindi cha mvua askari wetu wanalazimika kuhama kule juu kwa sababu kumekuwa na bwawa. Sasa pamoja na hiyo *program* ya kutengeneza nyumba zote za polisi lakini ningeomba kitu kimoja. Kama kuna uwezekano wa lile paa lifanyiwe dharura halafu masuala mengine yatafuata baadaye, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea ushauri wake tutaufanyia kazi na mara nitakapopata nafasi ya kuja Kiembe Samaki tutapata nafasi pia ya kushauriana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oliver Semguruka nimekuona.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona niweze kuuliza swali la nyongeza. Changamoto iliyopo Kiembe Samaki inafanana kabisa na changamoto iliyoko Wilaya ya Ngara kituo cha Polisi cha Rurenge kimchakaa kabisa mpaka kinavuja. Je, ni lini Serikali itakifanyia ukarabati kituo hicho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimwa Oliver kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatambua uchakavu wa Kituo cha Polisi Rurenge tena ambacho kiko karibu na mpaka. Kama nilivyoeleza katika majibu niliyomjibu hivi karibuni ni mpango wa Serikali kuvikarabati vituo vyote kikiwemo hiki cha Rurenge na hivi vituo vya mpakani Mheshimiwa Mbunge tutavipa msisitizo maalum, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara nimekuona.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba nimuulize swali la nyongeza Mheshimiwa Waziri kwamba kule Tarime eneo la Rorya, Sirari, Nyasicha, Muliva, Itilio, Nyanungu. Eneo hilo kuna malalamiko ya wananchi mengi kwamba wale maaskari wanatembea na marungu kwenye magari kwa hiyo, watu wakikamatwa wanapigwa sana. Nilitaka

niulize utaratibu wa sheria umebadilika au huu ni mtindo wa kule Tarime ndio tu upo kwa sababu ni kanda maalum? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Waitara Mbunge wa Tarime Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, si mpango wa wizara wala Jesho la Polisi kutembea na marungu kwenye magari kwa ajili ya kupiga wananchi wake. Lakini nafahamu kwamba kuna wakati Askari wanalazimika kukamata wahalifu na wahalifu wanapofanya upinzani nguvu inayotakiwa kutumika ni ile tu inayoshabihiana na nguvu pinzani lakini si marungu kwa ajili ya kupopoa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bakari Hamad swali la nyongeza.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nyumba za Askari katika kambi ya Askari Mfikiwa ni chakavu sana. Je, ni upi mpango wa Serikali katika kuziboresha nyumba zile?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi tunatambua uwepo wa uchakavu wa vituo na makazi ya Askari. Kama nilivyokwishakusema ni mpango wa wizara kufanya ukarabati wa majengo hayo kutegemeana na uwepo wa bajeti. Mwaka huu tutaanza na yale ambayo yapo kwenye kipaumbele tutaendelea na ukarabati kadri miaka inavyokwenda kulingana na upatikanaji wa fedha nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy Kilave nilikuona.

**MHE. DOROTHY G KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nina swali moja nyumba za bara pale Kilwa Road. Kuna maghorofa yalitangulia kujengwa sasa sijui ndio yameishia pale pale na wale wengine bado wako kwenye zile nyumba ambazo Kilwa Road Barax. Maghorofa yale yamejengwa vizuri lakini katikati pana nafasi sijui ndio mwisho pale maana yake zile nyumba sasa ni ndogo sana na zinavuja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Dorothy Kilave wa Temeke kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kota za Askari kule Temeke Kilwa Road unaendelea na kama pana dosari zozote ambazo zimeoneshwa na Mbunge kama maeneo mengine yanavuja tutamwelekeza *IGP* ili kumsimamia mkandarasi aweze kusimamia mjenzi ahakikishe kwamba viwango vilivyowekwa vinazingatiwa ili kuondoa hizi dosari ambazo zimeonekana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Jumanne Sagini kwa majibu hayo ya Wizara ya Mambo ya Ndani. Tunaendelea sasa na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo Mbunge wa Kishapu aulize swali lake.

Na. 266

**Kumaliza changamoto za mawasiliano ya simu katika baadhi ya Kata – Kishapu**

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka mawasiliano ya simu katika baadhi ya Kata Wilayani Kishapu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu Kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imepanga kufikisha huduma za mawasiliano ya simu katika Kata za Busangwa, Itilima, Masanga, Mwakiponya, Mwamalasa, Shagihilu na Talaga ndani ya mwaka wa fedha wa 2022/2023 ili kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu katika kata hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kata hizo zimejumuishwa katika zabuni inayotarajiwa kutangazwa kabla ya mwaka wa fedha wa 2021/2022 kukamilika kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze Serikali na hasa *Engineer* Kundo kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Lakini nimpongeze pia kwa namna ambavyo amefanya ziara katika Jimbo langu na kuiona changamoto hii kubwa katika eneo langu. Sasa kwa kuwa kata saba kati ya kata tisa ambazo zilikuwa na changamoto na sasa Kata ya Somagedi na Mwasubi bado zina changamoto ya aina hiyo hiyo. Je, nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba maeneo haya

yaliyo na changamoto ya mawasiliano ya simu na yenyewe yanafanyiwa kazi kwa haraka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo Mbunge wa Kishapu Kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kata ambazo amezitaja Mheshimiwa Mbunge zina changamoto ya mawasiliano lakini kati ya kata tisa kata saba anaenda kupata mawasiliano. Na haya maeneo katika hizi kata saba zote yanapatikana katika kitabu chetu cha bajeti ukurasa wa 153 ukianzia namba 578 mpaka namba 584 zote ni Kata za Kishapu ambazo zinaenda kupata huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaamini kabisa kwamba baada ya kukamilisha kata hizi saba basi kwa sababu utekelezaji hauwezi ukaenda kwa pamoja baada ya kukamilisha hizi basi tutaangalia uwezekano namna ambavyo tunaweza kuleta mawasiliano katika kata mbili ambazo zitakuwa zimebaki, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko nimekuona, Mheshimiwa George Malima.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kumekuwepo na mwingiliano mkubwa wa mawasiliano na minara ya *Safaricom* kwenye kata ambazo ziko mpakani kwa upande wa Tarime na Rorya. Na hii inapelekea gharama kubwa kwa watumiaji kwa maana inaingia kwenye *roming* lakini pia uhafifu wa mawasiliano. Sasa nilitaka kujua ni lini

Serikali itahakikisha inapeleka minara toshelezi ili wananchi wa kule waweze kupata mawasiliano bila kuingia upande wa Kenya wanakuwa kama wako Kimataifa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko Mbunge wa Viti Maalum Kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa katika maeneo ya Wilaya ya Rorya pamoja na Tarime kuna changamoto ya mawasiliano na changamoto yenyewe ni kuingiliana. Vilevile Serikali kupitia mradi wetu wa *special zone and boarders* tayari maeneo hayo tumeyazingatia kuhakikisha kwamba mawasiliano yanaenda kuimarishwa ili kusiwepo na mwingiliano wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tunaelewa kabisa mwingiliano unasumbua na unaingilia hata masuala ya kiuchumi na kiusalama. Serikali inajua hilo na inachukua juhudi mahususi kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto hiyo.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa George Malima, Mheshimiwa Furaha Matondo na Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Jimbo la Mpwapwa lina changamoto kubwa sana ya mawasiliano na hasa katika Kata za Luhambi, Lupeta, Mlembule, chitemo na Ihondo. Je, ni lini Serikali itaweka minara ya mawasiliano ili kutatua tatizo hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Mpwapwa Kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa maeneo mengi nchini bado yana changamoto ya mawasiliano. Lakini kwa maelekezo ya Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi ni kweli maeneo ni makubwa lakini hatuwezi kuyatekeleza ndani ya mwaka mmoja. Na ndio maana tunapanga mpango wa mwaka mmoja, tunapanga na mpango wa miaka mitano tunaamini kabisa kwa kipindi ambacho kuanzia sasa mpaka 2025 maeneo mengi yatakuwa yamepata suluhisho la mawasiliano kwa ajili ya wananchi wetu, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Furaha nilikutaja na Mheshimiwa Bilakwate.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Halmashauri ya Wilaya ya Ilemela Kata ya Sangabuye Kituo cha Afya hakuna mawasiliano. Kata ya Kayenze Kisiwa cha Bezi hakuna mawasiliano. Ni zaidi ya miaka minne sasa Serikali iliahidi kupeleka minara katika kata hizo. Je, ni lini Serikali itapeleka minara katika kata hizo ili wananchi wa kata hizo waweze kupata mawasiliano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Furaha Mbunge wa Viti Maalum Kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Sangabuye ni eneo ambalo liko pembezoni mwa Ziwa Victoria ambapo mwaka huu mwezi wa pili nilifanya ziara na nikajionea hali halisi. Na Serikali ilichukua juhudi mahususi za kuhakikisha kwamba tunatafuta

mtoa huduma akajenge mnara. Na tayari mkandarasi wa kwenda kujenga mnara katika eneo la Sangabuye tayari ameshapatikana. Hivyo tunasubiri tu muda wa utekelezaji ukamilike na wananchi wa Kata ya Sangabuye na Kituo cha Afya kilichopo pale waendelee kupata mawasiliano na vilevile wakinamama ambao wanatakiwa kulipa kwa kutumia M-pesa na Tigo-pesa basi haya mambo yote yaweze kwenda bila kuwa na shida yoyote, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilakwate nilikutaja.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwenye Wilaya Kyerwa mwaka 2020/2021 kwenye bajeti tulitengewa minara saba na Mheshimiwa Naibu Waziri ulifika Kyerwa ukatuahidi minara hiyo itajengwa lakini mpaka leo minara hiyo haijajengwa na wananchi wanaendelea kupata adha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Bilakwate Mbunge wa Kyerwa Kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa nilifika katika kata hizo na katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge. Vilevile labda nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge ni kwamba tunapotangaza *tender* na mtoa huduma akapatikana maana yake yeye anaingia sasa kwenye kutafuta mkandarasi ambaye anaenda kumjengea minara hiyo. Na sasa tayari watoa huduma washatujulisha kwamba wako katika mchakato wa kuhakikisha kwamba mkandarasi anapatikana kwa ajili ya kwenda kujenga ile minara. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge awe na

subira kidogo lakini utekelezaji wa Serikali pale inapoahidi ni lazima ahadi yake itatimizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKIT:** Ahsante sana nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia kwa majibu ya leo.

Tunamalizia Wizara ya mwisho kwa leo Wizara ya Afya Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 267

**Utoaji na upatikanaji wa huduma za afya**

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza:-

Je kuna Sheria ya Huduma ya Afya inayosimamia utoaji na upatikanaji wa huduma za afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya inasimamia Sheria zifuatazo thelathini zinazolenga kusimamia ubora, utoaji wa huduma, maadili ya kitaaluma, kiutumishi na upatikanaji wa huduma za afya nchini, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo swali la nyongeza.

**MHE: AGNES HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu ya Serikali naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Je, ni sheria ipi kati ya hizo sheria 30 inayosimamia wanawake wajawazito wakati wa kujifungua wanaopata huduma zisizoridhisha? Hilo ni swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na swali la pili; je, sheria hizo zinaruhusu malipo ya fidia kwa wagonjwa wanaopata huduma zisizoridhisha au zisizo na ubora zinazopelekea athari za kiafya au hata kifo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nijibu swali la Mheshimiwa Agness Hokororo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa namna ambavyo anafuatilia namna wananchi wanavyotolewa huduma za afya katika eneo lake. Ni kweli kwamba kumekuwepo na mambo anayoyasema kwa maana ya huduma ya mama na mtoto lakini si tu sheria, sheria za nchi yetu, utaratibu wa nchi yetu na kanuni za Wizara ya Afya zinataka mama mjamzito na watoto chini ya miaka mitano wapate huduma bure lakini sasa tunapokuja kujibiwa vibaya, kujibiwa kwa masuala ya fedheha maana yake kuna sheria za kiutumishi ambazo zipo zimeonyesha watu wanaofanya mambo yanayofanana na hayo lakini kuna sheria za maadili ya kitaaluma ambayo mara nyingi anapopatikana mtu ambaye amekuwa akijibu vibaya akifanya nini wakati mwingine anapitishwa kwanza kwenye sheria za maadili ya kitaaluma anawajibika lakini anaachiwa vilevile sheria za kiutumishi zichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge kama mdau mkubwa kwenye eneo hilo endelea kutusaidia na

kutusaidia kutengeneza ushahidi wa kutosha kuwapata watu wa namna hiyo ili waweze kushughulikiwa kulingana na taratibu na sheria, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani nilikuona.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wananchi wa Jimbo la Ushetu kwa kutumia nguvu zao wameweza kukamilisha zahanati saba; Zahanati ya Butibu, Zahanati ya Itumbo, Itebere, Makongoro, Manungu, Bugera na Misayo ambayo ni Zahanati tumeipa kwa jina la Eliasi Kwandikwa ambayo imejengwa kwa msaada wa Kampuni *GTI* na hiyo zahanati yenyewe tayari inavifaa tiba. Lakini sasa ni lini Serikali inatuletea vifaatiba na watumishi kwenye zahanati hizi ili wananchi waweze kupata matibabu yao maeneo ya karibu badala ya kuendelea kwenda zaidi ya kilometa 80 kupata matibabu.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwanza mimi na yeye ili tufanye mambo ambayo yanatekelezeka ametaja zahanati zenye tatizo cha kwanza awasiliane na Mganga Mkuu wa Wilaya yake kupitia Mkurugenzi ili walete mahitaji husika wa eneo hilo mimi na yeye tushughulikie hilo liweze kufanyika nanimuambie tu Mheshimiwa Mbunge pamoja na fedha ambayo Mheshimiwa Rais wetu ameshazipeleka *MSD* lakini kwenye manunuzi ya juzi ya fedha zile za UVIKO kununua vifaatiba kama *X-Ray, CT Scan* Serikali ime-*save* yaani imepata salio baada ya kununua kwa bei rahisi ime-*save* zaidi ya bilioni 17 na zote zinaelekezwa kwenye kununua vifaatiba na madawa kwaajili ya vituo vinavyoanzishwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista nimekuona, Mheshimiwa Felista nimekutaja.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna sheria inayo *guide* mama wajawazito na wagonjwa kwaajili ya kutibiwa. Je, nini upande wa pili wa Serikali kuhusiana na vituo vya afya ambavyo hakuna jengo la mama na mtoto mfano Kata ya Wazo ambapo kunatokea vifo vingi kutokana na kukosekana kwa jengo hilo? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Mbunge ni shahidi hapa kwamba kwa mwaka huu katika historia ya Tanzania kuliko wakati wote fedha nyingi zimepelekwa kwenye eneo la afya naniukweli kwamba hatutaweza kumaliza vyote kwa wakati mmoja lakini kwakweli hoja yako Mheshimiwa Mbunge niyamsingi, kimsingi basi shirikiana na halmashauri yako na hata leo tuandike vizuri tuhakikishe tunashirikiana na wenzetu wa TAMISEMI iingie kwenye utaratibu na kama haijawahi kuingia kwenye utaratibu tuanze sasa mchakato litekelezeke lakini kwa chini ya Rais Samia Suluhu Hassan wala usipate wasiwasi na hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Regina nilikuona.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwakuwa suala la huduma ya mama na mtoto imekuwa na changamoto kubwa.

Je, ni kwanini sasa Serikali isiweke kanuni inayosimamia Sera ya Huduma ya Mama na Mtoto? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo fupi Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali nyeti na la msingi la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba kwanza tukishaleta Sheria ya Bima ya Afya kwa wote tutakuwa tumemaliza mambo mengine yote mimi ninachomuomba Mheshimiwa Mbunge kwasababu tayari tumekuja kwenu na mmeona mchakato wetu unaoendelea wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote na unaendelea kwa sasa ikifika hapa Bungeni tuhakikishe tumetengeza sheria nzuri, utaratibu mzuri nataka kuwahakikishia haya matatizo yanayojitokeza kila siku tutakuwa tumeyatafutia suluhisho la kudumu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kimei nilikuona.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vituo vyetu vya afya kwenye Jimbo letu la Vunjo kuna uhaba mkubwa wa wahudumu lakini pia kuna wahudumu ambao wanataka kujitolea ili wasaidie na wenyewe wamesomea mambo hayo hayo ya ukunga nakadhalika na unesi lakini hawana kazi. Je, Wizara haioni umuhimu wa kuweka utaratibu wa kuwaruhusu hawa ambao wanataka wajitolee kusaidia kutoa huduma bure hata kama watalipwa kidogo na wananchi ili waweze kuchukuliwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza anachokisema Kimei ni kweli kipo na nimetembelea jimbo lake tumeliona hilo na ameshakieleza mara nyingi lakini sasa Mheshimiwa Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu alishaelekeza na tayari utaratibu, muongozo wa ajira ya kujitolea umeshatengenezwa kwa *level* ya Hospitali za Mikoa na kwenda juu. Sasa tunashirikiana na amesema atashirikiana na Mheshimiwa Bashungwa ili kutengeneza na utaratibu kwa kushuka chini tuone tunafanyaje hilo liweze kutekelezeka kwa urahisi lakini ni jambo jema sana kwasababu hata kwenye shule zetu tumeona kwamba kuna walimu wengi wanajitolea na

wanasaidia sana watoto nayo kwenye afya tungetamani tuwe na jambo kama hilo lakini tulitafakari kwa kina kabla ya kutekeleza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rwamlaza swali la mwisho la nyongeza kwa wizara hiyo.

**MHE. CONCHESTA LEONCE RWAMLAZA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Nchi yetu ni kutoa Huduma ya Afya bure kwa wazee lakini sera hii imekuwa haitekelezeki kwasababu hakuna sheria. Je, ni lini Serikali itatunga sheria ili kumbana mpeleka huduma na mtoa huduma ili sera hii iweze kutekelezwa sawasawa kwa wazee? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokisema Mbunge kipo sidhani kama tatizo ni sheria tatizo ni kwamba wazee kweli wamewekewa dirisha lao lakini wanapoandikiwa *prescription* na madaktari na baadhi ya vipimo wanapofika kwenye kufanya vipimo au kuchukua dawa wanakosa dawa husika na hilo ndiyo maana tunazungumzia suala la usimamizi wa dawa kwenye vituo vyetu na kuhakikisha dawa zipo kwenye vituo vyetu ambalo kwaweli kama Wizara ya Afya na TAMISEMI sisi wenyewe huku juu hatutaweza tunawaomba Waheshimiwa Wabunge, Baraza la Madiwani na Wakuu wa Wilaya wasimamie kwasababu kuna fedha nyingi zinakuja za *Basket Fund* na mambo mengine ambayo usimamizi ukifanyika tutapunguza tatizo kwa zaidi ya asilimia 80 lakini Mheshimiwa Mbunge tukishapitisha Muswada wa Bima ya Afya kwa watu wote maana yake kimsingi suala hilo tena alihitaji sheria suala hilo ni kwamba tutakuwa tumelitatua moja kwa moja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel kwa majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge muda wetu wa maswali ndiyo umefikia hapo sasa ni wakati wa matangazo naanza na wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Kuna wageni ambao wapo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, ni wageni 11 wa Mheshimiwa Spika ambao ni Waheshimiwa Wajumbe wa Jumuiya ya Idadi ya Watu na Maendeleo Zanzibar kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar wameambatana na watendaji kutoka Tume ya Mipango Zanzibar. Wageni hawa wametembelea Bunge kukutana na kujifunza *portfolio* ya masuala ya idadi ya watu katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Naomba msimame ni hao hapo Waheshimiwa wetu ambao wako kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, kutoka Zanzibar, karibuni sana katika mafunzo hayo na kuliona na kutembelea Bunge letu karibuni sana. *(Makofi)*

Pia kuna Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Hudhaima Mbarak Tahir, Mwenyekiti wa Jumuiya, karibu sana Mheshimiwa Hudahima Mbarak. *(Makofi)*

Mheshimiwa Yahya Rashid Abdulla, Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya, karibu Mheshimiwa Yahya. *(Makofi)*

Pia kuna Mheshimiwa Fatma Ramadhani Mohamed, Katibu wa Jumuiya. *(Makofi)*

Kuna Mheshimiwa Azza Januar Joseph, Mshika Fedha Baraza la Wawakilishi Zanzibar. *(Makofi)*

Kuna Mheshimiwa Abdullbaki Mwalimu Haji Afisa Mwandishi wa Taarifa Rasmi za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, karibuni sana

wageni wetu kutoka huko Zanzibar Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Pia tuna watendaji kutoka Tume ya Mipango kwenye Jukwaa hilo hilo la Mheshimiwa Dkt. Rahma Salim Mahfoudh, Katibu Mtendaji Tume ya Mipango Zanzibar na yeye pia anatoka Zanzibar. *(Makofi)*

Pia kuna Salama Ramadhani Makame, Kamishina Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watenda Kazi Tume ya Mipango Zanzibar. *(Makofi)*

Lakini pia Umrat Suleiman Mohammed Afisa Mipango Tume ya Mipango Zanzibar. *(Makofi)*

Kuna Mwadini Haji Kheir, Afisa Mipango Tume ya Mipango Zanzibar, kuna Ibrahim Abdalla Abdalla, Afisa Mipango Tume ya Mipango Zanzibar, na kuna Omar Makame Juma Afisa Mipango Tume ya Mipango Zanzibar. *(Makofi)*

Pia kuna wageni 81 wa Mheshimiwa Spika ambao ni Umoja wa Wanafunzi wanaotokea Mbeya wanaosoma Chuo Kikuu cha Dodoma *(MBESO UDOM),* karibuni sana wanafunzi wetu wa Mheshimiwa Spika kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma ambao mnatokea Mbeya. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni Wajumbe wa Bodi ya Huduma katika Soko la Samaki Feri kutoka Dar es Salaam Ndugu Benson Lutenta, Mwenyekiti wa Bodi ya soko, Ndugu Deni Mrema, Katibu wa Bodi ya Huduma ya Soko na Mkuu wa Soko na Mkuu wa Soko na pia tuna Ndugu Mbaraka Kilima, Mjumbe wa Bodi ya Huduma ya Soko na Mwenyekiti Kamati ya Wadau wa Soko, karibuni sana wageni wetu wa Naibu Spika katika jukwaa hilo la Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Pia tuna wageni 137 wa Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge ambaye ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi ambao ni viongozi na watendaji wa Wizara ya Taasisi zilizochini ya wizara hiyo wakiongozwa na Bwana Tixon Nzunda Katibu Mkuu Mifugo. *(Makofi)*

Na pia Ndugu Dkt. Rashid Tamatamah, Katibu Mkuu Uvivu. Karibuni sana wageni wetu wote mliokuwa hapo kwenye Jukwaa la Spika. *(Makofi)*

Pia kuna wageni wa waheshimiwa Wabunge wapo wageni mbalimbali wa waheshimiwa Wabunge waliotembelea Bunge naomba wasimame wote kwa umoja wao kwa pamoja ambao wamebaki. *(Makofi)*

Lakini pia tuna wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo kuna wanafunzi 100 na walimu 4 kutoka *Real hope Pre and Primary and Secondary Schools* ya Mafinga Iringa sijui kama wamepata fursa ya kuingia wanafunzi kutoka Iringa naona hawakuingia. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 60 kutoka Chuo cha Kilimo cha Sokoine *SUA* kilichopo Mkoani Morogoro ambao ni Makada wa Umoja wa Vijana UVCCM na wao pia naona hawajapata fursa ya kuingia. *(Makofi)*

Lakini pia tuna wanafunzi na walimu 44 kutoka shule ya Msingi Ngarenaro Mkoani Manyara na wao naona sijui wapo, wapo wale pale karibuni sana wanafunzi na walimu 44 kutoka shule ya Msingi Ngarenaro Mkoani Manyara, karibuni sana. *(Makofi)*

Nafikiri wageni wengine hawajapata fursa wanaweza kuingia baadaye tutaendelea kuwatangaza kwa ujumla wageni wetu wote ambao mmetembelea leo karibuni sana katika Bunge

letu na wale ambao mmejifunza kutoka Zanzibar karibuni sana kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Pia kuna tangazo hapa linaletwa kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Ofisi ya Bunge ilianza utaratibu ya kutoa fursa kwa Watumishi wa Bunge vijana ambao hawajawahi kupata mafunzo ya JKT kupata mafunzo hayo kwa lengo la kujenga nidhamu, uadilifu, utii ukakamavu, uhodari, uvumilivu na uzalendo kwa nchi yao. *(Makofi)*

Kwa kawaida mafunzo hayo hufanyika katika kikosi cha 834 KJ Makutupora kwa muda wa siku 38 katika Bunge hili la 12 baadhi ya Wabunge Vijana wamewahi kuhudhuria mafunzo hayo katika kambi mbalimbali hapa nchini kwa kuwa ofisi inakusudia kuomba nafasi ya kupeleka kundi lingine kuanzia mwezi Julai, 2022 Wabunge vijana wenye nia na utayari wa kupata mafunzo haya wanaombwa wajitokeze ili waweze kujumuishwa katika kundi hilo kwa kuwasilisha majina yao kwa Katibu wa Bunge. *(Makofi)*

Wabunge vijana nafikiri mmeelewa tangazo hilo na mimi nawashawishi muandike maombi kwa majina yenu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Katibu tuendelee na ratiba.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Hokororo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba mwongozo wako kutokana na tangazo umetoka kulitangaza sasa hivi ni kweli Wabunge vijana walienda kwenye mafunzo ya JKT, lakini ningependa Mwongozo wako kwa nini sasa haya mafunzo ya Wabunge vijana isiwe hiari iwe lazima ili Wabunge wote Vijana ambao hawajapita JKT wapite kwaajili ya kuwajengea uzalendo, ukakamavu ili nchi yetu iwe na askari wa akiba kuanzia humu Bungeni mpaka mtaani na sisi wengine tulienda ni ma-*service girl.*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hokororo nilikuona.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi naomba kuomba Mwongozo wako kwa kanuni ya 76 kuhusu jambo linaloruhusiwa au lisiloruhusiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa maswali na majibu swali langu namba 267 niliuliza maswali mawili ya nyongeza lakini sasa hayo maswali mawili ya nyongeza sidhani kama ni namba moja ama namba mbili ambalo lilipata majibu naomba mwongozo wako. Je, inaruhusiwa kwa Mheshimiwa Waziri kutokujibu maswali na kutokusema kwamba swali hilo nitapata majibu baadaye?

**MWENYEKITI:** Mwingine nilimuona amesimama Mheshimiwa Msukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Na mimi naomba Mwongozo kwa kanuni hiyo hiyo ya 76 kutokana na hilo tangazo lako la JKT maana JKT ni sehemu ya kufundishwa uzalendo na kwa vile hii Taasisi ya Bunge tunahitaji kuwa na uzalendo wa hali ya juu. Kwa nini tunabagua Wabunge vijana, kwa nini tusiende wote na wazee? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuna miongozo mitatu hapa. La kwanza kutoka kwa Mheshimiwa Ester, naomba tusikilizane sasa. Waheshimiwa naomba tusikilizane ili tupate majibu ya miongozo.

Hapa tuna Mwongozo wa kwanza kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya yeye anasema kutokana na hilo tangazo ambalo nimetoa, kwa nini hawa vijana isiwe lazima badala ya hiyari? Ni kwamba kwa vile hili limekuja ni tangazo na mimi nimelipokea hapa nimelitangaza. Kwa hiyo, naomba nilirudishe, tukae, tujadiliane vizuri halafu tuone umuhimu wa kufanya hiyo lazima kwa vijana ambao hawajapita huko jeshini. *(Makofi)*

Lakini suala lingine la Mheshimiwa Hokororo kuhusu swali lake namba 267 majibu hayakutosheleza anavyosema. Kwa vile yeye mwenyewe hajajua ni swali la kwanza ama la pili halijapata majibu sahihi. Naomba turudi kwenye *Hansard*. Katibu tutarudi kwenye *Hansard* ili tuone jinsi yalivyojibiwa na kama hayajajibiwa kiukamilifu basi tutaomba hayo majibu yaje tena kwa mara nyingine. Lakini naomba sana Mawaziri mjitahidi kujibu maswali kwa mujibu wa Wabunge walivyouliza. Msi-*skip* hata swali moja, tafadhalini sana Waheshimiwa Mawaziri muweze kujibu moja kwa moja maswali ambayo yameulizwa kwa umakini ili tusiwe na miongozo kama hii ya kuomba kwamba swali langu halijajibiwa vizuri. *(Makofi)*

Lakini Mheshimiwa Musukuma pia ameuliza suala hilo zuri sana na mimi nimelipenda. Mwongozo huo wa kwamba kwa nini wale hata wazee ambao hatujaenda tuweze kwenda hilo ni suala pia zuri naomba nalo nirudishe kwa wenzetu ili tulitafakari vizuri halafu tuone umuhimu wa sisi wengine ambao hatujaenda pamoja na mimi mwenyewe niweze kwenda. *(Makofi/Vicheko)*

Basi baada ya hapo Katibu tuendelee. *(Makofi/Kicheko)*

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, ndc – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza na hoja za Serikali. Sasa nitamwita hapa Waziri wa Mifugo na Uvuvi ili aweze kusoma hoja hiyo ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Karibu sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi. Naomba hotuba yangu hii iingie yote kwenye kumbukumbu za Bunge *(Hansard)* kwa kuwa ni ndefu na sitaweza kusoma yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia Kilimo, Mifugo na Maji, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Fungu 99 – Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2021/2022. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Kwa heshima, taadhima na unyenyekevu mkubwa namshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kuendelea kushika wadhifa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri unaolenga kuifanya nchi yetu iendelee kupiga hatua kubwa za maendeleo ya kiuchumi na kijamii na sisi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunaahidi kuendelea kumuunga mkono katika kuwatumikia wananchi hususan wafugaji, wavuvi, wachakataji, wasindikaji na wafanyabiashara wa mifugo na uvuvi na mazao yake kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Nitumie nafasi hii kumuombea kiongozi wetu kwa Mwenyezi Mungu, awe na afya njema, Mungu aendelee kumpa hekima na busara katika kuiongoza nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kumsaidia ipasavyo Mheshimiwa Rais kwa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi mahiri katika kuwatumikia wananchi ambapo katika kipindi cha uongozi wake tumeshuhudia mabadiliko makubwa katika utendaji wa Serikali ya Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kazi nzuri ya uratibu na usimamizi wa shughuli za Serikali. Pia, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha hotuba yake iliyotoa mwelekeo wa utendaji wa sekta zote ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti

wa Bunge na wa Kamati mbalimbali ambao mnatuongoza ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum; na Makamu wake Mheshimiwa Athumani Almas Maige, Mbunge wa Jimbo la Uyui kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2022/2023. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuendelea kuwawakilisha wananchi kwa umahiri mkubwa katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika majukumu katika Wizara mbalimbali wakiwemo Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Waziri wa Maliasili na Utalii; Mheshimiwa Januari Makamba, Mheshimiwa Hamad Masauni, Mheshimiwa Hussein Bashe, Mheshimiwa Nape Nnauye, Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji; na Manaibu Mawaziri Mheshimiwa Anthony Mavunde, Mheshimiwa Ridhiwan Kikwete, Mheshimiwa Steven Lemomo Kiruswa, Mheshimiwa Jumanne Sagini na Mheshimiwa Atupele Mwakibete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Wabunge wapya waliochaguliwa kuwawakilisha wananchi katika majimbo yao ambao ni Mheshimiwa Emmanuel Shangai, Mbunge wa Ngorongoro; Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, Mbunge wa Ushetu; pamoja na Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Mbunge wa Kuteuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Mheshimiwa Irene Alex

Ndyamkama, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Rukwa; Mheshimiwa William Ole Nasha, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji; Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; na Mheshimiwa Khatib Said Haji, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salaam za pole kwa familia za Marehemu, ndugu na wananchi ambao walikuwa wanawatumikia. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema Peponi; Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Mbunge wa Mkuranga kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, na nimshukuru kwa kunisaidia kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru sana Makatibu Wakuu wa Wizara Bwana Tixon Tuyangine Nzunda anayeshughulikia Mifugo, Dkt. Rashid Adam Tamatamah anayeshughulikia Uvuvi kwa kuwa viungo muhimu kati yangu na watumishi na kuniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, nawashukuru kwa dhati na kuwapongeza watumishi wote wa Wizara yangu kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Maswa Magharibi, na siku ya leo wamewakilishwa hapa na Waheshimiwa Madiwani wa Jimbo la Maswa Magharibi, pamoja na Kamati ya Siasa ya Wilaya yetu ya Maswa, kwa ushirikiano mnaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu, pamoja na kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa na kwa umuhimu mkubwa nimshukuru sana mke wangu, Mama

Joyce Ndaki. Huyu mama amekuwa akiniombea, akinitia moyo na kunipa kila ninachokihitaji ili kwamba moyo wangu uweze kutulia, lakini pia niweze kuwa na pumziko zuri. Nakushukuru sana mke wangu na Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2021/2022 idadi ya mifugo hapa nchini imeongezeka sana ikilinganishwa na mwaka wa 2020/2021 ambapo idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka milioni 33.9 hadi milioni 35.3, mbuzi kutoka milioni 24.5 hadi milioni 25.6 na kondoo kutoka milioni 8.5 hadi milioni 8.8. Aidha, kuku wameongezeka kutoka milioni 87.7 hadi milioni 92.8 na nguruwe kutoka milioni 3.2 hadi milioni 3.4. Aidha, Sekta ya Mifugo katika mwaka wa 2021 ilikua kwa kiwango cha 5% sawa na mwaka 2020 na mchango wake katika pato la Taifa ulikuwa 7%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Fungu 99 ilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 50. Hata hivyo, kiasi kilichokusanywa ni Shilingi 29,015,984,354.48 sawa na asilimia 69.6 ya lengo la makusanyo hadi tarehe 30 Aprili, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2021/2022, Wizara kupitia Fungu 99 ilitengewa jumla ya Shilingi 47,844,949,810. Kati ya fedha hizo, Shilingi 30,973,208,810 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 16,871,741,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na matumizi ya bajeti ya kawaida, hadi kufikia tarehe 30/4/2022, jumla ya shilingi 24,985,718,173.85 zimetolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambazo ni sawa na asilimia 80.06 ya bajeti. Kati ya hizo, shilingi 15,859,730,900 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na shilingi 9,125,987,273.10 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa 2021/2022, fedha za miradi zilizoidhinishwa ni fedha za ndani kiasi cha shilingi 16,871,741,000 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo ya sekta ya mifugo. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 shilingi 9,214,038,480 sawa na asilimia 55 zilikuwa zimepokelewa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na utekelezaji wa mpango kwa mwaka 2021/2022 uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita bilioni 3.1 mwaka 2020/2021 hadi kufikia lita bilioni 3.4 mwaka 2021/2022. Aidha, usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita milioni 75.9 2020/2021 hadi lita milioni 77.6 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa nyama umeongezeka kutoka tani 738,166 mwaka 2020/2021 hadi tani 769,966.7 mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia 4.3. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa wafugaji na kuongezeka kwa hamasa kwa wafugaji kuvuna mifugo yao na kupatikana kwa masoko ya nyama ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Bodi ya Nyama imeendelea kusimamia biashara ya nyama kwenda nje ya nchi. Hadi tarehe 30 Aprili, 2022 jumla ya tani 8,877.80 za nyama zimeuzwa zikijumuisha tani 1,390.86 nyama ya ng'ombe; tani 4,997.45 nyama ya mbuzi; tani 1,909.02 nyama ya kondoo; tani 5,000.7 nyama ya kuku; na tani 4,000.9 nyama ya nguruwe. Tani 300 za wanyama wengine zenye thamani ya Dola za Kimarekani 36,264,786.13. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 400.4 ikilinganishwa na tani 1,774.29 za nyama zenye thamani ya Dola za Kimarekani 4,290,000 zilizouzwa katika mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na uzalishaji wa kuku kwa mwaka wa 2021/2022; mashamba ya kuku ya wazazi nchini yameongezeka kutoka 22 hadi 24 yakiwa na uwezo wa kutunza

zaidi ya kuku wazazi milioni 1.3 ambayo yamezalisha vifaranga milioni 92.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na biashara ya mifugo na mazao yake katika mwaka wa 2021/2022 ng'ombe 2,194,937 na mbuzi na kondoo 1,782,010 wenye thamani ya Shilingi trilioni 1.3 waliuzwa katika minada mbalimbali hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na tozo, ada na tozo mbalimbali; kwa mwaka 2021/2022, tozo ya asilimia moja ya thamani ya mzigo, tozo ya Shilingi 100 kwa kilo ya nyama ya ng'ombe na Shilingi 50/= kwa kilo ya nyama ya mbuzi na kondoo inayouzwa nje ya nchi zilirekebishwa. Kwa sasa wafanyabiashara wanatozwa Shilingi 110,000/= kwa shehena. Aidha, Wizara inafanya mapitio ya kanuni mbili ili kuleta unafuu katika uzalishaji na biashara ya mifugo na mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na malisho, vyakula na maji. Katika mwaka wa 2021/2022 maeneo ya malisho yamefika hekta milioni 3.2 kutoka hekta milioni 3.1 mwaka 2021. Pia maeneo 22 ya malisho yenye jumla ya hekta 143,754.02 katika Mikoa ya Arusha na Manyara yamesajiliwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa vyakula vya mifugo umeongezeka kutoka tani milioni 1.2 mwaka 2020/2021 hadi tani milioni 1.4 mwaka 2021/2022 kutokana na ongezeko la viwanda kutoka 154 mwaka wa 2020/2021 kufikia 199 mwaka wa 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na utatuzi wa migogoro. Katika mwaka 2021/2022 mikutano 28 ya utatuzi wa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi imefanyika katika Mikoa ya Katavi, Rukwa, Pwani, Lindi, Mtwara, Tanga na Songwe. Kutokana na mikutano hiyo, migogoro 13 imetatuliwa na mingine ipo katika hatua mbalimbali za utatuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jitihada tunazoendelea nazo kwenye eneo la Msomera na eneo la Loliondo. Eneo lililotengwa kwa ajili ya malisho katika eneo la Kijiji cha Msomera Handeni ni hekta 22,746. Aidha, Wizara imejenga majosho mawili mapya na kukarabati josho lingine moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya imeanza utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu uhifadhi wa pori tengefu la Loliondo. Wizara imewaelimisha na kuwahamasisha kaya 228 za wafugaji katika Kata sita kuhusu ufugaji wa kibiashara na endelevu unaozingatia mazingira na umuhimu wa kutambua mifugo kwa hereni za kielektroniki. Pia ujenzi wa josho moja umekamilika na majosho tita ujenzi unaendelea katika hatua mbalimbali. Vilevile ng’ombe 1,252 wamehimilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ustawi wa Wanyama; matukio ya ukamataji wa mifugo usiofuata utaratibu hususan kwenye maeneo ya hifadhi yamepungua kutoka mifugo milioni 6.2 iliyokamatwa mwaka 2020/2021 hadi mifugo 3,343 iliyokamatwa mwaka 2021/2022. Hali hii imetokana na wadau mbalimbali kuelewa na kuzingatia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na huduma za ugani wa mifugo; katika mwaka wa 2021/2022 Wizara imenunua pikipiki 300 na kuzisambaza kwa Maafisa Ugani wa Mifugo katika mamlaka 141 za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2021/2022 wanawake 273 wamepatiwa mafunzo kupitia mashamba darasa manne ya ufugaji bora wa kuku yaliyoanzishwa katika Mikoa ya Pwani na Lindi ambapo vifaranga 5,500 vimesambazwa kwa vikundi 27 vya wanawake walioshiriki mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza Wizara itaanza kutumia mfumo wa kiektroniki kwa ajili ya kutoa vibali vya biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi. Tayari usanifu na utengenezaji wa mfumo huo uitwao *Mifugo Management Information System* umekamilika. Mfumo huo utaboresha mazingira ya ufanyaji wa biashara na utawezesha wafanyabiashara na wadau wengine wa sekta ya mifugo kupata vibali au kufanya usajili wa biashara za mifugo na mazao yake mahali walipo bila kulazimika kuja Wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kampuni ya *Ranch* za Taifa katika jitihada za kupunguza migogoro baina ya *NARCO* na vijiji jirani jumla ya ekari 6000 zimemegwa katika *Ranch* za Uvinza kwa ajili ya matumizi ya wananchi wa vijiji cha Chakuru na Mpeta Wilaya ya Uvinza, vilevile *NARCO* imepima eneo la *Ranch* ya Mwisatu na kutenga hekta 66, 215.76 zenye vitalu 89 kwa ajili ya wawekezaji na hekta 11,772.15 kwa ajili ya kuzigawa katika vijiji vinavyopakana na *Ranch* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kutumia fursa hii kufanya marekebisho katika kitabu cha randama ukurusa wa 42 kuhusu hoja ya Mheshimiwa Charles Mwijage, juu ya *Ranch* ya *NARCO* nipende kulitaarifa Bunge lako Tukufu kuwa kuna makosa ya kiuandishi kuwa katika kushughulikia mgogoro wa *Ranc*h ya Kagoma, Lora Katoro, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara ya Kisekta zitakaa na kuandaa mwongozo wa namna ya kushughulikia mgogoro huo, hususani Kijiji cha Katoro, kinachopakana na *Ranch* ya Kagoma lengo ni kuwawezesha wananchi wa Kijiji cha Katoro kuendelea na shughuli zao ikiwemo ufugaji, kwa mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2021 maabara ya *veterinary* wakala wa *veterinary* hapa nchini

umeanza uzalishaji wa chanjo ya mpya ya homa ya mapafu ya mbuzi uliosubiliwa kwa hamu, hii ni kwa sababu chanjo hii ilikuwa ikiagizwa nje ya nchi kwa gharama kubwa ya Shilingi 40 kwa dozi 100 ikilinganishwa na Shilingi elfu 30 kwa dozi 100 kwa chanjo inayozalishwa na kuuzwa ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama kubwa ya chanjo iliyokuwa ikiagizwa kutoka nje ya nchi ilisababisha mbuzi wengi kutokapata chanjo kwa sababu ya gharama na upatikanaji wa chanjo hiyo. Aidha *TVLA* imepata idhibati ya kimataifa katika uchunguzi wa magonjwa ya mifugo kupitia vipimo 10 vya kimaabara na kupewa namba ISO17025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye mabadiliko ya ukomo wa bajeti ya wizara katika mafungu yote mawili 99 na 64, Wizara ya Mifugo na Uvuvi iliongezwa ukomo wa bajeti kwa kiasi cha shilingi bilioni 100 kati ya fedha hizi shilingi bilioni 40 ni fedha za Fungu 99, sekta ya mifugo na shilingi 60 bilioni ni za Fungu 64 sekta ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeongezeka kutoka Shilingi 168 bilioni 252 milioni na saba hadi kufikia shilingi bilioni 268 milioni 252 na elfu saba kati ya fedha hizo shilingi bilioni 92 50 milioni 500 824 elfu ni kwa ajili ya sekta ya mifugo na shilingi 176,201,183,000 kwa ajili ya sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza sana na kumshukuru tena Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa sekta hizi mbili na kuziongezea bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2022/2023 upande wa mifugo katika mwaka wa 2022/2023 Wizara itazalisha mbegu dozi 1,500,000; na kuhimilisha ng'ombe 373,307 kuhusiana na Uzalishaji na Usambazaji wa Mitamba mwaka 2022/2023, Wizara itaimarisha mashamba ya kuzalisha mitamba ya Sao Hill , Kituro, na Mabuki kwa kuyapatia ng'ombe wazazi na vitendea kazi ikiwemo matrekta 3 na vifaa vyake, tanunua madume ya mbegu 366 kwa ajili ya kuboresha mbali za mifugo na itazalisha mitamba 3500 na kuisambaza kwa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Uzalishaji wa Nguruwe mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kushirikiana na *Tanzania Association of Pig Farmers* kuhimilisha nguruwe 600 na kuzalisha nyama ya nguruwe tani 46,000. Kuhusiana na biashara ya mifugo na mazao yake mwaka 2022/2023, Wizara itajenga minada minne ya upili katika maeneo ya Msomera Tanga Mkongeni Morogoro, Majimoto Katavi, na Utengule Mbeya kukarabati minada sita ya upili kujenga mnada mmoja wa mpakani wa Rorya kule Mara, na minada 15 ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na rasimali za malisho mwaka 2022/2023, Wizara itajenga malambo manne kukarabati malambo 17 kuimarisha mashamba 5 ya Serikali yanayozalisha mbegu za malisho na malisho kuanzisha mashamba darasa 100 ya malisho yenye ukubwa wa ekari tano kila mmoja katika mamlaka za Serikali za Mitaa na kushirikiana na wadau mbalimbali kutenga hekta milioni moja za maeneo ya malisho. Pia Serikali itaendelea kuwahamasisha wawekezaji katika sekta binafsi kuzalisha tani milioni 1580 za vyakula vya mifugo kilo 5281 za mbegu za malisho na marobota 60,000 ya *hay*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo mwaka 2022/2023 Wizara itaendelea kutambua na kusajili mifugo 45,000,000 kwenye mfumo wa kielektroniki. Uendelezaji wa maeneo ya Msomela la Lolihondo tutaendelea kuboresha eneo la Msomela Handeni. Wizara itaanzisha mashamba darasa yenye ukubwa wa ekari kumi kwenye kila kitalu, kimoja cha hekta 100 pia itajenga bwawa moja kwa ajili ya mifugo majosho manne kituo cha kukusanyia maziwa kimoja Kliniki ya Mifugo moja na kuhimilisha ng'ombe 6,000. Wizara inakusudia kufanya Kijiji cha Msomela kuwa Kijiji cha mfano kwa ufugaji wa kisasa hapa nchini na tutawaambia wafugaji watakuwa wanakuja kujifunza kwenye Kijiji cha Msomela namna ambavyo wafugaji watakao kuwa hapo, wale walioko hapo na wale watakao kuja hapa watakavyokuwa wakifuga kisasa kwa tija na kwa biashara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Loliondo itaanzisha mashamba darasa ya malisho ekari 22 kuihimilisha ng'ombe 4,000 na kutajenga bwawa moja. Kuhusiana na Huduma ya Afya ya Mifugo mwaka 2022/2023, Wizara itasambaza dozi 100,000,000 za magonjwa 13, lakini pia itachanja mifugo 80,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu unakwenda sana lakini nivumilie kidogo kuhusiana na *Ranch* ya Taifa *NARCO* kwa mwaka wa 2022/2023 Kampuni ya *NARCO* itatekeleza mpango wa mabadiliko *transformation plan for NARCO* ambao utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu hii ni katika jitihada za kuimarisha uzalishaji na biashara ya nyama na mifugo mpango huo kwa mwaka 2022/2023 unalenga kukodisha vitalu vitano vyenye ukubwa wa takribani hekta 32,500 kwa wawekezaji mahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yatakayoanza na mpango huo ni *Ranch* za Ruvu, Mzeri na Mwisatuu, aidha *NARCO* itanunua ngombe wazazi 1000 kwa ajili ya *Ranch* za *NARCO* Kongo na Mzeri itananunua mitambo ya shambani kwa ajili ya *Ranch i*kiwemo matreka matatu leki tatu za nyasi beila tatu mowa tatu itazalisha malisho na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhuisana na Bodi ya Maziwa katika mwaka 2022/2023, Bodi ya Maziwa itaanza kujenga vituo vya kukusanyia maziwa 10 kuratibu mpango Unywaji Maziwa Shuleni katika shule 52 itaongeza vituo 10 ya kuuzia maziwa katika Ofisi za Serikali kufanya ukaguzi kwa wadau 1,200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2022/2023, Bodi ya Maziwa kushirikiana na *TADB* - Taifa *International Land or Legs, Venture* 37 kuwa ufadhili wa B and Emelida *Gate* na mradi wote husika na ujenzi wa vituo vya kukusanyia maziwa usambazaji wa mitamba ya ng'ombe wa maziwa uhimilishaji na kuwajengea uwezo wadau katika minyororo wa thamani wa tasinia ya maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Sekta ya Uvuvi mwaka 2021 Sekta ya Uvuvi ilikuwa kwa asilimia 2.5 na ilichangia asilimia 1.8 pato la Taifa, aidha sekta ya uvuvi inatoa ajira kwa watanzania takriban Milioni 4.5 hadi tarehe 30 Aprili, 2022, jumla ya wavuvi wadogo wapatao 194,804 walishiriki moja kwa moja katika shughuli za uvuvi kwa kutumia vyombo vya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ya mazao ya uvuvi nje ya nchi hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2022 tani 34841.72 za mazao ya uvuvi na Samaki hai wa mapambo 16989 wenye

thamani ya Shilingi bilioni 475 waliuzwa nje ya nchi na kuingizia Serikali mrabaha wa shilingi bilioni 15.47 ukilinganisha na tani 32,962 za Samaki hai wa mapambo 104 wenye thamani ya Shilingi bilioni 460 waliouzwa nje ya nchi na kuingizia Serikali mrabaha wa shilingi bilioni 15.55 mwezi Aprili mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliendelea kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya wawekezaji kutokana na juhudi hizo sekta ya uvuvi imewezesha kuvutia uwekezaji mkubwa katika ufugaji wa Samaki kibiashara wenye thamani ya Shilingi bilioni 11 zilizowekezwa na ya Kampuni za Tilapia na *Tan green*. Kupitia uwekezaji huo, takriban tani 15,000 za samaki zinatarajiwa kuzalishwa kwa mwaka, pia Serikali imeingia mashirikiano na Serikali ya Misri, kupitia Kampuni ya Taifa ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji kwa lengo la kuwekeza kwa pamoja na Shirika la Uvuvi Tanzania yaani *TAFICO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana kutokana na jitihada za kukabiliana na uvuvi haramu ni kudhibitiwa kwa kutumia milipuko katika Ukanda wa Bahari ya Hindi kwa asilimia 95. Aidha, kwa upande wa maji baridi uvuvi haramu umepungua kwa asilimia 80. Wizara imechukua hatua stahiki za kisheria kwa watuhumiwa 1,123 waliobainika kujihusisha na vitendo vya uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2021/2022 katika sekta ya uvuvi sekta hii ya uvuvi ilipangiwa kukusanya Shilingi bilioni 40,000,000,000 kupitia Fungu 64. Hadi tarehe 30 Aprili, 2022, Shilingi 19,171,950,269 zilikusanywa sawa na asilimia 63.9 ya lengo la ukusanya hadi tarehe 30 Aprili, 2022, mwaka 2021/2022 fedha zilizoidhinishwa katika mwaka huo Sekta ya Uvuvi ilikuwa ni ya Shilingi 121,350,047,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 22,205,681,000 ni

kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 99,144,366,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa upande ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida, Fungu 64 ilitengewa jumla ya Shilingi 22,205,681,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 11,575,270,000 ni kwa ajili ya Mishahara Shilingi 10,630,411,000 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka 2021/2022 katika Usimamizi na ulinzi wa rasimali za uvuvi Serikali ilinunua injini za kupachika 12 ambazo zimepelekwa katika vituo vya usimamizi wa rasilimali za Uvuvi vya Mwanza, Geita Ukerewe Kanyigo Marehe na Simiyu. Pia Serikali imenunua boti za dolia 16 ambazo zimepelekwa kwenye vituo vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi vilevile wizara imepokea boti moja ya dolia na injini moja ya kupachika yenye nguvu farasi 40 toka kampuni ya GHL ambayo itatumika kuimarisha usimamizi katika ukanda wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo hifadhi za bahari na maeneo tengefu mwaka 2021 wizara kupitia kitengo cha hifadhi za bahari na maeneo tengefu inaendelea kusimamia maeneo 18 yanahusisha hifadhi za bahari tatu ambazo ziko katika mikao ya Mtwara, Mkoa wa Pwani na Mkoa wa Tanga. Hifadhi ya bahari silikati Tanga pamoja na maeneo tengefu 15 katika Mkoa ya Dar es salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya maeneo hayo ni kisiwa kidogo cha Shungimbili ambacho *MPRU* imeingia makubaliano na mwekazaji kampuni ya Tanda Tanzania *Limited* kujenga na kuendesha *hotel* ya kitalii ya nyota, tano pamoja na kulipa maduhuli ya Serikali wekezaji huu umeleta faida kubwa kwa nchi ikiwemo kutoa ajira kipato na

kuongeza idadi ya watalii kwa kuitangaza Tanzania ikiwemo kushinda tuzo za *Africa's reading luxury highland na world this reading exclusive private highland* 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Usimamizi wa Uvuvi katika Bahari Kuu mwaka 2021/2022, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu imetoa leseni 25 za uvuvi wa bahari kuu, kukodisha na kutoa kibali cha kuvua nje ya maji ya Tanzania kwa meli moja na kukusanya Shilingi bilioni 3.3 ikilinganishwa na idadi ya meli sita zilizopewa leseni na kukusanya jumla ya Shilingi 288,677,014 mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mamlaka imeingia makubaliano ya uvuvi na Kampuni ya Uvuvi ya *ALBACORA Group* kutoka Hispania ikiwa ni juhudi za kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi kupitia uvuvi wa Bahari Kuu. Katika kutekeleza makubaliano hayo tarehe 21 Machi, 2022, meli ya *PACIFIC STAR* inayomilikiwa na kampuni ya *ALBACORA Group* ilipokelewa katika Bandari ya Dar es Salaam na Viongozi wa Wizara husika za SMT na SMZ pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ALBACORA pamoja na kulipia leseni ya uvuvi ya kiasi cha Dola za Kimarekani 21,000, pia imelipa kiasi cha Dola za Kimarekani 400,000 kwa mwaka kwa meli hiyo ya uvuvi wa nyavu za kuzungusha *purse seine*, itashusha kiasi cha tani 100 za samaki wasiolengwa nchini na kuuza tani 300 za samaki waliolengwa kwa makampuni ya hapa nchini. Vilevile, kampuni hiyo itajenga kiwanda cha kuchakata samaki ambacho kitatoa ajira zipatazo 100 na kuongeza mapato yatokanayo na uvuvi wa bahari kuu kwa kusafirisha nje samaki na mazao yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuzaji Viumbe Maji, kama nilivyoahidi kwenye Bunge lako Tukufu mwaka jana, wizara kwa kushirikiana na mikoa ya Mwanza na Kagera imefanya tathmini na kuainisha maeneo 39 ya ufugaji wa Samaki kwa vizima katika Ziwa Victoria maeneo hayo kwa Mkoa wa Mwanza ni kama ifutatavyo, naomba nisiyataje yapo kwenye hotuba yangu maeneo yote yana uwezo wa kuweka vizimba 19,500 vitakavyotoa takribani ajira 5000 na tani 100,0000 elfu za Samaki zenye thamani ya Shilingi bilioni 600 kwa mwaka iwapo mbinu bora za uzalishaji zitazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili linalenga kupunguza gharama za awali za uwekezaji ili kuwawezesha wanawake, vijana na wananchi wa kawaida waweze kutumia fursa iliyopo kuongeza uzalishaji Samaki kutoa ajira kuongeza kipato na kukuza uchumi nchini, aidha wizara kupitia wakala wa elimu ya uvuvi na mafunzo kwa kushirikia na Mkoa wa Mwanza imetoa mafunzo kuhusu ufugaji Samaki kwenye vizimba kwa vijana 283 kutoka katika Halmashauri za Nyamagana, Misungwi Buchosa Sengerema Ukerewe Magu na Ilemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti kuhusiana na huduma za ugavi wa uvuvi, katika mwaka 2021/2022, wadau 22,233 kutoka halmashauri 20 wamepatiwa mafunzo rejea uvuvi na ukuzaji viumbe maji vyama 25 vya ushirika vimeanzishwa hivyo kufanya Vyama vya Ushirika vilivyotambuliwa hadi sasa kufika 172.

Mheshimiwa Mwenyekiti sera na utafiti *TAFIRI* imekamilisha utafiti wa uendelezaji wa mnyororo wa thamani wa dagaa na migebuka kupitia Awamu ya kwanza ya mradi wa *African Caribbean Pacific Countries* katika mikao na wilaya zilizopo katika mwambao wa Ziwa Tanganyika. Matokeo ya utafiti huu yamewezesha kuandaliwa kwa

mpango na uendelezaji wa mnyororo wa thamani ambapo katika kipindi cha miaka mitatu ijayo mradi utaboresha miundombinu ya uchakataji wa Samaki mialo na mifumo ya ubaridi na ugandishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sihara na shirika la uvuvi Tanzania *TAFICO* mwaka wa 2021/2022 Serikali iliahidi kununua meli mbili za uvuvi na viambata vyake katika *program* ya kuendeleza kilimo na uvuvi iliyofadhiliwa na mfuko wa kimataifa wa maendeleo ya kilimo *IFAD* kwa ajili ya Shirika la Uvuvi Tanzania, katika utekelezaji wa *program* hii kumekuwa na changamoto mbalimbali ikiwemo wafadhili kuchelewa kutoa fedha za mradi na hitaji la kufanyika kwanza kwa tathmini ya athali za kimazingira na kijamii kwa kutumia fedha za ndani za Serikali za SMT na SMZ.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa changamoto hii imetatuliwa ambapo muafaka umefikiwa kwamba *ESIA* ya uvuvi wa bahari kuu kwa SMT na SMZ itafanywa kwa kupitia fedha za mradi wa *program*. Katika mwaka wa 2021/2022 Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekamilisha ujenzi na ukarabati wa mialo ya kupokea Samaki Kayenze, Igombe Ihale na soko la Samaki Mbambabay, vilevile ujenzi wa ofisi ya vituo vya Nyakalilo na Sota unaendelea. Aidha kazi ya ukarabati wa vituo vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji vya Lubambagwe Luhila, Nyegedi, Lufula Mtwara zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021/2022 Wizara kupitia mradi wa usimamizi shirikishi wa uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi SWIOFish umekalimilisha ujenzi wa ofisi tano za *BMU* katika Halmashauri za Pangani Nkinga Bagamoyo. Lindi vijijini na Chalinze na kuzinunulia thamani za ofisi na vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mpango wa Fedha 2022/2023 upande wa Uvuvi, mwaka 2022/2023 *MPRU* itafanya doria za siku kazi 900 hili kuhakikisha kuendelea kuwepo kwa rasilimali za uvuvi nchini na kuhamamisha matumizi endelevu ya rasilimali hizo. Aidha *MPRU* itaimarisha utangazi wa vivutio vyake pamoja na kuboresha miundombinu ya utalii, wa kiokolojia ikiwemo kununua boti mbili zenye vioo chini pia *MPRU* itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa hoteli za kiikolojia za kitalii katika maeneo yaliyohifadhiwa ikiwemo visiwa vilivyopo Bahari ya Hindi kama vile Nyororo, Sinda, Kware, Kirui, Mbarakuni na Mbudya ili kuongeza idadi ya watalii na mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *MPRU* itakamilisha mazungumzo na Kampuni ya Nungwi *Dreams Resort Limited* ambayo imeonyesha nia ya kuwekeza katika huduma za hoteli za kiikolojia katika maeneo tengefu ya visiwa vilivyopo Bahari ya Hindi. Vilevile, Wizara itaendelea na maandalizi muhimu ya kupokea watalii wengi wanaotarijiwa kutembelea maeneo ya hifadhi za bahari na maeneo tengefu kutokana na mafanikio ya filamu ya Tanzania *The Royal Tour*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Usimamizi wa Uvuvi katika Bahari Kuu mwaka wa 2022/2023, Serikali kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu itatoa leseni 29 za uvuvi kwa meli za uvuvi wa Bahari Kuu kutoka ndani na nje ya nchi ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 2.1 zitakusanywa. Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na Kampuni ya *ALBACORA* itatekeleza mpango wa ujenzi wa kiwanda chenye uwezo wa kuchakata samaki tani 20 kwa siku, vyumba vya ubaridi viwili vyenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,400. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022/2023, Wizara itafanya zoezi la tathmini na kuanisha maeneo ya ufugaji wa samaki katika vizimba katika Mikoa ya Simiyu, Mara na Geita. Pia, Serikali itaanza utekelezaji wa mpango wa kuwezesha vijana na

vikundi mbalimbali kufuga samaki kwenye vizimba katika Ziwa Victoria kwa kuanzisha atamizi 246 zenye vizimba 985 vya ukuzaji viumbemaji kwa mikopo ya masharti nafuu kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara itaanzisha mashamba darasa 10 yenye mabwawa 40 kwa ajili ya vikundi vya wanawake na vijana katika halmashauri 10 nchini. Aidha Serikali itaiwezesha *TAFIRI* kuanzisha atamizi maalumu mbili za ukuzaji wa viumbe maji zenye vizimba 40 kitotoreshi, mabwawa ya kukuzia Samaki na mtambo wa kutengeneza chakula cha samaki katika vituo vya *TAFIRI*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ziara ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoifanya Nchini Marekani hivi karibu Kampuni ya *Yona Trading Group* imeonyesha nia kuwekeza Dola za Marekani Milioni 70 katika tasnia ya ukuzaji viumbemaji, fedha hizo zitatekeleza miradi ya ufugaji Samaki kwenye vizimba vya uvuvi katika Mkoa wa Kagera chini ya ushirikiano kati ya Wizara, Mkoa wa Kagera, Chuo Kikuu cha Nelson Mandela na Mfuko wa Kichocheo Maendeleo ya Kilimo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utafiti na shirika letu la utafiti *(TAFIRI)* tarehe 12 Mei, 2022 *TAFIRI* ilisaini hati ya maelewano na Shirika la Uwekezaji la nchini Oman liitwalo *Oman Investment Authority* ili kushirikiana kufanya utafiti wa wingi wa mtawanyiko wa samaki katika ukanda wa uchumi wa bahari makubaliano hayo yataiwezesha *TAFIRI* kufanyakazi muhimu kwa maendeleo ya Uchumi wa *Blue* katika mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile *TAFIRI* itaendelea kufanya tafiti za wingi, aina na mtawanyiko wa samaki katika Maziwa Makuu, Victoria, Tanganyika na Nyasa. Tafiti hizi ni muhimu kwani zitasaidia Wizara kuweka misingi bora ya usimamizi endelevu, rasilimali za uvuvi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Shirika la Uvuvi Tanzania *(TAFICO)* mwaka 2022/2023 Serikali itakamilisha zoezi la tathmini ya athari za kimazingira na kijamii katika ukanda wa Bahari Kuu kama sharti la kuwezesha uvuvi wa Bahari Kuu. Aidha Serikali kupitia *TAFICO* itaendelea na taratibu za ununuzi wa meli mbili za uvuvi na vifaa vyake kwa ajili ya kuvua katika Bahari Kuu zitakazonunuliwa chini ya *program* ya kuendeleza kilimo cha uvuvi inayofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo - *IFAD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali itaendeleza uboreshaji na miundombinu ya *TAFICO* iliyopo *RAS* Mkwavi Dar es Salaam vilevile Wizara itakamilisha zoezi la kutambua na kuhakiki mali za *TAFICO* zilizopo katika Mikoa ya Tanga, Pwani, Lindi, Mtwara, Mwanza, Kigoma, Mbeya na Njombe na Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na miradi ya maendeleo mwaka 2022/2023, Serikali itaendelea na ujenzi wa bandari ya uvuvi ambapo imetenga fedha za ndani Shilingi Bilioni 50 kwa ajili ya mradi huu, aidha Serikali itajengwa Mwalo wa Mchinga na masoko ya samaki Tunduma, Kigamboni, Mafia na Kipumbwi. Vilevile Serikali itajenga madarasa matatu, maabara katika kampasi ya *VETA* Mikindani – Mtwara, itakarabati vituo vya ukuzaji viumbe maji vya Luhila – Ruvuma, Nyengedi, Lindi na kujenga kituo cha Ruvura Mtwara. Wizara itaendelea na ujenzi wa kituo cha ukuzaji viumbemaji bahari Kunduchi - Dar es Salaam na Ofisi ya Utawala ya Hifadhi ya Bahari na maeneo tengefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuhitimisha naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja ama nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake katika mwaka wa 2021/2022. Aidha, niwashukuru wadau wa maendeleo wa ndani na nje kwa ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi wakiwemo nchi wahisani, Mashirika mbalimbali ya Kimataifa, Taasisi za Fedha za Kitaifa na

Kimataifa, Taasisi za Kihiyari sisizokuwa za Serikali na za Mashirika ya Kidini bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na ninyi Waheshimiwa Wabunge na Madiwani. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nimpongeze na kumshukuru tena Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoliongoza Taifa letu na anavyotusimamia katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi nina imani kuwa ndani ya uongozi wake tutahakikisha kuwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa itatekelezwa kikamilifu hususan katika sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii tena kuwashukuru na kuwapongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia Kilimo, Mifugo na Maji kwa maoni yao na ushauri uliolenga kuboresha na kuimarisha sekta za Mifugo na Uvuvi. Pia niwashukuru wadau mbalimbali katika Sekta za Mifugo na Uvuvi, Wafugaji, Wavuvi hususani wanaozingatia sheria katika utendaji wao. Napenda kuwaahidi kwamba Wizara yangu itaendelea kusimamia Sekta za Mifugo na Uvuvi na kuunga mkono juhudi za wafugaji wavuvi, wasindikaji na wafanyabiashara wa bidhaa za mifugo na uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Maswa Magharibi, ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono kutekeleza majukumu yangu ya Jimbo naya Kitaifa, niwahakikishie kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi na maarifa kwa moyo wangu wote na nguvu zote ili tulete mabadiliko ya kimaendeleo kwenye Jimbo letu lakini pia kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe pesa kupitia Bunge lako Tukufu. Mwaka 2022/2023 Wizara inaomba Bunge lako

Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Jumla ya Shilingi 268,252,007,000.00 kati ya fedha hizo Shilingi 92,508,240,000.00 ni kwa ajili ya sekta ya Mifugo na Shilingi 176,201,183,000.00 kwa ajili ya sekta ya Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya Mifugo. Wizara inaomba kutumia jumla ya Shilingi 92,050,824,000.00 kwaajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Mifugo, kati ya fedha hizo Shilingi 45,319,776,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 46,731,048,000.00 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wake ni kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Matumizi ya Kawaida Shilingi 45,319,776,000.00 kwa Mishahara ni shilingi 21,336,097,000.00. Matumizi Mengineyo - OC shilingi 23,983,679,000.00, Fedha za Matumizi ya Maendeleo shilingi 46,731,048,000.00. Fedha za Ndani shilingi bilioni 46,592,173,000.00 Fedha za Nje shilingi 138,875,000,000.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Mifugo na Uvuvi Sekta ya Uvuvi Fungu Namba 64 inaomba jumla ya shilingi 176,201,183,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo, kati ya Fedha hizo shilingi 40,522,421,000.00 ni kwaajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 135,678,762,000.00 ni kwaajili ya Matumizi ya Maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo.

Fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 40,522,421,000.00, Mishahara ni shilingi 12,624,592,000.00; Matumizi Mengineyo ni shilingi 27,897,824,000.00; Matumizi ya Maendeleo Shilingi 135,678,762,000.00; Fedha za Ndani shilingi 98,682,025,000.00 na fedha za nje ni shilingi 36,996,737,000.00.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Hotuba hii inapatikana katika *Tovuti ya Wizara: www.mifugouvuvi.go.tz*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MB) WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2022/2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI**

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia Kilimo, Mifugo na Maji iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99 – Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi) Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2021/2022. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2022/2023.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Kwa heshima, taadhima na unyenyekevu mkubwa namshukuru **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kuendelea kushika wadhifa huu.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutumia nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na kuifanya nchi yetu iendelee kupiga hatua kubwa za maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na sisi katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi

tunaahidi kuendelea kumuunga mkono katika kuwatumikia wananchi hususan wafugaji, wavuvi, wachakataji, wasindikaji na wafanyabiashara wa mifugo na uvuvi na mazao yake kwa maslahi mapana ya nchi yetu. Nitumie nafasi hii kumuombea kiongozi wetu kwa Mwenyezi Mungu, awe na afya njema, Mungu aendelee kumpa hekima na busara katika kuiongoza nchi yetu.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutumia nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kumsaidia ipasavyo Mhe. Rais katika kutekeleza majukumu yake.

**5.** ***Mheshimiwa Spika*****,** nitumie fursa hii pia, kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Husein Ally Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi mahiri katika kuwatumikia Wananchi ambapo katika kipindi cha uongozi wake tumeshuhudia mabadiliko makubwa katika utendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**6.** ***Mheshimiwa Spika*****,** nachukua nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa,** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kazi nzuri ya uratibu na usimamizi wa shughuli za Serikali. Pia, namshukuru na kumpongeza, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha hotuba yake iliyotoa mwelekeo wa utendaji wa sekta zote ndani ya Serikali.

**7.** ***Mheshimiwa Spika*****,** napenda kukupongeza wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wewe pamoja na Naibu Spika mmeliwezesha Bunge la **12** kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa kuzingatia Katiba, Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyowekwa.

**8.** *Mheshimiwa Spika*, naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum na Makamu wake **Mheshimiwa Athumani Almas Maige**, Mbunge wa Jimbo la Uyui kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2022/2023. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuendelea kuwawakilisha wananchi kwa umahiri mkubwa katika Bunge hili.

**9.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika majukumu katika Wizara mbalimbali wakiwemo **Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana (Mb.)**, Waziri wa Maliasili na Utalii; **Mheshimiwa Hamad Masauni (Mb.)**, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; **Mheshimiwa Hussein Bashe (Mb.)**, Waziri wa Kilimo; **Mheshimiwa Nape Nauye (Mb.)**, Waziri wa Habari Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; **Mheshimiwa Dkt. Angelina Mabula (Mb.)**, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; **Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.)**, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara; **Mheshimiwa Anthony Mavunde (Mb.)**, Naibu Waziri wa Kilimo; **Mheshimiwa Ridhiwan Kikwete (Mb.)**, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; **Mheshimiwa Lemomo Ole Kiruswa (Mb.),** Naibu Waziri wa Madini; **Mheshimiwa Jumanne Sagini (Mb.)**, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; **Mheshimiwa Atupele Mwakibete (Mb.)**, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

**10.*Mheshimiwa Spika*,** pia napenda kuwapongeza Wabunge wapya waliochaguliwa kuwawakilisha wananchi katika majimbo yao ambao ni **Mheshimiwa Emmanuel Shangai,** Mbunge wa Ngorongoro; **Mheshimiwa Emmanuel Cherehani,** Mbunge wa Ushetu; pamoja na Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mbunge wa Kuteuliwa.

**11.*Mheshimiwa Spika*,** Wizara ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha **Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama,** aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Rukwa, **Mheshimiwa William Ole Nasha**, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji; **Mheshimiwa Elias John Kwandikwa**, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ushetu na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, na **Mheshimiwa Khatib Said Haji**, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde. Naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salaam za pole kwa familia za marehemu, ndugu na wananchi ambao walikuwa wanawatumikia. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu ***mahali*** pema peponi, AMINA.

**12.*Mheshimiwa Spika*,** naomba nitumie nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega**, Mbunge wa Mkuranga kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi na ninamshukuru kwa kunisaidia kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara **Bw. Tixon Tuyangine Nzunda** (Mifugo) na **Dkt. Rashid Adam Tamatamah** (Uvuvi) kwa kuwa viungo muhimu kati yangu na watumishi na kuniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi. Kipekee, ninawashukuru kwa dhati na kuwapongeza watumishi wote wa Wizara yangu kwa kazi nzuri wanayofanya katika kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi nchini.

**13.*Mheshimiwa Spika***, naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Maswa Magharibi, kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu pamoja na kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo katika Jimbo.

## SEKTA YA MIFUGO (FUNGU 99)

## UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2021/2022

### Maeneo ya Kipaumbele katika Mwaka 2021/2022

**14**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 maeneo ya kipaumbele katika Mpango na Bajeti ya Wizara kupitia Fungu 99 yaliyotekelezwa ni pamoja na: -

(i) Kuimarisha afya ya mifugo;
(ii) Kuwezesha upatikanaji endelevu wa rasilimali za vyakula vya mifugo na maji kwa ajili ya mifugo;
(iii) Kuboresha kosaafu za mifugo ili kuongeza tija na uzalishaji;
(iv) Kuboresha biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi;
(v) Kuimarisha huduma za ugani, utafiti na mafunzo katika sekta ya mifugo;
(vi) Kuhamasisha uanzishwaji na kuimarisha vikundi na vyama vya ushirika vya mifugo na mazao yake;
(vii) Kusimamia na kuratibu shughuli za taasisi zilizo chini ya Wizara;
(viii) Kuboresha na kujenga uwezo wa rasilimali watu;
(ix) Kuboresha utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo katika sekta ya mifugo; na
(x) Kuimarisha uratibu na usimamizi wa wataalam wa sekta ya mifugo.

### Makusanyo ya Maduhuli

**15**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Wizara kupitia Fungu 99 ilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi **50,000,000,000**. Hata hivyo kiasi kilichokusanywa ni Shilingi **29,015,984,354.48** sawa na **asilimia 69.6** ya lengo la makusanyo hadi tarehe 30

Aprili, 2022. Upungufu huu kwa kiasi kikubwa umechangiwa na kipindi kirefu cha ukame pamoja na kupungua kwa biashara ya mifugo na mazao yake ndani ya nchi.

**Fedha zilizoidhinishwa kwa Ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo 2021/2022**

**16**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Fungu 99 ilitengewa jumla ya Shilingi **47,844,949,810.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 30,973,208,810** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **16,871,741,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

**Matumizi ya Bajeti ya Kawaida**

**17**. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe Aprili 30, 2022, jumla ya Shilingi **24,985,718,173.85** zimetolewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambazo ni sawa na asilimia **80.06** ya bajeti. Kati ya hizo, Shilingi **15,859,730,900.75** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na Shilingi **9,125,987,273.10** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo**

**18**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, fedha za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa ni fedha za ndani kiasi cha shilingi **16,871,741,000** kwa ajili ya bajeti ya maendeleo ya sekta ya mifugo. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 Shilingi **9,214,038,480** (sawa na asilimia **55**) zilikuwa zimepokelewa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.

**Marekebisho ya Sera, Sheria na Kanuni Katika Sekta ya Mifugo**

***Sera, Mikakati na Programu***

**19.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/2022 Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 ambapo mchakato wa kuihuisha unaendelea; Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo Tanzania (Tanzania Livestock Master Plan - TLMP) pamoja na Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) ya mwaka 2016/2017. Aidha, katika mwaka 2021/2022 Wizara imeandaa Mpango wa Mabadiliko ya Sekta ya Mifugo wa miaka mitano (2022/2023 – 2026/2027) ambao umeandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Awamu ya Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III) kwa kipindi cha 2021/2022 - 2025/2026; Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Malengo Endelevu ya Maendeleo (Sustainable Development Goals - SDGs); Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo; na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020.

***Sheria na Kanuni***

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kupitia na kufanya marekebisho ya Sheria za sekta ya mifugo ili kuboresha mazingira na kuwezesha ukuaji wa sekta ya mifugo kama ifuatavyo: -

(i) Sheria ya Tasnia ya Nyama SURA 421 *(Meat Industry Act, CAP 421)* imerekebishwa kupitia Marekebisho ya Sheria Mbalimbali *Written Laws (Miscelleneous Amendment) (No.9) Act, 2021;*

(ii) Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama SURA 180 (*Grazing Land and Animal Feeds Resources, CAP 180)* imerekebishwa kupitia

Marekebisho ya Sheria Mbalimbali *Written Laws (Miscelleneous Amendment) (No.9) Act, 2021;* na

(iii) Sheria ya Veterinari SURA 319 (*Veterinary Act, CAP 319*) imerekebishwa kupitia Marekebisho ya Sheria Mbalimbali *Written Laws (Miscelleneous Amendment) (No.1) Act, 2022*.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 sheria tano (**5**) za Sekta ya Mifugo zimetafsiriwa kutoka lugha ya kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili ambazo ni:-

(i) Sheria ya Veterinari SURA 319;
(ii) Sheria ya Ustawi wa Wanyama SURA 154;
(iii) Sheria ya Magonjwa ya Wanyama SURA 156;
(iv) Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo SURA 184; na
(v) Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Mifugo SURA 180.

***22.*** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya kanuni tatu (**3**) zimefanyiwa marekebisho chini ya Sheria ya Tasnia ya Nyama SURA 421 na Magonjwa ya Wanyama SURA 156 ambazo ni: -

(i) *The Meat Industry (Import and Export) (Amendment) Regulations, GN. No. 469T/2021;*
(ii) *The Animal Diseases (Animal and Animal Products Movement Control) (Amendment) Regulations, GN. No.496 E/ 2021*; na *(iii) The Animal Diseases (Artificial Breeding) (Amendment) Regulations GN.No.712/2021*.

**Hali Halisi ya Sekta ya Mifugo**

**23.*Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022 idadi ya mifugo hapa nchini imeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2020/2021 ambapo idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka

**milioni 33.9** hadi **milioni 35.3**; mbuzi kutoka **milioni 24.5** hadi **milioni 25.6**; na kondoo kutoka **milioni 8.5** hadi **milioni 8.8.** Aidha, kuku wameongezeka kutoka **milioni 87.7** hadi **milioni 92.8** ambapo kuku wa asili wameongezeka kutoka **milioni 40.4** hadi **milioni 42.7** na kuku wa kisasa wameongezeka kutoka **milioni 47.3** hadi **milioni 50.1**; na nguruwe kutoka **milioni 3.2** hadi **milioni 3.4** (Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2021). Aidha, Sekta ya Mifugo katika mwaka 2021 ilikua kwa kiwango cha asilimia **5.0** sawa na mwaka 2020 na mchango wake katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia **7.0** sawa na mwaka 2020.

**24.*Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita **bilioni 3.1** mwaka 2020/2021 hadi kufikia lita **bilioni 3.4** mwaka 2021/2022 (Bodi ya Maziwa Tanzania, 2022), ambapo kati ya hizo, lita **bilioni 2.3** zilitokana na ng'ombe wa asili na lita **bilioni 1.1** zilitokana na ng'ombe wa kisasa wa maziwa (**Kiambatisho Na. 1).** Aidha, kati ya ng'ombe **milioni 35.3** waliopo nchini ng'ombe wa kisasa wa maziwa ni **milioni 1.26** (Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2021).

**25.*Mheshimiwa Spika,*** usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita **milioni 75.9** mwaka 2020/2021 hadi lita **milioni 77.6** mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia **2.2**. Ongezeko hili limetokana na utoaji elimu ya ufugaji bora wa kibiashara wa ng'ombe wa maziwa; kuongezeka kwa idadi ya vyama vya ushirika wa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa; kuongezeka kwa viwanda vipya **6** ambavyo vinakadiriwa kusindika lita **milioni 1.01** kwa mwaka; pamoja na kuongezeka kwa vituo vya kukusanyia maziwa kutoka **221** mwaka 2020/2021 hadi kufikia **238** mwaka 2021/2022 ambavyo vinakusanya **lita milioni 64.2.** Aidha, viwanda vya kusindika maziwa vimeongezeka kutoka **99** mwaka 2020/2021 hadi kufikia **105** mwaka 2021/2022 (**Kiambatisho Na. 2**). Pia, Wizara imewezesha kuingizwa nchini bidhaa za maziwa kwa kutoa vibali **296** vyenye jumla ya lita milioni **5.2** *(Liquid Milk Equivalent* **-** *LME*) zenye thamani (*Free on Board - FoB*) ya Shilingi **11,126,526,195.**

**26.*Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa nyama umeongezeka kutoka tani **738,166** mwaka 2020/2021 hadi tani **769,966.7** mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia **4.3** ilipofika tarehe 30 Aprili, 2022 (**Kiambatisho Na. 1**). Kati ya hizo, tani **526,350.9** ni za nyama ya ng'ombe; tani **107,791.4** za nyama ya mbuzi na kondoo; tani **91,403.9** za nyama ya kuku na tani **44,420.3** za nyama ya nguruwe. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa wafugaji kuhamasika kuvuna mifugo yao na kupatikana kwa masoko ya nyama ndani na nje ya nchi.

**27.*Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai **bilioni 4.5** mwaka 2020/2021 hadi mayai **bilioni 4.9** mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la asilimia **8.8** mnamo tarehe 30 Aprili, 2022 (**Kiambatisho Na. 1**). Ongezeko hilo limesababishwa na kuimarika kwa vituo **28** vya kutotolesha vifaranga vya kuku vilivyopo nchini kutokana na uhamasishaji na mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta ya mifugo. Pia, wananchi wamehamasika kufuga kuku ili kujikomboa kiuchumi.

**28.*Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 vipande vya ngozi milioni **13.6** (ng'ombe milioni **4.2,** mbuzi milioni **6.9** na kondoo milioni **2.5)** vyenye thamani ya Shilingi **bilioni 28.5** vimezalishwa ikilinganishwa na vipande milioni **11.8** (ng'ombe milioni **4.2**, mbuzi milioni **5.9** na kondoo milioni **1.6)** vyenye thamani ya Shilingi **bilioni 25.9** vilivyozalishwa mwaka 2020/2021.

**29.*Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 jumla ya vipande vya ngozi **1,630,740** (ng'ombe **1,367,405,** mbuzi/kondoo **236,683** na punda **26,652**) vyenye thamani ya Shilingi **bilioni 10.05** viliuzwa katika nchi za Italy, Nigeria, Africa Kusini, Ghana, Pakistan, Marekani, China, Togo na Uganda, ikilinganishwa na vipande vya ngozi milioni **1,500,000** (ng'ombe **1,287,838,** mbuzi **36,259** na punda **175,903**) vyenye thamani ya Shilingi **bilioni 8.7** vilivyouzwa katika nchi za Ghana, Nigeria, China, Indonesia, Ethiopia, Kenya na Italy mwaka 2020/2021.

**Uzalishaji wa Mifugo na Masoko**

***Huduma ya Uhimilishaji***

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi imeendelea kuwezesha utoaji wa huduma ya uhimilishaji kwa wafugaji hapa nchini ambapo hadi tarehe 30 Aprili, 2022, jumla ya ng'ombe **53,410** wamehimilishwa katika mikoa **24** ikilinganishwa na ng'ombe **77,375** waliohimilishwa mwaka 2020/2021 (**Kiambatisho Na. 3**). Kupungua kwa ng'ombe waliohimilishwa kumetokana na kiangazi kikali kilichojitokeza mwaka 2021 na kusababisha uhaba wa maji na malisho, hivyo, kudhoofisha afya za mifugo.

**31.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kimetoa mafunzo ya uhimilishaji kwa wataalam **118** kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa na sekta binafsi (**Kiambatisho Na. 4**). Aidha, kupitia kambi za uhimilishaji jumla ya ng'ombe **3,500** wamehimilishwa.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mbari za mifugo hapa nchini Wizara imeendelea kukiimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kwa kukipatia vitendea kazi vikiwemo mtambo wa hewa baridi ya naitrojeni wenye uwezo wa kuzalisha lita **10** kwa saa; na basi lenye uwezo wa kubeba wanafunzi **30** kwa ajili ya mafunzo ya uhimilishaji nchini. Aidha, Wizara imenunua madume bora **6** ya mbegu aina ya Friesian (**2**), Ayrshire (**3**) na Boran (**1**) kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mbegu bora.

**33.*Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kuimarisha Vituo vitano (**5**) vya Uhimilishaji vya kanda ambavyo ni Kanda ya Kusini (Lindi), Kanda ya Kati (Dodoma), Kanda ya Mashariki (Kibaha), Kanda ya Nyanda za

Juu Kusini (Sao Hill) na Kanda ya Ziwa (Mwanza) kwa kuvipatia pikipiki moja kila kituo kwa ajili ya usafiri wa wataalam ili kurahisisha huduma ya uhimilishaji.

***Uzalishaji na Usambazaji wa Mitamba***

**34.*Mheshimiwa Spika,*** katika 2021/2022, jumla ya mitamba **12,622** ya maziwa na nyama imezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji. Kati ya hiyo, mitamba **2,680** imezalishwa katika Mashamba ya Serikali (**Kiambatisho Na. 5**) na mitamba **9,942** imezalishwa kutoka katika mashamba binafsi ikilinganishwa na jumla ya mitamba **16,809** iliyosambazwa mwaka 2020/2021 ambapo kutoka katika Mashamba ya Serikali ilikuwa mitamba **2,349** na kutoka kwa wafugaji binafsi ilikuwa mitamba **14,460.** Kushuka kwa uzalishaji na usambazaji wa mitamba kumetokana na ukame.

**35.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha mashamba ya Serikali ya kuzalisha mitamba, katika mwaka 2021/2022, Wizara imenunua ng'ombe wazazi **198** aina ya Borani kwa ajili ya Mashamba mawili (**2)** ya Kuzalisha Mitamba ya Ngerengere na Nangaramo ili kuongeza uzalishaji na usambazaji wa mitamba bora kwa ajili ya wafugaji na kuongeza uzalishaji wa maziwa na nyama.

***Uzalishaji wa Kuku na Mayai***

**36.*Mheshimiwa Spika***, kwa 2021/2022, Mashamba ya kuku wazazi nchini yameongezeka kutoka **22** hadi **24 (Kiambatisho Na. 6)** yakiwa na uwezo wa kutunza zaidi ya kuku wazazi **1,340,000**. Aidha, kuna vituo **28** vya kutotolesha vifaranga (**Kiambatisho Na. 7**) vilivyopo katika mikoa ya Dar es Salaam (**9**), Iringa (**2**), Njombe (**1**), Pwani (**11**), Kilimanjaro (**2**), Arusha (**1**), Mbeya (**1**) na Mwanza (**1**).

**37.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, jumla ya vifaranga **92,092,000** vimezalishwa na kusambazwa nchini. Kati ya hivyo, vifaranga **52,344,000** ni vya kuku wa nyama, vifaranga

**32,364,000** ni wa kuku chotara ambapo kati ya hivyo Sasso ni **18,720,000** na Kuroiler **13,364,000** na vifaranga **7,384,000** ni vya kuku wa mayai, ikilinganishwa na vifaranga **88,348,000** vilivyozalishwa mwaka 2020/2021. Aidha, jumla ya vifaranga **2,225,112** vya kuku wazazi na mayai **4,225,753** ya kutotoleshea vifaranga yaliingizwa nchini kutoka nchi za Ufaransa, Uholanzi na Zambia **(Kiambatisho Na. 8)**. Uzalishaji umeongezeka baada ya ongezeko la hamasa ya sekta binafsi katika uzalishaji, ikiwemo ujenzi wa viwanda vya kuzalisha vifaranga.

***Uzalishaji wa Nguruwe***

**38.*Mheshimiwa Spika***, katika 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na Chama cha Wafugaji wa Nguruwe Tanzania (TAPIFA) imeratibu zoezi la uhimilishaji ili kuondoa changamoto ya koo za nguruwe kuzaliana ndani ya mbari (*inbreeding*). Jumla ya nguruwe **287** wamehimilishwa katika mikoa ya Arusha, Morogoro, Dodoma, Mbeya, Pwani, Ruvuma, Katavi, Kilimanjaro, Njombe na Pwani ambapo uwezo wa kushika mimba ulifikia asilimia **86**.

**39.*Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, jumla ya tani **44,420.33** za nyama ya nguruwe zimezalishwa ikilinganishwa na tani **41,467.82** zilizozalishwa mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia **7.1.** Aidha, Wizara inahamasisha wafugaji wa nguruwe kutumia mbegu bora kwa teknolojia ya uhimilishaji. Pia, nitumie fursa hii kuzielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa machinjio ya nguruwe.

**Haki Miliki za Waboreshaji Mbari za Wanyama**

**40. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kufanya uchambuzi wa koo **12** za ng’ombe wa asili ambapo imebaini kuwa koo za ng’ombe aina ya Mkalama Dum ipo

katika hatari ya kutoweka. Ili kukabiliana na changamoto hii Wizara inafanya utambuzi na uchambuzi wa ng'ombe aina ya Mkalama Dum kwa ajili ya kuwahifadhi**.** Aidha, Wizara imewajengea uwezo wataalam **26** wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Mikoa ya Iringa (**4**), Singida (**5**), Dodoma (**4**), Shinyanga (**4**), Mara (**4**) na Kagera (**5**) kuhusu uchambuzi wa mbari za mifugo. Pia, wafugaji **148** wamehamasishwa na kushiriki katika uchambuzi wa mbari za mifugo ya asili aina ya Iringa Red, Singida White, Gogo, Sukuma, Tarime na Ankole.

**41.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/2022, jumla ya wahimilishaji **112** (**82** Sekta binafsi na **30** Serikalini) kati ya **871** waliopo nchini walipatiwa mafunzo kuhusu kanuni za uzalianaji kwa njia zisizo za asili (*artificial breeding regulations*) ya Mwaka 2020 na marekebisho yake ya mwaka 2021 katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha. Pia, Mfumo wa Kieletroniki wa Ukusanyaji wa Takwimu za Uhimilishaji na Uchambuzi wa Mifugo umeandaliwa ili kuwezesha uchaguzi wa mifugo bora ya mbegu. Aidha, elimu ya uchaguzi wa mifugo ya mbegu na uhifadhi wa mifugo ya asili imetolewa kwa jamii.

**Biashara ya Mifugo na Mazao Yake**

***Biashara ya Mifugo***

**42.*****Mheshimiwa Spika***, hadi tarehe 30 Aprili, 2022, jumla ya ng'ombe **2,194,937** na mbuzi/Kondoo **1,782,010** wenye thamani ya Shilingi **trilioni 1.5** waliuzwa katika minada mbalimbali hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe **1,843,904;** mbuzi/kondoo **2,081,233** wenye thamani ya Shilingi **trilioni 1.51** waliouzwa katika mwaka 2020/2021**.** Hadi tarehe 30 Aprili, 2022, jumla ya Shilingi **21,890,649,515.91** zilikusanywa kutoka katika minada ya awali, upili na mpakani kama maduhuli ya Serikali ikilinganishwa na jumla ya Shilingi **7,945,676,541.20** zilizokusanywa kutoka katika minada ya awali, upili na mpakani mwaka 2020/2021 kwa kipindi kama hicho. Ongezeko la idadi ya mifugo iliyouzwa minadani limetokana na

mahitaji mbalimbali ikiwemo nyama katika soko la ndani na nje ya nchi pamoja na hamasa ya uvunaji wa mifugo.

***Udhibiti wa Biashara ya Mifugo na Mazao yake***

**43.*Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Serikali imeendelea kujenga na kukarabati minada ya mifugo ili kuboresha mazingira ya biashara ya mifugo. Ukarabati na ujenzi wa minada **18** upo katika hatua mbalimbali ikiwemo mnada wa Pugu (Dar es Salaam), Wasso (Arusha), Kileo (Kilimanjaro), Gendi (Manyara), Meserani (Arusha), Horohoro (Tanga), Ndelema (Handeni), Chamgoi (Pwani), Malampaka (Simiyu), Buhigwe (Kigoma), Igunga na Ipuli (Tabora), Nyamatala (Mwanza), Rukole na Mutukula (Kagera), Kizota (Dodoma), na Magena na Kirumi (Mara). Ujenzi wa mnada wa kisasa wa Buzirayombo (Geita) awamu ya kwanza umekamilika. Pia, Wizara imekamilisha kazi ya kuandaa michoro mfanano ya kibunifu (*Standard Architectural Designs*) itakayotumika kama mwongozo wa ujenzi mpya, ukarabati na uboreshaji miundombinu ya minada ya awali, upili na mipakani pamoja na gharama zake.

**44.*Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kusimamia vituo tisa (**9**) vya utoaji huduma kwa wafanyabiashara wa mifugo na kudhibiti utoroshaji wa mifugo katika maeneo ya Serengeti (Darajani), Handeni (Ndelema), Loliondo (Wasso), Monduli (Makuyuni), Busega (Lamadi), Buhigwe (Mnanila), Misenyi (Kyaka), Makambako (Mtewele) na Momba (Tunduma).

**Kodi, Ada na Tozo Katika Sekta ya Mifugo**

**45. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kibiashara kwa kufanya mapitio katika ada na tozo mbalimbali. Katika mwaka 2021/2022 tozo ya asilimia moja (**1**) ya thamani ya mzigo (FoB Value), tozo ya **Shilingi 100** kwa kilo ya nyama ya ng'ombe na **Shilingi 50** kwa kilo ya nyama ya mbuzi na kondoo

inayouzwa nje ya nchi zimerekebishwa. Kwa sasa, wafanyabiashara wanatozwa Shilingi **110,000** kwa shehena. Maboresho hayo yamewezesha viwanda vinavyochakata nyama nchini kuongeza ushindani katika masoko ya kimataifa na kuongeza mauzo ya nyama nje ya nchi.

**46.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kutathmini kodi, tozo na ada mbalimbali zinazoonekana kuwa kero kwa wazalishaji na wafanyabiashara wa mifugo na mazao yake ili kuzifuta au kuzifanyia marekebisho. Aidha, Wizara imefanya marekebisho ya Kanuni za *The Meat Industry (Import and Export) (Amendment) Regulations, GN. No. 469T/2021*; na *The Animal Diseases (Animal and Animal Products Movement Control) (Amendment) Regulations, GN. No.496 E/ 2021* ili kuleta unafuu katika uzalishaji na biashara ya mifugo na mazao yake.

**Zao la Ngozi**

**47.*Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ubora wa ngozi, katika mwaka 2021/2022 jumla ya Wakaguzi wa ngozi **94** wamepatiwa mafunzo; vitambulisho na nakala ya Sheria ya Biashara ya Ngozi na Kanuni zake katika mikoa **13** ya kimkakati ikilinganishwa na Wakaguzi **60** waliopatiwa mafunzo katika mwaka 2020/2021. Aidha, wachunaji wa ngozi **560** wamejengewa uwezo katika Mikoa ya Iringa (**48**), Singida (**46**), Tabora (**80**), Geita (**35**), Dodoma (**67**), Mbeya (**61**), Mara (**68**), Arusha (**105**), Simiyu (**28**) na Manyara (**22**); na kutoa leseni kwa Wachunaji Ngozi **557**.

**48.*Mheshimiwa Spika***; katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya ngozi inaendelea kusimamia ubora wa ngozi zinazozalishwa hapa nchini na kuhakikisha kuwa ngozi zote zinapangwa katika madaraja kabla ya kuuzwa. Aidha, Wapanga Madaraja ya Ngozi **67** wamepatiwa mafunzo ya uchambuzi na upangaji madaraja kutoka katika mikoa mitano (**5**) ya Singida (**10**), Tabora (**11**), Shinyanga (**9**), Mwanza (**25**)

na Kagera (**12**) ili kuhakikisha kuwa ngozi zote zinapangwa kwa madaraja kabla ya kuuzwa.

**49.*Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na viwanda vya ACE Leather cha Morogoro na Himo Tannery Moshi imefanya tathmini na ufuatiliaji wa upatikanaji ngozi bora katika mikoa nane (**8**) ya Kagera, Morogoro, Kilimanjaro, Geita, Singida, Tabora, Shinyanga na Mwanza. Tathmini hiyo ilibaini kuwa ubora wa ngozi zinazozalishwa katika Machinjio za Kagera, Morogoro, Kilimanjaro na Geita umeongezeka kutoka asilimia **80** hadi **85** kutokana na mafunzo ya uchunaji ngozi na matumizi ya visu maalum vya kuchunia ngozi.

**50.*Mheshimiwa Spika***, viwanda vya kutengeneza bidhaa za ngozi vina uwezo wa kuzalisha jozi **2,855,600** za viatu kwa mwaka (**Kiambatisho Na. 9)**. Aidha, katika mwaka 2021/2022, kiwanda cha *Kilimanjaro International Leather Company Limited* kimeongeza uzalishaji wa bidhaa za ngozi kutoka uzalishaji wa viatu vya kike peke yake na kuanza uzalishaji wa viatu vya kiume, viatu maalum vya usalama katika maeneo ya kazi (*safety boots*) na viatu vya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari. Pia, kiwanda hicho kimeongeza uzalishaji wa viatu vya kawaida kutoka jozi **500** hadi **4,000** kwa siku, buti za jeshi kutoka **150** hadi **400** kwa siku na soli za viatu **4,000** kwa siku. Ongezeko hilo la uzalishaji limetokana na upatikanaji wa ngozi bora na masoko ya bidhaa za ngozi ambapo tayari Tanzania imepata soko jipya la bidhaa za ngozi hususan viatu katika nchi za Congo-DRC na Zambia.

**51.*Mheshimiwa Spika***, vipo viwanda vitano (**5**) vya kusindika ngozi nchini (**Kiambatisho Na. 10**). Aidha, viwanda vya ngozi vya *ACE Leather* na *Himo Tanneries* vinaendelea na usindikaji wa ngozi ambapo kiwanda cha *ACE Leather* kinasindika wastani wa vipande vya ngozi **100** kwa siku na kiwanda cha *Himo Tanneries* kinasindika wastani wa vipande vya ngozi **300** kwa siku.

**Rasilimali za Malisho, Vyakula na Maji kwa Mifugo**

***Malisho, Vyakula na Maji kwa Ajili ya Mifugo***

**52.*Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya imekamilisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo katika maeneo ya Chalinze, Longido na Simanjiro. Aidha, Wizara inaendelea na ujenzi wa malambo manne (**4**) katika maeneo ya Kimambi (Liwale), Matekwe (Nachingwea), Muhanga (Itigi) na Msaginia (Nsimbo) na uchimbaji wa visima virefu vitano (**5)** katika maeneo ya Matanzi (Mkuranga), Muhukulu Lilahi (Songea), Makatapora (Iringa), Lwami (Mwanga) na Kinamwigulu (Maswa).

**53.*Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2021/2022, Wizara imepima na kuweka alama zinazoonekana katika Shamba la Muhukulu Lilahi – Songea lenye ukubwa wa hekta **3,200** ambapo vitalu kumi (**10)** vya malisho vimetengwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imetenga jumla ya hekta **128,894.68** katika vijiji vya mikoa ya Pwani (**9,589.71**), Dodoma (**5,346.7**), Iringa (**8,855.58**), Mbeya (**6,423.40**), Kigoma (**5,559.79**), Njombe (**42,057.35**), Rukwa (**2,131.32**), Kilimanjaro (**19,449.12**), Singida (**6,799.77**), Ruvuma (**1,696.32**) na Lindi (**20,985.62**) na kuwezesha maeneo ya malisho kufikia hekta **3,189,456.94** kutoka hekta **3,060,562.27** mwaka 2020/2021 (**Kiambatisho Na. 11**). Pia, maeneo **22** ya malisho yenye jumla ya hekta **143,754.02** yaliyotengwa katika mikoa ya Arusha (hekta **111,955.89**) na Manyara (hekta **31,798.126**) yamesajiliwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 718 la tarehe 08/10/2021 (**Kiambatisho Na. 12**).

**54.*Mheshimiwa Spika*,** ili kuongeza upatikanaji wa malisho na mbegu za malisho, katika mwaka 2021/2022 Wizara imeendelea kuimarisha mashamba ya uzalishaji wa malisho kwa kuyapatia

mashine na zana muhimu kwenye uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho zikiwa ni pamoja na *Hay bailer (**2**) na Hay rakes (**2**)*. Vilevile, katika mwaka 2021/2022 Mashamba ya Wizara na Taasisi zake yamezalisha mbegu bora za malisho jumla ya kil**o 4,481.9** zikijumuisha kilo **2,570.6** jamii ya nyasi, mikunde kilo **435.6**, miti malisho kilo **25.5** na vipandikizi kilo **1,450.2**. Mbegu hizo zimeuzwa kwa wafugaji wa mikoa ya Kagera, Arusha, Tanga, Dodoma, Dar es Salaam, Manyara, Mbeya, Songwe na Pwani. Aidha, marobota ya hei **51,181** yamezalishwa na kuuzwa kwa wafugaji nchini.

***55.Mheshimiwa Spika*,** uzalishaji wa vyakula vya mifugo umeongezeka kutoka tani **1,200,000** mwaka 2020/2021 hadi tani **1,380,000** mwaka 2021/2022. Ongezeko la uzalishaji huu limetokana na Wizara kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji wa vyakula vya mifugo ambapo viwanda vya watu binafsi vya kuzalisha vyakula vya mifugo vimeongezeka kutoka **154** mwaka 2020/2021 kufikia **199** mwaka 2021/2022 (**Kiambatisho Na. 13**).

***56.Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na kuboresha ubora na usalama wa vyakula vya mifugo, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imetoa mafunzo kuhusu udhibiti wa sumukuvu kwenye rasilimali za vyakula vya Mifugo kwa maafisa ugani **510** wa mifugo na kilimo kutoka Halmashauri za Wilaya 11 za Urambo DC (**30**), Nzega DC (**76**), Nzega TC (**33**), Kibondo DC (**40**), Kasulu DC (**40**), Itilima DC (**50**), Buchosa DC (**51**), Bukombe DC (**71**), Newala DC (**43**), Nanyumbu DC (**36**) na Namtumbo DC (**40**) zinazotekeleza mradi wa kudhibiti sumukuvuTANIPAC. Yapo maeneo **327** ya kuuzia vyakula vya mifugo yanayoendeshwa na sekta binafsi **(Kiambatisho Na. 14)**. Aidha, katika kusimamia na kudhibiti ubora na usalama wa vyakula vya mifugo; mafunzo rejea yametolewa kwa wakaguzi **75** wa vyakula vya mifugo na maeneo ya malisho na kuwezesha kukagua maeneo **198** ya kuzalisha, **321** ya kuuza na **60** ya kuhifadhi rasilimali za vyakula vya Mifugo**.**

**Utatuzi wa Migogoro Kati ya Wafugaji na Watumiaji Wengine wa Ardhi**

***57***. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutatua migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi ili kuwawezesha wafugaji kujikita katika ufugaji bora na wa kisasa. Katika mwaka 2021/2022 mikutano **28** ya utatuzi wa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi imefanyika katika Mikoa ya Katavi (**4**), Rukwa (**4**), Pwani (**3**), Lindi (**10**), Mtwara (**2**), Tanga (**1**) na Songwe (**4**). Kutokana na mikutano hiyo jumla ya migogoro **13** imetatuliwa na mingine ipo katika hatua mbalimbali za utatuzi (**Kiambatisho Na.15**).

**Jitihada za Kuendeleza Eneo la Msomera na Loliondo**

**58.*Mheshimiwa Spika***, kazi ya kutenga maeneo kwa ajili ya matumizi mbalimbali, yakiwemo malisho inaendelea kufanyika katika kijiji cha Msomera kilichopo Wilayani Handeni Mkoani Tanga, ambapo maeneo ya malisho yanaendelea kupimwa na kuwekewa alama na pia kuyagawa katika vitalu. Ukubwa wa eneo lililotengwa kwa ajili ya malisho ya mifugo ni hekta **22,746.94** ambazo zimetengwa na zitapimwa na kuwekewa alama, pamoja na kugawa vitalu ili kurahisisha uendelezaji wake. Pia, inajenga majosho mawili (**2**) mapya na kukarabati moja (**1**) lililokuwa limeharibika.

**59.*Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Loliondo imeanza utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu uhifadhi wa Pori Tengefu la Loliondo. Ujenzi wa josho moja (**1**) umekamilika, ujenzi wa majosho sita (**6**) unaendelea na jumla ya ng'ombe **1,252** wamehimilishwa. Aidha, Wizara imetoa elimu kwa wafugaji juu ya umuhimu wa kubadili mfumo wa ufugaji ili uwe ufugaji wa kisasa, endelevu na wenye tija unaozingatia hifadhi ya mazingira na unaoendana na hitaji la soko la mifugo na mazao ya mifugo; la ndani na nje ya nchi. Pia, elimu ya umuhimu wa kulima malisho, kuhifadhi na kuendeleza maeneo ya malisho ili kuwa na malisho wakati wote wa mwaka ilitolewa. Vilevile, elimu ilitolewa kuhusu kuboresha mifugo kwa njia ya uhimilishaji ili kupata wanyama bora wanaokua

haraka na kutoa mazao ya nyama na maziwa kwa wingi; umuhimu wa kuogesha mifugo; kutumia chanjo mbalimbali kwa ajili ya kukinga wanyama dhidi ya magonjwa; na kutambua mifugo kwa hereni za kielektroniki.

**60.*Mheshimiwa Spika***, uhamasishaji kwa wafugaji Loliondo umefanyika ukishirikisha kaya **228** za wafugaji katika kata za Arashi (**23**)**,** Kirtalo (**112**), Oloipili (**4**), Ololien Magaiduru (**30**), Olosokwan (**43**) na Olgotorock (**16**). Ujenzi wa josho moja (**1**) umekamilika na majosho tisa (**9**) ujenzi unaendelea. Hata hivyo, uhamasishaji katika baadhi ya vijiji vya Digodigo na Malambo ulikwamishwa na mvua zilizosababisha njia isipitike.

**Ustawi wa Wanyama**

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** matukio ya ukamataji na utaifishaji wa mifugo usiofuata utaratibu hususan kwenye maeneo ya hifadhi yamepungua kutoka mifugo **6,245,356** iliyokamatwa mwaka 2020/2021 hadi mifugo **3,343** iliyokamatwa mwaka 2021/2022. Hali hii imetokana na wadau mbalimbali kuelewa Sheria ya Ustawi wa Wanyama SURA 154; na kanuni ya *Animal Welfare (Impounded Animal) Regulation GN No. 724 2020* na Sheria nyingine za nchi.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kupungua kwa idadi ya punda nchini na hatari ya kutoweka kwa kizazi cha punda ambapo kwa sasa idadi ya punda ni takriban **650,000**, katika mwaka 2021/2022 Wizara imesitisha shughuli zote za biashara ya uchinjaji wa punda nchini. Napenda, kutumia fursa hii kuwataarifu wawekezaji waliowekeza katika machinjio za punda nchini watumie miundombinu ya machinjio hizo kwa ajili ya kuchinja na kuchakata aina nyingine za mifugo hususan ng’ombe, mbuzi na kondoo.

***Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo***

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na Sekta binafsi imeendelea kutekeleza Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 19 ya mwaka 2008 kwa kutumia hereni za kielektroniki. Hadi kufikia Aprili 30, 2022, jumla ya mifugo **3,003,237** (Ng'ombe **2,648,498**, Punda **56,345**, Mbuzi **205,978** na Kondoo **92,416**) wametambuliwa na kusajiliwa. Faida za utambuzi na usajili wa mifugo kwa njia ya kielektroniki ni pamoja na:-

(i) Kuwa na takwimu sahihi za mifugo iliyopo nchini;
(ii) Kuwezesha biashara ya mifugo na mazao yake katika masoko ya kikanda na kimataifa;
(iii) Kudhibiti wizi wa mifugo;
(iv) Kuwezesha utambuzi na ufuatiliaji wa magonjwa ya mifugo ya mlipuko;
(v) Kuwezesha utambuzi na uboreshaji wa mbari pamoja na uendelezaji wa kosaafu za mifugo;
(vi) Kuwezesha mifugo kutambulika ilipo na umiliki wake na hivyo kuepusha wafugaji kutoka nje ya nchi kuingiza mifugo yao nchini kiholela na bila kutambuliwa.

**Huduma ya Afya ya Mifugo**

***Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo***

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kudhibiti magonjwa **13** ya kipaumbele (**Kiambatisho Na.16**) ambayo ni kikwazo katika uzalishaji na biashara ya mifugo na mazao yake. Magonjwa hayo yanaathiri wanyama na baadhi ya magonjwa hayo huathiri binadamu. Katika mwaka 2021/2022 Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutekeleza mikakati ya kudhibiti magonjwa ya mifugo yaenezwayo na wadudu ambapo masuala mbalimbali yametekelezwa kama ifuatavyo: -

(i) Jumla ya Halmashauri **162** zimegawiwa dawa za kuogesha mifugo lita **20,710** kwa ajili ya majosho **2,203** ili

kuogesha mifugo kwa bei elekezi ya Shilingi **50** kwa kila ng'ombe na Shilingi **10** kwa kila mbuzi na kondoo;

(ii) Jumla ya majosho **192** yenye thamani ya Shilingi **4,992,000,000.00** yamejengwa katika Mamlaka **85** za Serikali za Mitaa (**Kiambatisho Na. 17**);

(iii) Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022, jumla ya michovyo **474,171,560** (ng'ombe ni **237,085,780** mbuzi **175,443,477** na kondoo **61,642,303**) ya kuogesha mifugo imefanyika sawa na asilimia **79** ya lengo la michovyo **600,000,000** ikilinganishwa na michovyo **446,997,857** iliyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2021; na

(iv) Wizara kupitia Wakala ya Maabara ya Veterinari (TVLA) kwa kushirikiana na wadau imefanya utafiti na kugundua dawa ya kufukuza mbung'o na wadudu wengine (*repellant*) wanaosababisha kuenea kwa magonjwa ya mifugo. Kwa sasa dawa hiyo ipo katika hatua ya kusajiliwa ili ianze kutumika.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea na udhibiti wa magonjwa ya mifugo ya mlipuko kwa: -

(i) Kuchanja jumla ya mbuzi na kondoo **6,930,953** dhidi ya Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR); ng'ombe **11,400,433** dhidi ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP) na ng'ombe **19,992** dhidi ya Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD) katika Halmashauri **11,** ikilinganishwa na jumla ya kondoo na mbuzi **3,280,661** waliochanjwa dhidi ya ugonjwa wa Sotoka ya mbuzi na kondoo, ng'ombe **5,479,270** waliochanjwa dhidi ya Ugonjwa wa homa ya mapafu na **2,518,600** dhidi ya ugonjwa wa miguu na midomo mwaka 2020/2021;

(ii) Jumla ya dozi **201,497,319** zimetumika kuchanja kuku dhidi ya ugonjwa wa mdondo/kideri, kati ya hizo dozi **68,481,856** ni

za matone na dozi **133,015,463** za kuchanganya na maji (Lasota) ikilinganishwa na dozi **57,773,685** zilizotumika kuchanja kuku dhidi ya ugonjwa wa mdondo kati ya hizo dozi **35,474,800** zilikuwa ni za matone na dozi **22,298,885** za kuchanganya na maji (Lasota) mwaka 2020/2021;

(iii) Kiwanda cha *Hester Bioscience Limited* kwa mara ya kwanza kimeanza kuzalisha chanjo za magonjwa mbalimbali ya mifugo ambapo tayari kimezalisha dozi **6,300,000** za chanjo dhidi ya magonjwa ikiwemo Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (**3,000,000**), Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (**600,000**), Ugonjwa wa Mapele Ngozi (**1,500,000**), Mdondo (**600,000**) na Gumboro (**600,000**).

**66.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Shirika la Afya Duniani (WHO), Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau mbalimbali imeendelea kutumia Dhana ya Afya Moja katika kukabiliana na magonjwa ya wanyama yanayoathiri binadamu. Katika mwaka 2021/2022 mafanikio yafuatayo yamepatikana: -

(i) Jumla ya ng'ombe **2,520,471**, mbuzi **792,245** na kondoo **216,075** walichanjwa dhidi ya Ugonjwa wa Kimeta katika mikoa minne (4) ya Arusha, Songwe, Manyara na Kilimanjaro ikilinganishwa na ng'ombe **1,036,769,** mbuzi **680,906** na kondoo **192,906** walichanjwa dhidi ya Ugonjwa wa Kimeta katika mwaka 2020/2021;

(ii) Jumla ya mitamba **214,927** imechanjwa dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba katika Wilaya za Arusha, Karatu, Babati, Dodoma, Simajiro, Iringa na Njombe ikilinganishwa na mitamba **162,843** imechanjwa dhidi ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba mwaka 2020/2021;

(iii) Jumla ya matukio **98** ya Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa yalifuatiliwa katika Mikoa ya Tabora, Iringa, Singida, Dodoma, Rukwa, Arusha, Lindi, Morogoro, Kigoma, Shinyanga na Pwani. Aidha, jumla ya mbwa **1,608,344** na paka **6,833** walichanjwa dhidi ya Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa kupitia kampeni mbalimbali ikiwemo Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani inayoadhimishwa tarehe 28 Septemba kila mwaka ikilinganishwa na mbwa **812,712** na paka **4,152** waliochanjwa dhidi ya kichaa cha mbwa mwaka 2020/2021.

***Kuimarisha Uchunguzi na Upatikanaji wa Taarifa za Magonjwa ya Mifugo***

**67**. ***Mheshimiwa Spika,*** matukio ya magonjwa ya mifugo ya mlipuko yamepungua kutoka **449** katika mwaka 2020/2021 hadi **376** mwaka 2021/2022 sawa na punguzo la asilimia **16**. Aidha, katika mwaka 2021/2022 jumla ya mifugo **501,301** iliripotiwa kuugua ikiwemo ngómbe **458,112,** mbuzi **26,121,** kondoo **16,241** na nguruwe **827 (Kiambatisho Na. 18)** ambapo mifugo **213,503** ilikufa kutokana na magonjwa ikiwemo ngómbe **189,838**, mbuzi **20,511** kondoo **2,579** na nguruwe **575** ikilinganishwa na mifugo **520,901** iliyougua katika mwaka 2020/2021 ikiwemo ng'ombe **472,006** mbuzi **29,456,** kondoo **13,807** na nguruwe **5,632** ambapo mifugo **243,112** ilikufa kutokana na magonjwa.

***Ukaguzi wa Mifugo na Mazao yake na Kulinda Afya ya Jamii***

**68**. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na uratibu wa shughuli za ukaguzi wa mifugo na mazao yake kabla ya matumizi na kusafirisha ndani na nje ya nchi ili kulinda afya ya jamii dhidi ya madhara yanayotokana na magonjwa yanayoambukiza kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu. Katika kufikia azma hiyo katika mwaka 2021/2022 jumla ya ng'ombe **1,703,002,** mbuzi **911,988**, kondoo **266,888** na nguruwe **306,219** walikaguliwa na kuidhinishwa kwa matumizi ya binadamu. Aidha, jumla ng'ombe

**22,843** mbuzi na kondoo **50,643** walikaguliwa na kusafirishwa nje ya nchi. Vilevile, mifugo **2,190** wakiwemo ng'ombe **2,122** na mbuzi na kondoo **68** walikaguliwa na kuingizwa nchini kwa ajili ya mbegu bora.

**Baraza la Veterinari Tanzania**

**69. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania, imefanya ukaguzi wa vituo **840** vya kutolea huduma za afya ya wanyama katika Halmashauri **116**. Aidha, vyuo vitano (**5)** vya mafunzo ya afya na uzalishaji wa wanyama vya CANRE (Dar es Salaam), Chuo cha Mafunzo ya Afya Chato (Geita), LITA Mabuki (Mwanza), Igabiro (Kagera) na TRACDI (Dodoma) vimekaguliwa. Ukaguzi huo umebainisha umuhimu wa kuimarisha mafunzo kwa vitendo ili wahitimu wawe na weledi wa kutosha.

**70.*Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania imesajili madaktari wa wanyama **13** kati ya **70** waliotarajiwa kusajiliwa na kufanya idadi yao kufikia **1,076** kati ya hao wanaume ni **972** na wanawake ni **104**. Idadi ndogo ya madaktari wanaosajiliwa ikilinganishwa na lengo inatokana na kuanza kutekelezwa kwa Kanuni chini ya Sheria ya Veterinari SURA 319 inayowataka wahitimu wa Shahada ya Veterinari kujiunga na mafunzo ya uanagenzi kabla ya kusajiliwa. Aidha, wataalam wasaidizi wa afya ya wanyama **296** wameandikishwa na kuorodheshwa na kufanya idadi yao kufikia **4,637** ambapo kati yao wanaume ni **3,200** na wanawake ni **1,437**. Vile vile, leseni **45** zimetolewa kwa wakaguzi wa nyama, mbili (**2**) kwa wahimilishaji na tano (**5**) kwa wataalam wa maabara na kufanya wakaguzi wa nyama kufikia **902**, wahimilishaji **77** na wataalam wa maabara **70**. Pia, vituo **204** vya kutolea huduma za afya ya wanyama vilisajiliwa na kufanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa kufikia **2,089**.

**71.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Baraza la Veterinari imetoa elimu kwa wahitimu wa udaktari wa wanyama **63** kuhusu umuhimu wa mafunzo ya uanagenzi. Aidha, jumla ya vituo vya mafunzo ya uanagenzi vyenye uwezo wa kupokea wanafunzi wa uanagenzi **73** vimeandaliwa (**Kiambatisho Na.19**). Pia, mitihani ya kuandikishwa imefanyika kwa wahitimu **840** wa stashahada ya afya na uzalishaji wa wanyama.

**Ugani, Utafiti na Mafunzo**

***Huduma za Ugani wa Mifugo***

**72.*Mheshimiwa Spika,*** wapo Maafisa Ugani wa Mifugo **3,642** ikilinganishwa na mahitaji ya Maafisa Ugani **14,025**. Katika mwaka 2021/2022 Wizara imenunua pikipiki **300** na kuzisambaza kwa Maafisa Ugani wa Mifugo katika Mamlaka **141** za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma za ugani kutokana na Maafisa Ugani waliopo kukosa vitendea kazi.

**73.*Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo zinaendelea kuwawezesha Wafugaji na Wavuvi kuwasiliana na Maafisa Ugani kupitia mfumo wa kielektroniki uitwao ***Mobile – Kilimo* (M-Kilimo)** kwa ajili ya kuratibu utoaji wa huduma za ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mfumo huu wa MKilimo umetengeneza dirisha la kidigitali kati ya Wafugaji na Wavuvi kupitia simu zao za mikononi (simu janja au kitochi) na Maafisa Ugani kwa ngazi zote. Aidha, Wizara inaendelea na uboreshaji wa kituo cha pamoja cha kutoa huduma za ugani kwa njia ya mtandao (***call center***) ambapo Wataalam wa Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa wataweza kuwahudumia Wafugaji kwa njia ya kidigitali.

**74.*Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2021/2022, Wizara ilitoa mafunzo kwa wataalam wa Mifugo **277** yaliyowahusisha

Washauri wa Mifugo wa Mikoa **26** na Wakuu wa Idara za Mifugo na Uvuvi kutoka katika Mamlaka **184** za Serikali za Mitaa**.** Lengo la mafunzo hayo ilikuwa ni kuwajengea uwezo wataalam kuwa na uelewa wa pamoja katika utoaji wa huduma za ugani.

**75.*Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa Mashamba Darasa ya Mifugo kwa makundi mbalimbali ya jamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika mwaka 2021/2022, jumla ya wanawake **273** wamepatiwa mafunzo kupitia Mashamba darasa manne (**4**) ya ufugaji bora wa kuku yaliyoanzishwa katika Mikoa ya Pwani na Lindi. Aidha, jumla ya vifaranga **5,500** vimesambazwa kwa vikundi **27** vya wanawake walioshiriki mafunzo hayo.

**76.*Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara imewafikia jumla ya wadau **50,345** wakiwemo **2,560** kwa mafunzo rejea katika baadhi ya kata na vijiji vilivyoko katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa; **44,554** kupitia maonesho ya Kimataifa ya Biashara SabaSaba; na **3,231** katika Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani ambapo walipatiwa elimu kuhusu ufugaji bora, uzalishaji, usindikaji wa mazao yatokanayo na mifugo, hifadhi ya malisho pamoja na upatikanaji wa masoko. Aidha, jumla ya vipeperushi **8,685** na vitabu **429** vya ufugaji bora vilisambazwa kwa wadau.

***Uratibu wa Utafiti na Mafunzo ya Mifugo***

**77.*Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia shughuli za Utafiti wa Mifugo nchini. Katika mwaka 2021/2022, Wizara imefanya tathmini katika Taasisi kumi na moja (**11**) zinazofanya utafiti unaohusiana na Mifugo nchini, ambazo ni Taasisi ya Utafiti wa Mifugo yenye vituo nane (**8**), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, Chuo kikuu cha Dar es Salaam, Chuo kikuu cha Dodoma, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti (IITA), Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini

(IRDP) na Taasisi ya REPOA. Lengo la tathmini hiyo likiwa kubaini tafiti mbalimbali zinazofanyika pamoja na uzingatiwaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na utekelezaji wa Agenda ya Utafiti wa Mifugo nchini ya mwaka 2020-2025.

**78.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara ilizindua Mpango Mkakati wa Uboreshaji wa Kosaafu za Mifugo (*National Strategy Action Plan – NSAP for Animal Genetic Resources*). malengo mahususi ya Mpango Mkakati huu ni:-

(i) Kufanya uchambuzi yakinifu (*characterization*) wa Kosaafu (*Animal Genetic Resources*) pamoja na mifumo ya uzalishaji mifugo nchini;
(ii) Kuwezesha utumiaji endelevu wa Kosaafu kupitia teknolojia za kisasa na za asili;
(iii) Kutengeneza mfumo imara na wa uhakika wa uhifadhi kosaafu za mifugo nchini; na
(iv) Kuimarisha uwezo wa kitaasisi na wadau wanaohusika na uendelezaji mbari (*Varieties*).

**79.*Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara imefanya uratibu na tathmini katika vyuo vya Mafunzo ya Mifugo kumi na mbili (**12**) ikihusisha Wakala ya Mafunzo ya Mifugo LITA na vyuo vya Binafsi kumi na moja (**11**). Lengo likiwa ni uzingatiwaji wa utumiaji wa mitaala ya Wizara, uwiano wa wakufunzi na wanafunzi, miundombinu ya kufundishia na kujifunzia. Tathmini hiyo ilibaini kuwa vyuo hivyo vinazingatia mitaala na miongozo. Aidha, Chuo cha Afya Chato (*Chato College of Health Science and Technology*) kimekaguliwa na kukidhi vigezo hivyo Wizara imekipa idhini ya kutoa mafunzo ya mifugo. Pia, Wizara imewezesha jumla ya wanafunzi **12** kutoka Kampasi za LITA kwenda nchini Israel kwa ajili ya mafunzo ya utarajali (*Internship programme*).

**Taasisi Zilizo Chini ya Sekta ya Mifugo**

***Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)***

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yake mbalimbali, hadi kufikia Aprili 30, 2022, Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) ilikuwa na jumla mifugo kama ifuatavyo :-

**i.** Ng'ombe **23,991**, ikijumuisha ng'ombe **17,046** kutoka 2020/2021, ndama wapya **4,846** waliozalishwa na ng'ombe 2,099 walionunuliwa kutoka kwa wafugaji kwa ajili ya unenepeshaji;
**ii.** Mbuzi **4,446**, ikijumuisha **3,251** kutoka mwaka 2020/2021, **1,195** waliozaliwa na **10** walionunuliwa;
**iii.** Kondoo 4**,740**, ikijumuisha **3,565** kutoka mwaka 2020/2021 na **1,175** waliozaliwa; na
**iv.** Farasi **38** ikijumuisha **33** kutoka mwaka 2020/2021 na **5** waliozaliwa.

**81.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile Kampuni imefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo: -

(i) Eneo lenye vichaka ekari **800** limefyekwa kwa ajili ya kuruhusu ukuaji wa malisho katika Ranchi za Kongwa (ekari **500**), Ruvu (ekari **100**) na West Kilimanjaro (ekari **200**);
(ii) Mabwawa matatu (**3**) ya maji kwa ajili ya mifugo yamekarabatiwa katika Ranchi ya Ruvu;
(iii) Wafugaji **258** wamepatiwa ushauri wa kitaalamu katika vijiji vinavyozunguka Ranchi za NARCO;
(iv) Wanafunzi **295** kutoka katika Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo wamepatiwa mafunzo kwa vitendo; na
(v) Kushiriki kwenye Maonesho mbalimbali ikiwemo maonesho ya Tisa ya Kimataifa ya Kilimo na Mazingira Doha – Qatar, Siku ya Chakula Duniani na Maonesho ya SabaSaba.

**82.** ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kupunguza migogoro baina ya NARCO na vijiji jirani, jumla ya ekari **6,000** zimemegwa katika Ranchi ya Uvinza kwa ajili ya matumizi ya

Wananchi wa vijiji vya Chakulu na Mpeta Wilaya ya Uvinza. Vilevile, NARCO imepima eneo la Ranchi ya Mwisa II kiasi cha hekta **66,215.76** ambapo vitalu **89** vitagawiwa kwa wawekezaji. Aidha, NARCO imetenga eneo lenye hekta **11,772.15** katika Ranchi ya Mwisa II kwa ajili ya kuzigawa katika vijiji vinavyopakana na Ranchi hiyo.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuimarisha uzalishaji na biashara ya nyama na mifugo hai, Mradi wa Mabadiliko ya NARCO (*Transformation Plan for NARCO: TP-NARCO*) umeandaliwa ambao utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2022/2023 hadi 2024/2025.

***Bodi ya Nyama Tanzania***

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Nyama Tanzania (TMB) imeendelea kusimamia na kuendeleza tasnia ya nyama nchini kwa kuwezesha ufanyaji biashara ya nyama, ukaguzi, usajili na kutoa elimu na ushauri kwa wadau katika mnyororo wa thamani wa zao la nyama. Ili kuhakikisha nyama inayoingia sokoni ni bora na salama, wadau **2,563** katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Shinyanga, Mbeya, Mtwara na Mwanza walikaguliwa na kukidhi vigezo vya kufanya biashara. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia **40** ikilinganishwa na wadau **1,826** waliokaguliwa mwaka 2020/2021. Aidha, Bodi imesajili wadau wapya **2,206** wanaofanya shughuli za uzalishaji katika mnyororo wa thamani wa nyama ikilinganishwa na wadau **1,931** waliosajiliwa mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia **14**.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Bodi ya Nyama Tanzania imetoa elimu (SOPs) kwa wadau **8,413** waliopo kwenye mnyororo wa thamani wa uzalishaji nyama katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Shinyanga, Mtwara na Mwanza ikilinganishwa na wadau **2,873** katika mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia **192**. Aidha, vyama **7** vya wadau vya TAMEPA,

TPA, TABROFA, TALIMETA, TAPIFA, TCCS, na TALFA vimejengewa uwezo ili wanapozalisha wakidhi viwango vya soko.

**86.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Bodi ya Nyama, imeendelea kusimamia biashara ya nyama kwenda nje ya nchi. Hadi Tarehe 30 Aprili, 2022 jumla ya tani **8,877.80** za nyama zimeuzwa zikijumuisha tani **1,390.86** ya nyama ya ngómbe, tani **4,997.45** nyama ya mbuzi, tani **1,909.02** nyama ya kondoo, tani **5.7** nyama ya kuku na tani **4.9** nyama ya nguruwe na tani **300** za wanyama wengine zenye thamani ya dola za kimarekani **36,264,786.13.** Ongezeko hili ni sawa na asilimia **400.4** ikilinganishwa na tani **1,774.29** za nyama zenye thamani ya dola za Kimarekani **4,290,000** zilizouzwa katika mwaka 2020/2021.

**87.** ***Mheshimiwa Spika*****,** mafanikio ya mauzo makubwa ya nyama nje ya nchi yametokana na jitihada kubwa za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika kuboresha mazingira ya biashara, kuvutia uwekezaji mpya pamoja na majadiliano mazuri ya kibiashara yaliyosababisha kufunguka kwa masoko kati ya Tanzania na nchi za Hong Kong, Vietnam, Kuwait, Qatar, Umoja wa Falme za Kiarabu (Dubai), Oman, Jordan, Bahrain na Comoro.

**Bodi ya Maziwa Tanzania**

**88.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) imeendelea kusimamia, kuratibu na kuendeleza tasnia ya maziwa nchini. Katika mwaka 2021/2022 jumla ya wafanyabiashara **468** kati ya **533** waliokuwa wamelengwa walikaguliwa katika mikoa ya Mwanza, Dodoma, Shinyanga, Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam ikilinganishwa na wafanyabiashara **238** waliokaguliwa kipindi kama hicho mwaka 2020/2021 ikiwa ni ongezeko la asilimia **96.6**.

**89.** ***Mheshimiwa Spika*,** ili kudhibiti na kuendeleza tasnia ya maziwa nchini, katika kipindi cha mwaka 2021/2022, Bodi ya Maziwa Tanzania ilisajili jumla ya wadau **534** kati ya **567** waliolengwa; kati ya hao wazalishaji (**188**), wasindikaji (**13**), wafanyabiashara (**189**), waingizaji wa maziwa nchini **(52**), wauzaji wa maziwa nje ya nchi (**2**), wasambazaji (**34**), wakusanyaji (**4**) na maghala ya kuhifadhia maziwa (**52**) ikiwa ni ongezeko la asilimia **69.5** ikilinganishwa na wadau **315** wakiwemo wazalishaji (**20**), wasindikaji (**42**), wafanyabiashara (**145**), waingizaji wa maziwa nchini (**34**), wasambazaji (**26**), wakusanyaji (**5**) na maghala ya kuhifadhia maziwa (**42**) waliosajiliwa mwaka 2020/2021.

**90.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2021/2022, idadi ya viwanda vya kusindika maziwa nchini imeongezeka kutoka **99** mwaka 2020/2021 vilivyosindika lita milioni **75.9** hadi viwanda **105** mwaka 2021/2022 vilivyosindika lita milioni **77.6** ikiwa ni ongezeko la asimilia **2.3** (**Kiambatanisho Na. 2**). Aidha, Bodi ya Maziwa Tanzania imetoa vibali **296** vyenye jumla ya lita **5,168,815** zenye thamani ya Shilingi **11,126,526,195** ikiwa ni pungufu ya asilimia **3.15** ikilinganishwa na vibali **308** vyenye jumla ya lita **5,336,955** zenye thamani ya Shilingi **12,052,434,896** vilivyotolewa mwaka 2020/2021. Kiasi kikubwa cha maziwa haya yanatoka katika nchi za Afrika Kusini; Uganda; Kenya; Falme za Kiarabu; Uholanzi; na Ireland. Kupungua kwa kiasi cha maziwa kinachoingizwa nchini kimetokana na kuongezeka kwa uzalishaji na ukusanywaji wa maziwa na kuendelea kuimarika kwa viwanda vya ndani katika usindikaji wa bidhaa za maziwa.

**91.** ***Mheshimiwa Spika*,** elimu kuhusu Sheria ya Tasnia ya Maziwa SURA **262** na Kanuni zake ilitolewa kwa wadau wa tasnia ya maziwa. Aidha, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2021 hadi Aprili 30, 2022, Bodi ilitoa mafunzo kwa wadau **1,050** kati ya wadau **1,336** waliolengwa wakiwemo wafugaji (**788**), wasafirishaji (**75**), wasindikaji (**35**), wauza maziwa (**100**) na wasimamizi wa vituo vya kukusanyia maziwa (**52**) kutoka mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro, Mbeya Kilimanjaro, Pwani na Tanga; ikiwa ni

ongezeko la asilimia **438.4** ikilinganishwa na wadau **195** waliopatiwa mafunzo kipindi kama hicho mwaka 2020/2021.

**92.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Bodi ya Maziwa Tanzania imeendelea na uratibu wa mpango wa unywaji maziwa kwa watumishi wa umma kwa kuanza na vituo **10** vya ofisi za Serikali ambazo ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Kilimo, Wizara ya Fedha na Mipango; Bodi ya Maziwa, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; na Wizara ya Afya ambapo hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 jumla ya lita **11,972** za maziwa zimeuzwa. Nitoe wito kwa viongozi wote wa ofisi za Serikali kuunga mkono juhudi za Bodi ya Maziwa kwa kutumia maziwa yanayozalishwa na viwanda vya ndani ya nchi ili kukuza soko la ndani la maziwa.

**93.** ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Maziwa Tanzania imeshiriki katika uhamasishaji na maonesho mbalimbali ili kuhamasisha unywaji wa maziwa kupitia maonyesho ya Sabasaba na Siku ya Chakula Duniani, pamoja na kampeni za unywaji wa maziwa shuleni. Aidha, Bodi iliratibu na kusimamia maadhimisho ya Wiki ya Unywaji Maziwa Shuleni ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Mbeya, mwezi Septemba, 2021. Vilevile, jumla ya lita za maziwa **5,096.8** ziligawiwa kwa wanafunzi **3,000** walioshiriki maadhimisho hayo.

**94.** ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Maziwa Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya maziwa inaendelea na majaribio ya Mpango wa Unywaji Maziwa Shuleni kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini. Kupitia Mpango huo, jumla ya shule za msingi **39** zenye wanafunzi **13,701** zimeshirikishwa katika mikoa ya Arusha (shule **3** wanafunzi **1,520)**, Kilimanjaro (shule **24** wanafunzi **8,276**), Iringa (shule **8** wanafunzi **930**) na Mbeya (shule **4** wanafunzi **2,975**).

**Wakala ya Maabara ya Veterinari**

***95.Mheshimiwa Spika***, Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA) ina jukumu la kuzalisha chanjo za magonjwa ya mifugo, uchunguzi wa magonjwa ya mifugo, ubora wa rasilimali za vyakula vya mifugo na uchunguzi wa viuatilifu vya mifugo. Katika mwaka 2021/2022 TVLA imetekeleza yafuatayo: -

(i) Hadi Tarehe 30 Aprili, 2022jumla ya dozi **50,640,250** za aina saba (7) za chanjo za magonjwa ya kipaumbele zimezalishwa na kusambazwa nchini ikijumuisha dozi **48,770,350** za chanjo dhidi ya Ugonjwa wa Mdondo (TEMEVAC I-2); dozi **501,800** Ugonjwa wa Kimeta; dozi **84,700**
Ugonjwa wa Chambavu; dozi **985,600** Ugonjwa wa Mapafu ya Ng'ombe; dozi **3,800** Kutupa Mimba; dozi **328,100** za muunganiko wa Kimeta na Chambavu (TECOBLAX) na **65,900** za Ugonjwa wa Mapafu ya Mbuzi, ikilinganishwa na dozi **48,883,825** za chanjo zilizozalishwa kipindi hicho mwaka 2020/2021.

(ii) Jumla ya sampuli **17,123** za wanyama zimefanyiwa uchunguzi ambapo magonjwa ya Mdondo, Mafua ya Kuku, Ndigana Kali, Ndigana Baridi, Kutupa Mimba na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo yaligundulika. Vile vile, jumla ya sampuli **1,213** za vyakula vya mifugo zilifanyiwa uchambuzi na kubainika kuwa baadhi ya sampuli hizo zilikuwa na upungufu wa viini lishe, Madini na protini. Ushauri wa kitaalamu ulitolewa kwa wafugaji na wazalishaji wa vyakula hivyo ili kudhibiti magonjwa na kuzingatia viwango vya ubora wa vyakula vya mifugo.

(iii) Ujenzi wa jengo jipya kwa ajili ya utengenezaji wa chanjo za magonjwa yanayosababishwa na bakteria katika Taasisi ya Chanjo Kibaha umekamilika. Aidha, vifaa vya maabara vimenunuliwa vikiwemo *automated vaccine*

*filling and labeling machine*, *Biosafety Cabinets* (**5**), *Immuno fluoresence Microscope*, gari lenye mfumo baridi (**1**) na *Autoclave Machine*.

(iv) Ujenzi wa jengo jipya la maabara kwenye kituo cha Iringa upo katika hatua ya umaliziaji (**80%**). Jengo hilo litawezesha kuboresha utoaji wa huduma za kimaabara katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

**96.*Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kudhibiti magonjwa ya kipaumbele TVLA imekuwa ikifanya tafiti za uzalishaji wa chanjo za magonjwa ya mifugo. Katika mwaka 2021/2022 uzalishaji wa chanjo mpya ya Homa ya Mapafu ya Mbuzi (CCPP) uliosubiriwa kwa hamu umeanza na hivyo kufanya chanjo zinazozalishwa na Taasisi ya Chanjo Tanzania kuongezeka kutoka sita (**6**) na kufikia saba (**7**). Ugunduzi wa chanjo hiyo utakuwa mkombozi kwa wafugaji wa mbuzi ambao wamekuwa wakipoteza mifugo yao kutokana na vifo vinavyosababishwa na Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Mbuzi. Hadi tarehe 30 Aprili, 2022tayari dozi **87,750** zimezalishwa na mbuzi **865,518** wameshachanjwa dhidi ya ugonjwa huo.

**97.*Mheshimiwa Spika*,** ili kuwa na chanjo za kutosha za magonjwa ya mifugo kulingana na mahitaji nchini, Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya kuzalisha chanjo za magonjwa ya mifugo. Katika mwaka 2021/2022 ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuzalisha chanjo za mifugo cha *Hester Biosciences Africa Limited* cha Kibaha umekamilika na kimeanza uzalishaji wa chanjo za mifugo dhidi ya magonjwa ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe, Mapele Ngozi, Mdondo, Gumboro na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo ambapo hadi tarehe 30 Aprili, 2022 jumla ya dozi **6,300,000** zimezalishwa. Vilevile, Kampuni ya NOVABI imezalisha dozi **15,000,000** za chanjo aina ya TATU MOJA kwa ajili ya udhibiti wa magonjwa ya Mdondo, Ndui na Mafua ya Kuku.

**Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)**

**98.*Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) ina majukumu ya kufanya tafiti za mifugo na malisho ili kuibua teknolojia bora za kuongeza uzalishaji na tija**.** Katika mwaka 2021/2022, Taasisi imezalisha ng'ombe bora wa maziwa na nyama (*dual purpose*) **217** na mbuzi bora **131** ambao wamesambazwa kwa wafugaji kwa ajili ya mbegu katika maeneo ya Ifakara, Bahi, Dodoma Jiji, Tanga, Mbeya, Mtwara, Lindi, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Morogoro, Kilindi, Nyamagana, Pwani na Mpwapwa. Aidha, katika utafiti wa kuboresha mbari za kuku wa asili, jumla ya mayai **648** ya kuku aina ya Horasi yaliyorutubishwa yalisambazwa kwa wafugaji wa kuku katika Wilaya ya Mpwapwa kwa lengo la kuongeza tija ya uzalishaji wa kuku wa asili.

**99.*Mheshimiwa Spika,*** Katika kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa malisho kwa wafugaji, Wizara kupitia TALIRI ilifanya utafiti na kuzalisha mbegu bora za malisho ya nyasi aina tatu (**3**) za *Cenchrus ciliaris, Brachiaria (Cobra, Mulato II, Cayman, Xaeres, Piata* na *Basilisk) na Napier (*Kakamega I, Kakamega II, Ouma, Juncao na Asili*)*; na aina moja (**1**) ya mikunde ambayo ni *Canavalia Ensiformis*. Aidha, Taasisi ilizalisha kilo **2,200** za mbegu bora za malisho na vipandikizi vya malisho kilo **762** aina ya nyasi. Vilevile, TALIRI ilizalisha kilo **200** za mbegu za malisho aina za mikunde. Mbegu hizo zilisambazwa kwa wafugaji wa Tanga, Dodoma, Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Songwe na Pwani. Aidha, TALIRI ilizalisha na kusambaza marobota ya malisho makavu **17,756** marobota hayo yalisambazwa katika maeneo ya Tanga, Dodoma, Dar es Salaam, Mbeya, Songwe, Kongwa na Pwani.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, jitihada za kuimarisha vituo saba vya utafiti wa mifugo vilivyopo chini ya TALIRI ziliendelea ambapo Taasisi iliwezeshwa kununua magari mawili (**2**) na vifaa kwa ajili ya utafiti na uzalishaji wa malisho ikiwemo mashine tatu (**3**) za kukata majani (*mowers*), mashine tatu (**3**) za kufunga majani (*bailers*), mashine moja (**1**) ya

kukatakata malisho (*forage chopper*) na mashine moja (**1**) ya kukusanya majani wakati wa kuyafunga kwa ajili ya kuhifadhi (*hay rake*). Vifaa hivyo vitawezesha utafiti wa malisho katika vituo vya Kongwa, Mpwapwa, Tanga na Uyole.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** TALIRI kwa kushirikiana na ILRI na Kampuni ya kuzalisha vifaranga ya AKM-Glitters inaendelea na mradi wa kuwawezesha Wanawake na Vijana kujikwamua kiuchumi na kuboresha hali ya lishe katika kaya. Kupitia mradi huo jumla ya vifaranga **16,076** aina ya Kuroiler vilisambazwa kwa wafugaji katika vikundi **54** katika Halmashauri nne za Siha, Hai, Ruangwa na Mtama. Pia, TALIRI kwa kushirikiana na ILRI kupitia utafiti wa uboreshaji mbari za ng'ombe wa maziwa (*African Dairy Genetics GainsADGG)* imetoa mafunzo kwa wafugaji **16,327** wa ng'ombe wa maziwa nchini katika Halmashauri **24** za Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe. Vilevile, utambuzi wa vinasaba vya maziwa kwenye ng'ombe wa maziwa umefanyika kwenye ng'ombe **1,735** ambapo matokeo ya utafiti huu yatasaidia upatikanaji wa ng'ombe bora wa maziwa nchini.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** 2021/2022, TALIRI kwa kushirikiana na *PASS Trust* imeendelea kukisimamia Kituo Atamizi kwa ajili ya kuhimiza ujasiriamali kwa wafugaji vijana (*Incubation centre*) cha Kongwa ambapo jumla ya vijana **20** wamepatiwa mafunzo ya unenepeshaji mbuzi kibiashara kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Njombe, Geita, Morogoro, Simiyu, Mtwara, Pwani na Kigoma. Kupitia kituo hicho, jumla ya mbuzi **700** walinunuliwa na kunenepeshwa. Aidha, kituo kinakamilisha ujenzi wa miundombinu ya machinjio, mabucha na vioski vya nyama choma kwa ajili walaji.

**Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA)**

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA) imedahili jumla ya wanafunzi **3,972** katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ikilinganishwa na wanafunzi **3,592** waliodahiliwa katika mwaka 2020/2021. Idadi hii ni ongezeko la wanafunzi **380**, sawa na asilimia **10.6.** Aidha, idadi ya wanachuo wanaotarajiwa kuhitimu katika mwaka wa masomo 2021/2022 kutoka katika Kampasi za LITA ni **1,167** ikilinganishwa na wanafunzi **922** waliohitimu katika mwaka wa masomo 2020/2021. Idadi ya wahitimu ni ongezeko la wanafunzi **245,** sawa na **asilimia 27**. Ongezeko hilo limesaidia kuongeza wataalam wa mifugo nchini watakaochangia maendeleo ya mifugo.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuvitambua na kuviratibu vyuo vya binafsi vilivyosajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) vinavyotoa Mafunzo ya Mifugo kwa kutumia Mitaala ya Wizara. Vyuo hivyo vimeongezeka kutoka tisa (**9**) mwaka 2020/2021 hadi **11.** Vyuo hivyo ni pamoja na Visele, Kilacha, Hagafilo, CANRE, Kaole Wazazi, Igabiro, Karuco, Dabaga, TRACDI, Mahinya na Chuo cha Sayansi ya Afya na Teknolojia Chato. Aidha, vyuo hivyo vimedahili wanafunzi **905** mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na wanafunzi **870** waliodahiliwa mwaka 2020/2021. Idadi hii ni ongezeko la wanafunzi **35**, sawa na asilimia **4.**

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** 2021/2022, Wizara imeendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na ujenzi wa hosteli mbili (**2**) zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **208** kila moja katika kampasi za Morogoro na Mpwapwa; na ujenzi wa kumbi mbili (**2**) za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **240** kila moja katika kampasi ya Tengeru. Aidha, majengo ya utawala, madarasa na mabweni yamekarabatiwa katika Kampasi za Madaba, Mabuki na Buhuri. Pia, vifaa mbalimbali

vya maabara vimenunuliwa ikiwemo darubini **92** na stuli maalum za maabara **184** kwa ajili ya kuwezesha mafunzo kwa vitendo.

**106**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia LITA imewezesha mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji **17,350,** Wataalam wa Mifugo wa Jamii (WAMIJA) **38** na wasindikaji wadogo wa maziwa **25** kupitia utekelezaji wa mpango wa utoaji mafunzo ya muda mfupi kwa wafugaji nchini ukilinganisha na wafugaji **2,078** waliopatiwa mafunzo kama hayo katika mwaka wa fedha 2020/2021. Ongezeko hilo limetokana na utaratibu mpya wa kuanza kuwashirikisha wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa masomo badala ya mwaka wa pili pekee katika mafunzo kwa vitendo. Aidha, kaya **558** za wafugaji zilifikiwa na kupatiwa mafunzo ya nadharia na vitendo kupitia Programu ya Ujirani Mwema (*Outreach Programme***)**. Ili kurahisisha mawasiliano na utoaji wa mafunzo kwa wanafunzi na wakufunzi LITA imeanzisha maktaba mtandao (***e – library***) katika Kampasi za Morogoro, Tengeru na Mpwapwa.

## MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2022 /2023

### Sera, Sheria na Kanuni Katika Sekta ya Mifugo

**107.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(Agriculture Sector Development Programme – ASDP II).* Ili kuongeza tija na kufanya sekta ya mifugo iwe ya kibiashara na hatimaye kuweza kuongeza kipato kwa wananchi na kutoa mchango mkubwa katika Pato la Taifa, Wizara itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006. Pia, Wizara itafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa malengo ya Wizara pamoja na miradi ya mifugo, Wakala, Bodi na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** 2022/2023, Wizara itaendelea kuratibu na kuboresha Sheria zinazosimamia sekta ya mifugo ikiwemo Sheria ya Magonjwa ya Wanyama SURA 156 na Sheria ya Biashara ya Ngozi SURA 120. Pia, Wizara itafanya mapitio ya kanuni mbalimbali ili kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa sekta ya mifugo nchini.

**Huduma ya Uhimilishaji**

**109**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji kwa kuwezesha uzalishaji wa Hewa Baridi ya Naitrojeni ya kutosha kuwezesha huduma ya uhimilishaji. Aidha, kutokana na kuwa na mtambo mpya, Wizara kupitia NAIC itazalisha mbegu dozi **1,500,000;** na kuhimilisha ng'ombe **500,000**.

**Uzalishaji na Usambazaji wa Mitamba**

**110**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia mashamba matano (**5**) ya Serikali imepanga kuzalisha mitamba **3,500** na kuisambaza kwa wafugaji; kuimarisha mashamba mawili (**2**) ya kuzalisha mitamba ya Sao Hill na Mabuki kwa kuyapatia ng'ombe wazazi na vitendea kazi ikiwemo matrekta na vifaa vya kuvuna malisho.

**Uzalishaji wa Nguruwe**

**111**. ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kushirikiana na *Tanzania Association of Pig Farmers* (TAPIFA) kuhimilisha nguruwe **600** na kuzalisha nyama ya nguruwe tani **46,000.**

**Haki Miliki za Waboreshaji Mbari za Wanyama**

**112**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itandaa mkakati wa kuanzisha hifadhi ya kosaafu za mifugo na kusimamia utoaji huduma ya uhimilishaji mifugo.

**Biashara ya Mifugo na Mazao Yake**

**113**. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara inatarajia kujenga minada mitano (**5**) ya Mifugo ya Upili katika maeneo ya Msomera (Handeni), Mkongeni (Morogoro), Lugodaludali (Iringa), Majimoto (Katavi), na Utengule (Mbeya); pamoja na mnada mmoja (**1**) wa Mifugo wa mpakani katika wilaya ya Rorya (Mara), ili kuimarisha biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi na kuimarisha vituo vya doria vya kimkakati.

**Kodi, Ada na Tozo Katika Sekta ya Mifugo**

**114**. ***Mheshimiwa Spika,*** 2022/2023, Wizara itafanya marekebisho ya kanuni ya *Meat Industry (location, design, construction and operation of livestock markets) (Amendment) Regulation, 2022; na The Animal Diseases (Animal and Animal Products Movement Control) (Amendment) Regulations, 2022*. Maboresho hayo yatawasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango wakati akiwasilisha Muswada wa Sheria ya Fedha (*Finance Bill*) ya mwaka 2022/2023 ili kuboresha mazingira na kuchochea biashara ya mifugo na mazao yake.

**Zao la Ngozi**

**115**. ***Mheshimiwa Spika*;** katika mwaka 2022/2023, Wizara itatoa mafunzo kwa Wachunaji (**350**), Wakaguzi (**70**), na Wapanga Madaraja ya Ngozi (**40**) ili kuendeleza jitihada za kuboresha zao la ngozi. Aidha mauzo

ya ngozi yatafanyika kwa kutumia mfumo wa kielektroniki kwa lengo la kuboresha biashara ya ngozi. Pia mfumo huu ambao upo katika hatua za awali za utekelezaji utaleta tija katika soko la ngozi kwa kuwezesha kupatikana kwa bei shindani kulingana na daraja la ngozi. Mfumo huu pia utawezesha upatikanaji wa taarifa za soko la ngozi zikiwemo bei kwa kila daraja la ngozi na wanunuzi wa ngozi, na hivyo kupunguza tatizo la kutupa ngozi kwa kukosa wateja. Kwa upande mwingine mfumo utawezesha upatikanaji wa malighafi ya uhakika na yenye ubora kwa viwanda. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa ngozi itaendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Biashara ya Ngozi Na. 18 ya mwaka 2008 na Kanuni zake za mwaka 2010 ili kuendeleza tasnia ya ngozi.

**Raslimali za Malisho, Vyakula na Maji kwa Ajili ya Mifugo**

**116**. ***Mheshimiwa Spika;*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itajenga na kukarabati malambo/mabwawa manne (**4**) kwenye maeneo yaliyoathirika zaidi na ukame; kuimarisha mashamba ya Serikali yanayozalisha mbegu za malisho na malisho ya Vikuge, Langwira, TALIRI, LITA na NARCO kwa kuyapatia vitendea kazi vikiwemo matrekta nane (**8**), *mower* saba (7), *bailer* saba (7), *hay rake* **sita (**6); na kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutenga maeneo ya malisho yenye ukubwa wa hekta **1,000,000** Aidha, Wizara itaendelea kuwahamasisha wawekezaji katika ujenzi wa viwanda vya kusindika vyakula vya mifugo kuzalisha tani **1,580,000** za vyakula vya mifugo na kuzalishaji kilo 5,281 za mbegu za malisho na marobota **60,000** ya hei.

**Ustawi wa Wanyama**

**117**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kutoa elimu ya ustawi wa wanyama kwa wadau **4,000** hususan kuzingatia Sheria ya Ustawi wa Wanyama SURA 154 na kanuni zake.

**Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo**

**118**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kutambua na kusajili mifugo kwenye mfumo wa kielektroniki ili kusajili takriban mifugo **45,000,000** (ng'ombe, mbuzi, kondoo na punda) iliyopo nchini ifikapo Juni, 2023.

**Migogoro Kati ya Wafugaji na Watumiaji wengine wa Ardhi**

**119**. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kwa kushirikiana na Wizara zenye dhamana ya Ardhi, Kilimo, Maji, Maliasili, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wadau wengine itaendelea kutatua migogoro ya ardhi kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

**Uendelezaji wa Maeneo ya Msomera na Loliondo**

**120. *Mheshimiwa Spika,*** katika kutimiza azma ya kuendeleza maeneo ya malisho yaliyotengwa, Wizara katika bajeti ya mwaka 2022/2023 imepanga kuendeleza maeneo hayo kwa kutoa elimu kwa wafugaji juu ya kufyeka vichaka, kupanda malisho na kuanzisha mashamba darasa yenye ukubwa wa ekari kumi (**10**) kwa kila kitalu. Lengo ni kuhamasisha na kuwashirikisha wafugaji kufuga kisasa ili eneo hilo kuwa kitovu cha mfano katika ufugaji wenye tija zaidi. Pia, Wizara inatarajia kujenga bwawa moja (**1**) la kunyweshea Mifugo; kujenga majosho manne (**4**); kujenga kituo cha kukusanyia maziwa kimoja (**1**); kujenga Kliniki ya Mifugo moja (**1**) katika kijiji cha msomera; kutoa elimu ya ufugaji wenye tija; na kuboresha koosafu za mifugo kwa kuhimilisha ng'ombe **6,000** na kutumia madume bora.

**121. *Mheshimiwa*** *Spika*, katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kushirikiana na Halimashauri ya Loliondo kuanzisha na kuimarisha mashamba darasa ya malisho ekari **22** katika vijiji vinne (**4**) kila shamba ekari zisizopungua

tano (**5**) kwa ajili ya kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu uzalishaji wa malisho na mbegu za malisho ili Mbegu zitakazozalishwa zitumike kuboresha maeneo yaliyotengwa kwa malisho na kuendeleza kilimo cha malisho na uzalishaji wa mbegu za malisho. Aidha, Wizara itahimilisha ng'ombe **4,000** kwa ajili ya kuboresha kosaafu za mifugo ili kuongeza uzalishaji wa mifugo na mazao ya mifugo kwa ajili ya kuongeza kipato cha mfugaji na Taifa kwa ujumla. Pia Wizara itajenga bwawa moja (**1**) la kunyweshea Mifugo.

**Huduma ya Afya ya Mifugo**

**122.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara itawezesha usambazaji wa dozi **100,000,000** za chanjo za magonjwa **13** ya kipaumbele; kuchanja mifugo **80,000,000** dhidi ya magonjwa mbalimbali; kununua dawa za kuogeshea mifugo lita **22,000;** kujenga majosho **104;** na kuongeza uogeshaji wa mifugo kutoka lengo la michovyo **milioni 600** hadi michovyo **milioni 1,200** kwa mwaka.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa taarifa za magonjwa **13** ya mifugo ya kipaumbele na kutoa taarifa kwa wakati ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa hayo.

**Ukaguzi wa Mifugo na Mazao Yake**

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara kupitia minada, machinjio, vituo vya ukaguzi ndani ya nchi na mipakani (*Zoo-sanitary Inspection Border Posts*), itaendelea na ukaguzi wa mifugo na mazao mbalimbali ya mifugo ili kulinda afya ya jamii. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara inatazamia kuratibu uchinjaji na ukaguzi wa ng'ombe wapatao **1,800,000**, mbuzi **1,000,000**, kondoo **300,000** na nguruwe **350,000**.

**125.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara pia itaratibu ukaguzi wa mifugo na mazao mbalimbali ya wanyama ambapo ng'ombe wapatao **18,000**, mbuzi na kondoo **30,000** watakaguliwa na kusafirishwa nje ya nchi. Vilevile, ng'ombe wapatao **2,000**, mbuzi na kondoo **68** watakaguliwa na kuingizwa nchini. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na mazao mengine ya mifugo, Wizara inatazamia kufanya ukaguzi wa nyama ya ng'ombe tani **12,000**, nyama ya mbuzi na kondoo tani **9,000** kabla ya kusafirishwa nje ya nchi. Vile vile, kiasi cha nyama ya ng'ombe tani **200** zitakaguliwa na kuruhusiwa kuingizwa nchini.

**Baraza la Veterinari Tanzania**

**126**. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania itafanya ukaguzi wa vituo **2,175** vya huduma ya afya ya wanyama; maadili ya watoa huduma; kukagua vyuo **20** vinavyotoa na vinavyotaka kutoa mafunzo ya afya na uzalishaji wa mifugo; kusajili Madaktari **70** wa Wanyama; kuandikisha na kuorodhesha wataalam wasaidizi **3,000**; kutoa leseni **500** kwa wakaguzi wa nyama, wahimilishaji na wataalam wa maabara za veterinari; na kusajili vituo **1,000** vya kutolea huduma ya afya ya wanyama katika Mamlaka **184** za Serikali za Mitaa. Pia, Baraza litaendesha mitihani ya kuandikishwa kwa wahitimu **3,000** wa stashahada ya afya na uzalishaji wa mifugo.

**Ugani, Mafunzo na Utafiti**

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu Kampasi **8** za LITA na vyuo binafsi **11** vinavyotoa Mafunzo ya Mifugo ili kudhibiti ubora wa elimu inayotolewa katika vyuo hivyo. Aidha, Wizara itafanya kampeni ya uelimishaji kwa wafugaji ili kubadilisha mifumo ya ufugaji kuelekea katika ufugaji wa

kibiashara na wenye tija, Kampeni hii itafanywa na vyuo vya LITA na Maafisa Ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Pia, Wizara itaendelea kuratibu vituo saba (**7**) vya TALIRI na Taasisi kumi (**10**) zinazofanya tafiti za mifugo nchini. Lengo ni kuwa na tafiti zinazotatua changamoto za sekta ya mifugo kwa kuzingatia sheria na kanuni za utafiti kwa utekelezaji wa Agenda ya Utafiti wa Mifugo ya mwaka 2020 - 2025.

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kuboresha huduma za ugani kwa kununua pikipiki **1,000** na kuzisambaza kwa Maafisa Ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuwasajili Maafisa Ugani **3,000** na Wafugaji **1,000,000** katika Mfumo wa MKilimo; na kufanya mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani **300** wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Wizara itaanzisha mashamba darasa **30** ya mifugo.

**Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)**

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za Serikali kuchagiza maendeleo ya ufugaji wa kibiashara na wenye tija, Kampuni ya Ranchi za Taifa inakusudia kuvutia uwekezaji na kukodisha vitalu vitano **(5)** vyenye ukubwa wa takriban hekta **32,500** katika ranchi za Ruvu hekta **8,000**; Mwisa II hekta **21,000**; na Mzeri hekta **3,500** kwa wawekezaji mahiri kutoka ndani na nje ya Tanzania. Vitalu hivi vitatangazwa kwenye vyombo vya habari na Mfumo wa Ununuzi wa Umma (TANEPS). Wawekezaji watakaopewa kipaumbele ni wale watakaothibitika kuwa na mipango mahususi ya biashara (business plans) inayolenga kufuga mbegu bora za mifugo kwa ajili ya uzalishaji wa nyama na maziwa; uendelezaji wa nyanda za malisho ikiwemo kuzalisha mbegu bora za malisho; kuwapatia wafugaji wadogo nje ya ranchi soko la bidhaa zao ikiwa ni pamoja na kuwapatia mbegu bora za mifugo; kuleta teknolojia mpya katika ufugaji vikiwemo viwanda vya uchakataji mazao ya mifugo pamoja na kujali na kutunza mazingira.

**130.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Kampuni ya NARCO itaendelea kuongeza uzalishaji wa ng'ombe bora wa nyama kwa ajili ya soko la ndani na nje kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuzalisha ng'ombe bora **5,765**; kondoo **1,609**; na mbuzi **1,754**;

(ii) Kununua ng'ombe **13,683** wenye thamani ya **Shilingi bilioni 8.29** kwa ajili ya kunenepesha na kisha kuuzwa kwenye maduka ya nyama ya NARCO;

(iii) Kuuza jumla ya ng'ombe **16,009** ambapo kati ya hao ng'ombe **1,326** ni wazaliwa wa ranchi na kupata mapato ya Shilingi **bilioni 12.81**;

(iv) Kufyeka vichaka ekari **2,600**, kupima na kuweka alama za mipaka zinazoonekana katika ranchi **12** za Kagoma, Mabale, Kitengule, Kikulula, Missenyi, Kongwa, Mzeri, West Kilimanjaro, Kalambo, Usangu, Mkata na Dakawa;

(v) Kujenga mabwawa manne (**4**) katika ranchi za Kongwa, Ruvu, Mkata na Kalambo pamoja na kisima kirefu kimoja (**1**) katika ranchi ya Ruvu;

(vi) Kufanya Upelembaji na Ufuatiliaji (M&E) wa shughuli za uwekezaji katika vitalu **329** katika ranchi za NARCO;

(vii) Kuanzisha maduka manne (**4**) ya kisasa ya nyama katika mikoa ya Dar es salaam, Kilimanjaro, Arusha na Dodoma; na

(viii) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji **266** katika vijiji vinavyozunguka ranchi za NARCO na mafunzo kwa vitendo kwa wanachuo **300** kutoka katika Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo.

**Bodi ya Nyama Tanzania**

**131**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Bodi ya Nyama Tanzania itaendelea kuendeleza tasnia ya nyama kwa kuhamasisha uzalishaji, biashara na ulaji wa nyama bora na kusimamia tasnia ya nyama kwa kufanya ukaguzi wa maduka ya nyama **2,469**, machinjio **185** na viwanda vya kuchakata na kusindika nyama **31** na minada **254** kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo. Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na kutafuta masoko mapya ya nyama kwa lengo la kuwezesha mauzo ya nyama nje ya nchi kiasi cha tani **10,000** ili kuongeza mchango wa tasnia ya nyama kwenye pato la Taifa uendelee kukua.

**Bodi ya Maziwa Tanzania**

**132**. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Bodi ya Maziwa Tanzania itajenga vituo vya kukusanyia maziwa vinne (**4),** kuendelea kuratibu biashara ya maziwa, kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Unywaji Maziwa Shuleni katika shule **52** zenye wanafunzi **25,000**; pia, Bodi itaongeza maeneo ya kuuzia maziwa katika Ofisi za Serikali kutoka ofisi **10** hadi **20;** kufanya ukaguzi kwa wadau **1,200** kwenye maeneo ya mipakani, bandarini na viwanja vya ndege; kuwajengea uwezo wakaguzi wa maziwa wa Halmashauri **184**; kuwajengea uwezo wadau **400** wa maziwa; na kufanya usajili kwa wadau wapya **800**.

**Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania**

**133**. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Taasisi ya Chanjo Tanzania (TVI) itazalisha jumla ya dozi milioni **72.1** za chanjo za magonjwa saba (**7**); kukamilisha utengenezaji na uzalishaji wa chanjo ya Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR); kuendelea na utafiti wa utengenezaji wa chanjo ya Kichaa cha Mbwa; kununua vifaa vya maabara; na kununua

magari matatu (**3**) yenye mfumo baridi kwa ajili ya kusambazia chanjo.

**Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI)**

**134. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/2023, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania itaendelea kutekeleza tafiti **15** za mifugo na tatu (**3**) za malisho na kurasimisha aina tatu (**3**) za mbegu bora za malisho. Katika tafiti hizo TALIRI itaendelea na tafiti ya uhimilishaji wa mbuzi. Pia, TALIRI itaendelea kuimarisha ushirikiano wake na wadau wa utafiti ili kutekeleza kazi mbalimbali zinazohusu uzalishaji na uendelezaji wa teknolojia bora za uzalishaji wa mifugo na mazao ya mifugo ikiwemo maziwa, mayai, nyama na ngozi.

**135. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kuiwezesha TALIRI ili kuimarisha mashamba ya utafiti na uzalishaji ikiwemo kununua matrekta matatu (**3**), majembe ya kulima kwa trekta matatu (**3**) na vifaa vingine muhimu ili kuiwezesha Taasisi kuendelea kuchangia upatikanaji wa mbari bora za Mifugo, malisho na vyakula bora vya Mifugo.

**Wakala ya Mafunzo ya Mifugo (LITA)**

**136**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, LITA itadahili wanafunzi **4,257;** kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika Kampasi nane (**8**); na kuendelea kutoa huduma za ushauri na ugani kwa wafugaji kupitia programu ya mafunzo ya ujirani mwema (*outreach programme*).

## C. SEKTA YA UVUVI (FUNGU 64)

### Hali Halisi ya Sekta ya Uvuvi

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uvuvi ni miongoni mwa sekta muhimu za uchumi nchini inayochangia katika Pato la Taifa na kuondoa umaskini. Sekta hii inaongozwa na Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 ambayo inalenga kuimarisha usimamizi, uendelezaji, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na ukuzaji viumbe maji kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya uvuvi ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uvuvi inajumuisha shughuli za uvuvi katika maji ya asili na ukuzaji viumbe maji. Katika mwaka 2021, Sekta ya Uvuvi ilikua kwa asilimia **2.5** na ilichangia asilimia **1.8** kwenye Pato la Taifa. Aidha, Sekta ya Uvuvi inatoa ajira kwa watanzania takriban Milioni **4.5** katika mnyororo mzima wa thamani ambapo ajira za moja kwa moja kwa wavuvi ni **194,804** na wakuzaji viumbe maji ni **31,998**. Pia, Sekta ya Uvuvi inachangia katika kipato cha familia pamoja na kuongeza usalama wa chakula na lishe ambapo samaki huchangia asilimia **30** ya protini inayotokana na wanyama.

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli za uvuvi zinafanywa zaidi na wavuvi wadogo kwenye maji ya asili ambapo huchangia takriban asilimia **95** ya samaki wote wanaovuliwa nchini. Hadi tarehe 30 Aprili, 2022, jumla ya wavuvi wadogo wapatao **194,804** walishiriki moja kwa moja katika shughuli za uvuvi kwa kutumia vyombo vya uvuvi vipatavyo **57,991** na kuwezesha kuvuna tani **415,880.64** za samaki zenye thamani ya **Shilingi trilioni 2.80** (**Kiambatisho Na. 21**). Kati ya hizo, tani **367,003.33,** sawa na asilimia **88.25**

ni kutoka maji baridi na tani **48,877.30,** sawa na asilimia **11.75** ni kutoka maji chumvi.

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kuhamasisha, kuendeleza na kusimamia shughuli za ukuzaji viumbe maji nchini. Jumla ya wadau 12,902 walipata mafunzo mbalimbali kuhusu ukuzaji viumbe maji. Kati ya hao wadau 7,884 walipata mafunzo ya mbinu bora za ufugaji samaki na udhibiti magonjwa na 5,018 mafunzo ya kilimo cha mwani na uongezaji thamani. Jumla ya tani 28,856.87 za mazao ya ukuzaji viumbe maji zenye thamani ya Shilingi 184,719,770,930 zimezalishwa. Aidha, jumla ya vifaranga 30,632,528 vyenye thamani ya Shilingi **4,459,879,200** vimezalishwa nchini na vitotoleshi vya Wizara, Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 **(Kiambatisho Na. 22)**. Pia, jumla ya tani **2,156.1** za chakula cha samaki **(Kiambatisho Na. 23)** zenye thamani ya **Shilingi 6,468,300,000** zimetumika nchini hadi Aprili 30, 2022. Vilevile, vifaranga **373,200** vimepandikizwa katika malambo mbalimbali nchini ili kuongeza upatikanaji wa samaki.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** uvuvi wa kibiashara hufanywa na meli za uvuvi wa kambamiti kwenye maji ya ndani na kitaifa na meli kubwa katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari ambazo nyingi ni kutoka nchi za kigeni na zinalenga samaki aina ya Jodari na jamii zake. Katika mwaka 2021/2022, jumla ya meli sita (**6**) zilipata leseni ya kuvua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari. Kati ya hizo, meli tatu (**3**) ni za kigeni na meli tatu **(3**) ni za ndani. Meli hizo zimevuna jumla ya tani **437** za samaki. Pia, uvuvi wa kambamiti katika maji ya ndani na kitaifa unafanywa kuanzia mwezi Machi hadi Septemba katika kanda ya Kaskazini na mwezi Aprili hadi Agosti Kanda ya Kusini; kila mwaka. Aidha, katika msimu wa mwaka 2021 meli sita (**6**) zilipata leseni na kuvuna kiasi cha tani **85.84** za kambamiti zenye thamani ya **Shilingi bilioni 1.6** na tani **284.92** za samaki zenye thamani ya **Shilingi bilioni 1.3.** Katika

msimu wa mwaka 2022, jumla ya meli tisa (**9**) zimeomba kibali cha kufanya uvuvi wa kambamiti.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya uzalishaji, uchakataji na uhifadhi wa mazao ya uvuvi kwa kujenga na kukarabati mialo na masoko ya samaki ili kuthibiti viwango vya ubora na usalama kwa lengo la kukuza biashara ya mazao ya uvuvi ndani na nje ya nchi. Aidha, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022, jumla ya tani **34,841.72** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo vipande **169,089** wenye thamani ya **Shilingi bilioni 475.01** waliuzwa nje ya nchi. Pia, Serikali imeendelea kuratibu uingizaji wa mazao ya uvuvi kutoka nje ya nchi hususan samaki, ambapo hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022, jumla ya tani **4.75** za samaki na samaki hai wa mapambo vipande **895** wenye thamani ya **Shilingi milioni 154.23** wameingizwa nchini.

**143.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Usimamizi Shirikishi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi Nchini kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi, ulinzi na udhibiti wa rasilimali za uvuvi ili kuwa na uvuvi endelevu. Aidha, Wizara imeimarisha Kanda **4** na Vituo **36** vya Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi kwa kuvipatia vitendea kazi na watumishi.

**144.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imesaidia kuunganisha makampuni mbalimbali na huduma ya mikopo hususan kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kuwasaidia utayarishaji wa Maandiko ya Biashara (*Bankable Business Plans*). Aidha, hadi tarehe 30 Aprili, 2022, maombi ya mikopo yenye thamani ya **Shilingi bilioni 56.7** yamewasilishwa benki ya TADB ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 9.4** kimeshatolewa kwa wadau mbalimbali katika Sekta ya Uvuvi.

**145.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa kutunga Sheria mpya ya kusimamia uvuvi wa Bahari Kuu na Kanuni zake, kuainisha fursa za uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi, kuboresha Kanuni za Uvuvi na kuimarisha ushirikiano na Sekta binafsi na Wadau wa Maendeleo ili kuvutia Sekta binafsi kuwekeza katika Sekta ya Uvuvi. Aidha, Serikali imeendelea kuwekeza kwa kuboresha miundombinu ya uvuvi ikiwemo mialo **33** ya kupokelea samaki na masoko manne (**4**).

**146.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, uwekezaji mkubwa katika ufugaji samaki kibiashara wenye thamani ya **Shilingi bilioni 11** umefanywa na Kampuni za Tanlapia (Bagamoyo) na Tangreen (Magu). Kupitia uwekezaji huo, takriban tani **15,000** za samaki zinatarajiwa kuzalishwa kwa mwaka. Aidha, Serikali imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi ambapo hadi sasa kuna viwanda vikubwa vya kuchakata mazao ya uvuvi **16**, viwanda vya kati vitano (**5**) na viwanda vidogo **33**, maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi **90**, viwanda **13** vya kuchakata mabondo ya Sangara na viwanda vitano (**5**) vya kutengeneza zana za uvuvi. Pia, Serikali imeingia mashirikiano na Serikali ya Misri, kupitia Kampuni ya Taifa ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji (*National Company for Fishing and Aquaculture*), kwa lengo la kuwekeza kwa pamoja na Shirika la Uvuvi Tanzania - TAFICO.

**147.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imepata mzabuni (*China Harbour Engineering Co. Ltd)* kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko Mkoani Lindi. Aidha, ujenzi wa bandari hiyo unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Mei, 2022. Uwepo wa bandari ya uvuvi utaimarisha uvuvi wa bahari kuu, kutoa fursa za ajira kwa watanzania, kuongeza upatikanaji wa malighafi kwa viwanda vya kuchakata samaki na mazao ya uvuvi.

**148.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kukabiliana na vitendo vya uvuvi haramu katika maeneo ya bahari na maji baridi. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na jitihada hizo ni kudhibitiwa kwa uvuvi wa kutumia milipuko katika Ukanda wa Bahari ya Hindi kwa asilimia **95**. Aidha, kwa upande wa maji baridi uvuvi haramu umepungua kwa takriban asilimia **80**. Vilevile, Wizara imechukua hatua stahiki za kisheria kwa watuhumiwa **1,123** waliobainika kujihusisha na vitendo vya uvuvi haramu nchini.

**149.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya NMB, tarehe 31 Oktoba, 2021 imezindua Mpango wa Bima kwa wavuvi ujulikanao kama 'Bima ya Jahazi' kwa wavuvi wadogo. Kufuatia kuzinduliwa kwa mpango huo, Benki ya NMB imeingia Mkataba na Kampuni ya Bima ya *Britam* kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa Bima ya Jahazi. Bima hiyo inalenga kuwasaidia wavuvi wadogo kupata fidia na kugharamia matibabu pindi wanapopatwa na majanga mbalimbali, ikiwemo ajali na kuungua kwa mitumbwi.


**150.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo (*Environmental Management and Economic Development Organization – EMEDO)* itatekeleza Mradi wa **Shilingi bilioni 2.7** wenye lengo la kupunguza vifo vya wavuvi vinavyotokana na kuzama majini. Mradi huo ambao utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (2022-2025) utahusisha mikoa ya Mwanza, Mara na Kagera.

**MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022**
**Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2021/2022**

**151.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ilikadiria kukusanya Shilingi **40,000,000,000**

kupitia Fungu 64. Hadi tarehe 30 Aprili, 2022, Shilingi **19,171,950,269.11** zilikusanywa sawa na asilimia **63.9** ya lengo la kukusanya hadi tarehe 30 Aprili, 2022 (**Kiambatisho Na. 24**). Fedha hizi zimekusanywa kutoka vyanzo vifuatavyo: leseni za kusafirisha samaki na mazao yake (*Export Licences*); leseni za uingizaji mazao ya uvuvi (*Import Licences*); ushuru wa mrabaha (*Export Royalty*); mrabaha wa kuingiza mazao ya uvuvi nchini (*Import Royalty*), leseni za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu, tozo ya maabara; leseni za uvuvi wa kambamiti, mauzo ya vifaranga vya samaki na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi (***Kielelezo Na. 1***).

**Kielelezo Na. 1: Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi tarehe 30 Aprili, 2022**




**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** Miongoni mwa sababu za kutofikia lengo la makusanyo ni pamoja na kuwepo kwa mianya ya utoroshaji wa mazao ya uvuvi kwenye maeneo ya maji na mipakani; kuwepo kwa uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi; Upungufu wa watumishi wa Sekta ya Uvuvi kwenye vituo vya Ulinzi na Usimamizi wa rasilimali za Uvuvi na Uthibiti Ubora wa Viwango na Masoko; ufinyu wa bajeti na uhaba wa vitendea kazi kwenye baadhi

ya vituo kama magari, pikipiki na boti; na kuwepo kwa ukwepaji wa ulipaji wa ushuru (*Export Royalty*) kwa mazao yanayosafirishwa nje ya nchi.

**Fedha zilizoidhinishwa kwa Mwaka 2021/2022**

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Fungu 64 ilitengewa jumla ya **Shilingi 121,350,047,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 22,205,681,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 99,144,366,000** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Matumizi ya Bajeti ya Kawaida.**

**154.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara ya Mifugo na Uvuvi -Fungu 64 - Sekta ya Uvuvi, ilitengewa bajeti ya matumizi ya kawaida jumla ya **Shilingi 22,205,681,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 11,575,270,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na **Shilingi 10,630,411,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Hadi tarehe 30 Aprili, 2022, jumla ya **Shilingi 19,406,293,018** zimetolewa, sawa na asilimia **87.4** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 9,630,617,543.70** ni fedha za mishahara ya watumishi (PE) na **Shilingi 9,775,675,474.20** ni fedha za matumizi mengineyo.

**Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo**

**155**. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Fungu 64 – Sekta ya Uvuvi ilitengewa kiasi cha **Shilingi 99,144,366,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwa ni fedha za ndani na nje. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 62,550,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 36,594,366,000** ni fedha za nje. Hadi tarehe 30 Aprili, 2022, jumla ya **Shilingi 3,952,067,467** zimetumika ikiwa ni sawa na asilimia **6.3** kutoka vyanzo vya ndani.

**UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KATIKA MWAKA 2021/2022**
**Usimamizi wa Sera na Sheria**

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza Sera ya Uvuvi ya mwaka 2015 kupitia Sheria na Kanuni za kusimamia Sekta ya Uvuvi zikiwemo Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 pamoja na Marekebisho yake ya mwaka 2020; Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994; Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Na. 5 ya Mwaka 2020 na Kanuni zake za mwaka 2021, na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Na. 11 ya mwaka 2016. Lengo kuu la Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 ni kuimarisha usimamizi, uendelezaji, uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na ukuzaji viumbe maji.

**157.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali pia imeendelea kutoa elimu kuhusu sera ya uvuvi, sheria na kanuni za uvuvi kwa wadau wa uvuvi kupitia huduma za ugani, mafunzo rejea, semina, mikutano, elimu kwa umma (vipindi vya televisheni na redio) na maonesho ya kitaifa, kikanda na kimataifa pamoja na kusambaza nakala **900** za Sera ya Uvuvi. Lengo ni kujenga uelewa wa pamoja kuhusu dhana ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji endelevu.

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa 2021/2022, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilipokea hoja na malalamiko mbalimbali kutoka kwa wadau wa sekta ya uvuvi kuhusiana na maboresho yaliyofanywa mwaka 2020 katika Kanuni ya Uvuvi ya mwaka 2009. Pia, Wizara ilipokea hoja mahsusi kutoka kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Miongoni mwa hoja na malalamiko hayo yalihusu matumizi ya nyavu ambazo zimefanyiwa maboresho na wavuvi wenyewe kinyume na viwango vinavyokubalika; matumizi ya mtando (*Ringnet*) kwa ajili ya kuvua baharini muda wa mchana na kwenye kina chini ya mita 50; uvuvi wa kutumia mtando katika Ziwa Tanganyika wakati wa

mchana na chini ya mita 1,000 kutoka ufukweni; Viwango vya juu vya tozo na ada za leseni za mazao ya uvuvi; kubadili tafsiri ya vyama vya ushirika kwenye Kanuni husika ili itambue vyama vingine visivyo vya ushirika vilivyosajiliwa chini ya Sheria nyingine ikiwemo Sheria za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Malalamiko mengine yalihusu matumizi ya taa zinazotumia mwanga wa sola zenye uwezo usiozidi *Watt* kumi (10) na taa zisizozidi tano (**5**) kwa chombo cha uvuvi katika ziwa Tanganyika na matumizi ya jenereta katika bahari ya Hindi.

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mifugo na Uvuvi imefanyia kazi malalamiko na hoja zote za wadau wa sekta ya uvuvi na kutoa mrejesho kwa Wahusika. Aidha, tarehe 25 Agosti, 2021 na tarehe 30 Machi, 2022 Wizara ilipata fursa ya kukutana na Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo na kutoa mrejesho. Kufuatia hatua hizo, tayari Wizara imeandaa mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni ya Uvuvi ya mwaka 2009 ili kuboresha mazingira ya wavuvi na wafanyabiashara wa samaki na mazao ya uvuvi. Vilevile, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na wizara ya Fedha na Mipango kupitia Kamati ya Taifa ya maboresho ya Kodi imeandaa mapendekezo ya maboresho ya ada na leseni na tozo mbalimbali za kusafirisha nje mazao ya uvuvi. Hatua hii inalenga kupunguza gharama kwa wafanyabiashara, kuchochea uzalishaji na uwekezaji katika sekta ya uvuvi na hatimaye kuongeza mapato ya Serikali kupitia sekta ya uvuvi.

**160.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya marekebisho ya tozo za Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu za mwaka 2009 kupitia Tangazo la Serikali Na. 496B la tarehe 30 Juni, 2021 kwa lengo la kupunguza ada za utalii wa ndani, kuweka tozo kwa wakazi wa Afrika Mashariki pamoja na wageni wenye vibali nchini na kuweka tozo za mahoteli kulingana na uwekezaji wa hoteli.

Utekelezaji wa tozo hizo mpya ulianza kutumika mwezi Julai, 2021.

**161.** ***Mheshimiwa Spika**,* katika mwaka 2021/2022, Wizara imefanya tafsiri ya Sheria zinazosimamia Sekta ya Uvuvi katika kutekeleza Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 1 ya Mwaka 2021 (*Miscellaneous Amendment*) iliyopitishwa na Bunge lako tukufu ya kutaka Sheria zote kuwa katika lugha ya Kiswahili.

**Usimamizi wa Takwimu za Uvuvi**

**162.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Serikali imeendelea kuratibu, kukusanya, kuchakata na kusimamia upatikanaji wa takwimu za uvuvi kwa kuboresha mfumo wa kielektroniki (e-CAS) wa ukusanyaji takwimu za uvuvi kwa lengo la kuwa na uvuvi endelevu**.** Katika mwaka 2021/2022, jumla ya wavuvi **194,804** walitumia vyombo vya uvuvi **57,991** na kushiriki katika shughuli za uvuvi ikilinganishwa na wavuvi **195,435** waliotumia vyombo vya uvuvi vipatavyo **58,231** mwaka 2020/2021.

**163.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia mwezi April 2022, jumla ya tani **415,880.64** za samaki zenye thamani ya **Shilingi trilioni 2.80** zilivunwa, ikilinganishwa na tani **422,859.78** za samaki zenye thamani ya **Shilingi trilioni 2.62** zilizovunwa katika kipindi kama hiki mwaka 2020/2021 (**Kielelezo Na. 2**).

**164.** ***Mheshimiwa Spika***, kati ya tani **415,880.64** tani **288,165.61** sawa na asilimia **66.89** ni kutoka Ziwa Victoria, tani **73,506.78** sawa na asilimia **17.67** ni kutoka Ziwa Tanganyika, tani **48,877.30** sawa na asilimia **11.75** ni kutoka Ukanda wa Bahari ya Hindi, tani **5,115.21** sawa na asilimia **1.23** ni kutoka Ziwa Nyasa, tani **10,215.75** sawa na asilimia **2.46** ni kutoka maji madogo.

**Kielelezo Na. 2: Mlinganisho wa uvunaji wa Samaki kwa mwaka 2020/2021 na 2021/2022 hadi Mwezi Aprili, 2022.**




**165.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kuboresha mfumo wa kielektroniki (e-CAS) wa ukusanyaji takwimu za uvuvi na mfumo huo umewezesha ukusanyaji wa takwimu za uvuvi katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Bahari ya Hindi. Vilevile, Serikali imefanya ufuatiliaji na tathmini ya ukusanyaji wa takwimu za uvuvi katika Halmashauri **17** za Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *World Wide Fund for Nature* (WWF) imetoa simu janja (*smart phones*) kwa Maeneo ya Usimamizi wa Pamoja (*Collaborative Fisheries Management Areas* – CFMAs) katika Wilaya za Mafia, Kibiti, Kilwa, Mtwara vijijini na Kigamboni kwa ajili ya kukusanya takwimu za uvuvi pamoja na kuchukua matukio na taarifa nyingine za uvuvi. Pia, katika kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi, Serikali imetoa injini tatu (**3**) zenye nguvu za farasi **40** kwa wadau wa uvuvi kama ifuatavyo: Halmashauri ya Wilaya ya Mafia moja (**1**) kwa Idara ya uvuvi; na Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti kwa BMU mbili (**2**).

**Usimamizi na Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi**

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Usimamizi Shirikishi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi nchini wenye lengo la kuimarisha usimamizi na ulinzi wa rasilimali za uvuvi ili kuwa na uvuvi endelevu. Aidha, Mkakati unalenga kukuza uelewa miongoni mwa wadau wa uvuvi na kupunguza kero za wananchi kwa kuongeza uwazi katika utendaji wa majukumu ya kila siku. Pia, Mkakati umeweka bayana mfumo wa kudhibiti uingizaji, utengenezaji na usambazaji wa zana zote za uvuvi nchini.

**167.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kulinda na kusimamia rasilimali za uvuvi katika Bahari ya Hindi, maziwa, mabwawa na mito kwa kufanya doria shirikishi za mara kwa mara pamoja na operesheni maalum. Hadi tarehe 30 Aprili, 2022, jumla ya siku kazi **5,695** za operesheni maalum na doria shirikishi zimefanyika ikiwa ni **asilimia 73.01** ya lengo la siku kazi **7,800** kwa mwaka 2021/2022. Pia, Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Kudhibiti Uharibifu wa Kimazingira (*National MultiAgency Task Team* – NMAT) kimefanya operesheni tatu (**3**) katika Ukanda wa Ziwa Victoria, Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi na Bwawa la Mtera. Matokeo ya operesheni na doria yalikuwa ni kukamatwa kwa zana haramu za uvuvi na samaki wachanga (**Kiambatisho Na. 25**). Aidha, watuhumiwa **1,123** walikamatwa na kesi tatu (**3)** zimefunguliwa Mahakamani kufuatia makosa ya uvunjaji wa sheria.

**168.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi, vituo **36** vya Ulinzi na Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi vimepatiwa vitendea kazi, rasilimali watu na rasilimali fedha ili viweze kutekeleza majukumu ya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Aidha, Serikali imenunua injini za kupachika **12** ambazo zimepelekwa katika Vituo

vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi vya Mwanza, Geita, Ukerewe, Kanyigo-Marehe na Simiyu. Pia, Serikali imenunua boti za doria **16** ambazo zimepelekwa kwenye vituo vya ulinzi wa rasilimali za uvuvi (**Kiambatisho Na. 26).** Vilevile, Wizara imepokea boti moja ya doria na injini moja (**1**) ya kupachika yenye nguvu za farasi **40** kutoka Kampuni ya DHL ambayo itatumika kuimarisha usimamizi katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika.

**169.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi kwa kuvijengea uwezo Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi (BMUs) pamoja na kushirikiana na Mashirika yasiyo ya kiserikali kwa lengo la kuleta ufanisi na kuongeza tija. Hadi tarehe 30 Aprili, 2022, Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Raslimali za Uvuvi (BMUs) **784** vimeanzishwa nchini kwa mchanganuo ufuatao: Ziwa Victoria (**433**); Ziwa Tanganyika (**72**); Ziwa Nyasa (**29**); Ziwa Rukwa (**12**); Bahari ya Hindi (**173**); Nyumba ya Mungu (**20**); Bwawa la Mtera (**29**); Ziwa Kitangiri (**1**); Mto Ruhuhu (**11**); na Mto Kilombero (**4**). Aidha, Wizara imetoa mafunzo kuhusu dhana ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi unaozingatia ikolojia na mazingira kwa wavuvi **120** kutoka Vikundi vinne (**4**) vya BMUs vya Mandela, Mbamba Bay, Ng'ombo na Ngindo katika mwambao wa Ziwa Nyasa.

**170.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *Seasense* imeanzisha BMUs tatu (**3**) za Mtitimira, Namwedo na Namakongoro katika Mkoa wa Lindi na zimejengewa uwezo wa kusimamia rasilimali za uvuvi na kuandaa Sheria ndogo za kusimamia rasilimali za uvuvi. Pia, BMU hizo zimewezeshwa kuandaa mipango ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi. Aidha, BMUs zinazounda Maeneo matatu (3) ya Usimamizi ya Pamoja (*Collaborative Fisheries Management Areas* – CFMAs) katika Mkoa wa Lindi zimewezeshwa kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Pamoja wa rasilimali za uvuvi katika maeneo yao.

**171.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la *Mwambao Coastal Network Tanzania* imezijengea uwezo wa kusimamia rasilimali za uvuvi BMUs **16** katika Wilaya za Pangani (**9**) na Mkinga (**7**) kwa kuzipatia mafunzo ya ukusanyaji takwimu za uvuvi, utunzaji wa fedha, usimamizi na doria ambapo wadau **201** walishiriki. Aidha, BMUs **11** katika Wilaya za Pangani (**4**) na Mkinga (**7**) ziliwezeshwa kuandaa ramani zinazoonesha aina za rasilimali za uvuvi na mahali zinapopatikana kwa wingi katika maeneo yao.

**172.** ***Mheshimiwa* Spika**, Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa limeutangaza mwaka 2022 kuwa mwaka wa Uvuvi Mdogo na Ukuzaji Viumbe Maji (*International Year for Artisanal Fisheries and Aquaculture* - IYAFA 2022). Uamuzi wa kuadhimisha mwaka huu kuwa mwaka wa wavuvi wadogo na ukuzaji viumbe maji unatokana na mchango wao mkubwa katika kuzalisha mazao ya uvuvi ambayo ni chakula chenye protini nyingi na hivyo kuchangia katika kutatua changamoto za utapiamlo na magonjwa yanayohusiana na lishe. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani-FAO imefanya maadhimisho hayo kitaifa tarehe 6 hadi 8 Machi, 2022 Jijini Mwanza ambapo wadau mbalimbali walishiriki.

**Uthibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

**173.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kuimarisha uthibiti wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi kwa kufanya jumla ya kaguzi **8,598** za kuhakiki uimara wa mfumo wa uzalishaji wa mazao ya uvuvi yenye ubora na usalama. Kaguzi hizo zimefanyika katika viwanda **19** vya kuchakata samaki, viwanda **56** vya samaki hai, mialo ya kupokelea samaki **31,** masoko **4**, maghala ya kuhifadhia mazao yaliyokaushwa **39**, viwanda vya kugandisha samaki **31,** viwanda vya mabondo **13**, meli

kubwa **5** za uvuvi na vyombo **1,221** vya kusafirisha mazao ya uvuvi.

**174.** ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya kaguzi **1,468** zimefanyika viwandani ambazo ni kaguzi **1,152** za kawaida na kaguzi za kina **316**; kaguzi **1,666** zimefanyika kwenye maghala ya kuhifadhia samaki, viwanda vya kugandisha samaki, magari ya kusafirisha samaki, mialo ya kupokelea samaki pamoja na masoko ya samaki. Vilevile, kaguzi **5,464** ni kwa ajili ya uhakiki wa ubora na usalama wa mazao ili kutoa vyeti vya afya kabla ya kusafirishwa nje ya nchi.

**175.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Maabara ya Taifa ya Uvuvi imeendelea kuhakiki ubora na usalama wa samaki na mazao yake ili kukidhi viwango vinavyokubalika kitaifa, kikanda na kimataifa. Aidha, Maabara ya Uvuvi imepokea sampuli **2,027** na kufanya vipimo **6,411** vya uchunguzi wa vimelea na kemikali ambapo **Shilingi 409,450,000** zilikusanywa ikilinganishwa na sampuli **2,621** zilizopokelewa na vipimo **5,895** vyenye thamani ya **Shilingi 376,590,000** vilivyofanyika mwaka 2020/2021. Pia, Maabara imeendelea kuhuisha hadhi ya Ithibati kupitia kaguzi za kina za Taasisi ya Ithibati ya Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADCAS) na hivyo kufanikiwa kukidhi kiwango cha kimataifa cha ISO17025:2017.

**176.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kuimarisha mazingira ya uzalishaji, uchakataji, uhifadhi wa mazao ya uvuvi pamoja na miundombinu ya uvuvi ikiwemo mialo ya kupokelea samaki na masoko kwa lengo la kuthibiti viwango vya ubora na usalama. Aidha, hadi tarehe 30 Aprili, 2022, tani **34,841.72** za mazao ya uvuvi na samaki hai wa mapambo **169,089** wenye thamani ya **Shilingi bilioni 475.01** waliuzwa nje ya nchi na kuingizia Serikali mrabaha wa **Shilingi bilioni 15.47** (**Kiambatisho Na. 27**) ikilinganishwa

na tani **32,962.79** na samaki hai wa mapambo **104,524** wenye thamani ya **Shilingi bilioni 460.62** waliouzwa nje ya nchi na kuingizia Serikali mrabaha wa **Shilingi bilioni 15.55** mwezi Aprili, 2021. Aidha, Serikali imeendelea kusimamia uingizaji wa samaki ndani ya nchi kutoka nchi mbalimbali ambapo hadi tarehe 30 Aprili, 2022, jumla ya samaki wa mapambo **895** na tani **4.75** za samaki vyote vikiwa na thamani ya **Shilingi milioni 154.23** zimeingizwa nchini (**Kiambatisho Na. 28**) ikilinganishwa na samaki wa mapambo **50** na **tani 5.48** za samaki wenye thamani ya **Shilingi milioni 170.26** zilizoingizwa nchini mwaka 2020/2021.
177. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Mfuko wa Kuhifadhi Mazingira Duniani (*World Wide Fund for Nature* - WWF) ilivipatia vikundi **24** vya wanawake wasindikaji na wafanyabiashara wa samaki majokofu makubwa **24** ya kuhifadhia mazao ya uvuvi katika Wilaya za Mkuranga (**8**), Kibiti (**2**), Mafia (**5**), Kilwa (**5**) na Mtwara Vijijini (**4**) kwa lengo la kupunguza upotevu wa baada ya kuvuna na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi.

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu**

**178.** ***Mheshimiwa Spika***, Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu zinalenga kuhifadhi uoto wa asili, nyasi za bahari, matumbawe, mazalia na makuzi ya samaki, pamoja na kulinda na kuhifadhi samaki na viumbe waliohatarini kutoweka kama samaki aina ya papa potwe, Silikanti na viumbe vingine vya baharini kama Kasa na Kaa wanaokwea minazi waitwao tuyuyu (*coconut crab*). Vilevile, uhifadhi unalenga kulinda ndege wanaohama kutoka bara moja kwenda bara lingine, popo wanaokula matunda, viboko (wanaoitika kwa miluzi), magofu yenye historia za kusisimua na karakana za utengenezaji wa boti za asili. Aidha, maeneo hayo ya hifadhi yana vivutio mbalimbali vya utalii zikiwemo fukwe nzuri zenye mchanga laini na mweupe vinapatikana katika maeneo machache

sana hapa duniani na hivyo kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache zenye vivutio vya asili katika pwani na bahari.

**179.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) imeendelea kusimamia maeneo **18** yanayohusisha hifadhi za bahari tatu (**3**) ambazo zipo katika mikoa ya Mtwara (Hifadhi ya Ghuba ya Mnazi na maingilio ya Mto Ruvuma); Pwani (Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia); na Tanga (Hifadhi ya Bahari ya Silikanti Tanga) pamoja na maeneo tengefu (**15)** katika mikoa ya Dar es Salaam (**7**), Pwani (**3**) na Tanga (**5)**. Mojawapo ya maeneo hayo ni kisiwa kidogo cha Shungimbili ambapo MPRU imeingia makubaliano na mwekezaji kampuni ya *Thanda Tanzania Limited* kujenga na kuendesha hoteli ya kitalii ya nyota tano. Pamoja na kulipa maduhuli ya Serikali, uwekezaji huu umeleta faida kubwa kwa nchi ikiwemo kutoa ajira, kipato na kuongeza idadi ya watalii kwa kuitangaza Tanzania ikiwemo kushinda tuzo za *Africa's Leading Luxury Island* na *World's Leading Exclusive Private Island* 2021 kwenye tuzo za *World Travel Awards* kwa mwaka 2021.

**180.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kusimamia matumizi endelevu ya bioanuwai na mifumo ikolojia ya bahari jumla ya doria zenye siku kazi **480** zilifanyika hadi tarehe 30 Aprili, 2022, katika maeneo yote ya hifadhi za bahari na maeneo tengefu. Aidha, elimu kuhusu sheria na matumizi ya zana sahihi na uvuvi endelevu imetolewa ili kuhifadhi rasilimali za bahari kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

**181. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia MPRU ilishiriki katika maonesho ya kikanda na kimataifa yakiwemo maonesho ya **45** ya Biashara Sabasaba, Africa Mashariki (*EAC EXPO 2021*) pamoja na kujitangaza kupitia Utalii Popote, Kevi Business Media, Safari Channel, na Channel Ten. Hadi

tarehe 30 Aprili, 2022 jumla ya watalii **22,562** walitembelea maeneo ya hifadhi za bahari kati yao watalii wasio watanzania ni **12,257** na watanzania ni **9,049** ikilinganishwa na jumla ya watalii **17,292** ambapo watalii wasio watanzania walikuwa **9,659** na watanzania **7,633** katika kipindi kama hicho mwaka 2021.

**Usimamizi wa Uvuvi katika Bahari Kuu**

**182.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2021/2022, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (*Deep Sea Fishing Authority – DSFA*) imetoa leseni **25** za uvuvi wa bahari kuu, kukodisha (*chartering*) na kutoa kibali cha kuvua nje ya maji ya Tanzania kwa meli moja (*Pacific Star*) na kukusanya **Shilingi bilioni 3.3** ikilinganishwa na idadi ya meli sita (**6**) zilizopewa leseni na kukusanya jumla ya **Shilingi 288,677,014.7** mwaka 2020/2021. Mafanikio hayo yametokana na hatua zinazochukuliwa za kuvutia uvuvi katika bahari kuu ikiwemo kuweka mazingira wezeshi kupitia Sheria mpya ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Na. 5 ya mwaka 2020 na Kanuni zake za mwaka 2021.

**183.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Mamlaka imeingia makubaliano ya uvuvi na Kampuni ya Uvuvi ya ALBACORA Group kutoka Hispania ikiwa ni juhudi za kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Uvuvi kupitia uvuvi wa bahari kuu. Makubaliano hayo yatapelekea meli za kampuni hiyo kusajiliwa Tanzania na kufanya shughuli za uvuvi katika bahari kuu. Katika kutekeleza makubaliano hayo, tarehe 21 Machi, 2022, meli ya PACIFIC STAR inayomilikiwa na kampuni ya ALBACORA Group ilipokelewa katika Bandari ya Dar es Salaam na Viongozi wa Wizara husika za SMT na SMZ pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Aidha, ALBACORA pamoja na kulipia leseni ya uvuvi ya kiasi cha **Dola za Kimarekani 21,000**, pia imelipa kiasi cha **Dola za Kimarekani 400,000** kwa mwaka kwa meli hiyo ya uvuvi wa nyavu za kuzungusha (*purse seine*), itashusha kiasi cha

tani **100** za samaki wasiolengwa nchini na kuuza tani **300** za samaki waliolengwa kwa makampuni ya hapa nchini. Vilevile, kampuni hiyo itajenga kiwanda cha kuchakata samaki ambacho kitatoa ajira zipatazo **100** na kuongeza mapato yatokanayo na uvuvi wa bahari kuu kwa kusafirisha nje samaki na mazao yake. Aidha, watanzania wawili (**2**) watapatiwa mafunzo kila mwaka katika kozi za ubaharia nchini Hispania na kuajiri mabaharia Watanzania wasiopungua watano (**5**) kila mwaka.

**184.** ***Mheshimiwa Spika*,** Mamlaka imezijengea uwezo taasisi za utafiti na vyuo vikuu nchini kwa kutoa vifaa vya utafiti vyenye thamani ya **Shilingi 302,160,752**. Taasisi zilizopatiwa vifaa hivyo ni Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) na Taasisi za Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI na ZAFIRI). Aidha, DSFA imewajengea uwezo wavuvi wadogo kwa kuwapatia vifaa vya kuwawezesha wavuvi kukusanya takwimu vikiwemo GPS, mizani, *tablets* na simu janja.

**185.** ***Mheshimiwa Spika*,** Serikali kupitia DSFA imekamilisha ujenzi wa chelezo cha kupandishia boti za ukaguzi katika Ofisi za Mamlaka – Fumba, Zanzibar. Kukamilika kwa chelezo hicho kutapunguza gharama na kurahisisha shughuli za ukaguzi wa meli za uvuvi bandarini au maeneo ya karibu ya bandari. Aidha, Mamlaka imeendelea kudhibiti uvuvi haramu kwa kusimamia kikamilifu Sheria na Kanuni na kuboresha mifumo ya kufuatilia mienendo ya meli (*Vessel Monitoring System - VMS* na *Automatic Identification System - AIS*). Pia, doria saba (**7**) za anga zenye jumla ya masaa 64 zilifanyika katika bahari kuu kwa kushirikisha taasisi za SMT na SMZ ambazo hazikuonesha kuwepo kwa meli ya uvuvi iliyokiuka masharti au Kanuni za Uvuvi wa Bahari Kuu.

**186.** ***Mheshimiwa Spika***, Mamlaka kupitia programu ya ECOFish chini ya Kamisheni ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Commission* - IOC) iliandaa andiko lililowezesha kupata ufadhili wa jumla ya **Shilingi 508,000,000** kwa miaka mitatu (**3**), kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi wa bahari kuu. Aidha, Serikali kupitia DSFA ilikusanya maoni ya wadau kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, kuyachambua na kuandaa Andiko Dhana kuhusu mapendekezo ya vivutio kwa wawekezaji wa ndani na wa nje katika uvuvi wa bahari kuu nchini.

**Ukuzaji Viumbe Maji**

**187.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeendelea kuhamasisha na kuendeleza shughuli za ukuzaji viumbe maji nchini kupitia vituo vya Kingolwira (Morogoro), Ruhila (Ruvuma), Mwamapuli (Tabora) Nyengedi (Lindi), Rubambagwe (Geita) na Tanga (Machui). Katika mwaka 2021/2022, jumla ya vifaranga **2,352,350** vilizalishwa ikilinganishwa na vifaranga **1,901,717** vilivyozalishwa mwaka 2020/2021. Vilevile, vitotoleshi vya taasisi za Serikali vilizalisha jumla ya vifaranga **1,036,890**. Aidha, jumla ya wananchi **7,884** walipatiwa mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji samaki na udhibiti wa magonjwa. Pia, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI imetoa mafunzo kwa wanawake **5,018** ambao ni wakulima wa mwani katika mikoa ya Lindi (**2,210**), Tanga (**1,421**), Mtwara (**1,277**) na Pwani (**110**) kuhusu uzalishaji na uhifadhi wa zao la mwani ili liweze kukidhi viwango vya ubora. Vilevile, maafisa ugani **59** kutoka mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, Songwe, Ruvuma, Kigoma, Mbeya, Katavi na Pwani walipatiwa mafunzo rejea ya mbinu bora za ufugaji samaki ili kuwaongezea ufanisi katika kuhudumia wananchi.

**188.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kutoka ndani

na nje ya nchi kuwekeza katika mnyororo wa thamani wa ukuzaji viumbe maji. Vitotoleshi vya sekta binafsi vimezalisha jumla ya vifaranga **26,943,288** ikilinganishwa na vifaranga **18,071,752** vilivyozalishwa mwaka 2020/2021. Pia, jumla ya vifaranga **200,000** viliuzwa nchini Msumbiji. Aidha, idadi ya vitotoleshi imeongezeka kutoka **33** hadi **35**. Aidha, jumla ya tani **2,156.1** za chakula cha samaki zilitumika nchini ambapo kati ya hizo, tani **540.6** zilizalishwa nchini na tani **1,615.5** ziliingizwa kutoka nchi mbalimbali ikilinganishwa na tani **1,182.47** zilizotumika mwaka 2020/2021.

**189.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imefanya kaguzi za siku kazi **69** katika vitotoleshi vya samaki, viwanda vya vyakula vya samaki, na mashamba ya ufugaji samaki katika mikoa ya Mwanza, Mara, Pwani na Dar es Salaam ili kutoa ushauri na kuhakikisha kama bidhaa na huduma zinakidhi vigezo. Aidha, Serikali imeendelea kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (*VAT)* na ushuru wa forodha kwa ajili ya zana na pembejeo za ukuzaji viumbe maji ili kupunguza gharama za uzalishaji. Pia, wafugaji wadogo na maafisa ugani wameendelea kupatiwa mafunzo na miongozo ya utengenezaji chakula cha samaki kwa kutumia malighafi katika maeneo yao (*Farm-made feeds*).

**190.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imefanya kampeni maalum ya kuhamasisha matumizi ya fursa zilizopo za uchumi wa buluu kwa wadau **212** wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wilaya, Wakurugenzi wa Wilaya, na wataalam katika Mikoa ya Tanga (**69**), Pwani (**41**), Dar es Salaam (**23**), Lindi (**44**) na Mtwara (**35**). Aidha, fursa zilizojadiliwa ni ukuzaji viumbe maji bahari vikiwemo samaki aina ya mwatiko, majongoo bahari, unenepeshaji kaa na kamba koche, na kilimo cha mwani. Pia, Wizara imeanza ujenzi wa vituo viwili vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji bahari katika mikoa ya Mtwara na Dar es Salaam kwa ajili ya kutatua changamoto ya ukosefu wa mbegu za viumbe maji bahari na kuimarisha huduma za ugani katika ukanda wa pwani. Vilevile, Wizara

imepeleka watumishi tisa **(9)** nchini Thailand ili kupata mafunzo maalum ya uzalishaji mbegu za viumbe maji bahari ili kuhakikisha vituo vinafanya kazi kwa ufanisi pale vitakapoanza kazi.

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** idadi ya wakuzaji viumbe maji imefikia **31,998** kutoka **30,064** wa mwaka 2020/2021. Aidha, idadi ya mabwawa imeongezeka hadi kufikia **31,407** kutoka **30,032** ya mwaka 2020/2021**.** Pia, idadi ya vizimba imefikia **780** (Ziwa Victoria – **653**, Tanganyika – **3** na Malambo mbalimbali – **124**) kutoka vizimba **473** katika mwaka 2020/2021. Vilevile, uzalishaji wa mazao ya ukuzaji viumbe maji umeongezeka hadi kufikia tani **28,856.87** zenye thamani ya **Shilingi 184,719,770,930** kutoka tani **22,793.20** zenye thamani ya **Shilingi 166,387,340,000** katika mwaka 2020/2021. Uzalishaji huu unajumuisha tani **25,286.46** za samaki maji baridi (sato na kambale) zenye thamani ya **Shilingi 177,005,220,000;** tani **6.0** za samaki maji chumvi (mwatiko) zenye thamani ya **Shilingi 24,000,000;** tani **3,514.79** za mwani zenye thamani ya **Shilingi 3,690,529,500**; tani **74.85** za kambamiti zenye thamani ya **Shilingi 1,796,400,000**; tani **30** za kambakoche walionenepeshwa zenye thamani ya **Shilingi 2,700,000,000**; kilo **1,144** za kaa zenye thamani ya **Shilingi 19,085,352;** kilo **370** za majongoo bahari zenye thamani ya **Shilingi 22,200,000** na vipande **164** vya lulu vyenye thamani ya **Shilingi 1,799,900**.

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoahidi Bunge lako Tukufu mwaka jana, Wizara kwa kushirikiana na Mikoa ya Mwanza na Kagera imefanya tathmini na kuainisha maeneo **39** ya ufugaji samaki kwa vizimba katika Ziwa Victoria. Maeneo hayo kwa Mkoa wa Mwanza **30** ni kama ifuatavyo Sengerema (9), Buchosa (6), Misungwi (3), Nyamagana (3), Ilemela (2), Magu (2) na Ukerewe (5) na kwa Mkoa wa Kagera ni **9** kama ifuatavyo Misenyi (1), Bukoba DC (4) na Muleba (4). Maeneo hayo yote yana uwezo wa kuweka vizimba **19,500** vitakavyotoa takriban

ajira **5,000** na tani **100,000** za samaki zenye thamani ya shilingi **bilioni 600** kwa mwaka iwapo mbinu bora za uzalishaji zitazingatiwa. Zoezi hili linalenga kupunguza gharama za awali za uwekezaji ili kuwawezesha wanawake, vijana, na wananchi wa kawaida waweze kutumia fursa iliyopo kuongeza uzalishaji samaki, kutoa ajira, kuongeza kipato na kukuza uchumi nchini. Aidha, Wizara kupitia Wakala ya Elimu ya Uvuvi na Mafunzo (FETA) kwa kushirikiana na Mkoa wa Mwanza imetoa mafunzo kuhusu ufugaji samaki kwenye vizimba kwa vijana **283** kutoka katika halmashauri za Nyamagana, Misungwi, Buchosa, Sengerema, Ukerewe, Magu na Ilemela.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI na Halmashauri mbalimbali nchini, imepandikiza vifaranga **373,200** vya samaki katika malambo saba (**7**) ili kuongeza upatikanaji wa samaki ikilinganishwa na vifaranga **101,500** waliopandikizwa katika mwaka 2020/2021. Vifaranga hivyo vimepandikizwa katika malambo yaliyopo maeneo ya Tabora – Igogo, Igombe, Kazima na Mwamapuli (**156,000**), Simiyu - Zanzui (**94,000**), Ruvuma - Mhepai (**73,200**) na Rukwa – Malonje (**50,000**). Aidha, Wizara imetoa vifaranga **32,000** ili kukiwezesha kikundi cha UWASAI kilichoko Igunga kufuga samaki kwenye vizimba katika bwawa la Mwanzugi. Vilevile, Wizara imewezesha vikundi vitatu vya wakulima wa mwani kwa kuwapatia vitendea kazi vikiwemo kamba **725** na taitai **288,000** katika mkoa wa Tanga kwenye vikundi vya mwani katika vijiji vya Kijiru **(241)**, Moa **(243)** na Tawalani **(241)** zenye thamani ya **Shilingi milioni nne (4).** Vilevile, jumla ya vikundi vitatu vimepatiwa kamba **1,215** katika Mkoa wa Lindi kwenye vijiji vya Mchinga I (**405**), Mchinga II (**405)** na Kitumbikwera (**405**) zenye thamani ya **Shilingi 8,000,000/=** ili kuongeza uzalishaji wa mwani. Pia, Wizara imeendelea kushirikiana na majeshi ambapo imetoa jumla ya vifaranga **75,000** kwa 837 KJ Chita **(25,000)** na Gereza la Mollo –

Sumbawanga **(50,000)** ili kuyawezesha kuanza uzalishaji wa samaki na vifaranga.

**Huduma za Ugani wa Uvuvi**

**194.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kutoa mafunzo rejea kwa wavuvi na wakuzaji viumbe maji nchini ambapo jumla ya wadau **22,233** kutoka Halmashauri **20** nchini wamepatiwa mafunzo hayo. Halmashauri hizo ni: Sumbawanga, Nkasi, Tanganyika, Uvinza, Bukoba vijijini, Bukoba Manispaa, Muleba, Missenyi, Tanga Manispaa, Muheza, Mkinga, Pangani, Rorya, Musoma DC, Musoma MC, Kigoma MC, Kigoma DC, Mwanga, Simanjiro na Moshi DC. Aidha, Mafunzo hayo yanahusu uanzishwaji na uendeshaji wa vyama vya ushirika, matumizi sahihi ya zana ili kupunguza uvuvi haramu, ufugaji bora wa viumbe maji, uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi, udhibiti wa ugonjwa wa UKIMWI, kifua kikuu, madawa ya kulevya na magonjwa yasiyoambukiza.

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu Sera, Sheria, Kanuni za Sekta ya Uvuvi. Aidha, masuala kuhusu ukuzaji wa viumbe maji, uvuvi endelevu na uanzishwaji wa vya ushirika vya wavuvi na ukuzaji viumbe maji ambapo jumla ya wadau **47,731** walishiriki ambapo wadau **44,500** wamepatiwa elimu katika maonesho ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) na wadau **3,231** wamepata elimu katika maonesho ya siku ya chakula dunia.

**196.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa vyama vya ushirika vya wavuvi na wakuzaji viumbe maji katika Halmashauri mbalimbali ambapo jumla ya vyama vipya **25** vimeanzishwa na hivyo kufanya vyama vya ushirika vilivyotambuliwa hadi sasa

kufikia **172.** Aidha, injini saba (**7**) zimegawiwa kwa vyama saba (**7**) vya ushirika vya Kabwe (Nkasi), Mwamgongo (Kigoma Vijijini), Msangamkuu (Mtwara Vijijini), Mchinga (Lindi), Kilwa Kivinje (Kilwa), Igombe (Ilemela) na Chembaya (Buchosa).

**197.** ***Mheshimiwa Spika***, jumla ya vipindi **24** vya redio na **25** vya luninga vimeandaliwa na kurushwa hewani kuhusu usimamizi wa rasilimali za uvuvi na Ukuzaji viumbe maji ikijumuisha ufugaji wa samaki katika vizimba. Aidha, nakala **8,800** za machapisho yaliyohusu ufugaji bora wa samaki, athari za uvuvi haramu na uhifadhi bora wa mazao ya uvuvi yalichapishwa na kusambazwa kwa wadau wa uvuvi kwa lengo la kutoa elimu na uelewa kuhusu Sekta ya uvuvi.

**198.** ***Mheshimiwa Spika*,** Katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kutoa huduma za ugani nchini kwa kutumia Wagani **677** ikilinganishwa na hitaji la wagani **16,000** katika sekta ya uvuvi na hivyo kuwa na upungufu wa wagani **15,323**. Aidha, Wizara imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI ili kuajiri maafisa ugani wengi zaidi kwa lengo la kupunguza pengo hilo. Vilevile, Wizara imeendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuwekeza katika kutoa huduma za ugani ili kuongeza upatikanaji wa huduma hizo katika maeneo mbalimbali nchini.

**Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Uvuvi**
**Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania – TAFIRI**

**199**. ***Mheshimiwa Spika*,** Katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia TAFIRI imefanya tafiti mbalimbali kwenye maji ya asili na ukuzaji viumbe maji ambazo hutumika kuishauri Serikali kuweka mikakati ya uendelezaji na usimamizi wa Sekta ya Uvuvi nchini.

## Utafiti Bahari ya Hindi

**200.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu kwa kushirikiana na TAFIRI imefanya utafiti wa kutambua maeneo ya uvuvi kwa njia ya setelaiti. Aidha, TAFIRI inakamilisha programu tumizi (***mobile App*)** na lango la ujumbe wa simu (***SMS Gateway***) ili kuwawezesha wavuvi katika ukanda wa pwani kupokea taarifa za maeneo ya uvuvi yenye samaki wengi kupitia simu zao za kiganjani. Aidha, jumla ya wavuvi wadogo **3,360** wanufaika na mradi huu katika maeneo ya mwambao wa Tanzania ikiwemo Mafia, Nungwi, Wete, Bagamoyo na Kilwa. Teknolojia hii inasaidia wavuvi kupunguza gharama na muda wa kutafuta samaki kwa asilimia 50.

**201.** ***Mheshimiwa Spika***, TAFIRI imekamilisha utafiti wa kupunguza upotevu wa ubora wa samaki aina ya jodari na jamii zake kwa kutumia kichinjio cha samaki (*fish slaughter*). Aidha, wavuvi na wadau **220** kutoka Mikoa ya Dar es Salaam na Mtwara walifundishwa kuhusu matumizi ya teknolojia hiyo na kuongeza thamani ya samaki aina ya jodari na jamii zake na kupunguza kupotea kwa ubora wa samaki baada ya kuvunwa.

**202.** ***Mheshimiwa Spika***, TAFIRI kwa kushirikiana na Shirika la Sayansi-bahari Magharibi mwa Bahari ya Hindi (WIOMSA) inatekeleza utafiti wa majaribio wa uvuvi wa pweza kwa kutumia vyungu utakaowezesha kukamilika kwa mchakato wa kupata nembo ya kiikolojia kwa zao la pweza. Aidha, mafanikio ya utafiti huu yatawezesha kuondokana na uvuvi wa kutumia zana duni ya "mchokoo" isiyokuwa endelevu kwa uvuvi wa pweza na isiyokuwa rafiki kwa mazingira ya bahari hususan matumbawe.

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI inatekeleza mradi wa kuboresha teknolojia ya uzalishaji wa chakula hai cha samaki (viroboto maji-chumvi aina ya Artemia) kwa ajili ya ufugaji wa samaki kwa jamii ya pwani ya Bahari ya Hindi. Aidha, TAFIRI imetoa mafunzo kuhusu namna bora ya uzalishaji na uchakataji wa Artemia kwenye mashamba ya chumvi kwa wadau **16.**

**204.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha ujenzi wa Maabara ya Utafiti wa Uvuvi katika Kituo cha TAFIRI - Dar es Salaam na ukarabati wa jengo la Makao Makuu ambayo itaimarisha shughuli za tafiti za uvuvi na ukuzaji viumbe maji.

**Utafiti Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria**

**205.** ***Mheshimiwa Spika***, TAFIRI imekamilisha utafiti wa uendelezaji wa mnyororo wa thamani wa dagaa na migebuka kupitia awamu ya kwanza ya mradi wa *African Carribean and Pacific Countries* (*FISH4ACP*) katika mikoa na wilaya zilizopo katika mwambao wa Ziwa Tanganyika. Matokeo ya utafiti huu yamepelekea kutengenezwa kwa mpango wa uendelezaji wa mnyororo wa thamani ambapo katika kipindi cha miaka mitatu ijayo mradi utaboresha miundombinu ya uchakataji wa samaki, mialo na mifumo ya ubaridi na ugandishaji.

**206.** ***Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI inaendelea na utafiti wa wingi na mtawanyo wa samaki katika Ziwa Tanganyika. Pia, TAFIRI inaendelea na utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki katika Ziwa Victoria kwa kushirikiana na Taasisi ya Uvuvi ya Ziwa Victoria (LVFO) pamoja na nchi za Kenya na Uganda. Matokeo ya utafiti yatawezesha Serikali kuweka mipango na mikakati ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Tanganyika na Victoria.

**Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi – FETA**

**207.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu (Astashahada na Stashahada) na mfupi katika Tasnia ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji ili kupata wataalamu waliobobea katika fani husika ambao watakuwa chachu ya kuleta tija na kuongeza kasi ya maendeleo ya Taifa kupitia Uchumi wa Buluu. Katika kuwezesha wahitimu wa mafunzo husika kujiajiri na kufanya kazi kwa ufanisi, mafunzo hayo yametilia mkazo masuala ya ujasiriamali, ubunifu na kuongeza mafunzo kwa vitendo ili kuongeza ujuzi (*Competence Based Education*). 208. ***Mheshimiwa Spika,*** FETA imedahili jumla ya **wanafunzi 1,401** kwa masomo ya Astashahada na Stashahada katika Kampasi za Mbegani (Bagamoyo, Pwani), Nyegezi (Mwanza) na Kibirizi (Kigoma) sawa na ongezeko la **wanafunzi 144** ikilinganishwa na **wanafunzi 1,257** waliodahiliwa mwaka 2020/2021. Vilevile, FETA imeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi ili kuwajengea wananchi uelewa na kuwapa ujuzi wa kuzifikia fursa mbalimbali kupitia Uchumi wa Buluu.

**208.** ***Mheshimiwa Spika***, FETA imeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa washiriki mbalimbali ikiwemo wavuvi, wakuzaji viumbe maji, wachakataji na wanafunzi ili kuwajengea uelewa na kuwapa ujuzi wa kuzifikia fursa mbalimbali kupitia Uchumi wa Buluu. Mafunzo hayo yalihusu: Mbinu bora za uvuvi endelevu ili kuleta tija (**924**); Ufugaji wa samaki kibiashara ikijumuisha samaki aina ya Sato, Kambale na Mwatiko (**2,058**); Ufugaji wa Majongoo Bahari ambayo ni chanzo kikubwa cha mapato, kuanzia **Shilingi 80,000** mpaka **200,000** kwa kilo kulingana na ubora husika (**15**); Kuongeza thamani katika mazao ya uvuvi hasa samaki na mwani (**236**); mbinu za kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi baada ya kuvuliwa (post-harvest loss) (**389**);

uendeshaji salama wa vyombo katika maji (**140**); na uvuvi endelevu, utunzaji mazingira na vyanzo vya maji na ukuzaji viumbe katika maji kwa wanafunzi toka Vyuo Vikuu, Vyuo vya Kati, Sekondari na Msingi (**235**). 210.***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza weledi na ubunifu kwa wahitimu, FETA kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*National Council for Technical and Vocational Education Training* – NACTVET) limeendesha mafunzo kwa Wakufunzi **64** wa kampasi zote tano (Mbegani, Nyegezi, Kibirizi, Gabimori na Mikindani) kwa lengo la kuwajengea uwezo wa mfumo mpya wa elimu unaotilia mkazo mafunzo ya vitendo (*Competence Based Education Training* - CBET). Aidha, FETA imehuisha ithibati ya Kampasi ya Nyegezi (Mwanza) na mitaala mitatu (**3**) inayotolewa na Kampasi hiyo ili kuendana na wakati na kuongeza umahiri kwa wahitimu.

**Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

**211.** ***Mheshimwa Spika,*** Serikali imeidhinisha Muundo na mgawanyo wa majukumu ya Shirika la Uvuvi Tanzania ambapo hatua zinazoendelea ni teuzi mbalimbali za kujaza nafasi za watendaji wa shirika. Vilevile, Bodi ya TAFICO imeundwa kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Shirika na kutoa ushauri stahiki ili kuendeleza ustawi wa Shirika kwa maendeleo ya Taifa.

**212.** ***Mheshimwa Spika,*** Katika mwaka 2021/2022, Wizara imefanya ukarabati wa jengo la utawala ambalo linatumika kwa shughuli za ofisi. Aidha, kazi ya uhakiki mali za Shirika katika Mkoa wa Dar es Salaam imekamilika. Kwa sasa Ofisi ya Msajili wa Hazina (OTR) kwa kushirikiana na Wizara inaendelea na zoezi la kutambua na kuhakiki mali zilizopo mikoa ya Tanga, Pwani, Lindi, Mtwara, Mwanza, Kigoma, Mbeya, Njombe na Ruvuma.

**213.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Serikali iliahidi kununua meli mbili (**2**) za uvuvi na viambata vyake kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi inayofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) kwa ajili ya Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO). Katika utekelezaji wa programu hii kumekuwa na changamoto mbalimbali hasa kutokana na wafadhili kuchelewa kutoa fedha za mradi. Aidha, changamoto nyingine ni ugumu wa kutekeleza sharti la mkopo huu ambao ulitaka Serikali ya Tanzania kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii (ESIA) kwa miradi yote inayotekelezwa kupitia programu hii kwa SMT na SMZ kutumia fedha zake za ndani ikiwemo uvuvi katika bahari kuu na ununuzi wa meli. Majadiliano kuhusu utekelazaji wa masharti hayo umechukuwa muda mrefu hadi mwanzoni mwa mwaka huu ambapo muafaka umefikiwa kwamba ESIA ya uvuvi wa bahari kuu kwa SMT na SMZ itafanywa kwa kutumia fedha za mradi wa programu hiyo. Hivyo, hadi sasa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (SMT) na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (SMZ) zimekamisha hadidu za rejea za Mshauri Elekezi wa Kimataifa wa kufanya ESIA na kutangaza zabuni kimataifa na hatua iliyofikiwa ni kufanya uchambuzi wa zabuni hizo. Aidha, SMT na SMZ zimekamilisha msawazo wa meli zitakazonunuliwa na kuwasilisha kwa mfadhili wa programu. Vilevile, zoezi la kufanya ESIA kwa miradi mingine linaendelea kupitia wataalam wa ndani.

## MIRADI YA MAENDELEO YA SEKTA YA UVUVI

### Miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Programu ya ASDP II

**214.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara imekamilisha ujenzi na ukarabati wa mialo ya kupokelea samaki ya Kayenze (Ilemela), New Igombe (Ilemela) na Ihale (Busega). Aidha, ujenzi na ukarabati wa mialo ya Chifunfu (Sengerema), na Igabiro (Bukoba) unaendelea. Pia, ujenzi wa soko la samaki la Mbamba Bay (Nyasa)

umekamilika. Vilevile, ujenzi wa ofisi ya Kituo cha Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi cha Simiyu (Busega) upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji na ujenzi wa ofisi za Vituo vya Nyakaliro (Sengerema) na Sota (Rorya) unaendelea.

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kujenga na kukarabati vituo vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji vya Rubambagwe (Geita), Ruhila (Songea), Nyengedi (Lindi) na Ruvula (Mtwara). Aidha, majengo saba (**7**) (ya utawala, kitotoleshi, mgahawa, bweni, ghala, jengo la umeme, nyumba za watumishi) na ujenzi wa mabwawa tisa (**9**) katika Kituo cha Rubambagwe yapo katika hatua za mwisho. Vilevile, ukarabati na utanuzi wa vituo vya Ukuzaji Viumbe Maji vya Ruhila na Nyengedi unaendelea kwa kujenga vitotoleshi. Pia, ujenzi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari cha Ruvula na kituo cha kusambaza teknolojia za uvuvi na ukuzaji viumbe maji katika eneo la Nyakabindi Simiyu unaendelea.

**216.** ***Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka 2021/2022, Serikali imeanza kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko Mkoani Lindi. Aidha, Kampuni ya *China Harbour Engineering Co. Ltd* inatarajia kuanza ujenzi mwezi Mei mwishoni 2022 na ujenzi unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 24.

**217.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara inaendelea kuboresha mazingira ya utoaji elimu katika kampasi za FETA kwa kukarabati na kujenga kumbi mbili (**2**) za mihadhara (lecture theatres) zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **100** kwa kila ukumbi katika Kampasi ya Nyegezi (Mwanza), ujenzi wa maabara na kitotoleshi cha vifaranga vya samaki katika Kampasi ya Gabimori (Mara) na ujenzi wa maabara katika Kampasi ya Mikindani (Mtwara).

**Mradi wa Kikanda wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi SWIOFish (*South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth Project – SWIOFish*)**

**218.*Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) imekamilisha ujenzi wa ofisi tano (**5**) za BMUs katika Halmashauri za Pangani, Mkinga, Bagamoyo, Lindi Vijijini na Chalinze na kuzinunulia samani za ofisi na vifaa vya TEHAMA. Vilevile, imekamilisha ujenzi wa Maabara ya Utafiti wa Uvuvi katika Kituo cha TAFIRI Dar es Salaam na ukarabati wa jengo la Makao Makuu ya TAFIRI.

**Mradi wa Kuwezesha Kufanya Mapitio na Kuandaa Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi (The TCP/URT/3709 - *Technical Assistance to Develop Tanzania Fisheries Master Plan*)**

**219.** ***Mheshimiwa* Spika**, katika mwaka 2021/2022, Wizara imekamilisha kuandaa Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi (2021/2022– 2036/37) kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) wenye lengo la kutoa mwelekeo wa sekta ya uvuvi kwa kipindi cha miaka 15. Mpango huu umeandaliwa kwa kuzingatia dhana ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi na ukuzaji viumbe maji unaozingatia ikolojia na mazingira ambapo wadau mbalimbali walishirikishwa wakiwemo Wavuvi, Wakuzaji Viumbe Maji, Sekta Binafsi, Mashirika ya Kimataifa na Taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali.

**220.** ***Mheshimiwa* Spika**, Mpango Kabambe wa Uvuvi una malengo mahususi yafuatayo:-

(i) Kuimarisha usimamizi wa rasilimali za uvuvi ili kuwa na uvuvi endelevu unaozingatia dhana ya ikolojia na mazingira, sheria na kanuni;
(ii) Kuongeza upatikanaji wa ajira, usalama na uhakika wa chakula, uwezo wa uzalishaji, na kuwa sekta yenye ushindani inayochangia katika uchumi wa Taifa;
(iii) Kuimarisha ubia thabiti kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) katika Sekta ya Uvuvi;
(iv) Kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma za ugani wa Uvuvi;
(v) Kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora za viumbe maji na chakula cha samaki kwa gharama nafuu; na
(vi) Kuimarisha miundombinu ya kupokelea, kuchakata, kuhifadhi, kusindika na kuboresha biashara ya mazao ya uvuvi.

**MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**
**Maeneo ya Vipaumbele katika Mpango na Bajeti ya Mwaka 2022/2023**

**221**. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Sekta ya Uvuvi imepanga kutekeleza vipaumbele vinavyoendana na kufungamanisha Uchumi wa Buluu (*Blue Economy*) hususan matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi ikiwemo uvuvi kwenye maji baridi na maji chumvi. Vipaumbele hivyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha taasisi za sekta ya uvuvi kwa kukarabati na kujenga miundombinu, kuendesha TAFICO kwa ubia, kununua vifaa vya utafiti, mafunzo na ugani, pamoja na kuongeza upatikanaji wa wataalam.
(ii) Kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji kwa kujenga na kukarabati bandari ya uvuvi, mialo, mabwawa, masoko na vituo vya sekta ya uvuvi.

(iii) Kuimarisha uthibiti wa ubora, usalama na viwango vya mazao ya uvuvi kwa kununua vifaa vya kaguzi na chunguzi katika maabara za mazao ya uvuvi kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi;

(iv) Kuimarisha uwezo wa uzalishaji katika Bahari (maji ya kitaifa na Bahari Kuu) kwa kuweka mazingira wezeshi pamoja na kutoa mafunzo maalum ya uvuvi katika Bahari Kuu (EEZ) na kubadilishana uzoefu na nchi nyingine;

(v) Kuruhusu uvuvi wa kukokora kwa kutumia meli za uvuvi (mid-water trawling) katika eneo la bahari la maji ya kitaifa na bahari Kuu (EEZ);

(vi) Kuimarisha utafiti, huduma za ugani na mafunzo ya uvuvi;

(vii) Kuimarisha usimamizi na ulinzi shirikishi wa rasilimali za uvuvi kwa kutoa vitendea kazi na mafunzo kwa vituo na vikundi vya usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi na kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za uvuvi; na

(viii) Kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Mipango, Mikakati na Miongozo ya Sekta ya Uvuvi.

**Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2022/2023**

**221.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Fungu 64 inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi 60,000,000,000.** Vyanzo vikuu vya fedha hizo ni pamoja na; leseni za kusafirisha samaki na mazao yake nje ya nchi *(Export Licences*); leseni za uingizaji mazao ya uvuvi (*Import Licences*); mrabaha wa kuuza mazao ya uvuvi nje ya nchi (*Export Royalty*); mrabaha wa kuingiza mazao ya uvuvi nchini (*Import Royalty*), leseni za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu, tozo za huduma za maabara; leseni za uvuvi wa kambamiti, mauzo ya samaki na vifaranga vya

samaki na faini kwa makosa mbalimbali ya ukiukwaji wa sheria za uvuvi.

**Usimamizi wa Sera na Sheria**

**223.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara inatarajia kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kutafsiri Kanuni za Uvuvi zinazosimamiwa na Sekta ya Uvuvi kwa lugha ya Kiswahili ili kuwawezesha wadau mbalimbali kuwa na uelewa juu ya Kanuni hizo. Tafsiri hiyo itahusisha Kanuni ya Uvuvi ya mwaka 2009 (*Fisheries Regulation of 2009*); Kanuni ya Tozo za Maabara ya Uvuvi ya Mwaka 2012; Kanuni ya Uvuvi wa Bahari Kuu ya mwaka 2021 (*The Deep Sea Fisheries Management and Regulations of 2021*); Kanuni ya Tozo ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ya Mwaka 2009 (*Marine park (User Fees*) Regulations of 2009; Kanuni za Utafiti wa Uvuvi (Uvuvi na Ukuzaji Voiumbe Maji) yam waka 2020.

(ii) Kufanya maboresho ya Sheria ya Uvuvi Sura Na. 279 katika maeneo mbalimbali na kanuni zinazosimamiwa na Sekta ya Uvuvi kwa kuingiza marekebisho ya kanuni za uvuvi za mwaka 2009 na marekebisho yote ya mwaka 2018, 2019 na 2020.

(iii) Kutoa elimu juu ya sheria na kanuni zinazosimamiwa na Sekta ya Uvuvi kwa wadau mbalimbali.

**224.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, katika mwaka 2022/2023, Serikali itaendelea kusimamia Sera, Sheria na Kanuni za Sekta ya Uvuvi pamoja na kutoa elimu kwa wadau wa uvuvi na ukuzaji viumbe maji kupitia huduma za ugani, mafunzo rejea, semina, mikutano, elimu kwa umma (vipindi vya televisheni na redio) na maonesho ya Kitaifa.

**Usimamizi wa Takwimu za Uvuvi**

**225**. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kusimamia uvunaji endelevu wa rasilimali za uvuvi nchini, kuongeza wigo wa ukusanyaji takwimu kwa njia ya kieletroniki kwenye mabwawa ya Mtera na Nyumba ya Mungu, kufanya sensa za uvuvi katika Bwawa la Nyumba ya Mungu na Ziwa Nyasa. Aidha, Wizara itaendelea na ukusanyaji wa takwimu za uvuvi (*Catch Assessment Survey*) na ufuatiliaji katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Bahari ya Hindi na mabwawa ya Nyumba ya Mungu na Mtera. Pia, itaendelea kushirikiana na LVFO kutekeleza mikakati mbalimbali ya usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Victoria.

**Usimamizi na Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi**

**226.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara itafanya doria za siku kazi **8,400** ili kudhibiti uvuvi na biashara haramu katika maeneo ya maziwa makuu na Bahari ya Hindi. Aidha, Wizara itawezesha Kikosi Kazi cha Kudhibiti Uvuvi Haramu na Uharibifu wa Kimazingira (*National Multi-Agency Task Team*NMAT) kutekeleza majukumu yake katika maeneo ya maziwa makuu na Bahari ya Hindi. Vilevile, Wizara itafanya ufuatiliaji na tathmini kwenye utendaji wa vituo vya Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi na Uthibiti wa Ubora, Viwango na Masoko.

**227.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaimarisha Vikundi **200** vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za uvuvi (BMUs) na kuelimisha wavuvi wadogo **260** kuhusu usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi katika maziwa makuu na Bahari ya Hindi. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Asasi za Kiraia, Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi kuimarisha

usimamizi shirikishi na kuwawezesha wavuvi na wadau wa uvuvi.

**Uthibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi**

**228.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kufanya uthibiti wa ubora na usalama wa samaki na mazao yake ili kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara itawezesha Vituo **9** vya Uthibiti Ubora na Masoko wa mazao ya uvuvi na kufanya kaguzi za mara kwa mara **8,872**, na kaguzi **600** kwa kila robo mwaka. Pia, kwa kutambua umuhimu wa dagaa kama zao la kimkakati, Wizara itaandaa Mkakati wa Kuimarisha Mnyororo wa Thamani wa Samaki aina ya Dagaa katika Maziwa Makuu na Bahari ya Hindi.

**229.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Maabara ya Taifa ya Uvuvi, itaendelea kufanya upimaji wa samaki na mazao yake ili kuhakiki ubora na usalama unaokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Vilevile, Maabara itaendelea kuimarisha umahiri katika uchunguzi wa sampuli, miundombinu na kuongeza wigo wa upimaji hadi kufikia sampuli **5,100** zenye vipimo **14,700** vyenye thamani ya **Shilingi 810,000,000** ili kuhakiki ubora na usalama wa samaki na mazao yake.

**Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu**

**230.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Serikali itaendelea kuimarisha Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) na kuwezesha kutekeleza majukumu ya kulinda, kutunza na kusimamia mazalia ya samaki na mifumo ikolojia katika maeneo yaliyohifadhiwa. Aidha, MPRU itafanya doria za

sikukazi **900** ili kuhakikisha kuendelea kuwepo kwa rasilimali za uvuvi nchini na kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali hizo. Vilevile, MPRU itaendela kutoa mchango kwa jamii zinazopakana na maeneo yaliyohifadhiwa kwa kufadhili miradi ya maendeleo ikiwemo shule na vituo vya afya.

**231.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia MPRU itaendelea kutangaza maeneo yaliyohifadhiwa na vivutio vya utalii vilivyomo pamoja na kuboresha miundombinu ya utalii wa kiikolojia (eco-tourism) ikiwemo kununua boti mbili zenye vioo chini (glass bottom boat) ili kuongeza idadi ya watalii kutoka ndani na nje ya nchi na kuongeza mapato yatokanayo na utalii baharini. Aidha, MPRU itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa hoteli za kiikolojia za kitalii katika maeneo yaliyohifadhiwa ikiwemo visiwa vilivyopo Bahari ya Hindi kama vile Nyororo, Sinda, Kware, Kirui, Mbarakuni na Mbudya ili kuongeza idadi ya watalii na mapato ya Serikali.

**232.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itatekeleza mpango wa usimamizi mtambuka wa rasilimali za bahari zinazopatikana katika eneo la bahari na pwani linalopakana na nchi ya Kenya (*Transboundary Marine Conservation Area - TBCA*) pamoja na mpaka wa Tanzania na Msumbiji ili kuweza kusimamia kwa pamoja rasilimali hizo.

**233.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia MPRU itakamilisha mazungumzo na Kampuni ya Nungwi *Dreams Resort Limited* ambayo imeonyesha nia ya kuwekeza katika huduma za hoteli za kiikolojia katika maeneo tengefu ya visiwa vilivypo Bahari ya Hindi. Vilevile, Wizara itaendelea na maandalizi muhimu ya kupokea watalii wengi wanaotarijiwa kutembelea maeneo ya hifadhi za bahari na maeneo tengefu kutokana na mafanikio ya filamu ya Tanzania *Royal Tour*. Maandalizi

hayo ni pamoja na kufanya upembuzi yakinifu (*feasibility studies*) kwenye maeneo ya visiwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kitalii ikiwemo hoteli za kiikolojia, kujenga sehemu za malazi, kuweka miundombinu ya kuegesha boti (*mooring buoys*) pamoja na kuanzisha vituo vya kutolea taarifa kwa watumiaji wa rasilimali za bahari ikiwa ni pamoja na Watalii.

**Usimamizi wa Uvuvi katika Bahari Kuu**

**234.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu itatoa leseni **29** za uvuvi kwa meli za uvuvi wa Bahari Kuu kutoka ndani na nje ya nchi ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 2.1** zitakusanywa. Aidha, Mamlaka itaendelea na utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa kiwanda cha kuchakata samaki aina ya Jodari kwa kushirikiana na Mwekezaji Kampuni ya ALBACORA ya Hispania. Kiwanda hicho kitakapokamilika kwa awamu ya kwanza kitakuwa na uwezo wa kuchakata samaki takriban tani **20** kwa siku na vyumba vya ubaridi viwili (**2**) vyenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya samaki tani **2,400**. Pia, Mamlaka itaboresha mnyororo mzima wa thamani wa samaki aina ya jodari na jamii zake kwa kutoa mafunzo ya kuongeza thamani kwa wavuvi na wachuuzi wa samaki.

**235.** ***Mheshimiwa Spika*,** Mamlaka itaendelea kudhibiti uvuvi haramu kuendana na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Uvuvi Haramu, Usiotolewa Taarifa na Usiodhibitiwa kwa Kutumia Bandari (*Agrement on Port State Measures to Prevent, Deter and Eliminate Illegal, Unreported and Unregulated Fishing* - PSMA). Vilevile, Mamlaka itafanya upembuzi yakinifu wa matumizi ya ndege nyuki (*drone*) katika kufanya doria za anga katika bahari ili kupunguza gharama za uendeshaji wa doria za anga. Pia, Mamlaka itaratibu tafiti za uvuvi katika eneo la bahari kuu ili kuongeza

uwezo wa kusimamia na kuvutia uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu.

**236.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/2023, Wizara itakamilisha taratibu za kuorodhesha na kutangaza vivutio kwa wawekezaji wa ndani na nje katika uvuvi wa bahari kuu. Aidha, Serikali itakamilisha kutunga Sera ya Taifa ya Uvuvi wa Bahari Kuu ambayo inalenga kuvutia uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu, kuongeza biashara ya mazao ya uvuvi, kuimarisha ikolojia ya bahari na mazingira yake na kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuchakata na kusindika samaki ili nchi ifaidike na rasilimali za uvuvi kwenye bahari kuu.

**237.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi itaendelea kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za uvuvi wa bahari kuu kwa kuendesha doria za anga zenye masaa **72** na doria za kwenye maji. Aidha, Serikali itaboresha mifumo ya kielekitroniki ya kufuatilia mienendo ya meli zinazovua bahari kuu.

**Ukuzaji Viumbe Maji**

**238.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kuwezesha uendeshaji wa vituo vitano (**5**) vya ukuzaji viumbe maji (Ruhila – Ruvuma, Kingolwira – Morogoro, Mwamapuli – Tabora, Rubambagwe – Geita na Nyengedi – Lindi) ili viweze kuzalisha vifaranga **milioni 5** na kutoa mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji samaki. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia stahiki za uzalishaji wa mwani na uongezaji thamani katika ukanda wa pwani.

**239.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika mnyororo wa thamani wa ukuzaji viumbe maji hususan katika vitotoleshi

na chakula cha samaki ili kuzalisha vifaranga vya samaki **30,000,000** na tani **2,000** za chakula cha samaki. Aidha, Wizara itafanya tathmini na kupandikiza samaki katika mabwawa **20** katika mikoa ya Kilimanjaro, Dodoma, Singida, Shinyanga, Songwe, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Manyara, na Iringa ili kuongeza upatikanaji wa samaki.

**240.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itahamasisha matumizi ya teknolojia stahiki za uzalishaji wa viumbe maji na kuongeza thamani zao la mwani katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi. Aidha, Wizara itafanya tathmini na kaguzi zenye siku kazi **400** za uzingatiaji katika uanzishwaji wa miundombinu katika shughuli mbalimbali za mnyororo wa thamani wa ukuzaji viumbe maji ili kuhakikisha kuwa zinafuata sheria na pia huduma na bidhaa zinakidhi vigezo vya ubora.

**241.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itawezesha vikundi **15** vya wanawake, vijana na wenye ulemavu katika mikoa ya Tanga, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Dodoma, Mwanza na Kagera kupata pembejeo na zana za ukuzaji viumbe maji ili kuhamasisha ukuzaji viumbe maji. Aidha, Wizara itanunua maeneo kwa ajili ya upanuzi wa vituo vya ukuzaji viumbe maji Nyengedi – Lindi, Mwamapuli – Tabora na kuanzisha vituo vipya katika mwambao wa Ziwa Nyasa na Tanganyika**.**

**242.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea na zoezi la tathmini na kuanisha maeneo ya ufugaji wa samaki katika vizimba katika mikoa ya Simiyu, Mara na Geita. Pia, Serikali itaanza utekelezaji wa mpango wa kuwezesha vijana na vikundi mbalimbali kufuga samaki kwenye vizimba katika Ziwa Victoria kwa kuanzisha atamizi **265** zenye vizimba **1,060** vya ukuzaji viumbe maji kwa mikopo ya masharti nafuu kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB). Aidha, ili kuongeza kasi na tija katika utekelezaji wa mpango huo, Serikali

itaiwezesha TAFIRI kuanzisha atamizi maalum mbili za ukuzaji wa viumbe maji zenye vizimba **40**, kitotoleshi, mabwawa ya kukuzia samaki na mtambo wa kutengeneza chakula cha samaki katika Vituo vya TAFIRI vya Nyegezi (Mwanza) na Sota (Mara).

**243.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia ziara ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyofanya nchini Marekani hivi karibuni Kampuni ya Yona Trading Group (YTG) imeonyesha nia ya kuwekeza **Dola za Marekani milioni 70** katika tasnia ya ukuzaji viumbe maji. Fedha hizo zitatekeleza miradi ya ufugaji samaki kwenye vizimba na uvuvi katika Mkoa wa Kagera chini ya ushirikiano kati ya Wizara, Mkoa wa Kagera, Chuo Kikuu cha Nelson Mandela na Mfuko Kichocheo Maendeleo ya Kilimo Tanzania (*Tanzania Agricultural Catalytic Trust – TACT*).

**Huduma za Ugani wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji**

**244.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika mwaka 2022/2023, Wizara itahamasisha na kutoa mafunzo rejea kwa wadau wa uvuvi **25,000** kuhusu uvuvi endelevu na uendelezaji wa ukuzaji wa viumbe maji. Aidha, Wizara itawezesha vyama vya ushirika **83** vya wavuvi na wakuzaji viumbe maji kwa kuvipatia mafunzo na zana bora za uvuvi ikiwemo boti **250** ili kuwa na uzalishaji wenye tija. Vilevile, Wizara itaendelea kukusanya, kuchakata, kutafsiri, kusambaza matokeo ya tafiti na uhaulishaji wa teknolojia za uvuvi na ukuzaji viumbe maji kwa wadau wa Sekta ya Uvuvi. Pia, Wizara itaandaa na kurusha hewani vipindi **30** vya redio na **10** vya luninga kuhusu masuala ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji.

**245.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kushiriki na kuhamasisha wadau kushiriki katika maonesho ya Kitaifa na Kimataifa (Sabasaba, Nanenane, Siku ya Chakula Duniani na Siku ya Mvuvi Duniani) ili waweze kujifunza teknolojia

mbalimbali za uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji pamoja na kubadilishana uzoefu.

**246.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itawawezesha maafisa ugani wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji kwa kuwanunulia pikipiki **80**. Vilevile, itaendelea kuratibu utekelezaji wa Agenda ya Taifa ya Utafiti wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji (*National Fisheries and Aquaculture Research Agenda*) ya mwaka 2020-2025 na kuwezesha kufanya utafiti maalum (*commissioned research*) kwa ajili ya kupata majibu ya masuala ya kisera kwenye Sekta ya Uvuvi.

**Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Uvuvi Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania – TAFIRI**

**247.** ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara itawezesha Vituo vya TAFIRI vya Mwanza na Sota kufanya utafiti wa ufugaji viumbe maji kwa kuboresha kosafu za samaki aina ya sato, kuwezesha ufugaji wa samaki kwenye vizimba, na kuzalisha chakula bora cha samaki kwa kutumia malighafi zinazopatikana hapa nchini. Vilevile, TAFIRI itazalisha vifaranga **4,000,000** vya samaki na kuzalisha kiasi cha tani **36** za chakula bora cha samaki na kuzisambaza kwa wafugaji kwa bei nafuu ili kuchochea uzalishaji wa samaki kupitia tasnia ya ukuzaji viumbe maji.

**248.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia TAFIRI itafanya utafiti wa wingi na mtawanyiko wa samaki katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari (*Exclusive Economic Zone - EEZ*). Serikali imefanikiwa kupata meli kutoka shirika la uwekezaji la nchini Oman liitwalo *Oman Investment Authority* (OIA) chini ya *Al Wusta Fisheries Industry* (AWF) ambayo itashirikiana katika kufanya kazi hii muhimu kwa maendeleo ya Uchumi wa Buluu, na tayari Hati ya Maelewano (MoU) imesainiwa tarehe 12 Mei, 2022. Utafiti huu utaiwezesha Serikali kuweka mipango madhubuti ya uwekezaji katika uvuvi kwenye eneo la EEZ.

Vilevile, TAFIRI itaendelea kufanya tafiti za kujua wingi, aina na mtawanyiko wa samaki katika Maziwa Makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa). Tafiti hizi ni muhimu kwani zitasaidia Wizara kuweka misingi bora ya usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi katika maeneo haya.

**Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi – FETA**

**249.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi utaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili kuongeza wataalam watakaosaidia wananchi kunufaika na Uchumi wa Buluu. Aidha, FETA itadahili wanafunzi **1,600** wa mafunzo ya muda mrefu na wanafunzi **4,500** wa mafunzo ya muda mfupi katika kampasi zake zote. Ili kuendelea kutoa wahitimu wanaokidhi mahitaji ya soko ambao wana weledi, ubunifu, wanaoweza kujiajiri na kufanya kazi kwa ufanisi, Serikali itaendelea kuboresha na kuongeza miundombinu na vifaa vya kufundishia vya FETA katika Kampasi zake tano (**5**) za Mbegani, Nyegezi, Kibirizi, Gabimori na Mikindani.

**250.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo ya muda mfupi yatakayotolewa kwa makundi mbalimbali ya wadau wa sekta ya uvuvi wakiwemo wavuvi, wakuzaji viumbe maji, na wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi. Aidha, miongoni mwa aina ya mafunzo yatatolewa ni katika nyanja zifuatazo: unenepeshaji wa kaa, ukuzaji wa majongoo bahari na kambakochi, ukuzaji wa samaki katika vizimba na uongezaji wa thamani ya zao la mwani.

**Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

**251**. ***Mheshimwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Serikali itakamilisha zoezi la tathmini ya athari za kimazingira na kijamii katika ukanda wa bahari kuu kama sharti la kuwezesha uvuvi wa bahari kuu. Aidha, Serikali kupitia TAFICO itaendelea na

taratibu za ununuzi wa meli mbili (2) za uvuvi na vifaa vyake kwa ajili ya kuvua katika bahari kuu zitakazonunuliwa chini ya Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) inayofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD). Pia, Serikali itaendelea uboreshaji wa miundombinu ya TAFICO iliyopo Ras Mkwavi Dar es Salaam. Vilevile, Wizara itakamilisha zoezi la kutambua na kuhakiki mali za TAFICO zilizopo katika mikoa ya Tanga, Pwani, Lindi, Mtwara, Mwanza, Kigoma, Mbeya, Njombe na Ruvuma.

**MIRADI YA MAENDELEO YA SEKTA YA UVUVI**
**Miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Programu ya ASDP II**

**252.** ***Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka 2022/2023, Serikali itaendelea na ujenzi wa Bandari ya Uvuvi ambapo imetenga fedha za ndani **Shilingi bilioni 50** kwa ajili ya mradi huu. Aidha, Serikali itajenga mwalo wa Mchinga na masoko ya samaki Tunduma, Kigamboni na Mafia. Vilevile, Serikali itajenga madarasa matatu na maabara katika Kampasi ya Mikindani (Mtwara) na itakarabati Vituo vya Ukuzaji Viumbe Maji vya Ruhila (Ruvuma), Nyengedi (Lindi) na kujenga kituo cha Ruvula (Mtwara) na mashamba darasa mawili katika Manispaa za Songea na Mtwara.

**253.** ***Mheshimiwa* Spika,** Wizara itaboresha Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Kingolwira kwa kujenga kitotoleshi, mabwawa, visima na kununua mtambo wa kutengeneza chakula cha samaki. Vilevile, Wizara itafanya ujenzi soko la samaki Kipumbwi, kiwanda cha kutengeneza barafu na chumba cha ubaridi chenye uwezo wa kuhifadhi tani 40 za samaki katika Wilaya ya Pangani.

***Mradi wa Tanzania Scaling-up Sustainable Marine Fisheries and Aquaculture Management Project***

**254.** ***Mheshimiwa* Spika,** katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Mradi mpya wa "*Tanzania Scaling-up Sustainable Marine Fisheries and Aquaculture Management Project*" itafanya kazi zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa jengo la utawala la TAFIRI, ukumbi wa mikutano na makumbusho ya uvuvi katika Kituo cha TAFIRI, Kanda ya Dar es Salaam;
(ii) Ununuzi wa boti 70 za uvuvi katika Bahari ya Hindi zitakazotolewa kwa Vyama vya vya Ushirika na vikundi vya BMUs/CFMAs;
(iii) Kuendeleza na kukamilisha ujenzi wa majengo ya Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari, Kunduchi Dar es Salaam;
(iv) Kujenga mialo ya samaki katika maeneo ya Somanga (Kilwa), Sahare (Tanga), Kisiju (Mkuranga) na Bagamoyo (Bagamoyo);
(v) Kujenga chanja **10** za kukaushia mwani katika Halmashauri za Wilaya za Mtwara DC, Lindi DC, Lindi MC, Kilwa, Mkuranga, Mafia, Bagamoyo, Pangani, Tanga na Mkinga;
(vi) Kujenga maghala matano (**5**) ya kuhifadhi mwani katika Halmashauri za Mtwara DC, Kilwa, Lindi MC, Mafia, na Mkinga;
(vii) Kununua mashine tano (**5**) za kuchakata zao la mwani kwa Vyama vya Ushirika vya mwani katika Halmashauri za Mtwara DC, Lindi MC, Kilwa, Bagamoyo, na Mkinga; na
(viii) Kununua mtambo wa kutolea mafunzo ya mazoezi ya kuendesha Meli (3D *Full mission bridge fishing ship simulator*) katika Wakala wa Mafunzo ya Uvuvi (FETA) Mbegani, Bagamoyo.

**Mradi wa Kikanda wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi SWIOFish (*South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth Project – SWIOFish*)**

***255. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Mradi wa SWIOFish itaendelea na ujenzi wa Kituo cha Ukuzaji Viumbe Maji Bahari (*National Mariculture Resource Centre* – NMRC) kinachojengwa Kunduchi - Dar es Salaam na Ofisi ya Utawala ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) inayojengwa Wilayani Mafia.

**D. MASUALA MTAMBUKA KATIKA SEKTA ZA MIFUGO NA UVUVI**

**Dawati la Sekta Binafsi la Wizara**

***256. Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi la Wizara iliendelea kuwa kiungo kati ya Serikali na wadau mbalimbali wa sekta binafsi katika sekta za mifugo na uvuvi. Katika mwaka 2021/2022, Dawati hilo limesaidia kuunganisha kampuni zinazohitaji huduma ya mikopo hususan kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kwa kusaidia utayarishaji wa Maandiko ya Biashara (*Bankable Business Plans*) ambapo kampuni tatu (**3**) za sekta ya uvuvi na kampuni moja (**1**) sekta ya mifugo zimenufaika. Aidha, Dawati limewezesha kuongezeka kwa maombi ya mikopo ya wadau wa sekta za mifugo na uvuvi katika benki ya TADB

***257. Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2021/2022 Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilitoa mikopo ya moja kwa moja *(direct lending)* ya Shilingi **bilioni 1.9** ili kuwezesha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa; Shilingi **bilioni 2.8** kuwezesha ufugaji wa samaki; Shilingi **milioni 567** kuwezesha unenepeshaji wa ng'ombe na Shilingi **bilioni 8.6** kuwezesha ufugaji na utengenezaji wa chakula cha kuku. Hii inafanya jumla ya mikopo iliyotolewa kwenye sekta ya mifugo na

uvuvi kufikia Shilingi **bilioni 38.9** toka benki ilipoanza kazi zake za utoaji mikopo mwaka 2016

**258.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2021/2022 kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo *(Small holder Credit Guarantee Scheme)* Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilitoa dhamana ya jumla ya Shilingi **bilioni 5.34.** Kati ya hizo, kiasi cha Shilingi **milioni 162** kililitolewa kama dhamana kuwezesha miradi **18** ya ufugaji wa kuku; Shilingi **bilioni 5.078** kililitolewa kuwezesha miradi **21** ya ufugaji na unenepeshaji wa ng'ombe na mbuzi; **Shilingi milioni 26.5** kililitolewa kuwezesha miradi mitatu (**3**) ya ufugaji wa samaki na Shilingi **milioni 875.32** kililitolewa kuwezesha miradi minne (**4**) ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa. Hii inafanya jumla ya dhamana iliyotolewa kwenye sekta ya mifugo na uvuvi kufikia Shilingi **bilioni 9.18** toka mfuko ulipoanza kazi zake mwaka 2018.

**259.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2021/2022 TADB imeweza sekta za mifugo na uvuvi kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kushirikiana na *Bill and Melinda Gate Foundation* (BMGF) mradi wa ushirikiano kati ya wazalishaji na wasindikaji wa maziwa unaojulikana kama *Tanzania inclusive Producer Processor Partnership (Ti3P)* wenye lengo la kuongeza uzalishaji na usindikaji wa maziwa nchini umezinduliwa. Katika mradi huu wa miaka mitatu BMGF atatoa jumla ya ya dola za marekani million saba ili kusaidia uwekezaji katika sekta ya maziwa nchini katika maeneo ya Nyanda za Juu Kusini, Kaskazini, Mashariki na Kanda ya Ziwa. Mradi huu utavijengea uwezo vikundi vya wafugaji na viwanda vya kuchakata maziwa, kuwezesha upatikanaji wa pembejeo na mitamba na kuongeza uwezo wa viwanda kuchakata maziwa pamoja na kupanua soko la maziwa.

(ii) Ujenzi wa viwanda viwili vya uchakataji na usindikaji wa maziwa vilivyopo Kahama-Shinyanga na Tarime-Mara. Jumla ya Shilingi **bilioni 3.3** zimetolewa kwa viwanda hivi viwili vinavyokusanya maziwa kupitia vituo **15** vya kukusanyia maziwa vilivyoko katika mikoa sita (**6**) ya Geita, Kagera, Mara, Mwanza, Shinyanga na Simiyu;

(iii) Ufugaji wa samaki katika vizimba *(cage fish farming*) katika ziwa Victoria ambapo jumla ya **vizimba 70** vyenye thamani ya Shilingi **milioni 760** vimewezeshwa. Mradi huu utanufaisha wafugaji wa samaki **wapatao 70** waliopo katika mkoa ya Mwanza;

(iv) Upatikanaji wa **boti 30** za kuvulia zenye thamani ya Shilingi **320 milioni.** Mradi huu utawanufaisha wavuvi zaidi ya elfu **50** wanaofanya kazi zao katika ziwa Victoria; na

(v) Ufugaji wa samaki aina ya Sato kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya *Inpond Raceway System (IPRS)* katika wilaya ya Bagamoyo mkoni Pwani. Kiasi cha Shilingi **bilioni 2.4** kimetolewa kwa ajili ya kuwezesha mradi huo.

**260.** ***Mheshimiwa Spika,*** Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) imeidhinisha mikopo yenye thamani ya Shilingi **Milioni 989** kwa ajili ya vyama viwili (**2**) vya Wazalishaji wa Maziwa vya UTAMBUZI (Busokelo) ambao wamepata Shilingi **milioni 300** na Muungano wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Kilimanjaro (KDCJE) ambao wamepata Shilingi **milioni 689** kwa ajili ya kununua ng’ombe bora wa maziwa **290**. Vile vile, Dawati linaendelea kuhamasisha uundwaji wa vyama

vya ushirika vya mifugo na kuwaunganisha na taasisi mbalimbali kwa ajili ya uwezeshwaji wa mitaji na mafunzo.

**261.** ***Mheshimiwa Spika,*** takwimu za Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania zinaonyesha kwamba vyama vya ushirika vya ufugaji vimeongezeka kutoka vyama **117** mwaka 2020/2021 hadi kufikia **206** mwaka 2021/2022**.** Aidha, kwa upande wa vyama vya Ushirika vya Uvuvi vimeongezeka kutoka vyama **145** mwaka 2020/2021 hadi **172** mwaka 2021/2022, sawa na ongezeko la vyama **25**. Pia, Dawati la Sekta Binafsi limefanikiwa kutoa mafunzo kazi ya uandaaji wa maandiko ya kibiashara, ambapo vyama vya ushirika **18** vilivyopo Halmashauri za Pangani (**2**), Mkinga (**1**), Ilemela (**3**), Dodoma (**1**), Mafia (**1**), Bagamoyo (**3**), Ilala (**2**), Temeke (**2**), Kigamboni (**1**) na Nyamagana (**1**) vimeweza kuandaa maandiko mbalimbali yaliyowasilishwa TADB kwa ajili ya kuomba mikopo.

**262.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Dawati la Sekta Binafsi la Wizara ya Mifugo na Uvuvi wadau **218** wametembelewa na kupewa ushauri wa kitaalam; vikiwemo viwanda vya kuchakata samaki, wavuvi, wafugaji wa samaki katika vizimba na mabwawa. Pia, watalaam wa Dawati la Sekta Binafsi wametembelea na kukutana na wawekezaji wa sekta ya uvuvi ili kutoa ushauri wa kitaalam katika mikoa **14** ya Mbeya, Tanga, Mwanza, Simiyu, Geita, Kagera, Mara, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Kigoma, Dar es Salaam, Pwani na Lindi.

**263.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi kwa kushirikiana na Wakala wa Bima nchini (TIRA) limeratibu uanzishwaji wa Bima za Mifugo na Uvuvi ili kuwakomboa wafugaji, wavuvi na wafugaji viumbe maji na kurahisisha upatikanaji wa mikopo. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022, wanufaika wote wa mikopo iliyotolewa na Benki ya Kilimo kwenye sekta za mifugo na uvuvi walinufaika na bima hizo. Aidha, Dawati kwa kushirikiana na mashirika

mbalimbali ya Bima nchini linaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kujiunga na mfumo huo wa bima. Pia, ufuatiliaji wa bima kutoka taasisi nyingine kama vile Jubilee Insurance na NMB UMEBIMA umefanyika ili kuongeza tija kwenye uwekezaji wa sekta ya mifugo.

**264.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Dawati la Sekta Binafsi kwa kushirikiana na Wakala wa Bima nchini (TIRA) limeratibu uanzishwaji wa huduma ya Bima za Mifugo na Uvuvi. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022, vyama vya ushirika vitatu (**3**) vimejiunga na huduma ya bima ya mifugo ambapo jumla ya ng'ombe wa maziwa **162** wamekatiwa bima. Aidha, Dawati kwa kushirikiana na mashirika mbalimbali ya Bima nchini linaendelea kutoa elimu kwa wafugaji na wavuvi ili waweze kujiunga na huduma za bima.

**265.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2022/2023, Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi itaendelea kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta za mifugo na uvuvi kwa kuibua maeneo mapya ya uwekezaji; kuwajengea uwezo wafugaji na wavuvi kupitia vikundi na vyama vyao vya ushirika kufanya shughuli zao kibiashara; kufanya tafiti ya minyororo ya thamani na masoko; kuwaunganisha wawekezaji na taasisi za kifedha; na kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa uwekezaji katika Sekta za mifugo na uvuvi nchini.

**266.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Dawati la Sekta Binafsi itaendelea kuvijengea uwezo na kuviwezesha vyama vya ushirika kukuza na kuimarisha uzalishaji kwa kuviwezesha kupata mikopo yenye riba nafuu kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB). Vilevile, Wizara itahamasisha uwekezaji kwenye makundi maalumu ya vijana na kina mama kupitia ufugaji samaki kwenye vizimba, ufugaji wa samaki kwenye mabwawa, utengenezaji vyakula vya samaki, uvuvi na uchakataji wa

mazao ya kimkakati ya uvuvi, na ufugaji wa viumbe maji baharini.

**Utawala Bora, Jinsia na UKIMWI**

**267.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 vikao saba (**7**) vya Kamati ya Ajira vimefanyika vikiwemo vitatu (**3**) sekta ya mifugo na vinne (**4**) sekta ya uvuvi ambapo watumishi **32** wamethibitishwa kazini, watumishi **34** wamepandishwa vyeo, Watumishi **9** wamebadilishwa kada katika Sekta ya Mifugo. Aidha, watumishi wapya **20** wameajiriwa katika Sekta ya Mifugo na **72** katika Sekta ya Uvuvi. Vilevile, katika Sekta ya Uvuvi kulikuwa na ajira mpya **72**, uhamisho **33**, uteuzi nafasi (**2**), upandishwaji vyeo nafasi **15** na ubadilishwaji wa kada nafasi (**5**). Taarifa za watumishi **883** zimehakikiwa wakiwemo **503** wa sekta ya mifugo na **380** wa sekta ya uvuvi. Watumishi **20** waliostaafu wameondolewa kwenye Mfumo wa Taarifa za Utumishi na Mishahara. Pia usimamizi na ufuatiliaji wa utendaji wa kila siku kwa watumishi wa Wizara umefanyika. 268.***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza ufanisi kwenye utendaji kazi Wizara iwewawezesha watumishi **22** kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi. Watumishi nane (**8**) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu watumishi wanne (**4**). Aidha, watumishi **20** wamewezeshwa kupata mafunzo ya muda mfupi kuhusu masuala mbalimbali yakiwemo ukuzaji wa viumbe maji baharini, uendeshaji wa ofisi, usimamizi wa fedha na udereva ngazi ya juu.

**269.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 jumla ya watumishi **653** wa Wizara wakiwemo **503** wa sekta ya mifugo na **150** wa sekta ya uvuvi wameendelea kuhamasishwa kupima afya zao kupitia vikao na semina mbalimbali. Aidha, Wizara inaendelea kutoa posho kwa ajili ya kununua lishe bora kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

**270.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea na utekelezaji wa Afua za kujikinga na UVIKO–19 (Ugonjwa unaosababishwa na Virusi vya Korona – 2019) na uhamasishaji wa chanjo katika Sekta ya Uvuvi kwa kuwawezesha watumishi vifaa kinga kama vile Barakoa na vipukuzi (*sanitizer*). Pia, watumishi walipatiwa elimu juu namna bora za kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo.

**271.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Mkataba wa Huduma kwa Wateja umehuishwa kwa lengo la kuimarisha utoaji huduma kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa na kukubaliana kati ya Wizara na wadau.

**272.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kutekeleza Mfumo wa Wazi wa Upimaji wa Utendaji Kazi (OPRAS) ambapo watumishi 278 wamejaza fomu na kufanyiwa mapitio ya upimaji wa Utendaji kazi. Aidha, Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Utumishi na Mishahara (HCMIS) umeendelea kutumika kuingiza na kutunza taarifa za watumishi, kuhakiki mishahara ya watumishi kabla ya kulipa.

**273.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023 Wizara itaendelea kuhamasisha watumishi **933** kujikinga dhidi ya UVIKO – 19 na maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI na kupima afya zao kwa hiari wakiwemo **553** wa Sekta ya Mifugo na **380** wa sekta ya uvuvi; kuwezesha vikao vinne (**4**) vya Kamati ya Maadili; na kuwezesha utekelezaji wa Mifumo ya HCMIS, GSPP, Mikataba ya Utendaji Kazi na Mkataba wa Huduma kwa Mteja.

**274.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara imeomba kupatiwa nafasi mpya **90** katika Ikama ya Watumishi ambapo ajira mpya ni (**70**), uhamisho (**19**) na Uteuzi moja (**1**). Vilevile, vikao vinne vikiwemo viwili (**2**) vya Kamati ya Ajira na viwili (**2**) vya Baraza la Wafanyakazi vitawezeshwa, pia majukumu ya Vyama vya Wafanyakazi,

michezo, mabonanza, siku ya wanawake duniani na masuala ya jinsia yatawezeshwa.

**275.** ***Mheshimiwa Spika**,* Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa kwa kuelimisha watumishi 380 kuhusu miongozo, kanuni na Sheria za Utumishi wa Umma.

**276.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha watumishi wake kuendelea kupima afya zao na kujikinga dhidi ya magonjwa hayo pamoja na kutoa posho kwa ajili ya watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI. Pia, Wizara itaendelea kuchukua hatua stahiki za kujikinga dhidi ya maambukizi ya UVIKO-19 na magonjwa mengine ya kuambukiza.

**277.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaendelea kuhuisha taarifa za watumishi katika Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Utumishi na Mishahara (HCMIS), kuendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi na kuendelea kusimamia na kutekeleza Mfumo wa Wazi wa Upimaji wa Utendaji Kazi (OPRAS).

**Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

**278.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) imeanzisha jukwaa la kidigitali la mawasiliano kwa wafugaji liitwalo Ugani Kiganjani (*Digital Services Portfolio*) ambapo taarifa mbalimbali hupatikana. Taarifa hizo zinalenga kuwapa maarifa wafugaji na wavuvi kuhusu uzalishaji, magonjwa, chanjo na masoko ya mifugo na mazao yake. Aidha, mfugaji anaweza kuingia katika wavuti hiyo kwa njia ya simu janja, kompyuta au kishikwambi.

**279.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya *Trade Mark East Africa (TMEA)* imetengeneza mfumo wa kielektroniki wa utoaji vibali vya kusafirisha mifugo na mazao ya mifugo ndani na nje ya nchi uitwao *Mifugo Management Information System* (MIMIS). Mfumo huo utaboresha mazingira ya biashara za mifugo na mazao yake. Aidha, jumla ya miamala **162** imejengwa kwenye mfumo wa MIMIS na kuunganishwa na mfumo wa Serikali wa ukusanyaji wa mapato ya kodi, maduhuli, tozo na huduma (***Government electronic Payment Gateway*** - **GePG**). Pia, Taasisi ya TMEA katika kuimarisha ufanisi wa mfumo huo itaipatia Wizara vifaa vya kuwezesha usajili na utoaji wa vibali kwenye vituo vya utoaji wa huduma.

**280.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara kupitia Kitengo cha TEHAMA kimesanifu na kutengeneza *billing system* kwa ajili ya ukusanyaji maduhuli ya Serikali katika Sekta ya Uvuvi. Pia, Kitengo kimetengeneza *mobile application billing system* ambayo itasimikwa kwenye *Point on Sale* (PoS) za Sekta zinazotumika katika vituo vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi na Uthibiti wa Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi. Aidha, kukamilika kwa mifumo hii kutawezesha upatikanaji wa taarifa za makusanyo kwa wakati, kuokoa muda wa utoaji wa leseni za uvuvi na kuwezesha kutolewa hati ya madai maeneo ambayo hayana mtandao.

**281.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika usimamizi wa biashara za mifugo na mazao yake kwenye minada ya awali iliyo chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kupitia mfumo wa kieletroniki wa Tausi. Aidha, Wizara imeanza kutumia mfumo wa **e-Mrejesho** unaotoa fursa kwa wananchi au watumishi kuwasilisha mapendekezo, maoni, maswali na pongezi juu ya utendaji kazi wa Wizara.

**282.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutoa taarifa mbalimbali kwa wadau wa mifugo na uvuvi kupitia vipindi maalum vya radio na televisheni kwa kutayarisha na kurusha hewani jumla ya vipindi **47** vya televisheni na vipindi **84** vya redio (TBC 1, Channel Ten, TBC Taifa na Redio za Kijamii za CFM na Nyemo FM). Pia, Wizara imeandaa na kutoa taarifa kwenye magazeti mara **93**, majarida **11** ya mtandaoni, tovuti na mitandao ya kijamii mara **118**. Aidha, Wizara imepokea na kushughulikia malalamiko na maoni **104** kutoka kwa wananchi na wadau kwa njia ya simu na mitandao ya kijamii ya Wizara.

**283.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kusimamia, kutoa msaada wa kiufundi na kujenga uwezo kwenye mifumo ya kusimamia vibali vya kusafirisha mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi pamoja na kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo. Aidha, Wizara itatengeneza dirisha la kidigitali la usajili na uratibu wa huduma za ugani.

**284.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kutoa taarifa na maarifa kwa wananchi kuhusu shughuli mbalimbali za sekta ya mifugo na uvuvi kupitia vipindi maalum **52** vya redio, **52** vya televisheni, majarida **20** ya mtandaoni na magazeti. Pia, Wizara itaendelea kupokea na kushughulikia malalamiko na maoni kupitia mfumo uliohuishwa wa e-Mrejesho (www.emrejesho.gov.go.tz), simu na mitandao ya kijamii ya Wizara.

**285.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaimarisha mifumo mitatu (**3**) ya TEHAMA ya ufuatiliaji na tathimini wa Sekta ya Uvuvi (*M&E System*), utoaji taarifa za soko la mazao ya uvuvi na maeneo ya upatikanaji wa Samaki ukanda wa Pwani kwa wilaya tano (**5**) na kanzidata ya wafugaji wa viumbe maji na watengenezaji wa vyakula. Pia, Wizara itaendelea kusanifu na kutengeneza mfumo wa makusanyo wa

maduhuli na taarifa mbalimbali za Taasisi za Sekta ya Uvuvi za MPRU na FETA.

**Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi**

**285.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia hifadhi ya Mazingira ikiwa ni pamoja na kukabiliana na athari za Mabadiliko ya Tabianchi. Katika mwaka 2021/2022 Mafunzo yametolewa kwa wawezeshaji **72** kuhusu ufugaji unaozingatia hifadhi ya mazingira na kuhimili mabadiliko ya tabianchi *(Climate Smart Agriculture)* katika Halmashauri **12** za Mikoa ya Shinyanga (Shinyanga Manispaa, Shinyanga DC, Kishapu DC, Kahama Manispaa, Msalala DC, na Ushetu DC) na Geita (Geita TC, Geita DC, Nyang'wale DC, Mbogwe DC, Bukombe DC na Chato DC).

**286.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022 Wizara imefanya tathmini ya athari za Kimazingira na Kijamii (ESIA) katika utekelezaji wa Miradi miwili (**2)** ya maendeleo ili kuifanya Miradi hiyo iwe endelevu na kupunguza athari hasi katika Mazingira na jamii. Miradi hiyo ni ujenzi wa Minada ya Mifugo ya Mpakani ya Horohoro, Wilaya ya Mkinga - Tanga na Mtukula Wilaya ya Misenyi - Kagera. Tathmini hiyo ilibaini kuwa miradi hiyo imezingatia Sheria ya Menejimenti ya Mazingira SURA 191.

**287.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kusimamia uhifadhi na usimamizi wa mazingira ikiwa ni pamoja na ufanyaji wa tathimini ya athari za kimazingira na kijamii (Environmental and Social Impact Assesment – ESIA) kwenye miradi inayotekelezwa kupitia programu ya kuendeleza Kilimo na uvuvi (*Agriculture and Fisheries Development Programme – AFDP*) katika shughuli za uchimbaji wa visima (boreholes) na Ujenzi wa Mabwawa (Kingolwira na Mwamapuli), ujenzi wa soko la kuuzia samaki

(Kipumbwi-Pangani) na vichanja vya kuanikia dagaa (Bagamoyo).

**288.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Kitengo cha Mazingira imeendelea kutekeleza matakwa ya sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, ambapo imefanya jumla ya kaguzi **16** ili kuhakiki athari za kimazingira zinazosababishwa na shughuli za kibinadamu. Aidha, kaguzi nne (**4**) zimefanyika katika viwanda **11** vya kuchakata mazao ya uvuvi kutoka kanda ya Ziwa Victoria na kanda ya mashariki. Pia kaguzi **12** zimefanyika kwenye mabwawa **110** ya kufugia samaki na mashamba **13** ya ufugaji samaki kwenye vizimba na kutoa elimu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Vilevile, wadau **433** kutoka bwawa la Mtera na Nyumba ya Mungu walipatiwa elimu kuhusu kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na athari zitokanazo na shughuli za kibinadamu.

**289.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itawezesha mafunzo kwa wawezeshaji (ToTs) **192** kuhusu ufugaji unaohimili Mabadiliko ya Tabianchi *(Climate Smart Agriculture - CSA)* katika Mamlaka **32** za Serikali za Mitaa; kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii *(Environmental and Social Impacts Assessment – ESIA)*; na kufanya ukaguzi wa kimazingira *(Environmental Audit - EA)* katika miradi na miundombinu **10** ya Sekta ya Mifugo.

**290.** 290. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara itafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 katika shughuli za Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji kutoka ukanda wa Ziwa Victoria na maeneo ya Pwani ya Bahari ya Hindi. Aidha, Wizara itajenga uelewa kwa wadau **700** wa uvuvi juu ya hatua za kuchukua ili kupunguza athari za kimazingira zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi pamoja na shughuli za uvuvi na ukuzaji viumbe maji usiokuwa endelevu katika ukanda wa

Ziwa Tanganyika, Bwawa la Mtera na Nyumba ya Mungu, ikiwa ni pamoja na kuandaa mwongozo wa ufugaji Samaki unaozingatia uhifadhi wa Mazingira.

Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

**291.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa ili kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi. Kupitia ushirikiano huo, nchi yetu inapata fursa ya kushiriki na kutekeleza Sheria, Miongozo, Mikataba, Itifaki na Taratibu mbalimbali zenye lengo la kuimarisha sekta za mifugo na uvuvi hususan udhibiti wa magonjwa ya mifugo na samaki; biashara ya mifugo na uvuvi na mazao yake.

**292.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022 Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE) imeendelea kufuatilia viashiria vya Ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege unaoambukiza binadamu kutokana na kugusana na ndege wenye virusi vya ugonjwa huo. Ili kufanikisha ufuatiliaji huo jumla ya sampuli **640** zilichukuliwa kwenye maeneo hatarishi wanakotua ndege kutoka Bara la Ulaya na matokeo ya kimaabara yanaonesha mpaka sasa hakuna virusi vya ugonjwa huo hapa nchini.

**293.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara imeshiriki katika vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC ikiwemo kikao cha Kamati ya Sekta ya Biashara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kujadili masuala ya biashara ndani ya Jumuiya; pamoja na mkutano wa uzinduzi wa Taasisi ya Wanawake wa Afrika katika Rasilimali za Mifugo na Kilimo-Biashara (*African Women in Animal Resource Farming and Agribusiness-AWARFA*).

Kutokana na hizo juhudi za pamoja, sekta ya mifugo imeendelea kukua na kuimarika.

**294**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara imeshiriki kwenye mikutano na vikao mbalimbali vya Kikanda kama ifuatavyo:-

(i) Vikao vya IORA ambavyo vilipitia utekelezaji wa Mpango wa Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi katika Bahari ya Hindi, kubadilishana uzoefu wa usimamizi ili kuhakikisha nchi wanachama wa IORA zinanufaika na rasilimali za uvuvi kupitia Uchumi wa Buluu;
(ii) Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Nchi Wanachama wa LTA ambao ulijadili na kupitisha mkataba wa hatua za usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi na bonde la Ziwa Tanganyika;
(iii) Mikutano mbalimbali ya SADC ambapo Tanzania imeridhia na kusaini Mpango wa kuanzishwa kwa Kituo cha Kikanda cha Usimamizi na Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi na Kituo cha Pamoja cha Ukuzaji Viumbe Maji kwa nchi za Kusini mwa Afrika;
(iv) Mkutano wa OIE kupitia viwango vya afya ya viumbe maji na kurekebisha ili iweze kuendana na hali ya sasa ya biashara ya mazao ya uvuvi; na
(v) Mkutano wa IOTC ambao ulijadili mfumo wa mgawanyo wa mavuno (Quota system) ya samaki katika Bahari ya Hindi na kuwezesha nchi kupata mgawanyo mkubwa utakaotuwezesha kufaidika na rasilimali za uvuvi kupitia Uchumi wa Buluu.

**295.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Wizara imeshiriki katika vikao na mikutano ya LVFO ambapo Tanzania imeridhia kutumia Mwongozo wa Uchakataji na Biashara ya Mabondo utakaotumika na kusimamiwa na nchi za Afrika Mashariki; kuchangia **Dola za Kimarekani 600,000** kwa ajili ya kutekeleza Mkakati wa kuokoa Sangara

ujulikanao *Operation Save Nile Perch* (OSNP); na Mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Uvuvi (*Beach Management Unit Guidelines*)

**296.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi za Kikanda na Kimataifa katika sekta za mifugo na uvuvi ili kuimarisha mahusiano katika uwekezaji, masoko na tafiti.

***Uwekezaji Sekta ya Uvuvi***

**297.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Serikali imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi na maghala ya kuhifadhia na kugandisha mazao ya uvuvi ambapo hadi sasa kuna viwanda vikubwa vya kuchakata mazao ya uvuvi **16**, viwanda vya kati vitano (**5**) na viwanda vidogo **33** na maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi **90**. Vilevile, kuna viwanda **13** vya kuchakata mabondo ya Sangara na viwanda vitano (**5**) vya kutengeneza zana za uvuvi.

**298.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, uwekezaji mkubwa wenye thamani ya Shilingi **bilioni 11** umefanyika katika ufugaji samaki kibiashara na Kampuni za Tanlapia (Bagamoyo) na Tangreen (Magu). Uwekezaji huu utapokamilika, unatarajia kuzalisha zaidi ya tani **15,000** za samaki kwa mwaka. Aidha, Serikali imetia saini hati ya mashirikiano na Serikali ya Misri kupitia Kampuni ya Taifa ya Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji (*National Company for Fishing and Aquaculture*) ili kuwekeza pamoja na TAFICO. Mradi huo utajumuisha uzalishaji chakula cha samaki, ufugaji samaki, uchakataji wa mazao ya uvuvi, kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi na kuongeza thamani, kuwezesha uvunaji wa rasilimali za uvuvi katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari, kuwajengea uwezo watumishi wa sekta ya uvuvi na kuimarisha utafiti wa uvuvi na ukuzaji viumbe maji. Pia, Wizara itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuvutia

uwekezaji zaidi ikiwa ni pamoja na kutoa vibali bila gharama, kuwezesha misamaha ya kodi na ushuru kwa zana na pembejeo muhimu, na kuanisha maeneo mahsusi ya ufugaji samaki katika maziwa makubwa.

**299. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika tasnia ya Ukuzaji Viumbe Maji ambapo hadi tarehe 30 Aprili, 2022 kuna vizimba vya kufugia samaki **780**, mabwawa **31,407**, vitotoleshi **35** vya kuzalisha vifaranga vya samaki. Kuongezeka kwa vitotoleshi kutaongeza upatikanaji wa vifaranga vya samaki na hivyo kuongeza uzalishaji wa samaki.

**Gawio la Serikali katika Sekta ya Mifugo na Uvuvi**

**300**. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/2022, Taasisi, Bodi na Wakala zilizopo chini ya Wizara ambazo ni NARCO, LITA, TALIRI, TVLA, Bodi ya Nyama Tanzania, Bodi ya Maziwa Tanzania, TAFIRI, FETA na MPRU zimetoa gawio kwa Serikali lenye jumla ya Shilingi **152,203,000** kati ya fedha hizo, Shilingi **117,203,000** ni za Taasisi za Sekta ya Mifugo na **Shilingi 35,000,000** ni za taasisi za sekta ya uvuvi (**Kiambatisho Na. 20**) ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi **348,940,989.85** kilichotolewa mwaka 2020/2021. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha uwepo wa tija katika taasisi hizo ili kuweza kuchangia zaidi mapato katika mfuko wa Serikali.

**Michango katika Shughuli za Kijamii**

**301**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/2022, Taasisi, Bodi na Wakala zilizo chini ya Wizara zimetoa mchango wa Shilingi **202,468,500** ikilinganishwa na Shilingi **279,636,302.48** zilizotolewa mwaka 2020/2021. Michango hiyo ni kwa ajili ya kuchangia shughuli za maendeleo ya jamii ikiwemo uchanjaji mifugo, kutoa elimu kwa wafugaji, kuendesha elimu ya uhifadhi katika vijiji nje ya eneo la hifadhi

za Bahari na maeneo tengefu, kutoa misaada ya vifaa vya kielimu kwa shule za msingi katika Wilaya ya Mafia n.k.

**E HITIMISHO**

**302. *Mheshimiwa Spika*,** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2021/2022 yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, taasisi za fedha za Kitaifa na Kimataifa, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

**303. *Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kuzitambua na kuzishukuru nchi za Japan, Korea Kusini, Uingereza, Uholanzi, Ireland na Jamhuri ya Watu wa China kwa kuchangia katika maendeleo ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi. Naomba pia kutambua na kuzishukuru jumuiya za kikanda ambazo ni Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na Umoja wa Nchi za Ulaya (EU).

**304. *Mheshimiwa Spika***, Aidha, nazishukuru taasisi zinazoendelea kutuunga mkono kwa njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:- Taasisi ya Usimamizi wa Uvuvi Ziwa Victoria (*Lake Victoria Fisheries Organization-LVFO*), Mamlaka ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika (*Lake Tanganyika Authority-LTA*), Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi wa Jodari ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Tuna Commission-IOTC),* Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (*South West Indian Ocean Fisheries Commision- SWIOFC*), Umoja wa Nchi zilizoko katika Mwambao wa Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Rim Association* - IORA), *Western Indian Ocean Marine Science Association* (WIOMSA), Kamisheni ya

Usimamizi wa Nyangumi (*International Whaling Commission-IWC*), Kamisheni ya Bahari ya Hindi (*Indian Ocean Commission-IOC*), na Taasisi ya Wanawake wa Afrika katika Rasilimali za Mifugo na KilimoBiashara (*African Women in Animal Resource Farming and Agribusiness-AWARFA*).

**305.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitambue pia mchango wa mashirika mengine tunayoshirikiana nayo katika Sekta za Mifugo na Uvuvi ambayo ni: Shirika la Afya Duniani (WHO), Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (OIE), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Taasisi ya Rasilimali za Wanyama ya Umoja wa Afrika (AU-IBAR), Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Ireland (TEAGASC), Serikali ya Uholanzi na Serikali ya Japan kupitia Programu ya Uchumi na Maendeleo ya Jamii (*Economic and Social Development Programme – ESDP*), *Trade Mark East Africa* - TMEA na *Overseas Fishery Cooperation Foundation (OFCF) of Japan*.

**306.** ***Mheshimiwa Spika***, nazishukuru pia taasisi za Kifedha na Wadau wa Maendeleo kwa ushirikiano wao hasa, Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Korea (KOICA), Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Jamhuri ya Japan (JICA), Shirika la Misaada la Ireland (Irish Aid), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DfID), Shirika la Ushirikiano la Ujerumani (GIZ), Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden (SIDA); na mashirika ya IAEA, ILRI, CIAT kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**307.** ***Mheshimiwa Spika***, Aidha, napenda kuyashukuru Mashirika na Taasisi za hiari za *Bill and Melinda Gates*

*Foundation, World Wide Fund for Nature (WWF), Heifer Project Tanzania (HPT), Overseas Fisheries Cooperation Foundation of Japan (OFCF), Vetaid, Care International, Welcome Trust, World Vision, FARM Africa, Land O' Lakes, World Society for Protection of Animals (WSPA), Global Alliance for Livestock and Veterinary Medicine (GALVmed), Institute of Social Studies (ISS), International Land Coalition (ILC), Sea Sense, SmartFish, Marine Stewardship Council (MSC),* pamoja na Mashirika na Taasisi mbalimbali za humu nchini zinazojihusisha na uendelezaji wa Sekta za Mifugo na Uvuvi.

**308.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee nimpongeze na kumshukuru tena Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,** kwa namna anavyoliongoza Taifa letu na anavyotusimamia katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Nina imani kuwa ndani ya uongozi wake tutahakikisha kuwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 – 2025/2026 inatekelezwa kikamilifu hususan katika sekta za mifugo na uvuvi.

**309.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua nafasi hii tena kuwashukuru na kuwapongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia Kilimo, Mifugo na Maji kwa maoni yao na ushauri uliolenga kuboresha na kuimarisha sekta za mifugo na uvuvi. Pia niwashukuru wadau mbalimbali katika sekta za mifugo na uvuvi, wafugaji na wavuvi hususan wanaozingatia Sheria katika utendaji wa kazi zao kote nchini kwa kutunza, kuzalisha na kulinda rasilimali za Taifa. Napenda kuwaahidi kwamba Wizara yangu itaendelea kusimamia sekta za mifugo na uvuvi na kuunga mkono juhudi za wafugaji, wavuvi, wasindikaji na wafanyabiashara wa bidhaa za mifugo na uvuvi.

**310.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kurejea tena kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega,** Mbunge wa Jimbo la Mkuranga, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa ushauri na ushirikiano wake katika kusimamia majukumu ya Wizara. Aidha, natoa pia shukrani zangu kwa **Bw. Tixon Tuyangile Nzunda,** Katibu Mkuu (Mifugo) na **Dkt. Rashid Adam Tamatamah,** Katibu Mkuu (Uvuvi), Wakurugenzi pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi kwa kazi nzuri wanazozifanya.

**311.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Maswa Magharibi ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya jimbo na kitaifa, nataka niwahakikishie kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi na maarifa ili kuleta mabadiliko ya kimaendeleo katika jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

## F. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**312**. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/2023, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya Shilingi **168,248,787,000**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **52,047,604,000** ni kwa ajili ya Sekta ya Mifugo na Shilingi **116,201,183,000** kwa ajili ya Sekta ya Uvuvi. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo: -

### Fungu 99: Sekta ya Mifugo

**312.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaomba kutumia jumla ya Shilingi **52,047,604,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Mifugo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **35,036,988,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **17,010,616,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wake ni kama ifuatavyo:-

**(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida Shilingi 35,036,988,000**
- Mishahara **Shilingi 21,332,877,000**
- Matumizi Mengineyo (OC) **Shilingi 13,704,111,000**

**(ii) Fedha za Matumizi ya Maendeleo Shilingi 17,010,616,000**
- Fedha za Ndani, **Shilingi 16,871,741,000;** na
- Fedha za Nje **Shilingi 138,875,000.**

**Fungu 64: Sekta ya Uvuvi**

**314**. ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2022/2023, Wizara inaomba jumla ya Shilingi **116,201,183,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Uvuvi. Kati ya fedha hizo, Shilingi **23,349,646,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **92,851,537,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

(i) **Fedha za Matumizi ya Kawaida ni Shilingi 23,349,646,000.**
- Mishahara ni **Shilingi 12,719,235,000;** na
- Matumizi Mengineyo **(OC)** ni **Shilingi 10,630,411,000.00.**

(ii) **Fedha za Matumizi ya Maendeleo Shilingi 92,851,537,000**
- Fedha za Ndani: **Shilingi** 55,854,800,000; na
- Fedha za Nje: **Shilingi 36,996,737,000**

**315**. ***Mheshimiwa Spika*,** naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara:
www.mifugouvuvi.go.tz

**316**. ***Mheshimiwa Spika*,** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Mashimba Ndaki na hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamuita Mwenyekiti wa Kamati naomba nitambue wageni wa Mheshimiwa Mashimba Ndaki ambaye ni Waziri wetu wa Mifugo na Uvuvi, kwanza wapo wageni wa Kamati ya Siasa wakiongozwa na Mwenyekiti pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Maswa. Karibuni sana wageni wa Kamati ya Siasa kutoka huko Maswa. Pia tunao Madiwani kutoka Maswa pia wakiongozwa na Mwenyekiti. Karibuni sana na Madiwani wetu kutoka huko Maswa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa umuhimu wake naomba nimtambulishe Mke wake Mheshimiwa Mashimba Ndaki, ngoja nimuone kwanza yupo wapi ahaa yupo pale amesimama karibu sana wifi yetu, ndugu yetu tumesikia pongezi ambazo amezitoa kwako na shukrani kwa kweli Mungu aendelee kuwabariki hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ambao ni wafugaji 10 kutoka Chamakweza Chalinze, karibu sana wafugaji wetu kutoka Chamakweza huko Chalinze. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namuita Mwenyekiti wa Kilimo, Mifugo na Maji ili aweze kusoma taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pia watatoa maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 202/2023. Karibu sana Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ninayoiwasilisha imegawanyika katika sehemu kuu Nne ambazo ni: -

(i) Sehemu ya Kwanza ni maelezo ya jumla, inabainisha msingi na muundo wa Taarifa;

(ii) Sehemu ya Pili ni ufafanuzi na uchanganuzi inachambua matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji, upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati;

(iii) Sehemu ya Tatu inaripoti Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na uchambuzi; na

(iv) Sehemu ya Nne inamalizia taarifa kwa kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawanda ya uchambuzi wa taarifa. Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi inajumuisha Mafungu Mawili -Fungu 64 - Sekta ya Uvuvi na Fungu 99 - Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji wa makadirio ya mapato na matumizi yaliyochambuliwa, inaelezea maeneo makuu manne.

i) Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

ii) Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

iii) Utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi hadi kufikia mwezi Februari, 2022 na

iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi na tathmini ufafanuzi wa jumla sehemu hii inakusudia kujenga msingi wa ushauri wa Kamati kuhusiana na hoja ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Masuala yanayochambuliwa ni taarifa za utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi baada ya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo. Mambo yaliyochambuliwa ni pamoja na Ukusanyaji wa Maduhuli, Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya kawaida na Upatikanaji wa Fedha za kugharimia Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makusanyo ya Maduhuli kwa sekta ya Uvuvi katika mwaka wa fedha 2021/2022 Sekta ya Uvuvi - Fungu 64 ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni 40 kutokana na vyanzo mbalimbali kama vilivyobainishwa

kwenye taarifa ya Waziri. Hadi kufikia Februari, 2022 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi bilioni 14.1 ambayo ni sawa na asilimia 35 ya lengo la makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kiasi cha fedha kilichokusanywa kwa kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha ni chini ya asilimia 50 ya makadirio yaliyokusudiwa kukusanywa. Kutokana na muda mchache uliobaki kukamilisha mwaka wa fedha ni wazi kuwa hakuna matumaini ya kukamilisha makusanyo ya kiasi cha shilingi bilioni 25.9 zilizosalia. Kwa msingi huo, Kamati inasisitiza Serikali kuona umuhimu wa kupanga malengo ya makusanyo yanayoendana na uwezo wa makusanyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli kwa sekta ya mifugo. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 sekta ya Mifugo – Fungu 99 ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi Bilioni 50 zitakazotokana na vyanzo mbalimbali vya mapato kama ilivyoainishwa kwenye hotuba ya Waziri. Hadi kufikia Februari, 2022 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi bilioni 18.4 sawa na asilimia 36.88 ya lengo la makusanyo ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa wakati wa kipindi kama hiki walipaswa wawe wamefikia lengo la asilimia 75 ya lengo lililokusudiwa kulingana na makadirio yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kupungua kwa Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali kwa mwaka unaomalizika kumetokana na sababu mbalimbali zikiwemo janga la ugonjwa wa UVIKO -19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitekeleza miradi ya Maendeleo iliyotengewa jumla ya shilingi bilioni 116.0 kwa mchanganuo ufuatao kama Waziri alivyosema. Kwa mfano,

Sekta ya Uvuvi Fungu Na. 64 lilitengewa shilingi bilioni 99.1na Sekta ya Mifugo Fungu Na. 99 lilitengewa shilingi bilioni 16.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam kwa kukagua miradi iliyokuwa vipaumbele vya Wizara. Kwa sababu ya ufinyu wa muda, Kamati ilikagua miradi miwili inayotekelezwa na Sekta ya Mifugo, na mradi mwingine unaotekelezwa na Sekta ya Uvuvi kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa bwawa la kuvuna na kuhifadhi maji unaotekelezwa eneo la Chamakweza katika Wilaya ya Chalinze Mkoani Pwani; na

(ii) Ukarabati wa Makao Makuu ya Shirika la Uvuvi Tanzania *(TAFICO)* uliyoko Jiji la Dar es Salaam katika Wilaya ya Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha na kukaguliwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa ujenzi wa Bwawa la Chamakweza, unalenga kuhudumia wafugaji wa vijiji vitatu vyenye jumla ya mifugo 104,849 kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa maji kwa ajili ya kunywesha mifugo. Aidha, kukamilika kwa mradi huu kunalenga kuondoa migogoro ya muda mrefu baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi hususan wakati wa kiangazi. Taarifa ya Wizara ilionesha utekelezaji wa mradi huu umekamilika kwa asilimia 100 na kugharimu Shilingi milioni 671.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa ukarabati wa Makao Makuu ya Shirika la Uvuvi Tanzania *(TAFICO)* unalenga kutimiza azma ya Serikali ya kufufua Shirika hili kwa ajili ya kuboresha shughuli za uvuvi wa bahari kuu. Utekelezaji wa

mradi huu unagharimu Shilingi milioni 172.8 na ulitarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2022. Taarifa ya Wizara ilieleza kuwa utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 82.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kwamba:-

(i) Hakuna utaratibu rasmi uliowekwa wa namna bora ya ushirikishwaji jamii katika miradi inayojengwa na wakandarasi, tofauti na ile inayojengwa kwa utaratibu wa *force account* na hivyo kupelekea changamoto katika utekelezaji wa baadhi ya miradi. Kwa mfano, ujenzi wa Bwawa la Chamakweza;

(ii) Gharama zilizotumika kutekeleza ujenzi wa Bwawa la Chamakweza haziendani na thamani ya fedha iliyotumika kwenye utekelezaji wa mradi huu;

(iii) Bajeti inayoidhinishwa na kutolewa kuboresha Shirika la Uvuvi Tanzania *(TAFICO)* haikidhi mahitaji ya majukumu ya Shirika hilo katika kuwezesha nchi yetu kunufaika na uvuvi wa ukanda wa uchumi wa bahari na bahari kuu;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Sekta ya Uvuvi ilitengewa jumla ya Shilingi bilioni 161.3 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama ilivyofafanuliwa kwenye Kielelezo Na.1 kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa:-

(i) Fedha ya Matumizi ya Kawaida iliyopokelewa hadi kufikia mwezi Februari, 2022 ni asilimia 69 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida unaonesha mwenendo wa

kuridhisha na hivyo kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara; na

(ii) Fedha za Matumizi ya Maendeleo zinazotengwa ni kidogo ikilinganishwa na rasilimali nyingi zilizopo kwenye eneo la bahari, maziwa na mito. Pamoja na kiasi kidogo kilichotengwa, bado kiasi kilichoidhinishwa na Bunge na kutolewa na Serikali ni kidogo ambapo hadi mwezi Februari, 2022 Fedha za Maendeleo zilizotolewa zilikuwa asilimia 3.3 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa:-

(i) Jumla ya kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia Februari, 2022 ni asilimia 53 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, jambo ambalo siyo la mwenendo wa kuridhisha katika upatikanaji wa fedha; na

(ii) Fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni asilimia 32 tu, kiasi ambacho ni pungufu ya asilimia 68.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na takwimu hizo, Kamati inashauri utoaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida ni vyema ukaendana na utoaji wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo, kwa kuwa fedha za matumizi ya kawaida zinatengwa pamoja na mambo mengine, kuwezesha watendaji kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hivyo, kama hakuna uwiano wa utoaji fedha, upo uwezekano wa watendaji kupata ujira pasipo kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Kwa mfano, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida hadi kufikia mwezi Februari, 2022 ulikuwa ni asilimia 65 wakati upatikanaji wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo kwa kipindi hicho mwaka uliyopita ulifikia asilimia 32 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilishauri kuhusu mambo mbalimbali. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya ushauri. Mfano wa ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kuhusu kuongeza uwekezaji kwenye Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za utekelezaji zilionesha Serikali imeongeza bajeti ya Sekta ya Mifugo kutoka Shilingi bilioni 38.9 mwaka 2020/2021 hadi Shilingi bilioni 47.8 mwaka 2021/2022. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imeendelea kuongeza bajeti na kufikia shilingi bilioni 92.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ushauri ambao haujatekelezwa kikamilifu ulihusu Serikali kuharakisha ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko Mkoani Lindi. Kamati ilitoa ushauri huo kwa kuzingatia kuwa ujenzi wa bandari ya uvuvi ndiyo njia pekee itakayowezesha nchi yetu kunufaika na Uchumi wa Bluu kwa kutumia kikamilifu rasilimali zilizopo kwenye Bahari, Maziwa, Mito, Mabwawa na vyanzo vingine vya maji ili kuwezesha rasilimali hizo kuchangia ukuaji wa uchumi. Kamati inashauri kuwa bado kuna umuhimu wa kuendelea kuzingatia ushauri ambao haujafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekadiriwa kukusanya maduhuli na kutengewa Bajeti ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha na bajeti inayomalizika. Uchambuzi wa maduhuli na makadirio ya matumizi hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Shilingi bilioni 120 zinakadiriwa kukusanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 20 ikilinganishwa na lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Mchanganuo wa makadirio hayo unaoneshwa katika Kielelezo Na. 3 kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi umeonesha kwamba:-

(i) Makadirio ya Maduhuli ya Sekta ya Mifugo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yameongezeka kwa asilimia 23.33 ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022; na

(ii) Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Sekta ya Uvuvi imeongezewa ukusanyaji wa madhuhuli kwa zaidi ya asilimia 66.66 wakati mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa kipindi cha robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti ulifikia asilimia 35 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio ya Kamati kwamba, kutokana na ongezeko la bajeti kwenye sekta zote mbili, lengo la makusanyo litafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Mifugo na Uvuvi wanakadiria kutumia

shilingi bilioni 86 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Uchambuzi umeonesha kuwa, bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuna ongezeko la bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa asilimia 132.15 ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zinadhihirisha kuwa uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Mifugo na Uvuvi zimeongezewa msukumo katika bajeti. Hata hivyo, kiasi cha bajeti kilichoongezwa ni kidogo ikilinganishwa na majukumu makubwa iliyonayo Wizara katika kuhakikisha tija inaongezeka kwa kuimarisha Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bajeti ya Matumizi ya Kawaida, Kamati imejiridhisha kuwa makadirio ya sehemu hii ya bajeti yanaendana na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Jambo la muhimu ni Serikali kuhakikisha upatikanaji wa fedha unatolewa kulingana na mahitaji ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Makadirio ya Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo yamefafanuliwa kwenye Kielelezo Na. 5 kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati. Uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba:-

(a) Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeongezeka kwa asilimia 58.5 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa mwaka wa fedha 2021/2022;

(b) Tafsiri ya ongezeko hili ni kuwa Sekta ya Mifugo itapunguza tatizo la upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo na hivyo kupunguza vifo vya mifugo kutokana na uhaba wa maji na malisho;

(c) Kwa upande wa Sekta ya Uvuvi, inatarajiwa kuongezeka kwa upatikanaji wa samaki kutokana na

kuongezeka kwa uwezo na uelewa wa wavuvi kuhusu ukuzaji viumbe kwenye maji;

(d) Ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu, kwa mwaka inahitaji Shilingi bilioni 950 ikilinganishwa na bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambayo ni Shilingi 268.15; na

(e) Kiasi cha fedha kilichotengwa kwa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni sawa na asilimia 0.62 ya Bajeti ya Taifa ambayo ni Shilingi trilioni 51.63.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya tatu ni maoni na ushauri wa Kamati. Kutokana na uchambuzi wa Kamati, ushauri kuhusu maombi ya fedha kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sehemu kubwa ya ongezeko la bajeti limetokana na fedha za ndani na mikopo kutoka nje, Kamati inashauri Wizara kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kwa kuwa lengo la Serikali ni kuongeza tija katika uzalishaji, ni muhimu kwa Watumishi wa Serikali kuzingatia nidhamu kwenye matumizi ya fedha kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kujielekeza kwenye mipango inayotekelezeka ili kuleta maendeleo kwa wafugaji na wavuvi;

(b) Upo umuhimu wa Wizara ya Fedha kuipelekea Wizara nyongeza ya fedha za bajeti mapema; na

(c) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara uzingatie umuhimu wa kutatua changamoto zinazoikabili nchi yetu na dunia kwa ujumla ikiwemo tatizo la uhaba wa chakula, matatizo ya mabadiliko ya tabia nchi na ukosefu wa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo:-

(i) Kuongeza bajeti kwa ajili ya maeneo ya malisho ili kusaidia upatikanaji wa uhakika wa chakula cha mifugo na hivyo kuongeza thamani ya mifugo yetu kwenye ushindani wa soko;

(ii) Kutokana na umuhimu wa vitalu katika kuzalisha mifugo bora, zoezi la kupangisha vitalu lizingatie manufaa ya kufuga kisasa badala ya kuchunga. Aidha, Kamati inashauri Wizara ifanyie kazi changamoto za ugawaji vitalu;

(iii) Pamoja na kwamba sehemu ya nyongeza ya bajeti itaelekezwa kwenye ukarabati wa malambo, Kamati inashauri kiasi kikubwa cha fedha hiyo kielekezwe kwenye ujenzi wa malambo mapya hususan kwenye maeneo ya wafugaji yanayoathirika na ukame mara kwa mara;

(iv) Ili kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji inayotokana na wafugaji kuhamahama kutafuta malisho, Kamati inashauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi kushirikiana na Wizara ya Ardhi, kuandaa utaratibu wa kumilikisha wafugaji ardhi; na

(v) Ili kulinda, kuimarisha na kuvisaidia viwanda vya ndani kuongeza uzalishaji wa maziwa na kushindana kikamilifu kwenye soko, Kamati inashauri Serikali iondoe tozo kwenye uzalishaji wa maziwa yanayozalishwa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi:-

(i) Mikopo ya vijana inayotolewa na Halmashauri itumike kuwapatia vijana mikopo na elimu kuhusu mbinu bora

za ufugaji samaki kwenye vizimba na mabwawa ili kupunguza utegemezi kwenye uvuvi wa maji ya asili;

(ii) Kuhamasisha sekta binafsi kushiriki kikamilifu kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao ya samaki ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufanyia biashara;

(iii) Biashara ya Mwani inakua kwa kasi na inatekelezwa na wanawake, Wizara iandae mpango wa kuwaelimisha na kuwawezesha wakulima wa Mwani mbinu bora za kilimo hicho; *(Makofi)*

(iv) Ili kuimarisha biashara ya samaki nje ya nchi, viwanja vya ndege vijenge miundombinu ya kupozea (*cold rooms facilities)* kwa ajili ya kuhifadhi mazao ya samaki;

(v) Vituo vya barafu vijengwe kwenye maeneo yote yanayozalisha samaki kwa wingi; na

(vi) Wizara ihakikishe kwamba viwanda vya kuchakata mazao ya samaki vinavyojengwa nchini vinapata malighafi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kama inavyofahamika kama Sekta za Mifugo na Uvuvi ni Sekta za uzalishaji ambazo ni muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa na kuleta msukumo kwenye ukuzaji wa sekta ya viwanda, ukuaji wa sekta hizi una umuhimu mkubwa katika kuimarisha biashara za mazao haya ndani na nje ya nchi na kufanikisha utelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025), Malengo ya Maendeleo Endelevu na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020 - 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo ilichangia asilimia saba ya pato la Taifa na kwa ujumla nikichukulia

Sekta ya Kilimo ni Mifugo ikiwepo, Sekta ya Mifugo imechangia asilimia 40 ya pato hilo, inayotokana na uzalishaji wa nyama ya ng`ombe, tasnia ya maziwa na uzalishaji wa mbuzi, kondoo na kuku. Vilevile, Sekta ya Uvuvi inachangia takribani asilimia 1.8 ya pato la Taifa. Inatoa ajira kwa Watanzania takribani milioni 4.5, na kuchangia fedha za kigeni, kipato, chakula na lishe na huchangia asilimia 30 ya protini inayotokana na mazao ya wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi endapo itapewa fedha kwa ajili kufanya uwekezaji kikamilifu na kutumia vizuri rasilimali nyingi zilizopo nchini, Wizara hii ina uwezo wa kufanikisha mipango mbalimbali ya Serikali na kutengeneza faida ikilinganishwa na gharama zitakazowekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kutokana na umuhimu wao natamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutambua umuhimu wa sekta hizi na kuziongezea bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mashimba Ndaki (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Abdallah Ulega (Mb) kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao mmechangia kwa sehemu kubwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wakiongozwa na Katibu Mkuu - Mifugo Ndugu Tixon Nzunda na Katibu Mkuu – Uvuvi Ndugu Rashidi Tamatama kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati. Shukrani za Kamati ziwaendee pia Watendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa mipango madhubuti ya kuhakikisha Sekta za Mifugo na Uvuvi zinakuwa endelevu na zenye tija, kuchangia uchumi wa viwanda, kuinua kipato cha wafugaji na wavuvi pamoja na kuchaingia kikamilifu katika malighafi ya viwanda na hivyo kuinua pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nakushukuru wewe binafsi pamoja namshukuru pia Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge wote kwa namna mnavyotuongoza na kuliwezesha Bunge letu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, namshukuru pia Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge Ndugu Dickson Bisile, Makatibu wa Kamati Ndugu Rachel Nyega na Ndugu Eunice Shirima, wakisaidiwa na Ndugu Waziri Kizingiti, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**25 MEI, 2022**

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni,2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kufuatilia taarifa hii ipasavyo, naomba kutambulisha sehemu **NNE** za Taarifa hii ambazo ni: -

(i) Sehemu ya **Kwanza**: maelezo ya jumla, inabainisha msingi na muundo wa Taarifa;

(ii) Sehemu ya **Pili**: ufafanuzi na uchanganuzi inachambua matokeo ya Ukaguzi wa miradi ya Maendeleo, Taarifa za Utekelezaji, Upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati;

(iii) Sehemu ya **Tatu**: inaripoti Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na uchambuzi; na

(iv) Sehemu ya **Nne**: inahitimisha na kulishauri Bunge kuhusu hoja ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi aliyoitoa mapema leo.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni Masharti ya Kanuni za Bunge. Kifungu cha 6 (7)(a) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa za Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, yalichambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti hayo, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Katika hatua hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na matokeo yake ni taarifa hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi inajumuisha mafungu mawili yaani: Fungu 64 (Sekta ya Uvuvi) na Fungu 99 (Sekta ya Mifugo).

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi yaliyochambuliwa, inagusa maeneo makuu yafuatayo: -

i) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
ii) Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;
iii) Utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi hadi kufikia mwezi Februari, 2022; na
iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, maswala yaliyobainishwa hapo juu yanajitokeza katika Taarifa hii. Kwa muktadha huo, naliomba Bunge lako Tukufu lifuatilie kwa kina mtiririko wa Taarifa hii ili kupata egemeo la ushauri unaotolewa na Kamati.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inakusudia kujenga msingi wa ushauri wa Kamati kuhusiana na Hoja ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Masuala yanayochambuliwa ni Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

### 2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika**, ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi baada ya ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo.

Mambo yaliyochambuliwa ni pamoja na Ukusanyaji wa Maduhuli, Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya Kawaida na Upatikanaji wa Fedha za

kugharimia Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**2.2.1 Makusanyo ya Maduhuli kwa Sekta ya Uvuvi**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 **Sekta ya Uvuvi - Fungu 64** ilipanga kukusanya jumla ya **shilingi 40,000,000,000.00** kutokana vyanzo mbalimbali kama vilivyobainishwa kwenye Taarifa ya Waziri. Hadi kufikia Februari,2022 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi 14,071,066,990.37**, ambayo ni sawa na **asilimia 35** ya lengo la makusanyo.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kiasi cha fedha kilichokusanywa kwa kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha ni chini ya **asilimia 50** ya makadirio yaliyokusudiwa kukusanywa. Kutokana na muda mchache uliobaki kukamilisha mwaka wa fedha, ni wazi kuwa hakuna matumaini ya kukamilisha makusanyo ya kiasi cha **shilingi 25,928,933,010.00** zilizosalia. Kwa msingi huo, Kamati inasisitiza Serikali kuona umuhimu wa kupanga malengo ya makusanyo yanayoendana na uwezo wa makusanyo.

**2.2.2 Makusanyo ya Maduhuli kwa Sekta ya Mifugo**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 **Sekta ya Mifugo – Fungu 99** ilipangiwa kukusanya jumla ya **shilingi 50,000,000,000.00** zitakazotokana na vyanzo mbalimbali vya mapato kama vilivyoainishwa kwenye hotuba ya Waziri. Hadi kufikia Februari, 2022 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **18,441,137,310.47** sawa na **asilimia 36.88** ya lengo la makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa wakati wa kipindi kama hiki walipaswa wawe wamefikia lengo la **asilimia 75** ya lengo lililokusudiwa, kulingana na makadirio yaliyowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Kupungua kwa Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali kwa

mwaka unaomalizika kumetokana na sababu mbalimbali ikiwemo janga la ugonjwa wa UVIKO -19.

### 2.2.3 Upatikanaji wa fedha na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilitekeleza Miradi ya Maendeleo iliyotengewa jumla ya **shilingi 116,016,107,000.00** kwa mchanganuo ufuatao**: -**

**a)** Sekta ya Uvuvi (Fungu 64) ilitengewa **shilingi** 99,144,366,000.00 na

**b)** Sekta ya Mifugo (Fungu 99) ilitengewa **shilingi 16,871,741,000.00**.

**Mheshimwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya ziara katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam kwa kukagua miradi iliyokuwa vipaumbele vya Wizara. Kwa sababu ya ufinyu wa muda, Kamati ilikagua miradi miwili inayotekelezwa na Sekta ya Mifugo na mradi mwingine unaotekelezwa na Sekta ya Uvuvi kama ifuatavyo: -

i) Ujenzi wa bwawa la kuvuna na kuhifadhi maji unaotekelezwa eneo la Chamakweza katika Wilaya ya Chalinze mkoani Pwani; na

ii) Ukarabati wa Makao Makuu ya Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) ulioko jiji la Dar es Salaam katika Wilaya ya Kigamboni. Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha na kukaguliwa ni kama ifuatavyo: -

#### 2.2.3.1 Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Chamakweza

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa bwawa la Chamakwenza unalenga kuhudumia wafugaji wa vijiji vitatu vyenye jumla ya **mifugo 104,849** kwa lengo la kuhakikisha

upatikanaji wa uhakika wa maji kwa ajili ya kunywesha mifugo. Aidha, kukamilika kwa mradi huu kunalenga kuondoa migogoro ya muda mrefu baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi hususan wakati wa kiangazi. Taarifa ya Wizara ilionyesha utekelezaji wa mradi huu umekamilika kwa **asilimia 100** na kugharimu kiasi cha **shilingi 671,479,519.20**.

**2.2.3.2 Ukarabati wa Makao Makuu ya Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa ukarabati wa Makao Makuu ya Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) unalenga kutimiza azma ya Serikali ya kufufua Shirika hili kwa ajili ya kuboresha shughuli za Uvuvi wa Bahari Kuu. Utekelezaji wa mradi huu unagharimu shilingi **172,864,170.00** na ulitarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2022. Taarifa ya Wizara ilieleza kuwa, utekelezaji wa mradi huu umefikia **asilimia 82**.

**2.3 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati imebaini kwamba;

i) Hakuna utaratibu rasmi uliowekwa wa namna bora ya ushirikishwaji jamii katika miradi inayojengwa na wakandarasi tofauti na ile inayojengwa kwa utaratibu wa force account na hivyo kupelekea changamoto katika utekelezaji wa baadhi ya miradi. Mfano ni ujenzi wa bwawa la Chamakweza;

ii) Gharama zilizotumika kutekeleza ujenzi wa bwawa la Chamakweza haziendani na thamani ya fedha iliyotumika kwenye utekelezaji wa mradi huu;

iii) Bajeti inayoidhinishwa na kutolewa kuboresha Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) haikidhi mahitaji na majukumu ya Shirika hilo katika kuwezesha nchi yetu kunufaika na Uvuvi wa Ukanda wa Uchumi wa Bahari (EEZ) na Bahari Kuu;

## 2.4 Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Sekta ya Uvuvi ilitengewa jumla ya **shilingi 161,350,047,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama ilivyofafanuliwa kwenye **Kielelezo Na.1**. Aidha, jedwali hili pia linaonyesha hali ya upatikanaji wa fedha hadi kufikia kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha katika utekelezaji wa bajeti.

**Kielelezo Na. 1: Ulinganisho wa Bajeti iliyoidhinishwa kwa Sekta ya Uvuvi na kiasi cha Fedha kilichopokelewa hadi Februari, 2022**

| BAJETI ILIYOIDHINISHWA | | UPATIKANAJI WA FEDHA HADI FEBRUARI 2022 | | |
|---|---|---|---|---|
| **Kawaida** | 22,205,681,000.00 | **Kawaida** | 15,241,068,263.26 | **69%** |
| **Maendeleo** | 99,144,366,000.00 | **Maendeleo** | 3,217,386,249.00 | **3.3%** |
| **Jumla** | 112,350,047,000.00 | **Jumla** | 18,458,454,512.26 | **11.4** |

Chanzo: Uchambuzi wa Randama ya Sekta ya Uvuvi - Fungu 64

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa

i) Fedha ya Matumizi ya Kawaida iliyopokelewa hadi kufikia mwezi Februari, 2022 ni **asilimia 69** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida unaonesha mwenendo wa kuridhisha na hivyo kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

ii) Fedha za matumizi ya maendeleo zinazotengwa ni kidogo ikilinganishwa na rasilimali nyingi zilizopo kwenye Eneo la Bahari, Maziwa na Mito. Pamoja na kiasi kidogo kilichotengwa bado kiasi kilichoidhinishwa na Bunge na kutolewa na Serikali ni kidogo ambapo hadi mwezi Februari, 2022 Fedha za Maendeleo zilizotolewa zilikuwa **asilimia 3.3** tu.

**Kielelezo Na. 2:**
**Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo na kiasi cha Fedha kilichotolewa – Kwa Sekta ya Mifugo**

| BAJETI ILIYOIDHINISHWA | | | UPATIKANAJI WA FEDHA HADI FEBRUARI 2022 | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mchanganuo** | **Kiasi** | | **Mchanganuo** | **Kiasi** | |
| **Kawaida** | 30,973,208,810.00 | 5 | **Kawaida** | 20,047,331,851.73 | 5 |
| **Maendeleo** | 16,871,741,000.00 | 5 | **Maendeleo** | 5,376,919,278 | 2 |
| **Jumla** | 47,844,949,810.00 | 00 | **Jumla** | 25,424,251,129.73 | 3 |

Chanzo: Uchambuzi wa Randama ya Sekta ya Mifugo - Fungu 99

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa;

i) Jumla ya kiasi cha fedha kilichopokelewa hadi kufikia Februari, 2022 ni **asilimia 53** ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge, jambo ambalo si mwenendo wa kuridhisha katika upatikanaji wa fedha.

ii) Fedha zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni **asilimia 32** tu, kiasi ambacho ni pungufu ya **asilimia 68** ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na takwimu hizo, Kamati inashauri utoaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida ni vyema ukaendana na utoaji wa fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo kwa kuwa fedha za Matumizi ya Kawaida zinazotengwa, pamoja na mambo mengine, kuwezesha Watendaji kufuatilia Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hivyo kama hakuna uwiano wa utoaji fedha, upo uwezekano wa Watendaji kupata ujira pasipo kutekeleza

majukumu yao kikamilifu. Kwa mfano; upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya Kawaida hadi kufikia mwezi Februari, 2022 ulikuwa ni **asilimia 65** wakati upatikanaji wa fedha za kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa kipindi kama hicho ulifikia **asilimia 32** tu.

**2.5 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilishauri kuhusu mambo mbalimbali. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Taarifa ya Mtoa hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu kubwa ya Ushauri. Mfano wa Ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kuhusu kuongeza uwekezaji kwenye Sekta ya Mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za utekelezaji zilionesha Serikali imeongeza bajeti ya Sekta ya Mifugo kutoka **shilingi bilioni 38.9** Mwaka 2020/2021 hadi **shilingi bilioni 47.8** Mwaka 2021/2022. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Serikali imeendelea kuongeza bajeti na kufikia **shilingi bilioni 92**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ushauri ambao utekelezaji wake bado una sua sua ni ushauri uliohusu Sekta ya Uvuvi ambapo, Kamati ilishauri Serikali iharakishe ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko mkoani Lindi.

Kamati ilitoa ushauri huo kwa kuzingatia kuwa, ujenzi wa bandari ya uvuvi ndio njia pekee itakayowezesha nchi yetu kunufaika na Uchumi wa Buluu kwa kutumia kikamilifu rasilimali zilizopo kwenye bahari, maziwa, mito, mabwawa na vyanzo vingine vya maji ili kuwezesha rasilimali hizo kuchangia ukuaji wa uchumi, kuboresha maisha ya jamii, kuongeza ajira, kuongeza uwekezaji kwenye viwanda vya kuchakata samaki na mazao yake katika mnyororo wa thamani.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri uliotolewa, Kamati ina maoni kuwa bado kuna umuhimu wa kuendelea kuzingatia ushauri ambao haujafanyiwa kazi na hakuna sababu za msingi za kutouzingatia.

**2.6 Makadirio ya Maduhuli na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekadiriwa kukusanya maduhuli na kutengewa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kulinganisha na bajeti inayomalizika. Uchanganuzi wa Maduhuli na Makadirio ya Matumizi hayo ni kama ifuatavyo: -

**2.6.1 Makadirio ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika,** mtoa hoja alieleza kuwa, jumla ya **shilingi 120,100,000,000.00** zinakadiriwa kukusanywa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Kiasi hicho ni ongezeko la **asilimia 20** ikilinganishwa na lengo la maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Mchanganuo wa makadirio hayo unaoneshwa katika **Kielelezo Na. 3.**

**Kielelezo Na. 3:**
**Mchanganuo wa Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na Mwaka 2021/2022**

| Na. | Sekta | Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka 2021/2022 | % jumla kwa wizara | Makadirio kwa mwaka 2022/2023 | Ongezeko | Ongezeko kwa Asilimia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SEKTA MIFUGO | 50,000,000,000.00 | 5.55 | 60,100,000,000.00 | 10,000,000,000.00 | 20.00 |
| 2. | SEKTA UVUVI | 40,000,000,000.00 | 4.44 | 60,000,000,000.00 | 20,000,000,000.00 | 66.66 |
| | **JUMLA** | **90,000,000,000.00** | | **120,100,000,000.00** | **30,000,000,000.00** | **33.33** |

**Chanzo:** Randama za Fungu 99 na Fungu 64

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi umeonesha kwamba;
(a) Makadirio ya Maduhuli ya Sekta ya Mifugo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 yameongezeka kwa **asilimia 33.33** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.
(b) Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Sekta ya Uvuvi imeongezewa Ukusanyaji wa Madhuhuli kwa zaidi ya **asilimia 66.66** wakati mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa kipindi cha robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti ulifikia **asilimia 35** tu.
(c)
**Mheshimiwa Spika,** ni matarajio ya Kamati kwamba, kutokana na ongezeko la bajeti kwenye sekta zote mbili, lengo la makusanyo litafikiwa.

**2.6.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida**
**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Mifugo na Uvuvi wanakadiria kutumia **shilingi 86,916,508,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Uchambuzi umeonesha kuwa, katika bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuna ongezeko la bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa **asilimia 132.15** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Kielelezo Na. 4:**
**Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023**

| Na. | TAASISI | MAKADIRIO KWA MWAKA 2021/2022 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2022/2023 | ASILIMIA KATIKA ONGEZEKO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SEKTA YA MIFUGO | **30,973,208,810.00** | **46,488,725,000.00** | 50.09 |
| 2. | SEKTA YA UVUVI | **22,205,681,000.00** | **40,427,783,000.00** | 82.06 |
| | **JUMLA** | **53,178,889,810.00** | **86,916,508,000.00** | **63.44** |

**Chanzo: Randama za Fungu 99 na Fungu 64**

**Mheshimiwa Spika,** takwimu hizi zinadhihirisha kuwa uendeshaji wa shughuli za Wizara ya Mifugo na Uvuvi zimeongezewa msukumo katika bajeti. Hata hivyo, kiasi cha bajeti kilichoongezwa ni kidogo ikilinganishwa na majukumu makubwa iliyonayo Wizara katika kuhakikisha tija inaongezeka kwa kuimarisha sekta za Mifugo na Uvuvi.
Kwa upande wa bajeti ya Matumizi ya Kawaida, Kamati imejiridhisha kuwa makadirio ya sehemu hii ya bajeti yanaendana na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, jambo la muhimu ni Serikali kuhakikisha upatikanaji wa fedha unatolewa kulingana na mahitaji ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

### 2.6.3 Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo yamefafanuliwa katika kielelezo Na. 5

**Kielelezo Na. 5:**
**Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/2023**

| Na. | TAASISI | MAKADIRIO KWA MWAKA 2021/2022 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2022/2023 | ASILIMIA KATIKA ONGEZEKO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SEKTA YA MIFUGO | 16,871,741,000.00 | 92,050,824,000.00 | 92.4% |
| 2. | SEKTA YA UVUVI | 99,144,366,000.00 | 176,106,544,836.00 | 45.1% |
| JUMLA | | 116,016,107,000.00 | 286,157,368,836.00 | 58.5% |

**Chanzo:** Randama za Fungu 99 na Fungu 64

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba;
a) Bajeti ya Maendeleo ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeongezeka kwa **asilimia 58.5** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa Mwaka wa Fedha 2021/2022;

b) Tafsiri ya ongezeko hili ni kuwa Sekta ya Mifugo itapunguza tatizo la upatikanaji wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo na hivyo kupunguza vifo vya mifugo kutokana na uhaba wa maji na malisho;

c) Kwa upande wa Sekta ya Uvuvi inatarajiwa kuongezeka kwa upatikanaji wa samaki kutokana na kuongezeka kwa uwezo na uelewa wa wavuvi kuhusu ukuzaji viumbe kwenye maji; na

d) Ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu, kwa mwaka inahitaji **shilingi 950,000,000,000.00** ikilinganishwa na bajeti iliyotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ya ambayo ni **shilingi 268,157,368,836.00**.

e) Kiasi cha fedha kilichotengwa kwa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni sawa na **asilimia 0.62** ya bajeti ya Taifa ambayo ni **shilingi 41,063,915,287,000.00.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo ni wazi kutakuwa na ongezeko kwa kipato cha wavuvi na wafugaji, kuongezeka kwa ajira, kuongezeka kwa mapato ya Serikali na fedha za kigeni kutokana na mauzo ya bidhaa za mifugo na uvuvi nje ya nchi.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi wa Kamati, ushauri kuhusu maombi ya fedha kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni kama ifuatavyo:

### 3.1 Ushauri wa Jumla

Kwa sababu sehemu kubwa ya ongezeko la bajeti limetokana na fedha za ndani na mikopo kutoka nje, Kamati inashauri Wizara kutekeleza yafuatayo:-

a) Kwa kuwa lengo la Serikali ni kuongeza tija katika uzalishaji, ni muhimu kwa Watumishi wa Serikali kuzingatia nidhamu kwenye matumizi ya fedha kwa kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kujielekeza kwenye mipango inayotekelezeka ili kuleta maendeleo kwa wafugaji na wavuvi;

b) Upo umuhimu kwa Wizara ya Fedha kuipelekea Wizara nyongeza ya fedha za bajeti mapema.

c) Utekelezaji wa Mpango wa bajeti ya Wizara uzingatie umuhimu wa kutatua changamoto zinazoikabili nchi yetu na Dunia kwa ujumla ikiwemo tatizo la uhaba wa chakula, matatizo ya mabadiliko ya tabianchi na ukosefu wa ajira kwa vijana

**3.2 Sekta ya Mifugo**

i) Kuongeza bajeti kwa ajili ya maeneo ya malisho ili kusaidia upatikanaji wa uhakika wa chakula cha mifugo na hivyo kuongeza thamani ya mifugo yetu kwenye ushindani wa soko.

ii) Kutokana na umuhimu wa vitalu katika kuzalisha mifugo bora, zoezi la kupangisha vitalu lizingatie manufaa ya kufuga kisasa badala ya kuchunga. Aidha, Kamati inashauri Wizara ifanyie kazi changamoto za ugawaji vitalu.

iii) Pamoja na kwamba, sehemu ya nyongeza ya bajeti itaelekezwa kwenye ukarabati wa malambo, Kamati inashauri kiasi kikubwa cha fedha hiyo kielekezwe kwenye ujenzi wa malambo mapya hususani kwenye maeneo ya wafugaji yanayoathirika na ukame mara kwa mara.

iv) Ili kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji inayotokana na wafugaji kuhamahama kutafuta malisho, Kamati inashauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi kushirikiana na Wizara ya Ardhi, kuandaa utaratibu wa kumilikisha wafugaji ardhi.

v) Ili kulinda, kuimarisha na kuvisaidia viwanda vya ndani kuongeza uzalishaji wa maziwa na kushindana kikamilifu

kwenye soko, Kamati inashauri Serikali iondoe tozo kwenye uzalishaji wa maziwa yanayozalishwa nchini.

**3.3 Sekta ya Uvuvi**

i) Mikopo ya vijana inayotolewa na Halmashauri itumike kuwapatia vijana mikopo na elimu kuhusu mbinu bora za ufugaji samaki kwenye vizimba na mabwawa ili kupunguza utegemezi kwenye uvuvi wa maji ya asili.
ii) Kuhamasisha sekta binafsi kushiriki kikamilifu kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao ya samaki ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufanya biashara.
iii) Biashara ya mwani inakua kwa kasi na inatekelezwa na Wanawake, Wizara iandae mpango wa kuwaelimisha na kuwawezesha wakulima wa mwani mbinu bora za kilimo hicho.
iv) Ili kuimarisha biashara ya samaki nje ya nchi, viwanja vya ndege vijenge miundombinu ya kupozea (cold rooms facilities) kwa ajili ya kuhifadhi mazao ya samaki.
v) Vituo vya barafu vijengwe kwenye maeneo yote yanayozalisha samaki kwa wingi.
vi) Wizara ihakikishe kwamba viwanda vya kuchakata mazao ya samaki vinavyojengwa nchini vinapata malighafi ya kutosha.

**SEHEMU YA NNE**

**4.0 HITIMISHO**

**4.1 Maelezo ya Kuhitimisha**

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyofahamika, sekta za mifugo na uvuvi ni sekta za uzalishaji ambazo ni muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa na kuleta msukumo kwenye ukuaji wa sekta ya viwanda. Ukuaji wa sekta hizi una umuhimu mkubwa katika kuimarisha biashara za mazao haya ndani na nje ya nchi na kufanikisha utelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025), Malengo ya Maendeleo Endelevu na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020- 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Mifugo inachangia **asilimia 27** ya pato la Sekta ya Kilimo ambapo **asilimia 40** ya pato hilo inatokana na uzalishaji wa nyama ya ng`ombe, tasnia ya maziwa na uzalishaji wa mbuzi, kondoo na kuku. Vilevile, Sekta ya Uvuvi inachangia takribani **asilimia 1.7** ya pato la Taifa, inatoa ajira kwa watanzania takribani **milioni 4.5**, na kuchangia fedha za kigeni, kipato, chakula na lishe na huchangia **asilimia 30** ya protini inayotokana na mazao ya wanyama.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi endapo itapewa fedha kwa ajili kufanya uwekezaji kikamilifu na kutumia vizuri rasilimali nyingi zilizopo nchini, Wizara hii ina uwezo wa kufanikisha mipango mbalimbali ya Serikali na kutengeneza faida ikilinganishwa na gharama zitakazowekezwa.

**4.2 Shukurani**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kutokana na umuhimu wao natamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:

1. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Athuman A. Maige, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Dkt. Blz. Bashiru Ally Kakurwa, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Christopher Ole Sendeka, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Prof. Partrick A. Ndakidemi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Charles John Mwijage, Mb - Mjumbe

| | | | |
|---|---|---|---|
| 10. | Mhe. Munde Tambwe Abdallah, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Dkt. Rita Enespher Kabati, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Janejelly James Ntate, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Tumaini Brcyceson Magessa, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Jackson Gidion Kiswaga, Mb | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Benaya Liuka Kapinga, Mb | - | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Furaha Ntego Matondo | - | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Yahya Ali Khamis Mb | - | Mjumbe |
| 23. | Mohamed Suleiman Omar, Mb | - | Mjumbe |
| 24. | Micael Mwita Kembaki, Mb | - | Mjumbe |
| 25. | Mhe. Yustina Arcadius Rahii, Mb | - | Mjumbe |
| 26. | Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya, Mb | - | Mjumbe |
| 27. | Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutambua umuhimu wa sekta hizi na kuziongezea bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mhe. Mashimba Ndaki (Mb) kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao umechangia kwa sehemu kubwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi wakiongozwa na Katibu Mkuu - Mifugo Ndugu Tixon Nzunda na Katibu Mkuu – Uvuvi Ndugu Rashidi Tamatama kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati. Shukrani za Kamati ziwaendee pia Watendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa mipango madhubuti ya kuhakikisha Sekta za Mifugo na Uvuvi zinakuwa endelevu na zenye tija, kuchangia uchumi wa viwanda, kuinua kipato cha wafugaji

na wavuvi pamoja na kuchaingia kikamilifu katika malighafi ya viwanda na hivyo kuinua pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee nakushukuru wewe binafsi, naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyotuongoza na kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, namshukuru pia Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge Ndg. Dickson Bisile, Makatibu wa Kamati Ndg. Rachel Nyega na Ndg. Eunice Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Waziri Kizingiti, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Christine Gabriel Ishengoma (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI**

25 MEI, 2022

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma kwa uwasilishaji wa Taarifa ya Kamati. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaanza na uchangiaji naomba tutambue wageni wambao wemeingia wengine ni wageni wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambao ni wanafunzi 100 pamoja na walimu wanne

toka Shule ya *Realhope Schools* ya Mafinga iliyoko Mkoa wa Iringa, nafikiri wameshaingia naomba tuwaone. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka *Pre-primary* pamoja na *Secondary School* ya huko *Really Hope School* ambayo kwa mara hii wamefaulu vizuri wana naambiwa nawaombeeni kila la kheri muendelee zaidi hongereni sana na hawa waliopo aamini Mwenyezi Mungu atasaidia na ninyi mtafaulu vizuri sana karibuni sana. *(Makofi)*

Lakini pia, tuna wageni wa Mheshimiwa Mariam Ditopile ambao ni Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake kutoka hapa Dodoma ambao wao wanajishughulisha katika kuwasaidia wanafunzi walioshindwa kuendelea na masomo shuleni kutokana na changamoto mbalimbali. Karibuni sana, sijawaona, ni hao waliosimama ndiyo wameingia *okay* karibuni sana nawashukuru sana kwa kazi nzuri ya kujitolea mnayoifanya. Karibuni sana katika Bunge letu ni kazi ya kujitolea ambayo malipo yake makubwa yanatoka kwa Mwenyezi Mungu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa nitaendelea kutangaza kadri matangazo ya wageni yatakavyoletwa na sasa tunaanza na Uchangiaji wetu katika mjadala uliopo ya Taarifa hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Tutaanza na wachangiaji wale hawaanza kuchangia au wale ambao wamechangia mara ya kwanza na wao watapata dakika kumi kumi, baadaye tutandelea kupunguza kwa mujibu ambavyo watakuwa wamechangia. Tunaanza na Mheshimiwa Mariam Ditopile atafuatia Mheshimiwa Keneth Ernest Nollo na baadaye Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo wajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona na kunipa nafasi niweze kuchangia katika hotuba yetu hii ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza nipende kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na timu yao katika wizara kwa yale ambayo

wameweza kufanikiwa kuyafanya ambayo bado yapo kwenye mchakato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mwana CCM na huwa nikipenda kushauri ukweli napenda kutumia kati ya moja ya ahadi zetu za uanachama, nitasema ukweli daima fitina kwangu mwiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa Sangara katika Ziwa Victoria ni mbaya sana; sasa sijajua kama kwenye vipaumbele vya wizara yetu hii wameliona hili na kulitaka kulitafutia ufafanuzi. Kwa nini nasema hali mbaya? Sangara ni bidhaa kubwa sana katika Soko la Samaki la *Export* katika dunia, Europe ndiyo soko kubwa sana ambalo zaidi ya asilimia 70 ya mazao ya Samaki yanayotoka Afrika yanakwenda huko Europe, zaidi ya asilimia 70. Mwaka 2014/2015 Tanzania tulikuwa tunatoa zaidi ya tani 45,000 za minofu ya Sangara na mazao yake; lakini mwaka 2021 tumetoa tani 14,000 tu; lakini viwanda vyetu vilivyokuwepo mwaka huo 2014/2015 tulikuwa tunaajiri zaidi ya vijana 12,000 kwenye sekta hii. Nasikitika kusema ajira imepungua zaidi ya asilimia 50 na leo hii tuna takriban vijana 4,000 tu ambao wameajiriwa kwenye sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Wabunge wa Mikoa ya Mwanza na Jirani ni mashahidi, ukienda kuhoja wamachinga waliokuwepo mtaani, miaka kumi kumi na ngapi nyuma wengi walikuwa waajiriwa kwenye viwanda hivi; Lakini hapo zamani viwanda vilikuwa vinafanya kwa siku *shift* tatu na vilikuwa *operational* wiki nzima siku saba ndani ya wiki; lakini cha kusitika hali sasa hivi viwanda hivi vinafanyakazi kwa *shift* moja na nusu kwa siku na siku nne tu kwenye wiki. Kwa hiyo, nimetoa picha hii ili tujue leo *royalty* inakuwa inapatikana kwenye biashara ya sangara ndiyo ilikuwa inasaidia kuleta maendeleo kwenye nchi yetu; ilikuwa inasaidia kujenga hospitali, Vituo vya Afya na maeneo mengine ya kimaendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa nimeangalia sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri bado sijaona. Ninaamini jambo ambalo linasababisha hali hii ni uvuvi haramu. Lakini nimesikitika kuona kwamba katika vipaumbele vya wizara sijaona palipoandikwa kwamba mna mkakati wa aina gani madhubuti wa kupambana na uvuvi haramu. Lakini naweza kutoa tu maoni na kama mnayafanyia kazi mmesahau tu kuandika mtanitolea majibu huko wakati mnajibu hoja zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niulize Mheshimiwa Waziri nimefuatilia unazo takwimu kweli kuhusu viwanda ambavyo uko navyo, kwa sababu kati ya wageni mliowaalika wamiliki wa viwanda kuja kuhudhuria bajeti hii, mmewaalika Kampuni inaitwa *Prime Catch* lakini hii *Prime Catch* imefungwa miaka 10 iliyopita hakipo hiki kiwanda; kuna kiwanda kinaitwa *Vick Fish*, hakipo kilishafungwa hiki kiwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Uganda ambayo inasehemu ndogo sana ya Ziwa Victoria inatuongoza kwa kuwa na idadi ya viwanda vingi kuliko sisi; Leo hii kwenye nchi 10 Afrika zinazopeleka minofu ya Samaki kwenye soko la dunia Tanzania hatupo; Uganda ambao ni *landlocked country* inayo Ziwa Victoria peke yake haina ukanda wa Bahari kama wa kwetu ipo ni nchi ya 10 Afrika. Sasa naongea hivi kwa masikitiko makubwa sana, yapo maeneo Mungu ametubariki mno, kikubwa ni utashi wa kutambua tatizo lipo wapi tukapata uthubutu wa kushughulikia hili tatizo ili kunusuru hali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niulize huko nyuma kuna *operation* ilianzishwa kwa ajili ya uvuvi haramu, al-maarufu *operation* Sangara, nia ilikuwa njema lakini niulize kama wizara je, mnayo tathmini ya *operation* kwa sababu kwa wananchi leo ukiwauliza kuhusu *operation* hii ni majeraha matupu. *Operation* iliyokwenda kutia umaskini watu, iliyosababisha vifo kwa watu kupata mapresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui kwa upande wenu Serikali tunaomba mje na tathmini je *operation* hii ilikuwa na manufaa gani kwa nyie mnavyoona huko; na je mlichopanga kufanya kikaende ndivyo sivyo mnarekebishaje ili basi tuweze kuwa na mipango Madhubuti, kwa sababu nimesoma gazeti la *Guardian* la tarehe 20 Mei, 2022; Wizara mlitoa kauli kwamba mmejipanga kuwekeza fedha nyingi kwa ajili ya kupambana na uvuvi haramu. Sasa nataka kuliko kwenda kulitia tena Taifa kwenye hasara tujue ile *operation* ilifeli wapi, hasara ilikuwa wapi, ili kabla hamjachukua fedha hizi za umma kuziingiza huko tayari muwe na tathmini na tujue mmejipanga vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri unao maafisa wetu wa uvuvi katika kila nyanja kwa maana ya vijijini mpaka mikoani. Tumewaweka hawa kule kwa ajili ya kusimamia hizi rasilimali zetu kama vitendo hivi vinaendelea inamaana wao wanaviruhusu; wao ndiyo wapo kwenye mialo, wao ndiyo wapo kwenye *catchment area*; Je, mmewawajibisha vipi hawa wanaosimamia hii rasilimali iwe ya kinidhamu ama kiutendaji, je wanawaletea ripoti, hizo ripoti mnazifanyia kazi, je kama ni uzembe wao mmewachukulia hatua gani tuanze nao hao ili watatupa majibu mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongereni mmechukua hatua ya kukaa na wadau kwa maana ya wavuvi wadogo, wakubwa lakini na wamiliki wa viwanda. Tujiulize kila mmoja yuko *bitter* kwenye suala la uvuvi haramu, wote wahusika wako *bitter*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hebu tukae chini tena kama kila mtua anachukia Serikali, wananchi wanachukia, wadau wanachukia shida ni nini Uvuvi huu haramu unaendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunaona katika Ziwa Victoria tunali-*share* na majirani zetu kwa maana ya Uganda na Kenya na tunaona Uganda ndiyo inaongoza na Uganda ndiyo ina *control* bei, ina maana leo Uganda ghafla kwa vile wao ndiyo wameshika soko wanashusha bei inakuja kuathiri. Je, mmejipangaje kama Serikali katika kulinda hawa wavuvi wetu wasipate hii athari; cha kwanza kwa kukaa chini na hizi Jirani, kuona kama tunaweza kuwa na bei elekezi ili haya mabadiliko ya kiholela yasiathiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mjifunze kutoka Wizara ya Kilimo, leo hii wamekuja na bima kwa ajili ya wakulima wao kwa nini na sisi tusione namna ya kuwa na bima ya hawa wavuvi wetu ili hali inapotokea waweze kukaa vizuri lakini pia muone namna gani tunaweza kuwa na soko la uhakika; kuliko mtu anakwenda huko usiku kucha yupo gizani anavua halafu akirudi bei imeshuka na inakuwa hasara kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema tunalo Ziwa Tanganyika, dagaa zinazopatikana Ziwa Tanganyika ni dagaa ambazo ni nzuri haijawahi kutokea. Lakini nasikitika kusema mpaka leo biashara ya dagaa hizi ni kiholela; leo Ziwa Tanganyika, Rukwa, Katavi, Kigoma hakuna kiwanda kikubwa cha Samaki na ukiacha dagaa kule kuna Samaki nzuri, kuna migebuka, tunazo kuhe wanaita kuku wa ziwani, Serikali imejipangaje katika kuvutia uwekezaji wa kiwanda kikubwa kwenye Ziwa Tanganyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hamna taarifa ninayo, wako wawekezaji wanaotaka kuweka kiwanda kule lakini tangu waanze mchakato imekuwa mchakato mpaka mchakato. Fuatilieni, mjue kama kuna *engagement* Serikali muwasaidie basi wananchi wetu waweze kuongezewa thamani ya mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tuna mpango wa kuanzisha viwanda kwenye ukanda huu wa Bahari, kwamba kutoka Dar es Salaam mpaka Mtwara, Tanga huu ukanda wote. Miaka sita iliyopita nataka niulize je kipindi chote tangu tuanze kujinasibu na Tanzania ya Viwanda hasa kwa maeneo ambayo tunatumia rasilimali zetu; kwenye ukanda huu wa Bahari kuna kiwanda kipya kimeanzishwa mpaka leo; na kama hakijaanzishwa ni kwa nini; kwa sababu taarifa nilizokuwa nazo ni viwanda kufungwa tu sasa sijui inawezekana hatuna huo ufahamu basi wakati mnajibu hoja mje mtuambie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu tuanze adhma hiyo ya kuanzisha viwanda kwenye ukanda ule, viwanda vingapi vimeanzishwa na vina hatua gani, kama havijaanzishwa sababu nini, na tunajipangaje? Kwa sababu haiwezekani leo hii Morocco ambaye ana sehemu ndogo tu ya Bahari atuzidi sisi kwa ku-*export* mazao ya *Seafood* kwenda nje ya nchi, kwa kweli tunamkosea Mungu, Mungu ambaye ametubariki sisi eneo kubwa sana la Bahari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kengele imelia Mheshimiwa Mariam.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi napenda tu leo nimechangia kwa utulivu na hisia kwa sababu kama wizara hatutoweka mipango madhubuti katika kunusuru hali ya bahari na maziwa yetu yakaleta tija kwa Taifa, tutakuwa tunamkosea sana Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan ambaye ameonekana ni mtu mwepesi, msikivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo tulikuwa tunapiga kelele kuongezewa bajeti miaka yote lakini bajeti imeongezeka; kwa kweli niwaambie kweli wizara hii mmeniangusha, hotuba hii haijanigusa, naomba kama mna majibu ambayo kidogo yataamsha ari yangu na kuwa na matumaini mapya mje nayo wakati mnahitimisha mjadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mariam Ditopile tunaendelea na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi kuchangia kwenye Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi; awali ya yote kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Mifugo na Naibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizara hii sote tunaijua kwa nyakati nyingi imekuwa ni wizara ambayo haipewi kipaumbele, lakini wizara muhimu sana katika nchi yetu kwa maana inachangia pakubwa katika pato la Taifa. Nimeona jitihada nyingi sana za Mheshimiwa Waziri ambazo anazifanya katika sekta ya mifugo ikiwa kwenye ujenzi wa majosho. Wilaya yangu ya Bahi tumeweza kupata majosho nane katika mwaka wa fedha 2021/2022 na huko nyuma ilikuwa ni nadra sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuja na mfumo wa kuwa na hereni za kieletroniki jambo hili limefanyika sana katika nchi ya Botswana kwamba mifugo inavyopata *electronic* tag tayari tunakuwa tunajua taarifa ya mfugo ule lakini unaungamanisha na maeneo mengine kwa mfano *TRA* wanaweza kuwa wanajua taarifa za mifugo ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasaidia sana kwa maana ya kwamba mfugaji wetu sasa anaweza kwenda kukopesheka. Maana yake ana mifugo inayotambulika na utaratibu wake akiuza inajulikana kwamba ng'ombe mwenye *Serial Number* hii sasa ameuzwa. Kwa hiyo, haya ni mapinduzi makubwa na

Mheshimiwa Waziri kwa dhati kabisa nakupongeza kwa *initiative* hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuchangia katika maeneo matatu; la kwanza nianze katika suala zima la uuzaji wa nyama nje ya nchi. Nimefanya biashara hii kwa kiasi kukibwa lakini hatujawekeza vizuri katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumezuiliwa kuuza nyama yetu katika baadhi ya nchi, tumezuiliwa kwa sababu ya uchakavu wa machinjio ya Serikali, kwa sababu ya kuwa na hali mbaya ya mazingira. Hatuwezi kuuza Saudi Arabia, hatuwezi kuuza Falme za Kiarabu na maeneo mengine, lakini unavyokosa soko la Saudi Arabia ina maana umekosa fursa yote ya *Middle East.* Unavyokosa soko la Falme za Kiarabu ina maana umekosa kuuza *Middle East* yote, tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda chetu cha machinjio cha Kizota walikuja wataalam kukagua wakakuta kina hali mbaya, lakini kwa muda mrefu na wataalamu walishafanya tathmini hata tathmini ya hivi karibuni inatakiwa Bilioni Mbili na Milioni Mia Tano tu. Sasa Shilingi Bilioni Mbili na Milioni Mia Tano imetugharimu kwa kiasi kikubwa. Nikitaka mimi kuuza mbuzi au kondoo nje ya nchi au ng'ombe natumia viwanda vya watu wengine hapa, lakini itaonekana lebo ya mwenye kiwanda kile na siyo kampuni yangu, sasa huu ni unyanyasaji. Naweza nikafanyiwa fitina muda wowote nikanyang'anywa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Serikali na Mheshimiwa Waziri jambo hili uliahidi bajeti iliyopita, sasa Bilioni Mbili na Milioni Mia Tano kweli Serikali? tumekaa miaka Sita? Eneo lile la Kizota halikarabatiwi? Kama Serikali imeshindwa nipeni basi hata mimi! Shilingi Bilioni 2.5 ni kitu ambacho kinawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali kwenye jambo hili Bilioni Mbili na Milioni Mia Tano ni kitu cha aibu kukaa muda wote huo Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, tunalazimika kwenda kuchinjia ng'ombe wetu Kenya, mbuzi tunachinjia Kenya, kondoo Kenya. *Export* ya Kenya inaonekena sasa ndiyo kubwa kwenye mifugo, lakini ng'ombe wanavuka Namanga wanaenda kuchinjiwa kule na tunafanyiwa udalali mkubwa haijawahi kutokea na masharti makubwa. Sasa Mheshimiwa Waziri kweli Bilioni Mbili zinatufanya tuwe hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nisiseme sana na mengine yanayotokea kwenye viwanda vyetu vya hapa ndani, lakini Mheshimiwa Waziri kwenye hili kwa kweli, tusaidie kukarabati kiwanda chetu cha Kizota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunauza ng'ombe au nyama ya mbuzi na kondoo ikiwa ni katika hali ya kawaida ya *caucus,* lakini hatu-*process*. *Tanganyika Packers* tulikuwa nayo, nyama yetu hatupeleki iliyo-*processed,* tunapeleka kama tunavyopeleka mahindi ya kwenda tu kusaga nje. Sasa Mheshimiwa napata shida na mimi niliseme sana hili la ku-*process* nyama kama tu kiwanda hiki cha machinjio tu ya Bilioni 2.5 tunashindwa sasa nikianza kusema na habari kiwanda cha ku-*process* nitakuwa naongea kitu kikubwa. Hebu na hili nalo liangalieni sasa kwamba, tuweze kuuza mazao ya mifugo nje ya nchi badala ya kupeleka ng'ombe, nyama, ambazo wenzetu wanaenda ku-*process* upya kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu malisho. Wafugaji wetu ni wakimbizi ndani ya nchi yao, na tunalaumu kwamba, kwa nini wanahamahama, wanahamahama kutafuta malisho, lakini umiliki wa ardhi kwa ajili ya malisho bado haujakaa sawa. Mheshimiwa Waziri jambo hili liangalieni. Nchi ya Zimbabwe imepiga hatua kubwa sana na walipata mkopo kutoka *AU* kwa ajili ya kuzalisha malisho, ukienda nchi nyingi za Ulaya wenzetu

wameshafika hatua hiyo ya kulima malisho, habari ya kuacha ng'ombe azurure ajitafutie chakula ni kitu cha kizamani sana. Kwa hiyo, tuanze wafugaji wetu kuwatafutia maeneo kwa ajili ya malisho, pia wamiliki ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ng'ombe wetu na wanyama wetu katika soko la dunia nyama yake ni ngumu sana. Sote tunajua ng'ombe atoke Shinyanga mpaka Katavi kwa kuhamahama kwa hiyo, tunaharibu hali ya mifugo yetu, lakini kosa kubwa ni kwamba hatufanyi uwekezaji kwenye malisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni miundombinu. Ng'ombe na mifugo mingine hawapati maji, hatuna majosho. Sasa wekeni utaratibu na kama Serikali haiwezi kwenye hili, basi tuweke utaratibu wa wafugaji wetu wawe sehemu moja waji-*organize* waweze kufanya utaratibu wa kujenga miundombinu. Kwa hiyo, bado tuko katika karne ya kizamani. Kuna watu wengine wanasifia kwamba ng'ombe wetu hatuwatibu sana na madawa kwa hiyo ni ng'ombe wazuri. Dunia ya wapi nani anataka kula ng'ombe wana magonjwa? Anataka kula nyama ina magonjwa? Wanasema kwamba, kuku wetu wa kienyeji ni watamu, hiyo ni *wrong perception*. Nani anakula kuku anaumwa, anapona mwenyewe, anajitibu mwenyewe, hiyo ni nyama gani mtu anataka kula? Kwa hiyo, kwa sisi Kanda ya Kati msitupeleke kwenye hiyo habari kwamba, kuku wa kienyeji ni wazuri, tunakula wenyewe tu, lakini nani anaenda kula kuku hajawahi kutibiwa hata siku moja halafu unakula? Hivyo, nataka niseme jambo hili, hebu tutoke na mawazo ya kiufugaji wa kizamani. Dunia inabadilika, dunia inakimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala zima la vyuo vyetu vya mafunzo kwa ajili ya mifugo. Vyuo vina hali mbaya havipati bajeti zake, bado vinafundisha teknolojia ya kizamani, bado wana nadharia kubwa. Ukienda maeneo yale unashangaa tangu alivyojenga Mwalimu Nyerere majengo yale hayajaongezeka. Sasa kama hatuna *Training*

*Institute,* hatuna *researching centers* nzuri za mifugo, tutabaki kusema Tanzania ni nchi ya pili katika Afrika kwa kuwa na mifugo wengi, basi ni nyimbo, lakini ukija kwenye uhalisia hali yetu ni mbaya sana, hatujawekeza kwenye mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya Wizara hii imekuwa inapata fedha kidogo sana. Nami kwa kweli, siwezi kumlaumu hata Waziri, mwaka jana ilikuwa Shilingi Bilioni 243.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Keneth Ernest Nollo. Tunaendelea na Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi ajiandae.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi ya kuchangia Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza kabisa mimi naomba nisiipongeze Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wetu wa Ukanda wa Pwani hali zao ni duni sana kiuchumi na wote ni mashahidi. Mkoa wetu wa Tanga tuna bahari Wilaya ya Mkinga, Tanga, Muheza na Pangani katika Mkoa wetu wa Tanga. Mkakati waliokujanao mwaka jana ambao ndiyo mwaka wa fedha huu tunamalizia, walikuja na mikakati mizuri sana na mipango mizuri. Ukisikiliza mikakati yao ya mwaka jana mwaka wa fedha 2021/2022 na mipango yao ya mwaka 2021/2022 unasema basi hawa Wavuvi sasa hawaendi kutafuta kazi nyingine ya kufanya. Lakini cha kusikitisha mikakati ile ya mwaka jana ambayo walikuja nayo hakuna mkakati hata mmoja ambao wameutekeleza. Sasa Napata wasiwasi kama mikakati ile yam waka wa fedha 2021/2022 haikutekelezwa, sasa hivi tunakwenda kupitisha bajeti ya 2022/2023, sasa sijui hiyo watatekeleza vipi napata wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ukiangalia mikakati yao ya mwaka jana walituambia kwenye Bunge hili wataweka miamba ya kuvutia Samaki ili kuongeza uzalishaji kwenye ukanda wetu ule wa pwani kwa Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar-es-Salaam, Lindi na Mtwara. Hiyo miamba siyo kuiona tu hata kuisikia huko Pwani mimi ninakotoka sijaisikia! Sijaisikia na haipo. Hata Waziri wakati anasoma hotuba yake hakutaja kabisa pia hakutaja kwenye mwaka wa fedha huu anaohama nao kuwa labda tulishindwa mwaka huu, lakini mwaka unaokuja tutafanya, hawakusema! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye bajeti yao ya mwaka 2021/2022 walituahidi hapa watatengeneza vichanja kwa ajili ya kukaushia samaki na dagaa ili kuhakikisha wanapunguza upotevu wa mazao haya ya samaki. Baada ya kutuahidi yale kwa sababu niliuliza mpaka swali mwaka jana na nilijibiwa hapa nikaambiwa vichanja vile vinapelekwa, mimi nikaenda kule nikawaambia wanawake wenzangu wa Mkoa wa Tanga jamani jipangeni vichanja vinakuja na watu wamejiandaa vikundi viko kule wanasubiria vichanja. Vichanja mpaka leo havijaenda, imebakia miezi miwili tunamaliza hii bajeti hakuna kichanja kimekwenda. Sijasikia tena kwenye mpango wao hata kwenye hotuba sijasikia kuwa mwaka jana tuliahidi hivi lakini tumeshindwa na mwaka huu tutaendelea. Sijasikia na haipo na vichanja havipo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mwaka jana hapa walituahidi wakasema wataongeza uzalishaji wa barafu na kujenga *cold rooms* kwa ukanda, tena walisema siyo *cold rooms* tu *cold rooms* za kutosha kwa Ukanda mzima wa Pwani kuanzia Tanga mpaka Mtwara. Mpaka leo hivi ninavyosema sijaona *cold rooms* hata moja hata tu ya mfano huko ninakotoka haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia walituahidi hapa watakuja kuweka hizi *cold rooms* kwa sababu kama tunavyofahamu

mazao ya samaki huwa yanaharibika kwa muda mfupi sana, sisi tunaotoka Ukanda ule wa Pwani samaki huwa hawavuliwi siku zote ndani ya mwaka mzima, kuna siku samaki wanapatikana kwa wingi na kuna siku samaki hawapatikani kabisa, kwa hiyo lengo lao lilikuwa ni zuri kuwasaidia hawa wavuvi kwamba, zile siku wanazopata samaki kwa wingi wangeweza kuhifadhi hata zile siku ambazo hawapati samaki bado wangeweza kuendelea kufanya biashara, lakini haipo, haijatekelezwa, sijaisikia kwenye mpango uliopita na sijaisikia kwenye mpango huu tunaokwendanao, sasa sijui imepotelea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia walituahidi hapa mwaka jana watakuja kujenga soko la kisasa la samaki, baadhi ya maeneo likiwepo soko la samaki la Kipumbwi, Wilayani Pangani. Nalo nimesikia wamelisema, mwaka jana walisema watajenga kwa bajeti ile ya 2021/2022, hakuna msingi uliojengwa, hakuna hata soko lililoanza kujengwa. Kwenye bajeti hii wamesema tena tutajenga soko, wameliweka tena kwenye bajeti ya 2022/2023. Kwa hiyo, mwaka jana hata msingi tu, labda wangesema tumeanza tutaendelea, hata msingi tu haupo! Kwa hiyo, sasa napata wasiwasi sana na bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti yao pia ya 2021/2022 walituahidi hapa watanunua boti ya uvuvi kusaidia kule wavuvi wetu, sasa safari hii sijalisikia, badala yake sasa wamekuja kutuambia watanunua meli kubwa za uvuvi. Sasa kama yale boti hazikununuliwa hivi wataweza kweli kununua meli? Hapo napata wasiwasi? Badala yake sasa wametuambia walinunua boti za doria, siyo ya uvuvi tena. Wamesema tumenunua boti za doria, sasa nikawa sielewi nachanganyikiwa kabisa! Kwa hiyo, boti zilishindikana safari hii tutanunua meli kubwa za uvuvi, sijui ni meli tatu, sijui tano? Sasa napata mashaka kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Wizara kwa sababu mambo mengi hawajayatekeleza yale waliyotuahidi mwaka jana, naomba sasa watueleze mikakati yao hasa madhubuti ya mwaka huu 2022/2023 watakwenda kufanya nini ili kuongeza uzalishaji wa wavuvi hawa kwa maeneo yetu yale ya Pwani na maeneo mengine hata ambayo siyo ya Pwani lakini kwa wavuvi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia watatuhakikishia vipi, ni upi mkakati wao wa kuhakikisha wanawaunganisha wavuvi hawa na masoko? Waje hapa tuwe na mkakati wa uhakika, wavuvi wanahangaika sana, wanavua samaki wanazunguka nao kutwa nzima, mara wameoza, anakwenda anamwaga samaki. Sasa sielewi wakati kuna nchi kibao za jirani hazina kabisa bahari na wangependa wapate samaki kutoka kwetu, sasa sijui, Waziri aje na mkakati. Ni mkakati gani wa kuhakikisha wanawaunganisha wavuvi wetu na masoko ya uhakika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia waje watumabie hapa ni mkakati gani wanaokuja nao wa kuhakikisha wanawawezesha wavuvi wetu kuongeza thamani mazao yao haya ya bahari? Waje hapa na mkakati wa uhakika watuambie ni mkakati gani wameuweka wa kuhakikisha watawaunganisha hawa wavuvi wetu na taasisi hizi za kifedha ili waweze kupata fedha za kuendelea kufanya shughuli zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wetu wale wa Ukanda wa Pwani pia wamehamasika sana kulima zao hili la mwani. Kwenye hotuba ya Waziri sijasikia kabisa akiongelea, hajagusa kabisa! Lakini ninawashukuru Wizara walikuja kama mara mbili, mara tatu, kupitia Naibu Waziri wa Uvuvi kwa wakulima wetu wale wa mwani waliwaletea vifaa kama vile viatu na kamba. Waliwawezesha, lakini changamoto bado ni kubwa sana, zao hili la mwani kwa Wabunge wasiofahamu ni

zao muhimu sana, linatengeneza vitu vingi sana. Kwa mfano tunaweza kutengeneza sabuni ya unga…

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi yako Mheshimiwa.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia hili zao la mwani tunaweza kutengeneza sabuni ya unga, sabuni ya maji, sabuni ya kipande, mafuta ya mgando, mafuta ya maji na *juice* pia, Mheshimiwa Ulega anafahamu. Kwa hiyo, ninaomba sasa Wizara waje watuambie watawasaidiaje hawa wakulima wa mwani kupata masoko? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Mzamili Zodo. Tunaendelea na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi na Mheshimiwa Charles John Mwijage ajiandae. Hayuko Mheshimiwa Vita? Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mheshimiwa Vita yupo? Ahaa!, Mheshimiwa Vita.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo. Nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, kuna mtu mmoja ananiambia nisimame, nimesimama. Kama hawanioni nina mpango wa kununua vile viatu vinavyoitwa raizoni ili niwe navivaa wawe wananiona vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayoifanya, pia kwa kuwasilisha hotuba yao hapa Bungeni. Nchi yetu kijiografia imejaliwa katika maeneo mbalimbali ya kuzalisha kiuchumi. Kuna maeneo ya uvuvi ambayo katika Maziwa yetu Makuu wananchi wetu wanategemea uvuvi. Kuna maeneo ya bahari wanaoishi katika Visiwa vya Bahari na pembezoni mwa bahari

wanategemea uvuvi. Leo hii tuna maeneo pia ya Mikoa ambayo yanategemea mifugo, Mikoa ya Kaskazini na Katikati hapa. Kuna Mikoa pia inategemea kilimo, Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na Mwenyezi Mungu kutupa jiografia ya namna hii ni kwamba ili tuweze kuzalisha chakula, tuweze kufuga, tuweze kuvua pia na Samaki, sasa katika eneo letu la Mkoa wetu wa Ruvuma na hususan Wilaya ya Namtumbo ni wakulima. Tunategemea sana kilimo ndiyo kipato chetu cha uchumi wa wananchi wetu, sasa katika miaka hii ya karibuni, miaka miwili ya karibuni hapa kumetokea na mfumuko wa mifugo kuja katika Wilaya yetu ya Namtumbo, pia kumekuwa na Mikoa ambayo inatoa vibali vya kusafirisha mifugo hiyo itoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanatoa vibali vinavyosema ameruhusiwa aende bila ya kushirikisha mamlaka za Mikoa ambayo mifugo hiyo inakwenda kama wana mipango gani ya ardhi katika eneo lao la Mikoa hiyo. Sasa Mikoa ile inayokwenda mifugo hii, Serikali au Mamlaka ya Mikoa ikiwakamata wanaonesha vile vibali na wanasema kwamba, Katiba inaturuhusu, binadamu yeyote raia wa Tanzania unaweza kuishi mahali popote pale, lakini wanashindwa kusema kwamba, bila kuvunja sheria, sasa wanapozuiliwa wanasema wanaonesha vile vibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, kuwe na utaratibu mzuri wa mawasiliano ya ng'ombe au mifugo inakotoka kule wanaoomba kibali na mamlaka ya Mkoa ule iwasiliane na mamlaka ambayo yule mfugaji anataka kuhamishia ng'ombe wake kule ili waweze kuelewana, nafasi ipo au hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii katika Wilaya yangu ya Namtumbo wamejaa ng'ombe wengi sana. Sisi ni wakulima, mwaka jana tu 2021, tumezalisha zaidi ya tani 157,000 ya

mazao ya nafaka, ni mazao ambayo yanategemewa katika Taifa hili, lakini sasa kumekuwa na taharuki mwaka huu wa ng'ombe kulisha katika mazao hayo. Mkulima anaandaa shamba, analima anatafuta mbegu dukani, anapanda, anapalilia; anaenda kununua mbegu ambayo mwaka huu imezidi zaidi ya Shilingi 100,000/= anatia shambani, mahindi yanatoka ya kijani, mtu analeta ng'ombe analisha kwa dakika 20 au usiku mzima. Kwa hiyo, hii inaleta tafarani kati yetu sisi wakulima tusiozoea kuwa na mifugo, tuliozoea kuzalisha chakula kwa ajili ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sana, Serikali itambue kwamba sisi ni wakulima, lazima mje mtutambue kwa sababu hamjatambua kuna mifugo kiasi gani, kuna mifugo mingi sana kule Wizara haijafika kutambua shida hii ya mifugo kule. Kuna vuguvugu la magongano haya kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu mifugo ina thamani, lakini chakula pia kina thamani. Sasa unapohamisha mifugo kutoka eneo moja; kutoa tatizo mahali na kupeleka eneo lingine, ni sawasawa na kidonda, unakitoa mguuni, unakihamishia tumboni, kitakuua tu. Kidonda lazima ukitibie. Kwa hiyo, lazima tutafute utaratibu wa kutibu hili tatizo kuliko kukihamisha kidonda mguuni ukakiweka tumboni, kitakuua tu. Sasa Serikali au mamlaka ya mkoa fulani inapotuhamishia sisi tatizo, kama wao wana ugomvi kati ya wakulima na wafugaji, wanatuhamishia sisi ambao tulikuwa hatuyaelewi hayo, sasa wanatuhamishia tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Wizara ya TAMISEMI na Ardhi washirikiane waone jinsi gani ya kuwagawia maeneo wafugaji wasije wakaingiliana na wakulima ili sisi tuendelee kuzalisha chakula, tuendelee kupata maslahi yetu na kuendelea kuweka usalama wa chakula katika nchi yetu. Sisi sasa ndiyo watunga Sheria katika Bunge hili. Ni wakati sahihi sasa wa kuweka utaratibu

na mkakati endelevu utakaowezesha wafugaji na wakulima kufanya shughuli zao bila migongano yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo letu pia wafugaji wanaingia katika hifadhi. Kule tuna Hifadhi za Jamii na Jifadhi ya Taifa. Hifadhi ya Jamii WMAs zile tuliziweka kwa ajili ya kuhifadhi, kwa maana nyingine sisi ni wakulima na wahifadhi. Katika maeneo yale ya uhifadhi wa WMA, wakulima tulikuwa tunawazuia kabisa wasiingie kule, wakiingia wanapata adhabu kali sana. Sasa wafugaji ndio wameingia huko. Wakulima wanauliza, sisi mlikuwa mnatuzuia, wafugaji mbona wamekaa kwenye hifadhi na wanatuharibia vyanzo vya maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetengeneza miundombinu ya umwagiliaji, lakini wafugaji wanaenda kwenye vyanzo vya maji kutumia maji yale. Kwa hiyo, kazi yetu ya kilimo inakosa maji wakati wa kiangazi, tunashindwa kufanya kazi yetu. Kwa hiyo, ni jambo ambalo Serikali lazima ije Namtumbo, ije Mkoa wa Ruvuma kuangalia shida hii, ni kubwa. Tusingoje mpaka watu waanze kuuana kama Morogoro ndiyo Serikali ianze kuingia pale. Tunawaomba sana Serikali ije kuangalia tatizo hili tulionalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 13 Novemba, 2020 wakati anafungua Bunge hili la 12 Marehemu Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Magufuli alisema, Serikali itaongeza hekta kufikia milioni sita kutoka 2,788,000/= kwa ajili ya maeneo ya wafugaji, malisho na maji. Serikali mmefikia hatua gani katika hilo? Alisema mwaka 2020 tarehe 13 Novemba; Serikali ni ile ile Serikali ya Awamu na Sita, mama alipokuja alisema, "Kazi Iendelee." Kwa hiyo, moja ya kazi inayoendelea ni hii. Nawaomba sana Wizara mhakikishe kwamba tunatenga maeneo ili wasiingiliane wakulima na wafugaji, tuishi salama. Sisi wote ni Watanzania, lakini lazima tuwa-*guide* hawa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika ukusasa wa 47 imesema, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi imetenga jumla ya hekta 128,000 kwa mwaka huu na Mkoa wa Ruvuma umetengewa hekta 1,696 basi, kati ya 128,000 na kuna ng'ombe hatari huko. Ng'ombe wote waliokuwa huko kama sehemu hizi ambazo migogoro imetulia, ndiyo ng'ombe wote wale wamekuja Namtumbo Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sana mje mtuangalie. Mkoa wa Ruvuma umetengewa hekta 1,600 kwa ajili ya wakulima. Tunawaomba mwingiliano huu kati ya sekta ya maliasili, wana maeneo makubwa; ardhi, mifugo, TAMISEMI, mkae pamoja mtupangie ili hao wafugaji wapewe maeneo, wasiingiliane na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vita Kawawa. Tunaendelea na Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi na Mheshimiwa Charles John Mwijage ajiandae.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Uvuvi na Mifugo. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza, niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu na Watendaji wote katika Wizara kwa kazi wanayoifanya na hasa kwa hotuba yao waliyowasilisha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 wakati kama huu na wakati nachangia hotuba ya Wizara hii, nilishauri juu ya umuhimu wa Wizara kuwekeza kwenye ufugaji wa samaki kupitia vizimba. Nimefarijika angalau kwenye hotuba

iliyosomwa leo kuna mabadiliko yanaonekana angalau jitihada zimeweza kufanyika na kuongeza idadi ya vizimba, dhamira ikiwa ni kuimarisha ufugaji wa samaki na kuongeza mazao ya ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hatujafanya vizuri sana kwenye uzalishaji wa mazao ya samaki na ndiyo maana kama mchangiaji mmoja alivyosema hapa wakati anachangia ukiangalia mazao tunayozalisha na kusafirisha kwenda nje Tanzania pamoja na *advantage* tuliyonayo ya kuwa na maziwa, kuwa na bahari, bado hatujafanya vizuri sana. Ndiyo maana ukiangalia kwenye *sources* mbalimbali katika idadi ya nchi ambazo zinazalisha na kusafirisha samaki kwa wingi, kwa mfano Morocco ndiyo inaongoza kwa Afrika, Namibia, South Afrika, Mauritius na Senegal, lakini Tanzania kwenye tano bora bado hatumo, bado hatujafanya vizuri sana. Pamoja na kwamba kwa mwaka huu kwa takwimu zilizosomwa na Mheshimiwa Waziri, tumezalisha *metric ton* karibu 415,000. Mwaka juzi 2020 tulikuwa na *metric ton* karibu 393,000, ninaamini bado tunastahili kufanya zaidi ya hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tu kwamba pamoja na jitihada hizi tunazozifanya kuimarisha ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba, ni vizuri tukaangalia vile vile athari hasi za vizimba ili tuweze kuzifanyia kazi zisije kuathiri ufugaji wa asili wa samaki. Kwa sababu tunaweza kuwa tunalalamika samaki wanapungua, kumbe ni matokeo ya athari hasi za vizimba hizi; kunaweza kuwa na athari za kijenetiki na kadhalika. Kwa hiyo, ni vizuri tukaangalia vile vile kiutafiti kama zipo athari hizo, basi tuweze kuzifanyia kazi ili wakati tukiendelea na mpango huo ili wavuvi wetu wa asili wasije kuathirika na ufugaji wa vizimba ambao tunawekeza hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nilitaka kulichangia ni juu ya uvuvi wa samaki aina ya dagaa. Dagaa

ni samaki wanaopatikana kwenye maziwa tuliyonayo kwenye nchi yetu hii; Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Ziwa Victoria; na kwa sehemu kubwa inatoa ajira nyingi sana kwa wananchi wetu hasa akina mama na vijana. Hata hivyo kumekuwa na shida kubwa sana, na kwa mtizamo wangu Serikali haijawekeza ipasavyo katika kuongeza thamani ya mazao ya samaki hawa aina ya dagaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali, kwa mfano, mwaka 2021, Shirika la Chakula Duniani *(FAO)* kwa mujibu wa ripoti yao iliyotolewa mwezi Desemba inaonesha samaki hawa aina ya dagaa, pamoja na kuzalishwa lakini *post-harvest loss* ipo kwa karibu asilimia 16 na wakati wa masika/wakati wa mvua inaenda mpaka asilimia 60 jambo linaloifanya Serikali yetu kukosa mapato ya karibu Shilingi bilioni 50 kila mwaka kwa sababu ya kushindwa kuwekeza kwenye uvuvi huu na kuweza kuongeza thamani ya mazao haya yaweze kuuzwa na kusafirishwa nje ya nchi na kuweza kusaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naombe sana kama nilivyotangulia kusema, hii ni ajira kubwa sana ya wananchi hasa vijana na akina mama. Kwa takwimu mlizotoa kwenye hotuba yenu, wananchi karibu milioni nne wanapata kula yao na maisha yao kutokana na uvuvi. Pia uvuvi huu wa dagaa unaajiri karibu asilimia 70 ya wananchi na kutengeneza mzunguko mkubwa sana wa kipato kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali kupitia kwenye Wizara, wekezeni kwenye uvuvi huu wa dagaa mwasaidie wananchi wetu, tusiwe tunatoka tu kwenda kufanya *operation* na kuathiri maisha ya uvuvi wa watu wetu. Tuwekeze vile vile, tuweze kuwaelimisha na kuongeza mitaji yao wafanye uvuvi wa kisasa na kuongeza thamani ya mazao ya samaki hawa hasa dagaa. Kwa sababu

ikiongezeka thamani ya dagaa kama nilivyotangulia kusema, itaboresha sana maisha ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mchango wangu ulikuwa kwenye maeneo hayo mawili. Naomba sana wekezeni kwa kiwango kikubwa sana kwenye uvuvi wa dagaa. Tunapokuwa tunapoteza kwa mwaka Shilingi bilioni 50, ni pesa nyingi sana ambazo tungeweza tukafanyia mambo mengine mengi. Kwenye eneo kama la kwangu la Ukerewe pale, sehemu kubwa, zaidi ya asilimia 90 ya vijana na akina mama wanapata maisha yao kutokana na uvuvi wa dagaa, tuwawezeshe, tuwasaidie, tuongeze thamani ya mazao yao. Leo dagaa wanaovuliwa wanaanikwa kwenye mchanga, wakati mwingine wakati wa mvua hawakauki, inaathiri kipato kwa ujumla na maisha ya wananchi wa eneo langu la Ukerewe, naamini na kwenye maeneo mengine katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Serikali kupitia Wizara wekezeni kwenye eneo hili muweze kuwasaidia wavuvi wetu wa dagaa tuongeze thamani ya mazao yao, itasaidia sana uchumi wao na uchumi wa Taifa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naungana mkono hoja. Ahsanteni sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, tunaendelea na Mheshimiwa Charles John Mwijage, halafu Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, wajiandae.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ndugu na Wizara ile ya Kilimo ambazo ni sekta za kiuzalishaji. Nilishaeleza mwanzo umuhimu wa sekta hizi, sasa niende kwenye undani wa sekta hizi, *the*

*agricultural sector,* kwa wale ambao hawakusoma kilimo, inahusu mazao *(growing crops)* inahusu ufugaji wa ndege na kuku *(poetry)*, inahusu kufuga wanyama *(animal husbandry),* inahusu kufuga samaki *(aquaculture),* inahusu maua *horticulture* na *floriculture*. Sasa tunazungumza kile kipande kingine baada ya kumaliza kipindi kile cha kwanza kilichokwenda na zawadi ya mama Mkoa wa Kagera. Ngoja nichambue hii nione kama na hapa kuna zawadi ya mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwanza suala la ufugaji wa vizimba. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezungumza na mwaka jana, 2021 nilizungumza, kwamba Misri anafuga samaki tani 1,400,000, lakini maji aliyonayo Misri ni madogo, ni machache kuliko maji ya Tanzania. Nakubaliana kuna kampuni moja ya simu zamani ilikuwa na kaulimbiu inasema: "*Now You Are Talking.*" Naweza nikasema *Government, now you are talking, au now you are coming. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma taarifa ya Waziri anasema atatengeneza vizimba 19,500 na kufanya *environment impact assessment* ili atengeneze makazi kwa ajili ya ufugaji. Kagera atatupa maeneo tisa, lakini muhimu ni kwamba atazalisha tani 100,000. Kabla ya hapo tulikuwa tunazalisha tani 12,000. Tunatoka tani 12,000 anakwenda tani 100,000. Misri, *now we are coming* Misri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kuvutia kwamba mapato ya samaki hizo tani 100,000 ni Shilingi bilioni 600. Mauzo ya kahawa ya Tanzania kutoka Septemba, 2020 mpaka Septemba, 2021 ni dola za Kimarekani 163,000 au shilingi bilioni 383. Ina maana kwa kuwekeza kwenye vizimba vya Ziwa Victoria samaki watazidi kahawa, lakini hatutaacha kahawa, tutafanya kahawa, tunafanya na hiyo. Ndiyo hiyo Kamati yetu ilikuwa inalalamikia, ndiyo hiyo Kamati yetu ilikuwa inashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ambayo nami natumika naiunga mkono kwa maneno mawili; imeiambia Serikali changamoto za ugawaji wa vitalu zitatuliwe mara moja, nawaunga mkono. Jambo la pili, tuhimize kufuga, siyo kuchunga. Ndugu yangu Mheshimiwa Vita Kawawa kinachomwogopesha ni kuchunga, siyo kufuga. Tuhimize kufuga, siyo kuchunga. Huwezi kujenga uchumi wa nchi hii bila kufuga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze jambo lingine kuhusu upungufu; na katika hili namwomba samahani Mheshimiwa Mama Joyce, naishauri Serikali, simzungumzi mumeo Mheshimiwa Mama Joyce unisamehe, nanyi Wajumbe wa Kamati ya Siasa nazungumza kuhusu Serikali. Taarifa yote hatuzungumzi tutauza nini nje? Niliwaambia juzi, kiburi cha Ukraine anauza nje Dola bilioni 64 kwa mwaka, hatujazungumza hapa tunauza nini nje? Tunahitaji kuuza nje kusudi tuje tuweze kujenga Taifa imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake alitaja jina langu, baada ya kulitaja, simu zikaanza kurindima hapa; Wabaki Wabaki, umekuwaje Mwijage? Umekuwaje? Kwa nini Mheshimiwa Waziri alinitaja?

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, katika randama ukurasa wa 42, mimi ni Mbunge wa Muleba. Niliiuliza Serikali, mgogoro wa eneo la Mwisa II utatuliwe ili wananchi na wafugaji waendeshe shughuli kwa tija kubwa na kwa amani. Ndicho nilichoiambia Serikali. Mgogoro wa Mwisa II utatuliwe ili wananchi na wafugaji waendeshe shughuli kwa tija na kwa amani. Katika kuendesha tija kwa amani, wazalishe maziwa na bidhaa nyingine za kilimo, ndiyo nilimwuliza Waziri. Halafu nikasema, katika kumwuliza Waziri na Serikali yake, wananchi wa eneo la Lutoro wapewe ekari sita, siyo 'angalau'. Lile neno 'angalau' sikulisema. Wapewe ekari sita kutoka eneo la Mwisa II lenye hekta 67. Sikusema kutoka eneo la Mwisa II, rejea kwenye komuniki Mheshimiwa

Waziri. Ni pale walipo; na pale walipo nitakuja nikupe vifungu hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa akanijibu akasema suala la Mwisa II bado lipo chini ya uwezo wa Wizara, ambapo Wizara itashirikiana na mamlaka husika katika Mkoa wa Kagera kwa kumaliza suala hili. Nakubaliana naye. Kumbe kumaliza matatizo ya Mwisa, Waziri ana uwezo na mkoa una uwezo, mnasubiri nini sasa? Komuniki tuliandika, watu wanalala nje, mnasubiri nini? Watu wanalia, mnasubiri nini? Watu wanachunga kwenye makaburi ya watu, mnasubiri nini? Kumbe Mkoa wa Kagera unaweza, na Waziri anaweza, mnasubiri nini watu na wanalia? Nitaipata wapi zawadi ya mama hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende Lutoro. Aidha, mahitaji ya wananchi wa Lutoro yalibainishwa na Kamati Maalum ambayo iliwashirikisha wananchi kwenye funga na fungua semi "iliwashirikisha wananchi." Iliwashirikisha wapi? Wananchi ulikutana nao wapi? Nani alikutana na wananchi? Utakutana na wananchi wa Lutoro bila Mwijage, utawapata wapi? Hujawahi kukutana na wananchi. Kwa pamoja ilibainisha, eti ilibainisha watu wapewe kaya ekari mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lutoro wanampongeza Mheshimiwa Bashe kwa kusema atatoa ekari tano kwa mtu, hii haijawahi kukaa mahali popote, wanakudanganya. Nimekuomba samahani Mheshimiwa Mama Joyce, umwombee mumeo, huyu ni rafiki yangu. Halafu watasema; nisikilize, jambo la maudhi anasema, watapewa ekari mbili na endapo kutakuwa na mahitaji zaidi, wananchi wanatakiwa kushauriwa kutafuta maeneo hayo nje ya ranchi. Wananchi wanatakiwa kutafuta, watu wa Ngorongoro mbona hamkuwashauri waondoke? Wananchi wangu ndio mnawashauri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Rutoro ni la kisheria suala la Rutoro ni la utu suala la Rutoro ni la kisiasa! Mwaka 2015 *Gymkhana Club* Bukoba aliyepanda jukwaa ni mimi hali ilikuwa mbaya kule nenda kwenye *video* muangalie Rutoro ndio iliamua watu hawawezi kuondoka hiyo ndio iliamua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nikwambie nazungumka kwa ajili ya watu ya Kyebitembe naizungumzia Karambi naizungumzia Kasharunga Mubunda na Ngenge naizungumzia Rutoro mimi ni Mbunge wa Muleba ndio mwakilishi wa wananchi asitokee mtu yeyote akasema ndio mwakilishi wa wananchi ni mimi na Kikoyo hakuna wa kuchonga na nikifa mimi nitazikwa kwetu hakuna mwingine. Na niwaeleze watu wanakwenda eti Mheshimiwa Mwijage hamsemei mama unakwenda kwenye eneo la watu unachoma nyumba 280 unawaambia kazi iendelee Samia hoyee! kuna mtu atakujibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba 280 zimechomwa Migomba imekatwa halafu mtu anasema Mheshimiwa Samia hoye, sio Mheshimiwa Samia ninaye mjua Mama Samia anatoa zawadi nakubaliana na wewe ninachokueleza tukubaliane…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage naomba umalizie sentensi yako.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema Wizara yako Wizara ya Ardhi Wizara ya TAMISEMI tukae chini, chini ya Waziri Mkuu tuweze tukatafuta mstakabali wa suala hili vijiji vilivyopo pale vimeandikwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nakaa chini kabla sijakaa naomba mezani kwako niwasilishi mgogoro wa Muleba na Naruko naomba niuwasilishe mezani. *(Vicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa…

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wasaidizi wa Mheshimiwa njooni mchukue hapa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwijage. Tunaendelea na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud wajiandae. Mheshimiwa Simai Hassan hayupo.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Wizara ambayo ipo mezani kwetu tunayoijadili leo ni Wizara inayoenda kugusa hali halisi za watanzania kwa jina lingine kule mitaani hii tunapenda kuita Wizara ya kitoweo kwa sababu Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa bajeti yako kwa kiasi fulani imefanya kazi na imejibu hoja kwa kiwango kikubwa ambacho Wabunge tulitarajia kusikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri wewe ni rafiki yangu sana na urafiki wetu umekuja kutokana kwamba wewe unatoka eneo linalotoka wavuvi na mimi natoka maeneo yanayotoka wavuvi kule Zanzibar. Lakini ni ukweli kabisa sina lengo la kuzuia shilingi kwa namna yoyote ila wakati ambapo utapoweza kuwasilisha bajeti hii na kuja kutuhutubia kwa mara ya mwisho kufunga hotuba yako ukishindwa kutuelezea yale matarajio ambayo Wabunge sisi tulitarajia kuyasikia yawepo katika hotuba yako basi sisi tutaacha kujadili hotuba yako baadaye tutakuja yale

ambayo wananchi wametutuma tuje tuyazungumzie hapa kwasababu wao ndio wanapenda wayasikie hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni miongoni mwa nchi tatu bora ambazo zimejaaliwa kuwa na vyanzo vingi vya maji katika Bara la Afrika, Tanzania tumebahatika kuwa na mito mingi, kuwa na bahari kuu kuwa na maziwa mengi tu inasemekana hata chanzo cha mto *Nile* kinapatikana Tanzania na ndio maana nchi za jirani zetu zinazotuzunguka kama vile nchi za Malawi, Kongo, Zimbabwe zinategemea sana kupata samaki wao kupitia Tanzania kwa mfano Kongo na Malawi ni wafanyabiashara wakubwa sana wa dagaa kwa nchi ya Tanzania naizungumza hii kwasababu ya kuonesha jinsi gani umuhimu wa sekta hii ya mifugo ilivyo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake dagaa kwa kiasi kikubwa hata akinamama na wavuvi wadogo wadogo wana uwezo wa kuifanya hii shughuli, licha ya umuhimu wa sekta hii lakini bado sisi kama Serikali hatujawa *serious* katika kuwekeza na kutafuta wawekezaji watakaoweza kuja kui-*support* sekta hii na sina *doubt* na utendaji wa Mawaziri. Kwasababu wakati mwingine tunaweza kuwabebesha mzigo mkubwa Mawaziri nimejifunza kitu leo Waziri wa Uvuvi na Mifugo unatuwasilishia bajeti katika bajeti iliyopita utekelezaji wake maana yake fedha iliyokuja katika utekelezaji wa miradi ya bajeti ni asilimia 3.3 katika miradi ya maendeleo lakini kwenye mishahara asilimia 66. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi haya tunayoyapanga kwenda kutekeleza kama fedha usipopewa unakwenda kutekeleza nini, maana yake wakati mwingine tuna uwezo wa kumbebesha lawama mtu ambaye hastahili ingawa sio lengo, sasa kama kweli tunataka kunyanyua mifugo yetu kama kweli tunataka kuendeleza sekta ya uvuvi ni lazima Serikali tuangalie utaratibu wa kuwawezesha wavuvi wetu, hivi sheria na hizi taratibu za uvuvi ambazo zinaonekana

kwamba ni kikwazo kwa wavuvi wadogo na wavuvi wakubwa hakuna haja ya kuendelea nazo Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo hii unaweza ukatunga sheria ukamwambia mtu usivue sehemu fulani, nyavu fulani usitumie kuvua lakini ukashindwa kumpa mbadala wake hakuna anayependa kufanya uhalifu lakini mazingira wakati mwingine yanalazimisha na sheria ngumu zikachangia katika hayo. Mheshimiwa Waziri Serikali ione haja ya kuwarahisishia upatikanaji wa pembejeo za uvuvi itafute njia na ikae na wawekezaji watakaoweza kuisaidia sekta hii ya uvuvi watakaoweza kuwapatia wavuvi wetu vifaa vya uvuvi kama vile mashine, na pembejeo nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wavuvi wetu wanavua uvuvi ambao ni wa holela mtu anatoka anakwenda kuvua lakini hajui wapi anapokwenda anakwenda kubahatisha hajui samaki wapi anakwenda kuwakamata huku tutoke kwenye njia hizi za *local* sasa hivi twende na utaratibu unaokubalika tulingane na wavuvi wenzetu wa dunia za nchi nyingine. Katika hili nioneshe mfano mmoja nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kwa jitihada kubwa anazozifanya kupitia sera ya uchumi wa bluu lazima tumpongeze kwa hilo. Yeye sasa hivi ameshaandaa takribani boti 557 kwenda kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo na vi-holi vile vya kuvunia mwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hali kama hii wananchi wamekuwa wanavua maji madogo samaki wengi tunawaacha katika uvuvi wa maji marefu au bahari kuu lakini kule watafikaje? Vyombo wanavyotumia ni mtumbwi, mtumbwi hauwezi ukautumia kwa uvuvi wa maji marefu au uvuvi wa bahari kuu na ndio maana unasikia kesi nyingi zinakuja, Mamba kala Mtumbwi na abiria aliyekuwepo ndani yaani huu ndio ukweli ulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu sasa katika mazingira kama hayo ndio tunasema tunawathamini na kuwa-*support* wavuvi wetu sasa katika suala hili bajeti ya killimo ipo vizuri kwasababu asilimia kubwa imewagusa wananchi wadogo lakini sekta nyingine ipi inayowagusa wananchi wadogo na wakombozi wa maskini, ni sekta hiyo ya uchumi wa bluu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wale watu ambao wanaonekana hawana ajira watu ambao wanaharakati wanaona kwamba bamba gumu kwa upande fulani wa kimaisha wanajikita katika sekta hizi ya uvuvi na mifugo. Maana yake na sisi kama Serikali tuwatafutie njia sahihi tukae na tujue tunawa-*support* vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nikwambie kitu kimoja tujifunze kutoka kwa wenzetu nchi kama *Norway* iliyokuwepo Bara la Ulaya ni miongoni mwa nchi zinazojulikana kama *Nordic Countries* hii nchi inazalisha gesi nyingi nchi hii inazalisha mafuta mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kiukweli asilimia 70 ya uchumi wao inategemea uvuvi kwanini, wao wamewasaidia wavuvi wao na wakaipa thamani inayostahiki sekta hii ya uvuvi. Mheshimiwa Waziri katika hili unapozungumzia suala la zima la uvuvi, kilimo, ufugaji maana yake unazungumzia vitu tofauti na mazingira yatatofautiana, kwa kule Zanzibar sisi sekta ya uvuvi ndio mkombozi wetu, kwa sababu ardhi yetu sisi ni ndogo ukilinganisha na idadi ya watu. Lakini kwa huku upande wa bara kilimo lazima kitakuwa na tija na kitapewa *support* kubwa sasa sisi tunategemea hii sekta ya uvuvi zaidi ikilinganishwa na kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hali kama hii Mheshimiwa Waziri kumekuwa na changamoto kubwa mno kwa wavuvi wetu hususani katika masuala haya ya hawa

wanaohusika na huu uvuvi wa bahari kuu, changamoto za leseni ni bei kubwa mno Mheshimiwa Waziri kwa maskini, leseni za uvuvi wa bahari kuu maana yake ni changamoto kwa wavuvi, lakini isitoshe suala la kuwachaji mara mbili wavuvi wanaotoka Zanzibar *regardless* aina gani ya uvuvi kwa sababu vyombo vile wanakuwa wamevikatia leseni wanapokuja huku wanachajiwa tena leseni, matatizo kama haya ni masuala ya kukaa na kushirikiana na wale wenzenu wa Zanzibar kutafuta zile changamoto kuondosha hili migongano isiyokuwa ya lazima. . *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri najua Wizara yako ukiangalia waajiriwa wengi sio rasmi na hii ningependa unipatie ufafanuzi kitu kimoja Mheshimiwa Waziri, kuna suala zima la mvuvi na changamoto zinazowakabili lakini *research* fupi niliyoifanya kwamba changamoto hizi zinatokana kwamba wewe na Wizara yako humjui mvuvi ni nani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii ninazungumza na kama sio kweli basi ningeomba unifafanulie hakuna sheria ya Tanzania hii inayomtafsiri moja kwa moja maana ya mvuvi ni nani, naizungumza hii kwa hoja yangu. Hapa unaomba fedha kwenda kuwasaidia wavuvi unaomba fedha hizi kwenda kuwasaidia wavuvi lakini wavuvi ni nani wakati hatuwatambui katika sheria, umeweka tu katika sheria taratibu za uvuvi ukaweka aina za uvuvi lakini hakuna maana leo hii inapotokea fursa za mikopo…

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi yako Mheshimiwa.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja inapotoka fursa za mikopo zinaenda kwa wafugaji na wawindaji wa paa zile nyavu badala ya kwenda kuwindiwa baharini kwa sababu mtu leo atoke na mshipi aende kuingia chomboni utahesabu kama ni mvuvi kwa mujibu wa sheria zenu. Sasa hizi fedha badala ya kuomba kwenda kuwasaidia hawa wavuvi tuletee yaani omba fedha

hizi kwa ajili ya kurekebisha kwanza angalau hizi changamoto ndogo ndogo zinazotokana na… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashirikia kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Simai Sadiki. Tunamalizia na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kwanza kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira yake ya dhati kabisa kuhakikisha sekta zetu hizi za uzalishaji kilimo, Mifugo na uvuvi vinakwenda sasa kumuinua Mtanzania na kuinua uchumi wa Taifa hili, na hayo hayatekelezi kwa maneno bali anatekeleza kwa vitendo kwa maana kubwa kwamba sekta hizi ameziongezea bajeti katika matumizi yake kwa kipindi cha mwaka huu bajeti yetu ya Wizara hii imefikia bilioni mia moja tunapongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulea mimba ni kazi lakini kulea mwana ni kazi zaidi Serikali, Rais wetu, Viongozi wetu Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wanahangaika huku na kule kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati na kimaendeleo. Tunaomba fedha hizi zitumike kwa dhamira zilizokusudiwa zisiende kutumika kwa matumizi mengine kwa maana ya kwamba Serikali kupitia Wizara hii iwe wakali na iwe wasimamizi wazuri kuhakikisha fedha hizi zinafanya kazi zilizokusudiwa kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania na Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia sekta ya mifugo, sekta ya mifugo ina changamoto nyingi lakini kutokana na mpango wa Bajeti hii tuliyopewa na

Mheshimiwa Waziri baadhi ya changamoto nyingi zinakwenda kutatuliwa kutokana na fedha zitakazoingizwa kwenye bajeti tunaomba fedha hizi Mheshimiwa Waziri na wanaohusika na utoaji wa fedha, fedha hizi ziende kwa wakati na zitoke zote ili zikatekeleze hayo majukumu yaliyopangwa kumuinua mfugaji kumuinua mvuvi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uwekezaji katika sekta hii ya mifugo suala la ngozi, ngozi zetu bado zina changamoto katika soko la dunia masoko yapo lakini ngozi hazikidhi viwango. Wizara imetoa mpango wamesomeshwa Maafisa Ugani kwenda kuangalia madaraja ya ngozi, lakini hawa maafisa ugani wanatakiwa kufanya zaidi ni kumuelimisha mfugaji namna ya kuhakikisha ile ngozi haiharibiki na inapata madaraja ya juu mfano kuwapiga mikwaju hovyo wale wanyama ng'ombe inaharibu sana ngozi na inakosa thamani kuwachoma choma hovyo sasa hapa elimu itolewe kwa wafugaji kwamba sio nyama tu lakini hata ngozi ni bidhaa kubwa ambayo itamsaidia kuinua kipato chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la ndani kwa maziwa lipo natoa mfano *ASASI* anapata asilimia 60 tu ya mahitaji yake kutokana na uwezo wa kiwanda ana ukosefu wa asilimia 40 ili kukidhi mahitaji ya kiwanda nashauri kwa vile miundombinu ya uwekezaji pale ipo eneo karibu na *ASASI* basi tuongeze uhamasishaji wa ufugaji bora katika maeneo yale vijana tuwahamasishe wafuge kisasa tupate mazao bora ya maziwa kwa maana tayari soko kwenye eneo lile lipo la uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni soko la ndani wala sio soko la nje na hivi sasa mfano Kiwanda cha ASAS kina mpango wa kutengeneza maziwa ya muda mrefu kwa maana ya maziwa ya unga kwa hivyo watahitaji sana malighafi ya maziwa. Hilo soko lipo kwa maeneo ya Iringa.

Nikiendelea kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Serikali imezuia kiwanda cha kuchinja Punda na wameomba kwamba uwekezaji ule sasa ubadilike matumizi wachinje mbuzi, kondoo na ng'ombe hapa inaonekana kwamba soko la punda ni kubwa na linaweza likaongeza uchumi wa nchi na linaweza likatoa ajira kubwa kwa vijana na wanawake na wafugaji kwa jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ihamasishe ufugaji wa punda ili kukidhi masoko ya hawa wawekezaji waliokuja kuwekeza punda ili tuweze kupata fedha za kigeni lakini tuongeze ajira kwa vijana wetu hapa inaonekana punda wanatakiwa sana huko duniani sasa kama sisi punda wetu wamepungua tumezuia sasa hawa waliokuwepo tuongeze uzalishaji wawe wengi zaidi ili tupate hilo soko la punda duniani na vijana wetu wapate ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ufugaji mnahamasisha tuwekeze zaidi kwenye malambo kwa maana ya mabadiliko ya tabia nchi, yanaharibu sana upatikanaji wa uhakika wa maji. Nashauri wafugaji na wavuvi waitumie benki ya kilimo ile benki siyo ya kilimo peke yake, tutoe elimu kwa wafugaji wetu na wavuvi kwamba benki ya kilimo inawahusu wao pia wafugaji na wavuvi. Kwenye sekta ya uvuvi kwanza nipende kuchukua fursa hii kuwapongeza wavuvi wote Tanzania kwa kazi kubwa wanayoifanya. Uvuvi ni kazi ngumu unatoka usiku unaacha nyumba na watoto, unakwenda baharini hujui kama utafika au hufiki, hujui kama utakwenda au utarudi, hujui kama utavuna au hauvuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kazi tu ya kubahatisha vyombo vyenyewe ni duni hali ya bahari tunaijua haina muda haina wakati wakati wote inapata wazimu huko baharini. Nashauri Serikali iongeze uwekezaji kuinua wavuvi wadogo wadogo ili kunusuru Maisha yao lakini kupata tija ya kipato chao kwa muda wote huu wanafanya kazi tunapata

lishe tunapata vitoweo lakini bado hali ya mvuvi ipo chini na duni na hana kipato cha uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea ufugaji wa viumbe kwenye maji Wizara imeweka mpango mzuri napongeza Serikali kwa mpango huu tuimarishe na tushajirishe vijana wetu kuingia kwenye uwekezaji wa uvuvi kwenye maji, hivi viumbe maji sio samaki tu kuna kaa, kaa wana faida kubwa na wana fedha nyingi za kigeni lakini kuna majongoo, majongoo yanatakiwa sana duniani na yana fedha nyingi za kigeni kupitia majongoo, lakini katika uvuvi huu wa viumbe kwenye maji tunapata madini ya Lulu pale, tukiwafundisha wavuvi wetu namna ya kutengeneza Lulu tutapata fedha za kigeni kupitia madini ya Lulu, Lulu ni madini na yanapatikana kupitia viumbe kwenye maji na yanafugwa, Lulu haichimbwi, lulu inapatikana baharini na lulu inatengenezwa kwenye vizimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uvuvi wa bahari kuu Serikali ihakikishe kwamba tunawekeza zaidi kwenye bahari kuu, mipango na mikakati mingi tumeiona tunaomba mpango hii ifanikiwe kwa sababu tunahimiza uvuvi wa bahari kuu tunataka kulitumia shirika la *TAFICO*, Shirika la *TAFICO* linahitaji uwekezaji mkubwa linahitaji fedha nyingi kwa sababu ukiliangalia hayo maeneo yake ya uwekezaji tayari mmomonyoko bahari inakwenda kula yale majengo, kwa hivyo kwenye uwekezaji ule wa majengo kunahitaji fedha nyingi kuzuia bahari yale majengo yasiharibiwe na maji ya bahari yakianza kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na huyo ni mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu na muda wetu umefikia mwisho, kwa hiyo jioni tutaanza na Mheshimiwa Asya Mwadini Mohammed, Mheshimiwa

Simon Songe, Mheshimiwa Jafari Chege na Mheshimiwa Stella Manyanya.

Lakini kabla sijasitisha shughuli za Bunge kuna tangazo dogo Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa mnakumbushwa wale wote ambao hawakwenda kutembelea mabanda ya Wizara ya Madini yaliyopo kwenye maeneo ya Bunge hata wale ambao wameshakwenda lakini wanatamani kwenda tena basi mnakaribishwa kwa sababu leo ni siku ya mwisho.

Kwa hiyo nawaomba wote kuwakumbusha msisahau kupitia kwenye mabanda yetu.

Samahani ni Mabanda ya Wizara ya Nishati sio Madini kwa kweli hiyo ilikuwa imenikaa kichwani kwa hiyo ni nishati na siyo madini.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo niwatakie mchana mwema na ninasitisha shughuli za Bunge hadi saa Kumi na Moja Kamili Jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali.

**25 MEI, 2022**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na majadiliano sasa namuita Asya Mwadini Mohammed ajiandae Mheshimiwa Simon Songe na Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii muhimu ya Wizara ya Uvuvi kwa maslahi mapana ya Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nitoe pongezi zangu za kipekee kwa Rais wa Zanzibar Daktari Hussein Mwinyi kwa kuja na sera ya uchumi wa bluu. Ukisoma randama ya Uvuvi bajeti ya mwaka 2021/2022 kwa uvuvi wa bahari kuu ilitengewa bilioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi lakini kwa masikitiko makubwa mpaka Aprili mwaka huu hawakupewa chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii imeendelea tena kurejea yaleyale mambo wame-*copy* na ku-*paste* wameomba tena kwa Mwaka 2022/2023 bajeti hii ambayo leo tunaijadili wameomba tena Bilioni 50 kwa ajili wa ujenzi wa bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna ambaye hahitaji kuona maendeleo ya Taifa hili na tupo hapa kwa ajili ya kuitumikia Taifa letu, Mheshimiwa Waziri alipokuja kutoa hutuba yake alizungumza mambo mazuri sana na ukweli yakitekelezeka Tanzania itakuwa imepiga hatua kwenye Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu. *(Makofi*

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumza wanao mpango madhubuti kwenye hotuba yake kwamba wataweza kutoa vibali vya leseni vipatavyo 21 kwa meli za nje na za ndani kwa wawekezaji ambao watawekeza kwenye Bahari Kuu. *(Makofi*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama leo tunajielekeza kutoa leseni, yaani tunatoa leseni ili tuweze kuingiza vyombo nchini lakini *parking* ya vyombo hatuna, hili ni jambo la kusikitisha ni sawasawa na kutoka kwenda Mjini kununua *furniture* lakini huna nyumba ya kuviweka, maana yake hivyo vyombo utaishi navyo barabarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali kama tumeamua na tumejidhatiti kweli tunahitaji kwenda kwenye uvuvi wa Bahari Kuu ni lazima sasa tutumie nguvu za ziada ili Wizara hii iwezeshwe wapewe fedha haiwezekani vipindi viwili vya bajeti watu wanaomba kujenga bandari kitu ambacho ni maslahi ya mapana ya Taifa, kitu ambacho kitaingiza mapato kwenye Taifa hili halafu wanachinjiwa baharini hawapewi chochote, haiwezekani! Ukweli kwenye suala hili nitarudi kulishikia Shilingi Mheshimiwa Waziri alete-*commitment* hapa anawapa fedha kujenga bandari ama hatawapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma taarifa ya *ZAFICO* kwa sababu tukizungumza wavuvi wa Bahari Kuu ni sehemu ya Muungano. Kwa hiyo, kuna mashirika mawili ambayo yana-*practice* uvuvi wa bahari kuu ambao ni *ZAFICO* na *TAFICO* kwa Tanzania Bara, *ZAFICO* lipo kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia kuna changamoto mbalimbali ambazo *ZAFICO* wamezi-*mention* kwenye taarifa yao, kwanza wamezungumza *issue* ya leseni, wamezungumza *issue* ya leseni kwamba, kuna leseni ambazo

zitatolewa kwa kipindi cha miezi Sita ambapo meli ziwe zina urefu wa mita 24 na leseni hizo wanasema kwa wawekezaji wazawa *residential* watalipa Dola 4,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo na mkakati wa kwenda Bahari Kuu ni kuwanusuru wavuvi wetu wadogo ambao wanavua uvuvi ambao hauna tija wanapotea hovyo, wanapoteza mali zao na maboti yanazama na wanapoteza maisha yao, ndiyo maana tunataka ku-*move* kutoka kwenye huu uvuvi mdogomdogo watu ambao hawaeleweki waende kwenye uvuvi wa Bahari Kuu. Sasa huyu mwekezaji mdogo mvuvi mlalahoi anayetoka kwenye mazingira magumu kama aliyetoka Asya, kwamba leo unamwambia leseni kwa muda wa miezi Sita akalipe Dola 4,000 ambayo sawa na pesa ya Kitanzania 9,268,000.00. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza anakwenda baharini hakuna utaratibu maalum ambao umeandaliwa ndani ya bahari maana yake hakuna *GPS* ambazo zinasoma hapa kuna samaki au hapa hakuna. Kwa hiyo, anakwenda *yaallah Insha'Allah* maana yake anamuomba tu Mwenyezi Mungu nikipata hewala nisipopata mashallah, kwa hiyo, anakwenda tu moja kwa moja lakini atakapofika kule baharini pili akifika baharini muda ambao atautumia hawezi kuvua kwa siku moja akarudi wakati alipokuwa anaenda na kidau, leo atakaa pengine muda wa wiki moja ama zaidi ya wiki moja anasubiri kutafuta samaki ili aweze kurudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nje tu na hiyo gharama ya leseni maana yake wiki nzima anavyoingia baharini kutafuta hao samaki kuna gharama za mafuta ambazo meli inapaswa ikae itulie na isizimwe hata kwa muda wa dakika moja ndani ya wiki nzima. Mafuta ambayo wanayatumia hawa ndugu zangu wavuvi wawekezaji hawa ambao wanakwenda Bahari Kuu kwa chombo chenye urefu wa mita 24 maana yake mafuta hayatapungua kuanzia lita 9,000 na kuendelea, tena hapo watakaa kwa muda wa wiki moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mafuta mtu anayejaza, masikitiko mengine ni kwamba mtu anayejaza mafuta mwenye *Prado* yake nje anauziwa lita 3,000 lakini na mwenye meli ambaye anakwenda kufanya kazi anauziwa naye lita ile 3,000, hii siyo sawa! Kama kweli tunao mpango wa kuwasaidia wavuvi wetu, maana yake lengo la ku-*move* kwenda Bahari Kuu na watu wakajipige wakakope, wakafanyaje, tunahitaji kuwasaidia tujiandae hata tukafanye mazungumzo kwenye suala zima la mafuta, kuwe *at least* kuna ahueni wa tofauti ya mtu ambaye anayejaza gari kipande cha kawaida na huyu ambaye anaenda kufanya hii kazi kwa wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna gharama ambayo hiyo lita 9,000 wanayosema mafuta haya ili akae wiki nzima aweze kufanya kazi, ana uwezo maana yake lita 9,000 ukizidisha na 3,000 ya lita ya mafuta anaweza akatumia milioni 27 kwa wiki. Sasa milioni 27 hiyo jiulize kwa chombo chake cha mita 24 ndani ya wiki moja anao uwezo kweli wakupata samaki zaidi ya milioni 27. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali kwa namna bora, kwanza kabisa wakatengeneze bei za mafuta za kuwasaidia wavuvi wetu ambazo ziwe tofauti na za magari. Pili, kiwango cha kodi ambayo ni leseni ambayo nimeshaizungumza nayo kwa wazawa kama kweli tunahitaji kuwasaidia nayo ikapunguzwe. Kwasababu ukitoa hivi vitu vya mafuta maana yake kuna gharama nyingine za uendeshaji, wafanyakazi lazima awepo ndani ya wiki anunue chakula, lazima awe na chambo ambacho nacho ni changamoto nyingine. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kengele ya pili.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi mengine nitayaandika kwa maandishi.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ukipata hewalah ukikosa *ishallah*. Namuita Mheshimiwa Simon Songe ajiandae Mheshimiwa Jafari Chege, jiandae Mheshimiwa Stella Manyanya. *(Kicheko)*

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hotuba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi lakini kabla yayote nikutakie heri sana katika siku yako ya leo ya kumbukizi ya siku ya kuzaliwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante bwana.*(Makofi)*

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazofanya kwa ajili ya nchi yetu pia nimpongeze kaka yangu Mashimba na Mtani wangu Mheshimiwa Ulega kwa kazi ambazo wanafanya katika Wizara hii ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa nasoma bajeti hii ya leo na bajeti iliyopita nimejifunza suala moja. Kila siku Waziri wa Maji Mheshimiwa Aweso hapa amekuwa akisema wali wa kushiba unauona kwenye sahani lakini leo ninaona wali wa kushiba sijauona kwenye sahani kwasababu bajeti ya Maendeleo Sekta ya Uvuvi 2021/2022 tulipanga Bilioni 99 mpaka Aprili, 2022 fedha zilizopelekwa kwenye Wizara ni bilioni 3.9 sawa na asilimia Sita, hii haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuomba sasa Kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu Waziri wa Fedha aangalie Wizara hii kwa macho mawili kwa sababu kuna baadhi ya Wilaya kama Busega, chanzo cha mapato ni uvuvi. Kama wananchi wetu hawatapelekewa fedha kwa ajili ya uvuvi maana yake hatujataka kuwasaidia. Kwa hiyo, tukitaka

kuwasaidia Watanzania wavuvi lazima tupeleke fedha kwenye Wizara ya Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyokuwa najaribu kufikiri namna ya kuchangia kwa Kaka Mashimba nikasema nitamuonea bure, bali nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha aangalie namna ya kuwasaidia watu wa Wizara ya Mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo moja ambalo naomba nilichangie kwa msisitizo. Kuna hawa watu wanaitwa *BMU* yaani *Beach Management Unit,* wamekuwa ni shida kwenye taasisi zetu, wamekuwa ni shida kuanzia kwenye Halmashauri lakini wamekuwa ni shida mpaka kwa Wavuvi, sasa wamebadilisha namna ya kufanyakazi zao wanaanza kuwasumbua wavuvi usiku na kuwabambikizia kesi na kesho asubuhi kuwapiga faini isiyopungua milioni tano hii kitu haiwezekani ni lazima tufikirie namna iliyobora kwa ajili ya kulinda rasilimali za nchi hasa samaki bila kutumia nguvu nyingi ambazo leo wanatumia hawa *BMU*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaishauri Wizara ifanye mpango mkakati mzuri zaidi wa kuangalia namna ya kutunza na kuangalia hizi rasilimali za Ziwa kwa kutokuwatumia hawa watu ambao wanatusumbua sasa hivi, wavuvi wanawakimbia wanapigana na Mheshimiwa Ulega, nafikiri Bunge lililopita nilikuletea hizi kesi kuna watu Wanne walikufa kwa sababu ya kupigania na hawa watu wa *BMU* ni lazima tutafute namna iliyobora ya kuwasaidia Watanzania, namna iliyobora ya kuwashauri hawa wavuvi kutumia nguvu ambayo ni rafiki na isiwe nguvu ambayo ni hasi na kuendelea kupata maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili jambo pia kuna Maafisa wa Uvuvi kutoka Wizarani, hawa watu wanapoenda kwenye Wilaya zetu wanakuwa watu tofauti kabisa na Maafisa Uvuvi wa Halmashauri, unafikiri ni taasisi mbili tofauti,

utafikiri ni nchi mbili tofauti, hawa watu wa Wizara wanakuja na sheria zao, watu wa halmashauri kuna Afisa Uvuvi nae ana sheria zake, anafahamu hivi, hawa wanafahamu hivi wanawatesa wavuvi bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ninakuomba haya malalamiko tumeyaleta, tunaomba Maafisa wanaotoka kwenye Wizara ya Uvuvi, wanapofika kwenye Halmashauri zetu wawasiliane na Maafisa Uvuvi wa Halmashauri ili wawe kitu kimoja kwa ajili ya utekelezaji wa kazi ambao mtakuwa mmewatuma kwenda kufanya. Mimi kama Mbunge nikimuuliza Afisa wa Halmashauri anasema mimi sijui, siyo maagizo ya Wizara lakini Wizara wanasema haya ndiyo maagizo ambayo tumepewa sasa mnawatuma hivyo ni lazima waende wakashirikiane na watu wa Halmashauri ili wafanyekazi iliyobora na haya itatusababishia sasa wananchi wetu waweze kujifunza kupata elimu chanya kutoka kwa hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikiwaza mara nyingi tunapokuwa tunakomesha uvuvi haramu na tunaenda kumkatamata mvuvi, tunaenda kukamata samaki sasa najifikiria suala moja, hivi tumeshawahi kufikiria hao wanaoleta hizi nyavu? Tumeshawahi kufikiria juu ya viwanda, hivi inakuwaje mvuvi anaenda kununua nyavu na mwisho wa siku anaenda kukamatwa lakini kuna mtu ameingiza nyavu kapitia bandarini, kuna kiwanda kinatengeneza nyavu kipo Tanzania, haiwezekani katika akili ya kawaida! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Wizara sasa ifanye jukumu lake, kama kuna kiwanda kinatengeneza nyavu ambazo si halali ni lazima tuanzie huko kwenye chanzo badala ya kwenda kumsumbua Mtanzania ambaye inawezekana ni *layman* kama mimi, hajui chochote hata hizo tunazoita sentimeta Sita za nyavu yeye hajui, anapewa nne lakini kumbe ninyi mnataka sita na mwisho wa siku

mnamkamata na faini Milioni 20! Mtanzania anauza nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana kwenye hili tuanzie kwenye viwanda, tuanzie kwa watu wanaoingiza hizi nyavu, najua Ulega upo *smart* kwenye kukesha, nenda kakeshe bandarini, nenda kakeshe huko kwenye viwanda kuhakikisha kwamba hawa wanaoingiza nyavu ambazo siyo salama muanze nao huko kabla hamjafika kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia najifikiria swali moja, samaki anaenda kukamatwa pale sokoni kapita tayari Ziwani kuna mtu kakatisha ushuru, kachukua hela ka-*deposit* hela za Serikali tayari lakini mwisho wa siku mtu anaenda kukamatwa kwamba samaki siyo saizi inayotakiwa! Sasa najiuliza huyu aliyechukua ushuru wake yeye hawakuwaona hawa Samaki? Ni Mtanzania huyohuyo tunampa hasara mara mbili, Lazima tutafakari kama samaki alikuwa na shida, shida ianzie ziwani palepale na asiende kukamatwa kule sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine nichangie kwenye suala zima la mikopo. Siku zote tumekuwa tukiambiwa kuna mikopo ya wavuvi lakini wavuvi wa vijijini kama Busega hawanufaiki na hii mikopo, hawanufaiki na mikopo ya vikundi kwanini? Kwa sababu sijajua kama hii mikopo inaishia Mjini kule Vijijini haifiki. Mheshimiwa Waziri Mashimba nilishakufikia, nilishakuambia suala hili tusaidieni wananchi wetu nao waweze kunufaika na mikopo inayotolewa na Wizara yako ili waweze kupata vifaa vya uvuvi kama vile *engine,* kama vile nyavu waweze kununua kutokana na ile mikopo ambayo mtakuwa mmewapa. Niombe sana suala hili tulichukulie maanani lakini kama itabidi Wizara yako watu watoke maofisini waende huko *site* wakawafundishe namna ya kuunda vikundi ili hawa watu waweze kujua namna ya kuunda vikundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani sana Wizara yako sasa iamke kuhakikisha kwamba tunaenda kufanyakazi yenye tija kwa wananchi hasa wa Jimbo la Busega ambako kuna Ziwa nawewe bahati nzuri umefika mahapa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ulifika pale Nyamikoma tukiwa na wewe, alianza kufika Mheshimiwa Mpina akiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi lakini pia na wewe ulivyoteuliwa tu ulifika pale Nyamikoma. Mliahidi kuwepo na mwalo wa kisasa, kwenye bajeti ya mwaka jana mliweka fedha kwa ajili ya ujenzi wa mwalo lakini mpaka sasa hivi tunavyozungumza hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefika ofisini kwako nimepata majibu kwamba mmetangaza Mkandarasi, ninavyokwambia mpaka leo hakuna cha Mkandarasi, hakuna kinachoendelea katika mwalo wa Wanyamikoma. Ninakupongeza katika mwalo wa Ihale angalau kazi imefanyika pale tulipata milioni 162 ninakushukuru sana Ulega ulifika pale tukapiga siasa kidogo, wananchi wakafahamu juhudi ambazo unazo, lakini sasa tumalizie na huu mwalo ambao tumekuwa tukiuahidi zaidi ya awamu tatu. Mheshimiwa Mpina aliahidi pale nafikiri ilikuwa mwaka 2018 na wewe Mheshimiwa Mashimba umeahidi pale 2021 sasa tuende tukafanye kazi tupate fedha ili tuweze kutengeneza ule mwalo wa kisasa kama ambavyo uliahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna suala ambalo nilichangia hata bajeti iliyopita. Mmekuwa mkisema kuna ukosefu wa samaki viwandani. Nami nafikiria suala moja, tutaendelea kusema hakuna samaki kwenye viwanda vyetu kwa sababu ya bei ya samaki. Hakuna mwananchi ambaye anateseka usiku kucha ataenda kuuza samaki kilo moja kwa Shilingi 8,800/=. Hakuna mwananchi atakayeenda kuuza samaki kilo tano, kwa maana ya kilo moja kwa Shilingi 11,500 likiwepo na bondo lake, haitawezekana, kwa sababu bondo

lina bei kubwa. Mwananchi anaamua sasa bora agawe zile samaki kipande kipande, auze kidogo kidogo, lakini mwisho wa siku anufaike na bondo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishauri Wizara mwaka 2021, mkitaka kufanikisha eneo hili na kuwasaidia Watanzania, ni lazima ijulikane kiwandani, bei ya mnofu ijulikane, na bei ya bondo pia iweze kujulikana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Simon.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege halafu ujiandae Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami nimepata ridhaa ya kuchangia Wizara hii ya Uvuvi na Mifugo, kwa hiyo, nianze tu kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri na namna ambavyo wamejipanga kuhakikisha yale ambayo wamekusudia kwa maslahi mapana ya wananchi yanatimia. Mwenyezi Mungu awape nguvu ili mwendelee kuitumikia Wizara hiyo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili kabla sijaanza kuchangia. Kwanza nakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunipa majosho saba kwenye kata saba kwenye bajeti ya mwaka uliopita; Bukwe, Kigunga, Kinyenche, Nyamagaro, Kitembe, Nyahongo na Mirare. Pamoja na kunipa majosho haya niseme tu Mheshimiwa Waziri, hitaji langu lilikuwa ni zaidi ya hii, kwa sababu shughuli kubwa ya kiuchumi ndani ya Wilaya yangu ukiacha kilimo, shughuli ya pili ni uvuvi, na ya

tatu ni mifugo. Kwa hiyo, natamani sana Kata zifuatazo: Kata ya Baraki, Kinyenche, Komugarabo, Nyaburongo, Ikoma, Kisumwa, Kirogoloche na Nyaburongo ziingizwe kwenye Mpango. Nitakuandikia vizuri ili angalau tuone namna gani unatusaidia kwa mwaka wa bajeti unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kunipatia fedha hizi za majosho, Mheshimiwa Waziri nikwambie kwamba mpaka sasa hazijaanza kufanya kazi. Sina imani kama wataalam wanakwambia. Hazijaanza kufanya kazi kule vijijini kwa sababu ya namna mlivyozitengenezea utaratibu wa utekelezaji wake. Haya ndiyo tulikuwa tukisema hapa kwamba fedha mnapeleka vizuri, lakini utekelezaji wake unakuwa mgumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mmewaambia Halmashauri itafute Mkandarasi. Inampata Mkandarasi, josho moja mmetenga Shilingi milioni 18; Mkandarasi anatakiwa afanye kwa kiwango kidogo kidogo, ana-*rise certificate,* Halmashauri inaleta kwenu Wizara, Wizara mnaanza kuandaa malipo, na mpaka uende kumlipa Mkandarasi imechukua muda mrefu. Wamegoma kutekeleza hili. Kwa hiyo, naomba ule utaratibu ubadilike. Pelekeni fedha kwenye Halmashauri kama ambavyo Wizara ya Afya na Wizara nyingine zinavyopeleka fedha, zipelekeni kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuogopa kupeleka shilingi milioni 18 na wakati Wizara nyingine zinawapelekea mpaka shilingi milioni 500. Unashindwaje kumwamini Mkurugenzi kwa shilingi milioni 18 peke yake? Niliona wakala umeandikwa na Katibu Mkuu, naomba huu muu-*review*. Wapelekeeni wao wapange namna ya ujenzi wa haya majosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mmepeleka *program* ya hereni, kuvalisha hereni kwenye masikio ya ng’ombe, sina shida na utekelezaji wake, lakini bei mliyoweka kwa

mwananchi wa kawaida shilingi 1,750 ni kubwa sana. Naomba sana muu-*review* hii ili angalau wananchi wote waweze kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ambalo ni muhimu sana, Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikisema, mpaka wa Kirongwe ambao unatuunganisha kati ya Kenya na Tanzania, zaidi ya kilomita 60 ndani ya mpaka ule, kwa maana ukitoka Bukura kule, Roche, unakwenda mpaka Tarime Vijijini, lile eneo liko wazi. Ukimuuliza leo Afisa Mifugo, mpigie simu, atakwambia kwa siku moja ng'ombe wanaopita bila kulipa ushuru siyo chini ya 300 mpaka 500. Wanapita, wanavuka wanakwenda. Hakuna mnada wowote na hakuna Afisa Mifugo yoyote anayesimama, na hata akisimama, eneo la kilomita zaidi ya 60, anasimama wapi ambapo anaweza kutengeneza *control?*

Mheshimiwa Naibu Spika*,* tukaleta ushauri hapa kwamba eneo kubwa kama hili muweze mnada wa pili ili angalau mnada ule uweze ku-*regulate* na kusimamia mapato yenu mnayopoteza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napiga hesabu hapa, kwa mwaka fedha mnayopoteza kama wanapita ng'ombe 300, ushuru mliotakiwa mpate shilingi 25,000 kwa ng'ombe, maana yake kwa mwaka mzima ninyi Wizara mmekubali na mmeridhia kupoteza zaidi ya Shilingi bilioni mbili na kitu kwa kila mwaka ambayo ni fedha mngeweza kuikusanya kwa kujenga soko la shilingi milioni 200 au shilingi milioni 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri hii aichukulie *very serious*. Mnaweza mkawa mnakuja mnasema Serikali haina fedha, lakini pale fedha inapotea hadharani. Naomba sana hili, nje ya kujenga soko, muende mka-*review* bei ya ng'ombe hiyo mnayofanya shilingi 25,000 kwa mfugo mmoja. Wale wananchi wanalalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujue ukitaka kuchukua fedha, tengeneza *friendship.* Tengeneza mahusiano kati yako na yule unayechukua kwake. Shilingi 25,000 kwa mfugo ni kubwa. Mtu ana ng'ombe zaidi ya 500 au 600, atatafuta mbinu tu za kuwakwepa ili msichukue ile fedha. Kaeni nao muone namna ya kuzungumza kutengeneza *friendship* ili waweze kulipa hii kodi ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, niende sasa kuchangia kwenye Wizara ya Uvuvi. Niseme tu kabisa Mheshimiwa Waziri, kiukweli tunashindwa namna ya kukukamata wewe, na kwa sababu Waziri wa Fedha yupo, tumegundua namna ambavyo hatujawa *serious* sana kwenye sekta ya uvuvi. Hii ndiyo inatu-*cost* leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya ambayo asilimia ndogo sana ya maji ya Ziwa Victoria ina asilimia tano mpaka asilimia sita imeingia kwao, lakini wao wana-*export* sangara wengi kuliko sisi Tanzania. Rorya peke yake, mzunguko wa maji ndani ya wilaya, nimezungukwa na maji zaidi ya asilimia 76. Yaani Kenya wana asilimia tano, lakini wana-*export* sangara wengi kuliko mimi niliyezungukwa na maji kwa asilimia 76. Hatujawahi kujiuliza ni kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Uganda wale nao leo Mheshimiwa Mbunge alikuwa anachangia hapa asubuhi, wao wameamua, wako *serious* kwenye uvuvi, wameona namna ambavyo samaki wanavyoendelea kukosekana, wameanzisha uvuvi wa vizimba. Sisi kama Serikali hatujaamua namna gani tunaondoka hapo, hata nikiwauliza, toka tumeanza *program* ya uvuvi haramu 2015/2016 ni nini tume-*archive*? Kwa sababu lengo lilikuwa ni kuwanusuru sangara wasiendelee kwisha ziwani. Mbona sangara hawaongezeki badala yake wanapungua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, Mheshimiwa Waziri umefanya *presentation* lakini hujatuambia sasa nini kinachosababisha sangara hawaongezeki, pamoja na kudhibiti na kuwa wakali kwenye uvuvi haramu? Ni kwa nini? Ni kwa sababu hatujaamua kuwa *serious. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wavuvi wangu ndani ya Wilaya yangu ya Rorya, Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikikwambia sana; nje ya u-*seriousness* wale masikini wa Mungu, wanapanda ziwani, wanakaa zaidi ya siku nne au siku tano anatafuta samaki. Anakuwa ameingia gharama zote kuwapeleka wale wavuvi, kununua mashine, chakula na kitu vingine. Akimaliza uvuvi, anashuka chini anakamatwa na watu wanaitwa mama yao. Sijui kama Mheshimiwa Waziri unaifahamu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wanaitwa mama yao, hawana utofauti na wale panya *road* wa Dar es Salaam. Wanawapiga, wanawanyang'anya hizi mali zao, wanawanyang'anya samaki, wavuvi wanarudi bila kitu, wanalia. Kuna watu Mheshimiwa Waziri wamefilisika; kuna watu kule wametumia mikopo yao kwa ajili ya ku-*invest* kwenye uvuvi, hawaeleweki; kuna watu wamehama. Leo ukienda Sota pale Shirati, mitumbwi ilikuwa zaidi ya 200 mpaka 300, wamekimbia, kuna mitumbwi 20 tu. Nafiriki Mheshimiwa Naibu Waziri analifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwenye hili, Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, Waziri wa Ulinzi, Waziri wa Mambo ya Ndani na wote ambao wanahusika katika pandikizi hili, mwingilie kati muone namna ya kuwasaidia wavuvi wetu. Wenzetu, ukienda Kenya na Uganda kila leo kule ziwani wanalinda. Wako *serious* wanalinda rasilimali. Hawa ndiyo ukiwauliza wale wavuvi, utasikia tumepigwa na Waganda, tumepigwa na Wakenya, wanataja hadharani, lakini hatujaona u-*seriousness* wa Serikali kuwasaidia wale wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tunasema tuko *serious* kusaidia sekta ya uvuvi, tunaisaidiaje? Kama watu wanafilisiwa, kama watu wanaondoka, wakija huku wanakamatwa na kanuni za uvuvi haramu, hatuwezi kuwasaidia. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwenye hili atafute namna ambayo tunaweza tukawasilikiza wale wavuvi na namna ya kuwasaidia wale wavuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu kwenye hilo, tunazungumza kwamba tuko tayari kuboresha na kuimarisha ulinzi kule ziwani; mtakubaliana nami kwamba katika mali ambayo hailindwi ni samaki. Leo ukienda kwenye madini, tumeweka walinzi kule wanalinda; ukienda pale *Tanzanite* inalindwa *day and night;* ukienda kwenye sekta nyingine zozote zile ambazo zinazalisha maliasili zinalindwa; ukienda *TANAPA,* wanalinda. Leo ninyi ni mashahidi, ukienda ziwani hakuna ulinzi wowote unaolinda malighafi tunazozalisha ziwani ili zisisafirishwe kwa njia haramu kwenda nje ya nchi, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, anasema *operation* zilifanyika mara tatu. Wenzetu kule Kenya na Uganda *brother,* hawafanyi *operation,* wako ziwani wamepiga kambi, wanahakikisha wanachokichuma kinarudi ndani ya nchi yao, wanakizalisha, wanakipeleka nje. Sisi tunafanya *operation* mara tatu, na *operation* nyingi mnazozifanya ni za kushughulika na hawa wavuvi haramu peke yake. Hamshughuliki na malighafi ambayo inatolewa, wenzetu wanakuja wanachukua ndani ya Tanzania wanapeleka nje, hakuna ulinzi kule ndani, hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namba, lazima tubuni, tutafute namna ambayo itaimarisha ulinzi kwenye malighafi zetu tunazozalisha ndani ya nchi. Tudhibiti wale ambao wanakuja kwetu wanachukua samaki wanapeleka nje. Mtawapa wengine sifa ya kuonekana wana-*export* zaidi

kwenda nje ya nchi kuliko sisi. Leo tunazungumza, Kanda ya Ziwa, zaidi ya asilimia 75 ya *product earning* ambayo tunaipata kama mapato ya nje, inatoka Kanda ya Ziwa, lakini wale ndio kila siku mnasikia wanalia, wanapigwa, wananyang'anywa mali zao, hawana vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vizimba tunavyozungumza, vinazungumzwa kwenye karatasi, kule ukienda vizimba halisia hakuna. Namna gani tunawasaidia wale wananchi wa Kanda ya Ziwa? Mkoa wa Mara, nje ya kilimo shughuli kubwa ya kiuchumi kwenye Mkoa ule ni uvuvi. Sisi tunatamani tuone namna gani Wizara mmejipanga kusaidia kwenye sekta ya uvuvi Mkoa ule wa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwenye hivi vizimba ambavyo tunapitisha kwenye bajeti yake leo, ahakikishe angalau asilimia 60 mpaka 70 inakwenda kule kuwasaidia wananchi wetu, kwa sababu vinginevyo tutaendelea kutegemea uvuvi wa baharini, uvuvi wa kwenye maziwa lakini hauko *productive.* Kule wanakokwenda masikini ya Mungu mnajua namna ambavyo wanakutana na zile changamoto. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aone namna ya kuwasaidia hawa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Jafari. Kengele ya pili hiyo.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyanya na Mheshimiwa Florent Kyombo ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiendelea kuifanya pamoja na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu kabisa, kwanza nawashukuru sana kwa josho ambalo walitupa la kule Iringa, limekamilika na soko ambalo limejengwa pale Mbambabay nalo limekamilika. Nawashukuru sana. Siyo kawaida kwa Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi kuweza kufanya kazi kubwa kama hiyo, kwa sababu tulizoea kuwasikia tu katika masuala ya kukamatakamata nyavu na nini, lakini sasa naona mnaenda kuwezesha hawa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na fedha ambayo imetolewa mwaka huu 2022 katika bajeti yao, lakini bado tunaona kwamba Wizara hii inastahili kuongezewa bajeti ikizingatiwa kwamba asilimia kubwa ya wananchi wanaishi katika miambao ya maziwa yetu ambayo ni makuu matatu, Ziwa Rukwa na pia ukanda wa bahari. Watu hao mara nyingi ukifuatilia, kwa kweli wengi wao bado ni masikini. Kwa hiyo, wanahitaji kuwezeshwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nililoongelea kuhusu suala la soko, lile soko inawezekana lisikidhi matumizi yake kutokana na wananchi wa maeneo yale ya mwambao wa Ziwa Nyasa, ambapo urefu wa ule mwambao ni takribani kilomita 150, lakini zana zao za kuvulia ziko duni sana. Mara nyingi nimekuwa nikiomba kwamba kwa nini hao vijana wasiwezeshwe hasa kupata injini za boti kwa mkopo, siyo bure? Ninachopingana nacho ni jambo moja tu la kuwalazimisha kukaa kwenye vikundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye masuala ya uvuvi kuna watu wana tabia ya kuwa na mazao ya aina tofauti

tofauti. Kuna siku mtu anaweza akaamka akasema mimi leo Hapana, siendi ziwani. Leo sitaingia kwenye maji, na kwa hali ya Ziwa Nyasa linahitaji sana kuwa na chombo ambacho ni madhubuti. Sasa kwa misingi hiyo, akipewa mkopo huyo kijana ambaye amethubu, bado hawezi kuvua peke yake, atakuwa anashirikiana na wenzake. Kwa maana hiyo, ajira nyingi zitatengenezwa na wakati huo tutaweza kupata mazao yanayotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi sana kunatokea vifo kutokana na mitumbwi duni wanayoitumia ambayo haina injini za boti. Kwa hiyo, naomba sana, kwa unyenyekevu kabisa, katika mwambao wa Ziwa Nyasa kwa kweli hawajapewa zana za kutosha hasa hizo injini za boti. Nimekuwa nikizungumza mara kwa mara, hata ukisikiliza leo katika maelezo ya bajeti hii, mambo mengi yaliyozungumza mazuri, yako kwenye ukanda wa bahari, yako angalau kule Ziwa Victoria, lakini haya maziwa mawili; Tanganyika na Nyasa ni kidogo sana, yaani yanatajwa tu kiujanjaujanja fulani hivi. Huoni kamili kwamba kuna mradi gani madhubuti unaopelekwa huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, msitake tuwe tunaanza sasa kusema kwa nini unapeleka huko? Kwa nini unapeleka huko? Hii ni nchi moja, na kama ni nchi moja itendewe haki. Haiwezekani bajeti kubwa katika hiyo mliyopewa yote inaenda upande mmoja au sehemu chache wengine wanabakia kuwa masikini. Ukizungumzia sijui mambo gani, huko huko. Hata kaka yangu Mheshimiwa Katani pale, alifikia kusema hivyo akaonywa, lakini bado tunasema ndiyo ukweli. Kwa nini maeneo mengine hayaangaliwi inavyotakiwa? Yanapewa fedha kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hayo mliyosema sijui kujenga vizimba sijui vitu gani, ukiuliza vizimba vingapi vinaenda Ziwa Tanganyika au Ziwa Nyasa utakuta pengine ni

sawa na hakuna. Ndugu zangu hii nchi ni moja, na pengine maeneo hayo ndiyo yanapiga kura nyingi kuliko hata maeneo mengine. Kwa nini mnatufanyia hivyo? Naomba safari hii kwa kweli nisikie kinagaubaga katika hizo injini za boti zitakuwepo, na zitapelekwa kiasi gani katika upande wa Ziwa Nyasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, niseme tu kwamba vilevile tumezungumzia juu ya kuwawezesha vijana kupata ajira zao, kwa sababu sio wote wanapitia mpaka elimu ya masomo ya juu, lakini hakuna mitaala ile ambayo inaweza ikaelimisha watu kwa vitendo kujua kwamba watajifundisha kuvua au kutengeneza zana mbalimbali kama boti na wakapata vyeti. Unakuta watu kama hao hawatambuliki, kumbe watu siku hizi wanapenda kutembea na vyeti. Ni namna gani Wizara yenu itaunganika na Wizara ya Elimu katika huu mchakato unaoendelea wa kutoa mafunzo kwa vijana hasa wale ambao hawajamaliza masomo yao yaani wale *dropouts,* wanaweza wakajikita katika maeneo hayo, kwa sababu wao wanapenda kwenda katika masuala ya kiuvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tumeona katika Wizara ya Kilimo wanapima afya ya udongo. Ninyi Wizara ya Mifugo na Uvuvi, hasa kwenye uvuvi mnapima vipi afya ya ziwa kujua kwamba eneo hili lina samaki wengi na eneo hili halina samaki wengi? Ninyi mnatumia mbinu gani kuwaelimisha wananchi ili wajue kwamba eneo fulani usiwe unaenda, nenda eneo fulani ambalo mara nyingi utapata samaki na kuna mazalio, labda muepuke kuvua hapo, vueni hapa ili mradi wapate faida inayokusudiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama wenzenu wanapiga hatua katika maeneo yao na ninyi vilevile sasa mtusaidie kuweza kuona kwamba mtu asiwe anatembea usiku kucha anavua, usiku kucha anaparaza mtumbwi, anahangaika kutafuta Samaki, mpaka inafika asubuhi

hajapata hata samaki mmoja, kumbe amepigananao chenga humo humo kwenye ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwenye suala la mifugo. Wilaya ya Nyasa hasa maeneo ya mwambao kuna changamoto kubwa sana ya ugonjwa wa mapafu ya ng'ombe. Hawana ng'ombe wengi sana, lakini huyo huyo mmoja au watatu walionao ni muhimu sana kwao. Sasa unakuta mara nyingi utaambiwa ng'ombe alipochinjwa alikuwa na konokono; anaumwa sijui konokono; wanaita konokono, lakini hakuna tiba zinazoeleweka kabisa kwamba kukitokea tatizo fulani wanaenda mahali fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata zile ruzuku zinazotolewa kwa ajili ya ng'ombe, kule sijui kama hata zinafika. Nimefuatilia, hakuna ruzuku iliyofika siku za karibuni, na zile dawa ni ghali, nyingine zinafika mpaka Shilingi 35,000/=, wakati mwingine wanamtibu ng'ombe kwa madawa chungu mbovu, yaani ni ile tu kukisia sasa tumtibu kwa magonjwa ambayo wanahisi ndiyo yatakuwa yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalam wa mifugo pia ni wachache sana katika Wilaya ya Nyasa. Kwa hiyo, naomba kuiangalia wilaya hiyo ili kuiwezesha sasa kuweza kupata wataalam watakaoweza kusaidia katika maeneo hayo ya mifugo hususan katika ng'ombe na mbuzi vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamalizia ya kwangu, nisije nikasahau, nilikutana pia na viongozi wa Chama cha Wavuvi pale *Canteen,* wamenipa maelezo yao, naomba niwakabidhi na yenyewe, mtayapitia kadiri walivyoandika wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, vilevile kuna kuwezesha vijana katika masuala ya mabwawa ya samaki hasa Ukanda wa Juu katika Tarafa ya Mpepo, yaani Kata ya Kingerikiti, Mipotopoto, Luhangarasi, Tingi na

Lumeme; tuseme kata nane za Tarafa ya Mpepo. Naomba wawezeshwe kwa sababu hao wangependa sana kufuga Samaki. Nilileta barua kwako Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, naamini katika bajeti hii utakuwa pia nao umewakumbuka ili waweze kupata kitoweo na pia afya njema kutokana na samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kimsingi tunaona Wizara hii ikijitahidi kwenda lakini bado tunasisitiza umuhimu wa wavuvi na watu wa mifugo kupewa fedha ya kutosha ili nao waweze kufanya kazi zao vizuri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili hiyo.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Florent Kyombo, jiandae Dkt. Oscar Ishengoma.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia katika Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa nia njema ya kutaka maendeleo katika ufugaji, uvuvi na maendeleo kwa ujumla katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya pekee nimpongeze sana Waziri, Mheshimiwa Mashimba Ndaki; Naibu Waziri, Mheshimiwa Abdallah Ulega kwa kazi nzuri mnayoifanya kwa kushirikiana na Katibu Mkuu, Tixon Nzunda, Naibu Katibu Mkuu; Wakurugenzi wote wa Wizara; watumishi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi zake, mahsusi pia na watumishi wote wa Halmashauri 184 ambao wanasimamia eneo hili la Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais kupitia wizara yetu hii kwa Wilaya ya Misenyi kututengea milioni 350 kujenga mnada wa mpakani *boarder market* na sasa hivi mnada huo unajengwa kwetu ni faraja kwa sababu utainua uchumi wa wana Misenyi uchumi wa wana Kagera lakini pia na soko la mifugo ndani ya Mkoa wa Kagera litakuwa limepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kidogo kuhusiana na mazingira ya upangishaji katika Ranchi zetu za Taifa kupitia *NARCO*, kwanza kwa nafasi ya pekee nimpongeze Meneja wa *NARCO* Profesa Peter Msofe pamoja na watumishi wote wa *NARCO* kuanzia ngazi ya Taifa lakini mpaka ya *ranch* wanaposimamia katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera ni mkoa ambao una Ranchi nyingi kuliko mikoa mingine yote nchini Tanzania, tunazo Ranchi sita tunayo Kagoma, Kitengule, Kikukura, Mabale, Mwisa na Misenyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia wingi wa Ranchi hizi maana yake idadi ya mifugo ambayo iliyoko Tanzania mingi imekuwa *based* katika Mkoa wa Kagera. Lakini cha kushangaza Mkoa wa Kagera ni mojawapo mkoa maskini kuliko mikoa yote Tanzania kwa taarifa za *GDP* ambazo zimetolewa na sababu zake ni nini ambazo zimetolewa na sababu yake ni nini kama alivyosema kaka yangu Mheshimiwa Mwijage ufugaji unaoendelea ndani ya ranchi zetu ni uchungaji na sio ufugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ambayo sio malengo mahususi ya Serikali tukijiringanisha na nchi jirani Uganda sisi tunafanya kazi kwa ushirikiano na wenzetu wa Uganda, tunatembeleana kuangalia anachofanya mwezetu wa Uganda na wanachofanya watanzania, katika nchi ya Uganda hatuongelei ukubwa wa eneo hatuongelei uwingi

wa idada ya mifugo tunaangalia *productivity* katika eneo ulilonalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaangalia mfugaji ndani ya nchi ya Uganda anazo heka 400 tu mle ndani ana ng'ombe 150 *productivity* inayotoka katika eneo hilo ni kubwa kuliko mfungaji wa Tanzania ambaye ana hekta 6000 ana ng'ombe 1000, wapi tunakwama?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwapenda wafugaji wetu, kupitia *NARCO* wamekodisha kwa utaratibu mzuri wanaandika *business plan* lakini kuna mambo ambayo kama Taifa kama Serikali tunahitaji kuyasimamia ili hawa wafugaji sasa ndani ya *Ranch* zetu wawe wafugaji kweli na sio wachungaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza, zipo changamoto mbalimbali katika eneo hili ambazo ziko *silent* kwa Serikali yetu au kama inazifanyia kazi basi si kwa kiwango kile ambacho kingeweza kuwasaidia wafugaji wetu wakapiga hatua kubwa. Suala la kwanza tunalo suala la wizi katika ranchi zetu wizi ni mkubwa sana na wizi asilimia 90 mifugo inaibiwa kwenda nchi za jirani kama mnavyojua Mkoa wa Kagera tumepakana na nchi zote lakini n'gombe wanaibiwa lakini Wakuu wetu wa Wilaya zinazozunguka mahali pale wanajitahidi kadri wanavyoweza lakini wamewezeshwa kiasi gani na wizara yetu kuhakikisha sasa wanalinda mifugo yetu wanalinda wananchi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya tunaielewa lakini hakuna sehemu ambayo toka inatoka wizarani kupeleka katika wilaya zetu ili vyombo vyetu vya ulinzi na usalama viweze kufanya kazi kwa ufasaha, nitafika sehemu ambayo nitashauri hizo fedha zitoke wapi kwenda katika kusaidia vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ili wananchi waendelee kufuga.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuangalie miundombini mfugaji anatakiwa kuwekwa bwawa anatakiwa kuweka josho ni mfugaji gani wa Tanzania ataweza kununua *excavator* ang'oe miti yote katika hekta zake alizopewa achimbe mabwawa sasa Serikali inatakiwa kuja na utaratibu ambao inaweza kuwatafutia mikopo kwa kuwapa vifaa, lakini naweza kutafuta vifaa vya Serikali tumeona Wizara ya Ardhi, walinunua vifaa vya kupima Tanzania nzima, ukitaka kupima halmashauri unaenda pale Wizara ya Ardhi wanakupa vifaa unapima halafu unarudisha sasa na Serikali hapa kupitia Wizara ya Mifugo walitakiwa wawe na vifaa kama ni ma-*excavator* wanayo watu wakitaka kuchimba mabwawa wapewe wachimbe mabwawa halafu watakataka katika hela zinazotokana na uuzaji wa mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili halipo inakuwa ni ngumu sana kuelewa ni wakati gani anaweza kufanikiwa. Lakini zipo changamoto za mbegu, dawa za kuongeshea mifugo, chanjo zote hizo ningeomba Serikali ije na majibu ya kuhakikisha kwamba inakuwa na mkakati madhubuti kwamba wananchi wetu basi wanapewa ruzuku au inaweka utaratibu mzuri waweze kufanikiwa katika hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri eneo lingine ni upimaji mpya ambao ulifanyika ndani ya vitalu unajua wakati wa upimaji mpya kuna maeneo mengine Serikali ilisaidia sana kutatua migogoro. Nimwambie Mheshimiwa Waziri kuna maeneo mengine ambapo tumeleta mgogoro zaidi tumechukuwa maeneo ya vijiji yakaingia kwenye *Ranch* za Taifa, tuangalie kwa mfano ukienda kule kwangu nenda Kijiji cha Bunga utaona vitongoji cha Rwambogo na Shantabwa vyote vimeingia katika *Ranch* ambapo awali haikuwa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda pale Kakuyu uangalie Kitongoji cha Katangiliza chote kimingia kwenye *Ranch*

ninacho kitalu namba kumi Mheshimiwa Waziri unakijua kiko na kesi lakini kesi ikiisha wananchi wameshaomba hekta 2000 wapeni walime mifugo na wananchi vyote vinategemeana tusipende sana mifugo tukaacha wananchi wakilima na mifugo yenyewe basi inakuwa ni rahisi kuweza kutumia kwa hiyo, niombe kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la uvamizi wa tembo mimi naomba mshirikiane na Wizara yetu ya maliasili na utalii kwa mfano kwenye *Ranch* za Misenyi na mabahi ni nusu na nusu na ng'ombe. Kwa hiyo, niwaombe sana, kila siku napigiwa simu za kuhakikisha kwamba tunaenda kufukuza hao tembo, Mkurugenzi wangu hana *resource* za kutosha bunduki sijui tunazo mbili risasi lakini Wizara ya Mifugo ni lini mmetuchangia angalau risasi au bunduki kule hamna naomba tu hiyo inawezekana na wizara inakusanya fedha nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri kidogo kwenye tangazo la *GN* namba 35 la mwaka 2018 kupitia tozo za minada tunayo minada ya aina tatu tunao mnada wa awali *primary market* tunao *secondary market* wa pili tunao na boda. Niombe wizara hii iangalie vizuri eneo hili Wizara ya Mifugo katika ng'ombe mmoja kwa mfano nikiongelea mnada wa boda inachukuwa kibali cha kusafirisha ng'ombe kwenda nchi ya jirani shilingi 25,000 inachukuwa tozo ya ushuru shilingi 4,000 halmashauri inaambulia shilingi 1,000; buku tu Wizara inachukuwa shilingi 29,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ardhi ile iliyoko pale yote ni halmashauri watumishi hata kama wote ni watanzania ni wa wizara wote wako chini ya Mkurugenzi *resource* anazotumia kwenda kusimamia pale ni za halmashauri elfu moja Mheshimiwa Waziri kitu cha kwanza naomba ukiangalie hicho gawana mapato yale angalau ile elfu nne ya tozo mnaweza mkaigawa katika halmashauri ikachukuwa elfu tatu nyie mkabaki na 2,000 na kibali cha kusafirisha unakuta

wewe unachukuwa 27,000 halmashauri inachukuwa elfu tatu itasaidia na hiyo mnaweza mkaitolea maelekezo kamati ya ulinzi na usalama inapata fedha za kwenda kufanya dolia lakini pia majosho yanajengwa kupitia halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe hilo wana Misenyi walinituma kwa dhati niwashukuru kwamba leo mmetuanzishia mnada wa *boarder market* lakini niombe sasa Serikali kupitia wizara yetu hii mje na majibu kwa wana Misenyi kwamba tunaingia *MoU* uendeshaji.

**NAIBU SPIKA**: Ahsante Mheshimiwa Kyombo kengele ya pili.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi hii naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Dkt. Ishengoma jiandae Boniface Mwita Kitere.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupewa fursa ya kuchangia hoja ambayo iko mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kazi kubwa anayoifanya ya kulijenga Taifa hili. Kwa wizara hii niwashukuru kwa kuleta habari njema katika Mkoa wa Kagera kwa vizimba 9 ambavyo wametupatia, na vinne vinakwenda wilaya ya Muleba wanakwenda kututengenezea ajira hii ni habari njema kwa wakazi wa Muleba na wakazi wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru tena kwa kutupatia boti moja na injini moja Wilaya ya Muleba kama ambavyo nimekuwa nikichangia ni wilaya yenye visiwa vingi

yenye maji mengi lakini pia yenye matatizo mengi vizimba vinne tunashukuru tukiongezewa vingine viwili tutashukuru zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niende kuchangia suala la migogoro kati ya wakulima na wafugaji katika Wilaya ya Muleba. Naomba niseme ni Mbunge wa Wilaya ya Muleba, Wilaya ya Muleba tuna Kata 43 lakini ni wilaya yenye majimbo mawili ya uchaguzi niko mimi na yupo kaka yangu Charles Mwijage. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi amechangia lakini kilio chetu migogoro au mgogoro mkubwa wa ardhi ambayo *NARCO* ameichukuwa ameivamia, bila kufuata taratibu za kisheria na ninashangaa sijui kama *NARCO* wana mwanasheria pale. Hili utengeneze *Ranch* hii ardhi ya halmashauri ichukuliwe kwa ajili ya matumizi ya umma upo utaratibu. Huwezi kuamka asubuhi unakwenda unavamia ardhi ya halmashauri yeyote kwa kisingio chochote kile bila kufuata utaratibu unasema naanzisha *Ranch* hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa Mwisa na Utoro au hizi *Ranch* za Rutoro na Mwisa imeanzishwa kinyume cha sheria cha sheria za nchi hii. Rutoro kilikuwa Kijiji tangu mwaka 1976 mwaka 2005 *NARCO* wakaenda wakapima *Ranch* pale mwaka 2010 Serikali hii Tukufu ikapandisha hadhi Kijiji cha Rutoro ikawa kata vile vitongoji vilivyokuwa chini ya kile Kijiji ikapandishwa hadhi vikawa vijiji, sasa nashindwa kuelewa *NARCO* wamepima vitalu mwaka 2005 sijui kwa mamlaka ipi lakini Serikali mwaka 2010 inapandisha vile ambavyo vimepimwa kama vitalu inaipa hadhi ya kata na vitongoji inaipa hadhi ya kijiji sielewi hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria tunazitunga sisi wenyewe na lazima mashirika na taasisi za Serikali zifuate sheria. Katika mgogoro huu wa Mwisa unahusisha kata saba Mheshimiwa kaka yangu Mwijage asubuhi amesema

wananchi ambao wako kwenye hizo Kata za Kebitemba, Karambi Kasharunga Mbunda Burungula Genge na Rutoro ambazo zina vijiji 12 vitongoji 19 wako kwenye kilio na kazi ya mama ni kupangusa watu wanaolia machozi namuomba mama awapanguse hao watu wa vitongoji 19 awapanguse machozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamelia sana naomba kilio chao kifike mwisho. Lakini *NARCO* wamekwendaje kwenye eneo la Mwisa na lenyewe ni kizungumkuti hakuna sheria yoyote ile ambayo wameifuata kama nilivyotangulia kusema ili ardhi yoyote itwaliwe lazima Sheria ya Ardhi ya Vijiji ifuate sheria namba tano ukisoma kipengele cha *section 4 subsection one* ya sheria ya ardhi ya vijiji ili waanzishe *Ranch* Rais lazima atwae lile eneo na anapolitwaa kuna hati ambayo inatolewa na nimesoma bajeti ya Mheshimiwa Waziri wakati anasoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma kiambatisho kwenye hotuba yake kiambatisho namba 15 imeongelea migogoro ya *NARCO* kiambatisho namba 12 ameongelea maeneo ambayo yametwawaliwa na *NARCO* yametolewa *notice* ya Serikali lakini kiambatisho 11 ameongelea maeneo ambayo yametwawaliwa bila *notice* ya Serikali sasa nashangaa unatwaaje maeneo unaanzisha ufugaji bila kufuata sheria hakuna *notice* hakuna nini tunashindwa kuelewa nchi tunaipeleka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi ardhi yao imechukuliwa kinyume cha sheria hapa tunapoongea kwenye lile eneo ambalo wametwaa kinyume cha sheria hakuna *notice* na nitamuomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hapa atuambie bila kupepesa macho eneo la Rutoro *notice* ambayo inakupa mamlaka ya kulichukuwa ni *notice* ya mwaka gani ya tarehe ngapi, ya siku gani utuambie na wananchi wasikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utuambie eneo la Mwisa umelipatajepataje kama kuna *notice* ya Serikali utuambie *notice* namba ngapi kama hakuna *notice* uwaambie wananchi wa Mwisa ambao leo wananyanyaswa wanaamishwa na hakuna mtu ambaye anafuata hata sheria ya kuhamisha makaburi mnaleta mifugo mnalishia kwenye makaburi ya wazazi wetu wazee wetu ambao wamepumzika pale hatuwezi kukubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama hakuna *notice* hiyo tuwatangazie wananchi ambao wanahamishwa waendelee kuishi kwenye maeneo yao mpaka utaratibu utakapofuatwa. Mheshimiwa Rais anayo madaraka akiamua atatwaa ile eneo afuate utaratibu.

**NAIBU SPIKA**: Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kengele ya pili hiyo ahsante.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** Mheshimiwa Naibu Spika sitaunga hoja mkono mpaka nipate maelezo ya kina tupate zile *notice*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Getere jiandae Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, kwanza nimshukuru waziri mwenyewe na Naibu Waziri wake na watendaji wake wote wanaofanya kazi wanafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Mashimba wewe ni ndugu yangu na unafanya kazi na unatembea kila mahali tunakuona unafanya kazi na Ulega lakini kiukweli wizara ambayo siielewe ni hii hapa. Siielewi kwa sababu gani najiuliza hivi sisi watanzania kwa nini tunakariri maneno tumekariri maneno kwa nini? *Zero grazing* kwa nini

tunakariri? Wafugaji wanaangaika kila nchi kila mahali wanaangaika tuna pori mapori ya *NARCO* ambayo yana uwezo wa kuchukua ng'ombe 61,000 waliopo sasa hivi ni 19 *zero grazing* kwa nini tunaangaika wenzetu hawana maeneo? Nchi yetu bado nzima ukienda singida ukienda maeneo ya mapori yapo ya kutosha tuna Hifadhi za Taifa ziko 22 zinazofanya kazi na kutoa hela ni tano tu 17 zimelala.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna *game reserve* uwa najiuliza hivi maana ya *game reserve* ni ni hivi neno *reserve* maana yake nini? Maana yake sijui ukipata shida usaidiwe ziko 27 zinafanya kazi 5 tu, tuna *open area* tuna maeneo ya wazi mengi tu tuna misitu, wafugaji wanauwa ng'ombe eti Wizara ya Mifugo na Uvuvi kazi ya kufanya ni kupeleka hereni yani wananchi wale wanateseke wewe wanaenda tena na hereni wananchi wanateseka uwapi malambo, hivi hii wizara ikoje? Hivi tukifanya *zero grazing* watanzani hivi minada ya watanzania si ndio *study tour* yao hivi leo mbuzi unaweza kwenda mnadani ukanunua mbuzi mmoja laki moja utaweza?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi mbona Wabunge wote kila mnada mnaenda na watu wanaishi pale kwa starehe kwa nini tusitafute *solution* ya wafugaji tukawapa maeneo. Sikubaliani leo kwamba pori fulani tuwape wafugaji tukiwapa pori tuwapangie vitalu, na walipe kodi leo ukienda Misenyi ng'ombe wale walioko *NARCO* misenyi ile inahitaji ng'ombe 15 wako ng'ombe 900 kila mahali mashamba ya Serikali yapo hayana ng'ombe wafugaji wanateseka kila mahali na ng'ombe tunakula nyama tunakunywa maziwa kuashia koo imeisha ipo tu *why*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe waziri najua unafanya kazi na wenzako sasa mkae kwa kweli hii bajeti tutawapitishia lakini bajeti ijayo mtatuambia hivi kazi kweli humu ndani ikoje? Hivi kuna nini kwa nini watu wanateseka? Amezungumza Mbunge mmoja hapa ukianza kuzungumza

habari ya mfugaji umezungumza mwananchi, watu wanateseka mali zao zinaisha, nenda umasaini ng'ombe zinaisha kila mahali nenda Mara juzi nimekwenda pale Mto Mara mtu wangu amenywesha ng'ombe mkasema mavi yamekuja ng'ombe wahame, mavi yanauwa samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jamani ehe! tukubaliane kwamba hawa wafugaji mnataka tuweje? Tuna nchi yetu ina mifugo mingi, tunakula nyama mnadani, tunatosheka na nyama, halafu tunafilisi watu tuteseke, kwanini tuteseke? Kwa nini wananchi wateseke na nchi yao ipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani nendeni Hispania, mimi nimekwenda Hispania pale, wana eneo kama Mkoa mzima, wanazo *block* za kutosha, wana ng'ombe wa kutosha. Hiyo haitoshi, Mheshimiwa Waziri Mashimba hebu nikuulize swali, hivi leo una ng'ombe wapo hapo *NACRO* – Kongwa, hivi ukichukua madume kwa sababu dume moja linazalisha majike 25, hivi ukichukua madume yale ukawagawa hata kwenye Kata madume 40 ni ng'ombe 1,000 tukaanza kubadilisha ufugaji wetu kwa kutumia madume yetu, hivi shida iko wapi? Shida ni nini?*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani Mwalimu Nyerere alipeleka ng'ombe kila mahali kila kijijji, leo hakuna kitu, mnaacha wafugaji wanaisha lakini mnadani mmekaa na vitabu mnakusanya ushuru, mnakusanya wapi? Mnada wa kwenda Kenya badala ya kwenda Tarime mpakani alivyozungumza Mbunge hapa mnaweka kirumi, maana yake ndiyo nini kirumi mimi sielewi sasa, yaani mnapokwenda kuweka mpakani kirumi ukienda Misenyi tunapambana na Uganda kwa malisho, mnasema Uganda wanakuja kulisha huku ndani, hivi pori limejaa na majani yapo, kwa nini watu wasilishe, shida nini? Mkae mpange! Wizara hii nami naanza kuitilia mashaka, hivi kweli mnapigania ng'ombe au mnampigania nani? mnapigania samaki au mnampigania nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naomba mkae…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere hebu subiri kidogo hapo, Mheshimiwa Lucy uko salama hapo? Upo salama, kama upo salama kaa pembeni, maana yake! Haya Mheshimiwa Getere endelea. *(Kicheko)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipunguza, maana yake jazba ni kubwa sana kwa sababu mimi kuna vitu naviangalia miaka nenda rudi, miaka nenda rudi, watu wanahama wanafilisika, mtu alikuwa na ng'ombe 1,000 zinakuwa mia mbili, zinakuwa mia, zinakuwa sifuri, kila mwaka watu wanahama, ardhi ipo imejaa Tanzania, hamuweki!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mashimba sasa nikuulize swali, juzi nilikuja ofisini kwako na Diwani na Kata ya Salama na Kata ya Kiloleli mkatuambia mnatupa majosho yale mawili, Kiloleli na Salama Kati, mkatuonesha bajeti je, hizo fedha ziko wapi? Mpaka leo hatuzioni, eti Wizara ya Kilimo fedha zake Milioni 18 za kwenda kuchimba majosho mpaka sitolewe kwenye Wizara! Eti yenyewe haitoi Wizara, yaani humo ndani kuna matatizo humo ndani! Hii Wizara muitengeneze, ninawaomba Watendaji wenu muwatengeneze ninyi ni viongozi wazuri, nawashukuru sana muendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze na ajiandae Mheshimiwa Yustina Rahhi.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami nichangie kwenye eneo hili la Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Mifugo aliwahi kuja Jimboni kwangu kwa lengo moja la kuhakikisha kwamba anagawa vizimba au *blocks* kwenye eneo la *ranch* ya Wizara ya Mifugo ili kusudi watu wanaofuga Ng'ombe waweze kupeleka ng'ombe zao pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa hilo lakini pia kwa kazi ile iliendelea pia kwa sehemu imekamilika. Sasa bado kazi ya kuelimisha wale Wasukuma, na wewe ndiyo uje uongee kisukuma na waondoe ng'ombe katika vijiji vyote 61 vya Wilaya ya Uvinza. Sasa hivi wakulima wanalima na hawavuni kwa sababu ya ng'ombe zilivyotapakaa katika Jimbo na vijiji vyote. Sasa Ng'ombe tunazipenda zina maziwa, zina nyama lakini sasa utakula nyama na maziwa bila ugali? Haiwezekani! Sasa uje.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa wapi?

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Huku.

**T A A R I F A**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa tu taarifa mchangiaji anayeendelea kuchangia aondoe neno Wasukuma maana anagusa kabila la watu wengi ambao tumo hata humu ndani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa hiyo siyo, ungesema kuhusu utaratibu kwa sababu umetumia Kanuni tofauti, lakini na wewe Mheshimiwa Bidyanguze jaribu kuji-*refrain* kutumia majina ya watu.*(Makofi)*

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sizungumzi hivyo kwa nia mbaya lakini ndiyo wafugaji na ndiyo matajiri wa ng'ombe, Waha hatufugi ng'ombe sisi ni wakulima. Kwa hiyo, akija yeye ana lugha ambayo ataweza kuongea nao ili waweze kuondoa ng'ombe katika vijiji na waweze kupelekwa katika eneo ambalo Waziri alikuja kuliandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niondoke kwenye eneo hilo la mifugo ambayo mifugo yetu katika eneo la Wilaya ya Uvinza inakaribia takribani mifugo Laki Mbili na mifugo haiharibu tu mazao ya wakulima inaharibu na *reserve* ya misitu ya Serikali ambayo imewekwa pale, ambayo lengo la Serikali kuacha misitu ile ni kuendelea kuwa na mvua na sifa ya Mkoa wa Kigoma ni kweli kwamba hatujawa na ukame hata siku moja, sasa kwa ujio wa hizi ng'ombe Laki Mbili maana yake kama Serikali haikufanya juhudi ya kuhamisha hizo ng'ombe maana yake na Kigoma tunakwenda kuwa na jangwa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihamie kwenye eneo la uvuvi. Naomba nikupongeze Mheshimiwa Waziri pia Naibu Waziri nikupongeze. Mheshimiwa Waziri, ulipokea ujumbe wa Wavuvi kutoka Mkoa wa Kigoma kwa ujumla wake wavuvi wa Jimbo la Kigoma Kaskazini na Kigoma Mjini Pamoja na Kigoma Kusini. Ulitoa elimu nzuri na sasa hivi Waziri au Naibu Waziri anapokwenda katika Jimbo la Kigoma Kusini au Kigoma kwa ujumla haendi tena kuchoma nyavu hafanyi hiyo kazi tena, kwa sababu tayari elimu ilikwisha patikana. Juzi alikuwepo Naibu Waziri, kwakweli hakuna nyavu alizooneshwa ili achome, kwa hiyo Waziri elimu ile uliyotoa wakati wale viongozi wa uvuvi wamekuja ile elimu iko vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hilo bado tunahitaji Wizara iweze kuwasaidia wavuvi wetu vifaa vya kisasa vya uvuvi. Sasa hivi wavuvi wa Ziwa Tanganyika katika

Majimbo Matatu wanakwenda kuvua na wanarudi bila samaki, wanarudi bila dagaa na vyombo wanavyotumia ni vilevile walivyokuwa wakitumia zamani wakati samaki zikipatikana na dagaa zikipatikana. Kwa hiyo, nadhani imefika wakati sasa Wizara ilete wataalam, iweze kubuni ni vyombo gani vya kisasa viweze kuletwa katika Mkoa wa Kigoma kwa maana ya wavuvi wetu waweze kufaidi matunda ya nchi ili waweze kuvua. Siamini kwamba samaki katika Ziwa Tanganyika hawamo! Kwa mujibu wa tafiti zilizopita samaki bado ni wengi ingawaje nimeongea na Afisa Uvuvi ameniambia kwamba *TAFIRI* wamefanya utafiti mwingine, tunaomba Wizara utafiti huo uletwe tujue samaki wapo kiasi gani na wapo katika maeneo gani? Tumechoka wavuvi wetu kwenda kuvua kwa kubahatisha gharama ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze shirika moja linaloitwa 'TUUNGANE' hili shirika linawasaidia wananchi wa jimbo la Kigoma Kusini sijui kama majimbo mengine kama wapo lakini hawa ndiyo ambao kidogo wanawasaidia wavuvi katika Ziwa Tanganyika. Nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri amekuja mara mbili mfululizo pale Buhingu, Nakatumbi, wamejengewa vyombo vya uvuvi viwili vya thamani ya Milioni 38, jambo la kuunga mkono na jambo la kupongeza sana hawa watu wanaojiita tuungane ni shirika zuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Buhingu pia wanajenga mwalo wenye thamani ya Milioni 300 unaweza ukaona kama ni shirika …

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Bidya kengele ya pili.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi naomba kwa hayo machache niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni muda huu wa jioni, ni wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge waliotembelea Bunge jioni hii wasimame kwa pamoja. Wageni wote wa Waheshimiwa Wabunge simameni kwa pamoja. Karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 35 wa Chuo cha Uuguzi Shirati kilichopo Rorya Mkoani Mara. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, jiandae Mheshimiwa Mohamed Kassinge, jiandae Mheshimiwa Bulaya na baadae Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana na mimi kupata fursa hii ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Mifugo. Nami vilevile nitoe pongezi kubwa kwa Rais wetu Mama Samia Suluhu kuweza kuweka bajeti kubwa katika Wizara hizi za kisekta za uzalishaji kwa kuwatia moyo Watanzania kujikwamua na umaskini ambao umekuwa kikwazo kikubwa kwa wafugaji na wakulima.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fursa kubwa sana katika sekta hii ya mifugo kuweza kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kuweza kutusogeza katika uchumi wa kati, kwa sababu kwanza ukiona Tanzania tumezungukwa na Maziwa Makuu ambapo tungeweza kufanya uvuvi katika Maziwa Makuu na tungeweza kupata tija samaki tukaweza pengine kuwauza nje na ikachangia katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba sekta hii bado haijafanya vizuri, kwamba mchango wake kwa Pato la Taifa bado ni chini ya asilimia 10, bado inachangia kati ya asilimia Saba mpaka Nane, sasa hebu ona jinsi tulivyo nyuma lakini tukiwa *proud* tu kwamba Tanzania sisi ni wa pili

kuwa na mifugo mingi, sasa pia hatujaweza kutumia fursa hiyo kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni wa pili katika kuwa na mifugo mingi Afrika lakini Tanzania hii pia ni ya pili katika kuwa na udumavu wa mifugo, sasa hii ina-*reflect* nini? Ina-*reflect* tu kwamba ulaji au upatikanaji wa mazao ya mifugo bado upo chini na ubora wake upo chini, ndiyo maana hata bado tunaingiza mazao haya ya mifugo kama nyama tunaingiza kutoka nje, maziwa, Samaki sasa tuone kwamba tunapaswa kufanya nini, bado ukienda hoteli za kitalii, ukienda *supermarket,* utakuta kwamba mazao ya mifugo bado tunaingiza kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Waziri ameweza kuona ni kwanini tuna kipato kidogo kutokana na mazao ya mifugo, amesema mojawapo ni kuwa na kosafu za mifugo yetu, tuna asilimia 90 ya mifugo ni mifugo yetu ya asili ambayo kosafu ndiyo sababu pengine ya kuwa na tija ndogo, vilevile magonjwa ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli bado hatujawa na sheria, kwa mfano tunamajosho huko sheria ya kuogesha mifugo bado hatujaweza kuisimamia na ndiyo maana majosho sehemu nyingine pia yapo hayatumiki ni bahati tu kwamba mifugo ya kienyeji ina ustahimilivu mkubwa, lakini inang'atwa na kupe, inatembea na kupe, inakuwa na minyoo, ndiyo maana mifugo yetu haina ubora.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni la malisho pamoja na maji. Naipongeza Wizara kwa *intervention* inazofanya katika matatizo haya. Kwa mfano, Wizara imetenga karibu bilioni 3.9 katika kubadilisha kosafu za mifugo kwa kufanya uhimilishaji. Sasa uhimilishaji huu namuomba tu Waziri kama kweli ana nia njema, kazi hii ambayo itafanywa na Maafisa Ugani huko kwenye Halmashauri kwa wafugaji, kwa kuwa amenunua pikipiki za Maafisa Ugani wa Mifugo

basi angewapatia kabisa mitungi ya kubeba *liquid nitrogen* ili huko kwenye makundi haya ya mifugo ya asili waweze kufanya uhimilishaji ambao kwa vyovyote vile ni ngumu kufanya uhamilishaji kwa sababu mifugo hii ya asili inachungwa pamoja, mitamba pamoja na madume. Pengine basi angeweza kusambaza hata madume labda madume bora ya mbegu kuweza kufanya uhimilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nakisemea kituo cha *NAIC* kinachozalisha hizi *artificial insemination* tunachokituo kimoja kiko Arusha na hali yake si nzuri, uwezo wa kuzalisha mbegu za kutosha za kusambaza Tanzania nzima bado ni mdogo, pengine Waziri ningeshauri tu kwamba kama kuna uwezekano wa kufanya *extension,* kwa mfano mifugo iliiyopo Dodoma kutegemea *NAIC* iliyopo Arusha peke yake bado haiwezi kutosheleza, mifugo iliyopo Shinyanga, Mwanza utegemee *NAIC* peke yake na kwa sababu umewekeza kidogo huko *NAIC* uhimilishaji gharama yake ni kubwa. Kwa mfano, kwa sasa hivi ukimpandisha ng'ombe mmoja unampandisha kwa elfu ishirini pengine hata asiwe na mimba urudie. Kwa hiyo, na gharama hizi zipunguzwe ili wafugaji wengi waweze kutumia hizi *artificial insemination. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namna nyingine ambayo umeona ni kubadilisha kosafu ni kuzalisha mitamba kwenye mashamba ya *Sao Hill* pamoja na *NARCO* na kwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hii mitamba sasa isambazwe huko vijijini kwa akina mama, tunaweza tukawashauri akina mama zetu ile asilimia kumi ya mkopo anaopata mapato ya ndani kutoka Halmashauri wanaweza wakawekeza huku wakajenga mabanda mazuri ili sasa Wizara mitamba hiyo isambaze kwa akina mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna asasi isiyo ya Kiserikali kama *Heifer International* imefanikiwa sana katika kusambaza mitamba kwa namna kwamba ukipeleka mitamba hiyo hata

mitano katika kijijini kimoja itasambaa na kijiji kizima itajaa kwa maana ya kukopesha mtambo, utampa mama akizaa anampandisha yule ndama na akishampandisha anampa jirani yake. Kwa hiyo, mifugo hii itazunguka na kwa ajili hiyo akina mama watapunguza umaskini. Kwa hiyo, hilo moja naomba tu isambazwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, *intervention* nyingine uliyofanya ni katika kuzalisha malisho ya mifugo. Ni kweli wazo hili ni zuri lakini uzalishaji huu kwa maeneo ambayo hakuna miundombinu ya umwagiliaji, malisho haya yatazalishwa kama mazao mengine wakati wa masika kwa maana hiyo wakati wa masika malisho yatakuwa mengi, tukirudi kwenye kiangazi changamoto ya malisho itakuwa palepale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sambamba na kusambaza hii ambapo umetenga karibu Bilioni 1.2 umesema utaweka na mashamba darasa kwenye Serikali za Mitaa, mimi nishauri tu kwamba usambazaji wa mbegu za malisho ziendane na kuwawezesha wafugaji kuweza kuhifadhi sasa malisho ya mifugo ili ije iwasaidie kipindi cha kiangazi, wakatengeneza ma-*bell* ya *hay* wasile kile kipindi cha kiangazi iwasaidie, vinginevyo tutafika kiangazi bado kutakuwa na changamoto ya malisho.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi cha kiangazi ng'ombe mpaka wanakorogewa uji na wengi wanakufa, kwa hiyo hii ni hatari sana lazima tupeleke teknolojia kuhifadhi malisho kwa wafugaji wetu tukitaka tuwasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mchango wangu mwingine ni kwenye vituo vya kukusanya maziwa. Kiukweli maziwa kipindi cha masika maziwa ni mengi sana na kwa sababu maziwa ni mengi kina mama au watu waliopo vijijini wanashindwa kuyapeleka kwenye masoko hii ni kwasababu pengine mifugo yetu ya asili hii anakamua labda nusu au mpaka lita mbili sasa hizo chache hawezi kwenda kilometa

chache kufuata soko la maziwa. Tungeweza kuweka hivi vituo bado hizi zingekuwa *payroll* za akina mama kama ameweza kupeleka hata lita mbilimbili kwa wiki ana hakika tu kabisa kwamba anazo pesa za kuweza hata kununua *supplement,* hata dawa za mifugo kama Serikali inashindwa pengine kupeleka vituo vingi vya kukusanya maziwa hata inaweza ikashawishi ushirika ulioko kijijini hata SACCOS lakini hii ni muhimu sana, asilimia karibu 66 au theluthi ya maziwa tunayotumia humu ndani yanatoka kwa mifugo*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa kengele ya pili. Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, jiandae Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, jiandae Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ili nami jioni hii ya leo niweze kutoa mchango wangu wa maoni katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwa upande wangu binafsi, kipekee kabisa lazima niishukuru Wizara na Uongozi wa Wizara kwa maana kile ambacho nilikiwasilisha mwaka 2021, karibu asilimia 66 kimechukuliwa na Wizara na kufanyiwa kazi. Naishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upekee kabisa niishukuru na niipongeze Serikali ambapo mwaka 2021 wakati nachangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii, nilishauri kwamba katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo, lengo la Serikali la kujenga Bandari za Uvuvi, Kilwa Masoko ifikiriwe na iwekewe kipaumbele kwa sababu kuna kina cha asili. Nashukuru Wizara imepokea hili na limefanyia kazi na mpango huu sasa unakwenda kutekelezwa. Pongezi sana kwa Rais Samia, Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini rai yangu katika mpango huu wa Bandari ya Uvuvi ambayo inakwenda kuanza

kujengwa mwishoni mwa mwezi huu kama ambavyo Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeelezea katika ukurasa wa 104, kwamba ameshapatikana Mkandarasi ambaye ni *China Harbour Engineering Co. Limited,* na mchakato wa kuanza ujenzi unaanza mwisho wa mwezi huu wa Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu nini katika hili? Moja, ni kwamba wakati tunajenga bandari hii, ilikuwa ni finyu kwa mahitaji ya wakati huo na kwa maana hiyo sasa hivi inakwenda kupanuliwa. Kwa maana hiyo, pembezoni mwa eneo la bandari na gati kuna miundombinu mingine ikiwemo makazi pamoja na nyumba nyingine kwa matumizi mbalimbali. Tafsiri yake ni kwamba kunahitajika kulipia fidia kwa waliokuwa wanahusika na maeneo haya. Naomba Wizara ikahakikishe inalipa fidia kwa wakati ili kuepukana na migogoro tunapokwenda kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati kama hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu ya pili katika eneo hilo, bandari hii inakwenda kufungua fursa nyingi sana ikiwa ni pamoja na viwanda vya kuchakata samaki pamoja na mazao mengine ya bahari. Naomba na nitoe rai sana kwa Wizara, viwanda hivi visiende kutengenezwa au kujengwa kilomita 100 kutoka maeneo ya uzalishaji. Itakuwa ni jambo la ajabu, na la kituko, na la kuongeza gharama zisizo na sababu. Sisi Kilwa tuna ardhi ya kutosha ya kuweza kupanua viwanda hivi vya kuchakata, kusindika, mazao ya bahari pamoja na samaki kwa sababu uzalishaji utakuwa mzuri kwa kuwa bandari iko pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu nyingine, tunapozungumzia bandari ya uvuvi, tafsiri yake ni kwamba tunakwenda sasa kunasibisha pamoja na masuala mengine yanayoendana na uwepo wa bandari ya uvuvi ikiwemo Chuo cha Uvuvi. Tunapozungumza, tuna chuo chetu kikubwa maarufu cha uvuvi Mbegani, pia kuna chuo kingine kidogo cha Mtwara Mikindani. Kwa fursa hii ya uwepo wa Bandari ya

Uvuvi Kilwa Masoko, naomba Chuo cha Uvuvi kijengwe Kilwa Masoko na eneo la kutosha tunalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho katika rai yangu kwenye eneo hili la bandari, litaendana na uwepo wa miundombinu mingine rafiki kwa ajili ya kuwezesha bandari yetu sasa ifanye kazi vizuri. Hapa sasa nakusudia kuzungumza kwa Kimatumbi, maana yake tunahitaji *access roads to the port*. Kwa maana hiyo sasa, barabara tuliyonayo ya kilomita karibu 30 kutoka bandarini Kilwa Masoko mpaka Nangurukuru ilikuwa ya viwango vya wakati huo kwa matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, ihakikishe kwamba kilomita 30 hizi za kutoka Bandari Kilwa Masoko mpaka Nangurukuru, zinakuwa katika viwango kwa ajili ya matumizi bandari kubwa ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshmiwa Naibu Spika, baada ya eneo hilo la bandari ya uvuvi, niendelee kukumbusha rai ambayo niliitoa mwaka 2021 wakati nachangia Wizara hii, kwamba kutokana na uzalishaji mkubwa wa samaki Kilwa, hususan Kilwa Kivinje, tunahitaji soko la samaki pale Kilwa Kivinje. Bahati mbaya sana katika mapitio ya mpango wa bajeti hii inayoishia Juni, sijaona utekelezaji wala mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na nikumbushe kwamba Soko la Samaki pale Kilwa Kivinje ni muhimu. Kama macho yangu hayakupitia vizuri wakati napitia bajeti na randama, basi Waziri atakapokuja kufanya *sum-up* aelezee hilo kwamba tuna mpango gani sasa wa kujenga Soko la Samaki pale Kilwa Kivinje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe takwimu; hatuzungumzi kwa ajili tu ya kupendelea kwa sababu Kilwa Kivinje tunahitaji Soko la Samaki, hapana, Mkoa wa Lindi peke yake, wavuvi ni zaidi 6,000. Katika wavuvi zaidi ya 6,000 wa Mkoa mzima wa

Lindi, wavuvi zaidi ya 5,000 wanapatikana Wilaya ya Kilwa. Ndiyo maana tukasema ni fursa ya kutengeneza Soko la Samaki Kilwa Kivinje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nije sasa katika Sera, Sheria na Kanuni kama ambavyo Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeelezea ukurasa wa 109 mpaka 110. Kwenye eneo hili, nashukuru hatua za awali zimeanza. Mwaka 2021 wengi tulichangia sekta hii ya uvuvi na tulikuwa tukilalamikia mabadiliko ya Kanuni za uvuvi za mwaka 2020, ndiyo kilio kikubwa cha wavuvi wetu. Masuala ya makatazo ya uvuvi wa usiku, makatazo ya *ring net* na mambo mengine mengi ambayo tuliyajadili, ni kwa sababu ya mabadiliko ya kanuni ya mwaka 2020. Hapa mmesema mnakwenda kubadilisha Kanuni za Mwaka 2009, hazikuwa na matatizo makubwa sana, matatizo makubwa yalijitokeza kwenye mabadiliko au marekebisho ya Kanuni hizi za mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upekee wa mwaka 2021 nilitoa kifungu ambacho ndiyo kimeleta changamoto zote hizi. Naomba nirudie hapa, hiki ni Kifungu cha 66 au Kanuni ya 66 ya mabadiliko ya Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2020, Kanuni ndogo ya kwanza na kifungu dada (d) na Kifungu gaga (g), vikaangaliwe kwa umakini. Mmeitisha wadau wa uvuvi, mmeitisha Kamati ya kupitia mapendekezo yenu, Kamati ya Sheria Ndogo; nilitamani sana sisi ambao tunaotoka kwenye sekta za uvuvi tungealikwa ili tutoe hizi *inputs* ambazo sisi ndio wadau husika, tunajua taratibu za uvuvi. Kama mtaitisha tena Kamati ya kupitia, kwa maana ya Kamati ya Sheria Ndogo, nitoe rai sana, sisi tunaotoka kwenye sekta za uvuvi tualikwe tukatoe maoni yetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, ni kengele ya pili. Ahsante.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda umeisha! Basi mengine nitachangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Kakoso, lakini ataanza Mheshimiwa Tunza kwa dakika 10 na Mheshimiwa Kakoso dakika tano.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kuwa hai na kuwa na afya njema ya akili jioni ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natokea Mtwara. Mtwara tuna Bahari ya Hindi yenye kina kirefu na samaki wengi sana tu, lakini tunashindwa kuwapata kwa sababu ya uwekezaji finyu katika sekta hii, hivyo kupelekea uvuvi kuonekana kama ni shughuli ndogo ndogo ya watu wanyonge ambao hawajiwezi. Ukisoma, utaona kuna nchi nyingi duniani zimenufaika, zinaingiza pato kubwa la Taifa kwenye nchi zao kutokana na sekta hii ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua hii Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina watu wawili. Mheshimiwa Ulega yeye ni mtaalam wa uvuvi, tulitarajia kwamba tunavyokwenda kwenye mambo ya uvuvi, kwa sababu yupo mtaalam, aweze kulipeleka hili gurudumu mbele. Mheshimiwa Ndaki yeye ni mtaalam wa mambo au ana uzoefu na mambo ya mifugo, tulitarajia kule kwenye mifugo nako kufanye vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo kubwa sana la kusikitisha, miongoni mwa Wizara ambazo mimi naweza kusema kama Serikali haizitilii maanani ni Wizara hii ya Mifugo

na Uvuvi. Wakati mwingine tunatamani kuwalaumu hawa Mawaziri, lakini watafanya kazi wakati fedha hawana? Mimi ndiyo swali langu la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2021 wakati nachangia kwenye Wizara hii, nilisema nimepata mshtuko, watu wakacheka. Nilisema nimepata mshtuko kwa sababu fedha za maendeleo ambazo zimetengwa ni nyingi wakati hii Wizara hawawapi fedha, kwa nini wanawaacha wanatenga fedha nyingi na hawawapi? Kilichotokea ni nini? Wamewatenga fedha za maendeleo kwenye Sekta ya Uvuvi, (mimi leo nitajikita tu kwenye uvuvi) wametenga Shilingi bilioni 99.14; fedha za ndani shilingi bilioni 62.5 na fedha za nje shilingi bilioni 36.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka tunakuja leo kwenye Hotuba ya Waziri, fedha ya maendeleo ambayo imepelekwa Wizara hii ni Shilingi ngapi? Shilingi bilioni 3.95. Tunakaa hapa tunafanya nini? Huyo ndio unamtegemea sasa aende akafanye shughuli mbalimbali za maendeleo kwenye sekta ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupa mifano michache, si tuliwapitishia hizi! Kazi ya Bunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali, tukapitisha, tukasema tunawashauri, tunawasimamia; sijui tumefeli kuwasimamia, sielewi, lakini habari ndiyo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakupa mifano, katika bajeti ile walikuwa na malengo, pamoja na mambo mengine wanasema: "ukarabati na utanuzi wa kituo cha ukuzaji viumbe maji, Ruira Songea. Shilingi ngapi imetengwa? Shilingi milioni 791. Mpaka hapa tunapoongea, hata shilingi 10/= haijaenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati na utanuzi wa kituo cha ukuzaji viumbe maji Nyengedi, Lindi; kuna Tandahimba huko kwetu Mtwara na wapi; shilingi ngapi zimetengwa?

Shilingi milioni 715; mpaka leo tunapoongea hata shilingi 10 haijaenda. Ujenzi wa kituo cha ukuzaji viumbe maji bahari cha Ruvula, kipo Mtwara kwetu huko; shilingi ngapi? Shilingi milioni 983; mpaka hapa tunapoongea, hata shilingi 10 haijaenda. Sasa nimekupa mifano michache. Kuna watu wa *TAFIRI* ndiyo tunategemea huko utafiti na vitu vingine vikafanyike. Walitengewa shilingi milioni 700; hata shilingi 10 haijaenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakaona wajifariji kidogo, wakapunguza tena bajeti ya maendeleo kwa mwaka huu ambao tunaoujadili; kujifariji tu kwa sababu umetoka shilingi bilioni 99, umepewa shilingi bilioni tatu. leo unapunguza, shilingi bilioni 92, unataka kuniambia huo muda uliobaki ninyi mtapata hizo fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *concern* yangu kubwa, sisi tunaotoka maeneo ya wavuvi, tunajua ni namna gani Sekta ya Uvuvi ina umuhimu kwa watu wetu na kwa wananchi wetu. Yaani kama mnavyoona kwenye maeneo mengine, wao wana migodi huko ya madini wanachimba wanapata fedha, nasi tunaotoka kwenye maeneo ya uvuvi, tunajua umuhimu wake. Kutufanyia mambo kama haya, siyo sawa. Wapeni hela hawa Mawaziri wafanye kazi, tuje hapa tuwaulize hawafanyi kazi wakati fedha mmewapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha yupo hapa, mwaka 2021 alitusikia, na leo anatusikia, na nawaambia tukirudi mwakani Mwenyezi Mungu akitupa uhai, tunakuja kuyajadili mambo haya haya. Tunafanya mambo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, kule Kilwa Masoko wametenga shilingi bilioni 50 mwaka 2021 kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi, haikutoka hata shilingi 10; mwendelezo ule ule! Mwaka huu tena wametenga shilingi bilioni 59, Mheshimiwa Waziri akija hapa kumalizia hoja yake,

naomba atueleze zile shilingi bilioni 50 za mara ya kwanza zinakwenda lini? Vile vile hizi zitakwenda? Tunachotaka sisi, bandari ile ikijengwa vizuri ndiyo ile dhana ya Uchumi wa Bluu inaanzia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani, hivi tangu nchi hii ipate uhuru, leo ni miaka sitini ngapi, bado tunazungumzia watu wanaenda kuvua na boti za kusukuma na makasia? Wapeni fedha *TAFIRI* wafanye utafiti, wawaambie watu samaki wako wapi? Waambie watu mazalia ya samaki yako wapi? Mnafanyaje, hamtoi fedha? Kuna Waziri, kuna Katibu Mkuu, wanafanya nini kama Serikali, kama Wizara ya Mheshimiwa Mwigulu haitoli fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na kusema hii Wizara haifanyi kazi, lakini anayekwamisha kwa kiasi kikubwa Wizara hii isifanye kazi ni Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Kwa hiyo, tukimtafuta mchawi, wa kwanza ni Wizara ya Fedha na Mipango. Yaani hawa watu wa Mifugo na Uvuvi, nitakuja kuwasema hapa baada ya kuona wamepewa fedha na wameshindwa kufanya kazi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, ni kengele yako ya pili.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, lakini ujumbe huo ufike na ufanyiwe kazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, dakika tano.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa jitihada wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo ninalozungumzia zaidi ni eneo la Ziwa Tanganyika hasa kwenye Sekta ya Uvuvi. Ziwa Tanganyika ni ziwa ambalo lina kina kirefu na wavuvi ambao wanavua kwenye eneo la Ziwa Tanganyika wanavua uvuvi wa kubahatisha. Naiomba sana Serikali ielekeze nguvu kuwasaidia hawa wavuvi kwa kuwapelekea zana za kisasa ili waweze kujikwamua katika shughuli zao za kiuchumi, bila hivyo hawawezi kabisa kujikwamua. Kwa sababu eneo la Ziwa Tanganyika ni eneo ambalo mvuvi anaweza akakaa hata mwezi mzima asipate mazao ya uvuvi kutokana na kina kirefu kilichopo Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kuiomba Serikali, punguzeni tozo kwa wavuvi. Eneo hili linawakwamisha sana wavuvi. Unakuta mvuvi mmoja analipia leseni ya mtumbwi, analipia leseni yake kama mvuvi, analipia leseni ya wavu na analipia leseni ya umiliki wa chombo. Kwa hiyo, mtu mmoja analipa leseni karibu nne. Naiomba sana Serikali ikae iangalie jinsi gani ya kuwasaidia hawa wavuvi kupunguza zile kero ili wavuvi waweze kujikwamua katika shughuli zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alifanya ziara kwenye eneo la Jimbo langu. Amefika eneo la Ikola; ule mwalo ulishamezwa, nilimwomba awajengee mwalo kwenye Kata ya Karema ili wavuvi hawa wanaovua kwenye Ziwa Tanganyika, eneo la Kata ya Karema wapate sehemu ya kuhifadhi mazao yao. Naomba sana hili alifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine kwenye Sekta ya Uvuvi ni eneo la mazalia ya samaki. Eneo hili ni muhimu sana kwa Wizara ili itenge maeneo muhimu ndani ya Ziwa Tanganyika ambayo yatasaidia sana kuwa na mazalia ya samaki ambayo yatakuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni uthibiti wa nyavu haramu zinatokea nchi jirani ya Burundi. Zile nyavu za filamu ni mbaya sana ambazo kipande cha nyavu kikakatikia kwenye ziwa kinaendelea kuua samaki na vizalia vyote vilivyoko kwenye ziwa. Naomba hili mlifanyie kazi ili wavuvi wawe na uvuvi endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie Sekta ya Mifugo. Tunamwomba Waziri aje na mpango mkakati wa kuboresha ranchi za Taifa ili ziweze kuwasaidia wafugaji wakubwa na wadogo. Pia tunamwomba aje kutujengea majosho kama alivyokuwa ameahidi alipokuwa amekuja kwenye ziara kwenye Jimbo langu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa hizo dakika tano…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa dakika chache, nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka eneo la watu wanaofuga na wanaovua. Mheshimiwa Waziri, *uncle,* Halmashauri ya Bunda unaijua, wanafuga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ulega Halmashauri ya Bunda unajua wanavua, lakini Wizara hii hamjatuendea haki zaidi ya miaka mitatu mfufulizo tumekuwa tukiomba majosho, tumekuwa tukiomba mtukarabatie na kutujengea uzio kwenye minada, tumekuwa tukiomba machinjia kwa sababu lililopo ni la mwaka 1979 Mheshimiwa Ester Bulaya sijazaliwa. Lakini Mheshimiwa Ulega

umejibu swali hapa maswali yangu ya kuomba vikundi vya uvuvi, Kikundi cha Wauza Samaki Bunda Mjini, Kikundi cha Ushirika cha Uvuvi cha Nyatwali vipatiwe mikopo; wameitikia wito wa Serikali wa kuvua kisasa, hivyo vifaa vya kisasa hawana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana sasa Mheshimiwa Waziri sisi tunauhitaji wa majosho Matano, Halmashauri ya Mji wa Bunda ina Kata 14, Kata saba ziko vijijini huko wanafuga. Tulikuwa tumeomba majosho Matano na ninajua kwenye fedha za majosho mnazo; Anko naomba hata mawili kwa mwaka huu wa fedha mahitaji yapo kwenye Kata ya Kunzugu, Mchalo, Kabasa, Waliku na Guta. Tunaomba walau kwa kuanzia mwaka huu wa fedha mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri unajua sisi Bunda tuna minada mitatu, lakini tunaomba walau kwenye minada miwili wa Bitalaguru Kata ya Kabasa na wa Kinyambwiga Kata ya Kunzugu. Halmashauri iliomba Milioni 257 kwa ajili ya hii minada na tukikarabatiwa tukaweka na uzio; mosi itasaidia utoroshaji wa mifugo lakini vilevile tutachangia hii Halmashauri mpya ya Bunda ili iweze kukusanya mapato na kufanya maendeleo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri tulikuwa tunaomba machinjio na tayari tulishakuwa tumeomba milioni 150 kupitia mradi wa *TACTIC* bado hatujapata. Tunaomba machinjio, lile lililopo ni la mwaka 1979 wala Bulaya sijazaliwa, nimezaliwa, nimekuwa Mbunge, tunaomba machinjio mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ulega, umenijibu maswali zaidi ya mara tano kuahidi vikundi, leo hapa sema neno; vikundi vyangu vya wavuvi na vinanisikia sasa hivi vinahitaji fedha waweze kuvua kisasa na waweze kujiendeleza kimaisha. Amesema Mheshimiwa Tunza, hii

sekta ya uvuvi mnaona kama ya watu maskini maskini hapana wawezesheni ili na wenyewe kama watanzania wengine. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante muda wako umekwisha. Mheshimiwa Edward Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayofanya kwa wizara hii, tumeona bajeti imeongezeka; nimpongeze pia Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya wizara hii kwa kazi wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka uliopita wafugaji walipata taabu kubwa sana kutokana na ukame; na Mheshimiwa Naibu Waziri alinitembelea tarehe 14 Januari, 2022 kuona athari za ukame kwenye Jimbo la Kiteto. Tulipata hasara karibu ya ng'ombe 25,000 kwa sababu ya ukame. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri alifika na aliona athari ambazo zimeletwa na ukame na nakushukuru kwa majosho Matano kwa vijiji vya Makame, Mwitikila, Lolela, Ngabolo na Katikati. Lakini kwa kuwa Kiteto ni Wilaya kubwa yenye mifugo wengi sana bado tuna upungufu wa majosho na tulitegemea bajeti hii mtatuongezea majosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukame wa mwaka jana umetokana na kukosekana kwa mvua na malisho. Kwa hiyo, tunategemea wizara hii, kipindi hiki mje mlete bajeti ambayo inaleta *solution* kwa ajili ya mabwawa. Na mnafahamu nimeandika barua katika kuomba mabwawa. Natamani baadaye wakati mnahitimisha bajeti yenu mtupe majibu kwa sababu wafugaji hawa wanataka kusikia majibu yenu. Kwa kuwa tayari kuna dalili kwamba mwaka huu pia ni kama kidogo hivi; natarajia kabisa wizara ituambie baadaye mmejipangaje sasa ili madhara haya ambayo yanatokana na ukame isirudi kwa namna ambayo imefanyika mwaka

jana, kwa kuandaa wafugaji na kuandaa maeneo kama ambavyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Hereni ambalo limeendelea sasa. Ushauri wangu, elimu haipo sana ya kutosha kuhusu suala hili Mheshimiwa Waziri; tunawaombeni sana mtoe elimu kwa wafugaji wafahamu logic ya hii Hereni nini na pia tunaweza kusikia kelele kwamba bei hii ni kubwa kidogo kwa hiyo muangalie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri ulifika Kiteto na ulitoa ahadi ya vitambaa vile vya magonjwa haya ya Ndorombo, tunatarajia baadaye wakati unahitimisha kwenye bajeti yako wananchi wa Kiteto wasikie majibu, tukipata vitambaa hivi tukaweka kwenye maeneo ya malisho itasaidia kupungu magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wizara hii inaangalia mifugo, siku hizi tumepata janga kubwa sana mahusiano siyo mazuri sana kati ya Wanyamapori, Hifadhi zetu na Wafugaji. Tunataka wizara kwa kuwa tulishazungumza hapa *concept of one Government* Wizara ya Maliasili na Utalii na Mifugo mzungumze ili kuondoa matatizo hayo kwa wafugaji.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kwa mchango mzuri.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alifika jimboni kwangu Singida Kaskazini Kitongoji cha Mukulu, Kata ya Mughunga mwishoni mwa mwaka 2021 na kuwaahidi wananchi wa kitongoji hicho kuwa atawajengea josho la mifugo. Wananchi wale walifurahi sana kwa ahadi hii ya Serikali kwa sababu wanapata taabu sana kuogesha mifugo yao ukizingatia ni jamii ya wafugaji na maisha yao yote yanategemea mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumkumbusha Mheshimiwa Waziri kuhusu ahadi hii kwani wananchi wananikumbusha mara kwa mara na wanaisubiri huduma hii kwa hamu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuishauri Wizara kuanzisha viwanda vya kusindika nyama. Ni muhimu sana kuanzisha viwanda maeneo ya Singida, Dodoma, Shinyanga, Arusha na maeneo yanayofuga ng'ombe kwa wingi ili kuongeza thamani ya mifugo yetu na kuweza kuuza nyama nje ya nchi hususan Visiwa vya Comoro ambavyo vinategemea sana nyama kutoka Tanzania badala ya kusafirisha ng'ombe walio hai, tuweze kusafirisha *processed meet*.

Pia ni muhimu kuanzisha viwanda vingi vya maziwa nchini, jambo hili litainua uchumi wetu na kuajiri vijana wetu waliopata mafunzo mbalimbali hususan katika fani husika ya uzalishaji, usindikaji, masoko na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusisitiza sana suala la josho la mifugo kama alivyoahidi Mheshimiwa Waziri kwa

wananchi wa Jimbo la Singida Kaskazini Kitongoji cha Mukulu ambacho hakina kabisa huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 49 na ukurasa wa 88 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la migogoro ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Nipongeze Wizara kwa kutatua migogoro hii ambapo Mkoa wa Lindi imetatuliwa migogoro kumi. Aidha, kwa mpango wa mwaka 2022/2023, Wizara itaendelea kutatua migogoro husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kuwa Wizara ijikite kwenye kuzuia migogoro zaidi kuliko kusubiri itokee ndipo watatue. Ni vema Wizara ikafanya tathimini ya mifugo hitajika kila Mkoa au Wilaya na hatimaye kuweka mikakati ya kudhibiti kuongezeka kwa mifugo katika maeneo husika.

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Rais kwa kazi kubwa anayofanya katika kuisaidia sekta ya uvuvi. Pia nimpongeze Waziri na Naibu pamoja na uongozi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kuhusu zao la samaki ambalo wananchi wa maeneo ya maziwa na bahari wanategemea sana kwa kufanya biashara ya Samaki. Kwa vile samaki wanawategemea kufanya biashara naiomba Serikali iwawezeshe wavuvi kwa kuwanunulia vyombo vya kuvulia ili waweze kukuza zao hili, na wananchi waweze kukuwa kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichangie kuhusu leseni kuwa inaleta changamoto katika maeneo ya pwani, hivyo

niiombe Serikali iweke njia rahisi ya kupata leseni ili kuondoa changamoto hii ili wananchi waweze kufanya biashara hii na kujipatia kipato na kuongeza mapato katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu; katika kuudumisha Muungano wetu namuomba Waziri wa Wizara ya Uvuvi awe na mawasiliano mazuri na Wizara ya Uvuvi Zanzibar ili kuwafanya wavuvi wadogo wadogo kupata kipato na kuongeza uchumi wa nchi yetu na pia kuiunga mkono dhana ya uchumi wa buluu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchangia bajeti ya Wizara ya Mifungo na Uvuvi ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi zake nzuri anazozifanya katika Taifa letu. Aidha, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tuna wavuvi wengi wadogo wadogo lakini bado hali za maisha sio nzuri na kwa vile wameshavuua muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, ni lazima tuanzishe viwanda vya Samaki ili kuweza kuwatengezea mazingira bora wavuvi wetu na wale wadogo wadogo ambao watavua bahari kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali iweke *cold room* (majokofu) ya kuhifadhia samaki kwa vile tunajikita katika uvuvi wa bahari kuu. Tukiwa na sehemu hizi tunavutia meli nyingi kuja kuvua nchini kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali iweke mikakati endelevu ya muda mfupi wa kuimarisha na kuwasaidia wavuvi ili kuwa na uwezo kamili na kuvua kwenye bahari kuu, kwa kufanya hivi kutasaidia ajira katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapaswa kutoa mafunzo kwa wavuvi wetu wadogo ili kuimarisha uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunaiomba Serikali kuimarisha upatikanaji wa masoko ya kimataifa ya kuuza samaki. Jambo hili ni muhimu na litasaidia kuitangaza zaidi nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake. Aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, viongozi wote na watendaji wote Serikalini kwa jinsi walivyosimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM yam waka 2020 – 2025; hongereni sana na Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii muhimu sana kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunaiomba sana Serikali iiongezee bajeti ya Wizara hii kwani kuna mahitaji makubwa sana ya rasilimali watu, miundombinu, vitendea kazi na mahitaji makubwa ya kukabiliana na majanga ya ukame, magonjwa na upungufu wa maeneo ya malisho.

Pili, kwa kuwa sekta hii ya mifugo imekuwa na mchago mkubwa katika pato la Taifa na wafugaji wanakabiliwa sana na maeneo ya malisho ni wakati muafaka kwa Taifa letu kusimamia mkakati wa kubadilisha koo za mifugo kwani hatua hii itawafanya wafugaji kuwa na mifugo wachache na watakaohimilika kutunzwa, kuhudumiwa na kuongeza mapato kwa mfugaji na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kuondoa upungufu wa Maafisa Ugani Serikali iangalie utaratibu wa kuwaajiri na kuwapanga kulingana na wingi wa mafugo na kuwapangia majukumu ya kila siku kwenye vituo vya mafunzo kila kata na kijiji badala ya wao kutafutwa na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo wengi wao hupenda kupangwa kwenye Makao Makuu ya Halmashauri hata kama wako wachache badala ya tarafa, kata na kijiji, hali inayowafanya mchango wao wa kitaalamu kutokuonesha matokeo makuu kwa Serikali na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa minada yetu tunaishauri Serikali iweke mizani ya kupima mifugo kwani hakuna uhalisia wa pande zote mbili (muuzaji na mnunuzi) hivyo basi hapo ni lazima matumizi ya vipimo vitumike kuleta uhalisia kwa kuanza na minada mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa sekta ya uvuvi Serikali itoe waraka wa maelekezo ya usimamizi kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa kuwatumia Maafisa Maliasili wa ngazi hizo katika kuzuia uvuvi haramu kwenye mabwawa na maziwa madogo kwani hakuna Maafisa Uvuvi wa kutosha na athari ni nyingi sana kutokana na uvuvi unaoendelea huko kwenye maziwa hayo kwa mfano Ziwa Tlawi Mbulu na Ziwa Babati na Basutu Hanang.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Mifugo na Uvuvi Ndugu Mashimba Ndaki, Naibu wake Ndugu Abdalah Ulega, wataalamu wa Wizara na wadau wa sekta hizi kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kilimanjaro una fursa nyingi za kufuga aina mbalimbali za wanyama kama vile ng'ombe na mbuzi wa maziwa na nyama, kondoo, nguruwe, sungura, kuku, bata na samaki kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya mlimani (Kilimanjaro) yanaweza kutumika kwa ufugaji wa ndani *(zero grazing)* kwa ng'ombe wachache na mbuzi wa maziwa, nguruwe, sungura, kuku na bata.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la ukanda wa tambarare kwenye Kata za Arusha Chini na Mabogini lina wafugaji wa Kimasai na lina uwezekano wa kuzalisha kwa tija ng'ombe, mbuzi na kondoo wa nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi za wafugaji wa Jimbo la Moshi Vijijini, aina za kienyeji za wanyama (ng'ombe, mbuzi, nguruwe na kuku) wanaofugwa ni kikwazo kikubwa kwenye maendeleo ya sekta ya mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya uvuvi inaweza kuwapatia wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini kipato kikubwa iwapo itaendelezwa. Hili litawezekana ikiwa wananchi watapatiwa mafunzo ya kitaalamu ya jinsi ya kufuga na kukuza samaki kwa kutumia teknolojia ya mabwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufugaji endelevu wa samaki unaweza kutatua changamoto za umaskini kwa kuwaongezea kipato na kuchangia kikamilifu kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Arusha Chini kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu, wavuvi wanaweza kusaidiwa na Maafisa Ugani wa uvuvi mbinu bora za ufugaji wa samaki, ikiwepo matumizi ya vizimba. Uwekezaji wa vizimba unaweza kufanyiwa majaribio kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha ufugaji wa ng'ombe, mbuzi wa maziwa na nyama, kondoo, nguruwe, sungura, kuku, bata na samaki katika Jimbo la Moshi Vijijini, ninaishauri Wizara itusaidie yafuatayo:-

Kwanza, naishauri Serikali kwa kushirikiana na wadau wa mifugo na uvuvi wafanye utafiti na kuangalia changamoto na fursa zilizopo katika Jimbo la Moshi Vijijini ili wajue pa kusaidia.

Pili, naishauri Serikali ipeleke wataalamu wa mifugo kutoa mafunzo ya ufugaji bora wa mifugo ya kimkakati yenye tija katika Jimbo la Moshi vijijini.

Tatu, naishauri Serikali iwe na programu maalumu ya kuzalisha mitamba wa maziwa wenye sifa zinazohitajika ikiwa ni pamoja na mifugo mingine kama mbuzi wa maziwa, ng'ombe wa nyama, nguruwe na kuku. Wafugaji wengi katika Jimbo la Moshi Vijijini hawana mbegu bora za ng'ombe wa maziwa. Kwa ujumla huwa wanabahatisha.

Nne, naishauri Serikali ihamasishe kuanzishwa kwa vikundi vya ushirika wa wafugaji mifugo na samaki katika Jimbo la Moshi Vijijini ambavyo itakuwa rahisi kuwapatia huduma za mitaji na utaalamu.

Tano, naishauri Serikali itupatie wataalamu wa kuchimba mabwawa katika Jimbo la Moshi Vijijini.

Sita, naishauri Serikali ianzishe Kituo cha Kanda cha kuzalisha vifaranga wa samaki jimboni kwangu ili wafugaji wavipate kwa urahisi kama vile vilivyopo kwenye Mikoa ya Morogoro, Tabora, Ruvuma, Lindi, Tanga na Geita.

Saba, naishauri Serikali iwezeshe wazalishaji vifaranga binafsi katika Jimbo la Moshi Vijijini ili wasaidie juhudi za Serikali kwenye kukuza hii sekta.

Nane, naishauri Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Moshi, wawezeshe kupandikiza vifaranga bora vya samaki katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, kwani wavuvi waliniambia kwenye kampeni kuwa samaki wamehama ikiwa na maana kuwa wamepungua. Hii ni pamoja na kuanzisha uvuvi wa vizimba.

Tisa, naishauri Serikali iwe na huduma za uhakika za ugani katika Jimbo la Moshi Vijijini ikizingatia lishe ya samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi, napendekeza Serikali ifanye majaribio ya kutumia vizimba kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu ili kuongeza tija kwenye ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishauri Serikali iwekeze kwenye kuanzisha mashamba darasa ya ufugaji bora wa mifugo ya kimkakati na samaki jimboni kwangu Moshi Vijijini ili wajifunze kwa vitendo kama ilivyowasilishwa kwenye hotuba ya bajeti yam waka 2022/2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kinipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika hotuba hii ya makadirio na mapato ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwasilisha hotuba hii katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha na umakini mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu unyanyaswaji wa wavuvi katika baadhi ya bandari; napenda kuchangia hotuba kwa kutoa masikitiko yangu makubwa juu ya namna ya tabia mbovu ya baadhi ya Maafisa wa Uvuvi wanaojuilikana kama watu wa *marine*. Watu hawa wamekuwa wakiwapa shida kubwa wavuvi hasa wanaotoka upande mmoja wa Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi wanaotoka Zanzibar wamekuwa na utaratibu wa asili kuja kuvua huku Bara. Wanapotoka Zanzibar huwa wanakuja na vielelezo vyote vinavyohalalisha kuwepo kwao. Vielelezo hivyo ni pamoja na leseni za uvuvi, barua kutoka maeneo wanayotoka kwenda maeneo wanayofikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosikitisha ni kwamba wakifika katika maeneo husika huwa wanaambiwa kuwa vielelezo vile havitambuliki na kutakiwa kutafuta vingine kwa bei kubwa sana.

Aidha wanapoenda kuvua huwa wanawavizia na kuwasingizia kuwa wameharibu mazingira, hatua hii huwapelekea kuwanyang’anya leseni zao za uvuvu na

kuwapiga faini kubwa sana ambayo kuna wakati huwa wanashindwa kulipa. Wanaposhindwa kulipa huwa wanawanyang'anya mashine zao za uvuvi mpaka watakapokamilisha malipo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya bandari hizo zinazowapa shida wavuvi ni pamoja na Mnyanjani, Mwarongo, Kigombe na Mwarongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika jambo hili kwa Wizara ni kufuatilia tatizo hili mapema kabla halijageuka kuwa ni kero za Muungano ambazo Serikali yetu inajitahidi sana kuziondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina hoja zifuatazo; kwanza Mkoa wangu wa Iringa tuna wafugaji na wavuvi kwenye Bwawa la Mtera. Bajeti ya mwaka 2021/2022 Wizara iliahidi mikakati ifuatayo:-

(a) Kutengeneza vichanja vya kukaushia dagaa na Samaki;

(b) Wataongeza uzalishaji wa barafu na kujenga *cold rooms.* Hadi sasa wananchi wavuvi mkoani kwangu wanasubiri *cold rooms* kwa ajili ya kuhifadhia Samaki; na

(c) Mliahidi kununua boti za uvuvi, hatujapata bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifugo mingi malisho yake ni changamoto kiasi kwamba mazao yake yanakuwa kidogo. Ushauri wangu:-

(a) Wizara ihimize uandaaji wa malisho ya mifugo. Tuelimishe wananchi kilimo cha majani kwa mifugo

na tuwawezeshe wafugaji kuwa na malisho ya mfano.

(b) Wizara itafute soko kwa wavuvi na wafugaji wetu ili wavue na kufuga kisasa.

(c) Wizara itoe mafunzo, ihimize wananchi kuwa katika vikundi na kuwawezesha ufugaji wa mifugo na samaki pia mshirikiane na Halmashauri zetu katika mikoa yote ili kuinua wananchi na kuwaunganisha na taasisi za kifedha.

(d) Wizara itengeneze vichanja kwa ajili ya kukaushia Samaki.

(e) Wafugaji wakubwa kama ASAS Iringa azidi kupewa wataalamu ili aweze kufanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji

wa ustawi wa jamii na maendeleo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya mwaka wa kilimo 2019/2020 inaonesha kuwa idadi ya ng'ombe ilikuwa milioni 35.3; kati ya hao, wakulima wadogo walikuwa na ng'ombe milioni 35.1 na mashamba makubwa yalikuwa na ng'ombe 142,968. Aidha, wakulima wadogo walikuwa na mbuzi milioni 25.5 na mashamba makubwa mbuzi 33,847. Kwa upande wa kondoo wakulima wadogo walikuwa na kondoo milioni 8.8 na mashamba makubwa kondoo 24,075.

Vilevile nguruwe waliofugwa na wakulima wadogo walikuwa milioni 3.2 na mashamba makubwa yalikuwa na nguruwe milioni 3.4 na kulikuwa na jumla ya kuku milioni 92.8 ambapo wakulima wadogo walikuwa na kuku milioni 80.1 na mashamba makubwa yalikuwa na kuku milioni 12.7. Pamoja na idadi hiyo kubwa ya mifugo, mchango wa sekta ya mifugo na uvuvi wa asilimia saba bado ipo chini sana na tija ikiboreshwa kuna fursa kubwa ya sekta hii kuchangia sehemu kubwa ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Tanzania kuwa nafasi ya tatu kwa nchi za Bara la Afrika na kuchangia katika uchumi wa Taifa, sekta hii ya mifugo na uvuvi inazalishwa kwa tija ndogo. Katika hali hii, sekta ya mifugo haijamsaidia mfugaji na mvuvi kwa kiasi kikubwa kunajinasua kwenye umaskini na kimeendelea kutoa mchango mdogo kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ichukue hatua zaidi ili kuboresha sekta ya mifugo na uvuvi ikiwemo ujenzi wa mabwawa, kuwezesha mashamba ya kuzalisha lishe/chakula cha mifugo, kuwezesha sekta binafsi kuzalisha mitamba ya kisasa na vifaranga wa samaki. Napendekeza Serikali ianzishe vitalu vya mifugo katika Kata ya Mjele na Mshewe, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, ikiwemo kuchimba mabwawa na visima. Pia napendekeza kuwezesha kuanzisha mashamba makubwa ya kuzalisha lishe ya mifugo ikiwemo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali imalizie kujenga kiwanda cha nyama cha Utengule (Mji Mdogo wa Mbalizi) ambacho kwa muda mrefu ujenzi umesimama pamoja na kuwepo vifaa vyote muhimu vilivyotolewa na wafadhili. Kutokana na kuwepo uwanja wa Kimataifa wa Songwe ambao ni wa kimkakati kusafirisha mazao ya kilimo na mifugo kwa masoko ya nje, napendekeza umaliziaji wa kiwanda hiki cha nyama na pia uwezeshaji wa vitalu vya kunenepesha mifugo katika Kata za Mjele na Mshewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iongeze Maafisa Ugani, waliopo kwenye Halmashauri ya Mbeya ni wachache na wale waliopo hawaonekani kutoa huduma za ugani kwa wananchi. Wizara iweke msukumo wa kuhamasisha, kuanzisha na kutoa elimu kuhusu kilimo cha malisho ili kuwezesha malisho kutosheleza mifugo mwaka mzima. Pia Serikali iongeze kasi ya uzalishaji wa mitamba kutokana na idadi ndogo ya ng'ombe wazazi kwenye mashamba ya Serikali na matumizi madogo ya teknolojia ya uhimilishaji kwa kutumia mbegu bora za mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwepo na mkakati wa kuongeza mazao ya uvuvi ili kuwezesha samaki wapatikane kwa tija kuwezesha ushindania kwa soko la nje. Vijana wenye nia thabiti na wanaopenda kujishughulisha na ujasiriamali wa ufugaji samaki kwenye mabwawa watambuliwe na uwekwe

utaratibu maalum wa uwezeshaji kupitia Halmashauri zao kupata mitaji na utaalam wa kufuga samaki kwenye vizimba na mabwawa na hivyo kuweza kujiajiri wenyewe na kujipatia kipato.

Aidha, Serikali ishughulikie changamoto ya chakula cha samaki na uhaba wa vifaranga hapa nchini. Vijengwe vitotoleshi vingi katika vituo vya ukuzaji viumbe maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, dakika 10.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii naomba pia vilevile nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mashimba Mashauri Ndaki na kwa namna hiyo pia vilevile naomba nichukue fursa hii kuwashukuru Makatibu wetu Wakuu, Ndugu Tixon Nzunda na Dkt. Rashid Tamatamah lakini na watendaji wote katika wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee niwashukuru wajumbe wa Kamati yetu wakiongozwa na Mwenyekiti Dkt. Christine Ishengoma; lakini vilevile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametuchangia kwa kutupa mawazo, fikra na maoni mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Mkuranga kwa kuweza kuendelea kuniunga mkono wakati wote na kuhakikisha kwamba shughuli zinakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Waheshimiwa Wabunge wengi wamejadili na katika mijadala iliyokwisha kupita; la kwanza, limekuwa ni jambo linalohusu uwezeshaji wa wavuvi.

Naomba niwaeleze kwamba jambo hili limetamkwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi; lakini pia limetamkwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan na Serikali ya Awamu ya Sita kwa utayari wa kukamilisha ahadi hizi zilizotajwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Wabunge wengi wameonesha wasiwasi, nikianza na Mheshimiwa Mwantumu Zodo, ambaye alieeleza juu ya miradi iliyokwisha kupangwa katika bajeti ya mwaka 2021/2022 na haikutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ile ilihusu vichanja, *cold rooms*, ilihusu mambo mbalimbali yaliyowahusu wavuvi ikiwemo na zile alizoziita matumbawe feki ambayo sisi tunaita *FADS*, yaani *Fish Aggressive Devices*. Nataka nimuhakikishie ya kwamba fedha zote zile zilizoandikwa katika mwaka ule tumehama nazo, ilipatikana changamoto ambayo tumeieleza katika risala yetu iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri na ninataka nimuhakikishie yeye na Wabunge wote ya kwamba vile vichanja vilivyosemwa vitapatikana katika vijiji alivyovitaja vya Mkoa wake wa Tanga kuanzia Moa, Mwandusi, Tawalani, hiyo Mkinga yote itapata lakini vitakwenda mpaka kule Mtwara alipoishia kusema Mheshimiwa Tunza Malapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakae mkao wa utayari waendelee kuwahakikishia wavuvi wetu hasa wakulima wa Mwani na tena kwa umuhimu zaidi mwaka huu tumeongeza si vichanja vile 52 vitakavyotawanyika mkoa wote katika kilomita zote 1400 lakini tumeongeza zaidi. Katika mpango tulionao mpaka mashine za kukaushia Mwani zipo zimeandikwa katika bajeti hii; na moja ya fedha Bilioni 60 zilizoongezeka zitakwenda kufanya kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, lengo letu ni kuongeza thamani ya mazao yetu na katika kuongeza huku thamani wizara imejipanga vyema. Tumepata wadau ambao wapo *serious* kwa mfano wadau tuliowataja katika risala kama vile *DHL* tumekwenda kwa pamoja mkakati wetu wa masoko *marketing strategy* ambapo tunawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kwa pamoja; vile vikundi lengo letu kila kikundi kimesajiliwa, kipate *TBS certificate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia vilevile kiwe na *Barcode* yake. Mkakati wetu vikundi vyetu hivi viede kidigitali ndiyo uchumi wa Bluu, uchumi wa kidigitali kwa sababu masoko ya nje yamefunguka na yapo moja kwa moja, tunataka tuukate ule mnyororo wa madalali ili mzalishaji aliyeko kule Moa au Tanganyika anayetengeneza dagaa lake, awe na uwezo wa moja kwa moja kulitangaza soko lake na aweze kuuza bidhaa ile pasipo na shaka yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, ili niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge ambao wameonesha kuwa hawana hakika kwamba kama je hizi fedha zitarudi tena au ziliandikwa halafu ndiyo zimepotea, hizi fedha zipo na nataka niwahakikishieni ya kwamba zitakwenda kufanya ile kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu spika, wapo watu waliozungumzia Bima. Nataka niwaambie kwamba bima ya mifugo na bima ya wavuvi tayari kwa kushirikiana na wizara dawati letu la Sekta Binafsi limeshaanza kufanya kazi na ndiyo maana tumepata mikopo, mikopo imepatikana kwa wavuvi wengi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kutaja hapa baadhi ya vikundi ambavyo vimeanza kupata mikopo hiyo. Kule Ukerewe ambako Mheshimiwa Mkundi amesema kipo Kikundi

cha Bukasiga kimepata mkopo wa zaidi ya Shilingi Milioni 200. Lakini vilevile pale Sengerema kwa maana ya kikundi cha Kasalazi kimepata mkopo wa zaidi ya Shilingi Milioni 300 na kimeanza kufanyakazi hii hapa; pale Kikumbaitale Geita kwa maana ya Chato wamepata mkopo wa zaidi ya Milioni 200; na kule Kigoma Katonga wamepata zaidi ya Milioni 100; pale Kigoma tena Ujiji kwa maana ya kikundi cha Sangara *Beach* Amcos kimepata zaidi ya Milioni 70; kwa hivyo, tukichukua fedha hizi za *TADB* na mkakati tulionao wa hivi fedha tulizopata kwa jitihadi kubwa iliyofanywa na Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, nina hakika kwamba sasa kazi yetu itakwenda kuwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, unaweza ukaona Wabunge wengi wameshauri kwa sababu kila mmoja anaona namna ambavyo *stock* inapungua katika maji yetu ya asili; na kwa hivyo tuna umuhimu mkubwa wa kuwekeza katika ufugaji wa Samaki na ndiyo maana Serikali imedhamiria kuwekeza katika kuwa-*train* vijana na wale vijana wote wanakwenda kuwezeshwa kupata mikopo isiyokuwa na riba kupitia Benki yetu ya Kilimo ya *TADB* kupitia hizi fedha zilizoongezeka ambazo ni takriban Bilioni 60; kwa hivyo, tutakuwa na vituo atamizi zaidi ya 200 katika maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia tumeona tuanze huko kwa kuwa utafiti umekwishakufanywa na uwezeshaji sasa utakwenda kuwezesha vizimba zaidi ya 900 ambavyo vitakwenda kuwaajiri vijana zaidi ya 1500.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge naomba mtuunge mkono kwa sababu kazi kubwa na nzuri inakwenda kufanywa. Baadhi yenu hapa mmetushauri juu ya kwa nini mavuvi bado ni ya kienyeji? Program yetu inakwenda kuwezesha kununuliwa kwa boti zaidi ya 320, zitakazokwenda kuenea baharini kote kule, hizi boti ni za

kisasa zitakuwa na *fish finders, GPS,* na tayari *TAFIRI* wameshafanya hii kazi, kazi ya kujua wapi Samaki wanapatikana na program imeshatengeneza tunaita *PFZ* kwa maana ya *Potential Fishing Zones.* Kwa hivyo, naomba muwe na Imani na muhakikishe ya kwamba tunaungwa mkono katika bajeti hii na kwa kweli kabisa mambo haya ya Uchumi wa Bluu sasa yanakwenda kufanyiwa kazi. kwa upande wa mifugo pia vilevile kwa ufupi sana tumejipanga na tutakuwa na atamizi za vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulianza hii kazi pale Kongwe *TARIRI*. Kwa mumalizia naomba kwa heshima kubwa na taadhima Waheshimiwa Wabunge muendelee kutuamini, mtuunge mkono, mtupitishie bajeti yetu hii na *Inshaallahu Taallah* nawahakikisha ya kwamba kazi hii kubwa na nzuri inakwenda kufanywa. Ahsanteni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mtoa hoja dakika 20.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kukushukuru kunipa nafasi ili niweze kuhitimisha hoja ambayo tumekuwa nayo toka asubuhi. Lakini nikushukuru sana kwa usimamizi wa Bunge lako hili Tukufu; lakini pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja hii toka asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge ambao wamechangia hoja hii ni 22 kwa sababu ni wengi siwezi kuwataja kwa majina; lakini hawa wamechangia kwa kuzungumza lakini pia wapo waliochangia kwa maandishi Wabunge watatu; pia nitambue mchangiaji na hotuba ya Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji wamechangia kwa sehemu kubwa sana juu ya bajeti yetu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda ni mchache nadhani nitatumia muda huu kufafanua hoja

chache tu kwa sababu ya muda. Na hoja nyingi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge tutazijibu kwa maandishi lakini nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wabunge ambao wamechangia kwa maandishi au kwa kuzungumza kwa sababu yote waliyoyazungumza ni masuala yaliyokuwa yanalenga kutuelekeza, kutushauri lakini kutoa mapendekezo ambayo yakifanyiwa kazi yamkini kazi yetu ya mwaka wa fedha ujao 2022/2023 ikawa kazi njema na ikaendelea kuwasaidia watanzania na ikaendelea kuleta tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa nchi yetu, mama Samia Suluhu Hassan kwa kutuongezea bajeti lakini pia kwa kujali sana sekta hizi za uzalishaji kwa sababu safari hii sekta za uzalishaji karibu zote zimeongezewa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nianze sasa kujibu hoja moja moja kwa kifupi lakini kama nilivyosema tutajibu kwa maandishi kwa kueleweka vizuri na Wabunge wote ambao hoja zao wamezitoa zitajibiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Mariam Ditopile kuwawezesha wavuvi wadogo, limekwisha kusemwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, tutafanya hivyo. Tuna mpango wa kuwapa boti 320 tena zaidi lakini boti hizi zitakuwa ni *special* sana; zitakuwa na *GPS, Fish hold*, vifaa vya ubaridi, *Fish finder*, hizi boti zinauwezo wa kubeba tani 1.5.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hebu rudia boti ngapi? Mheshimiwa Waziri hebu rudia boti ngapi?

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni boti 320.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tunza umeisikia hiyo? Haya endelea bwana. *(Makofi/Vicheko)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia *TAFIRI* tumefanya utafiti kutambua maeneo yanayofaa kwa uvuvi na *program* tunaikamilisha ili kutumia kitu kinaitwa lango la simu ili kuwezesha wavuvi kupata taarifa za maeneo ya uvuvi moja kwa moja kwenye simu zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mariam pia alikuwa ana hofu juu ya upungufu wa samaki kwenye viwanda vyetu. Kupungua kwa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Viktoria, hususan samaki aina ya sangara, kunatokana na sababu mbalimbali na suala kubwa kabisa lililosababisha mojawapo ni uvuvi haramu. Sasa alitaka kujua mkakati wetu wa kudhibiti uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, kuanzia mwaka uliopita umekuwa ule wa kushirikisha wadau wote wa uvuvi. Ni kweli tumefanya kazi kubwa kupitia *operations* tulizozifanya, lakini kufanya *operations* peke yake tuligundua kwamba haitoshi, tukaona ni vizuri tushirikishe wadau wote kuanzia wavuvi wote wanaovua kwenye maziwa na kwenye bahari, lakini pia kuzishirikisha Serikali zetu za Mitaa, Halmashauri zetu pamoja na Serikali za Mikoa zihusike moja kwa moja kwenye masuala haya ya kudhibiti uvuvi haramu, kwa sababu Serikali ni moja. Haiwezi kuwa ni Serikali inayotoka Dodoma kwenda kudhibiti uvuvi haramu kule Bunda au Rorya ni mbali sana wakati kuna Serikali pia kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mkakati wetu ulikuwa ni huo wa kufanya zoezi hili liwe shirikishi, Serikali nzima ihusike, pia wadau wote wahusike ili tuweze kudhibiti uvuvi haramu kwenye nchi hii. Tunajua wote samaki ni rasilimali inayomsaidia kila Mtanzania. Samaki hawa wakitusaidia leo tu kesho wasitusaidie ni bahati mbaya sana maana kesho watakuwepo watoto wetu, wajukuu zetu, na wanadamu

wengine watakuwepo, sasa watakuta nini kama hatushirikiani kwa pamoja kudhibiti rasilimali hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kutoa elimu, pia tumeendelea kufanya maboresho ya kanuni zetu ili tuweze kudhibiti sawasawa suala hili, tumeendelea pia kutoa elimu ya uvuvi endelevu kwa jamii za wavuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ambavyo vimefungwa siyo lazima sana kwamba vilifungwa kwa sababu, sangara hawapo. Vingine vimefungwa kwa sababu ya *management,* matatizo ya ki-*management,* vingine kwa sababu ya matatizo ya uendeshaji, na kadhalika. Si sawa sana kusema viwanda vimefungwa kwa sababu, sangara walikuwa kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara ya dagaa kwenye Ziwa Tanganyika. Mheshimiwa Naibu Waziri ameieleza vizuri sina sababu ya kuirudia, lakini nieleze labda kuhusiana na kuongeza thamani ya dagaa na kupunguza upotevu wa mazao ya dagaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika Ziwa Viktoria, Serikali kupitia mradi au kupitia pesa za mkopo wa masharti nafuu ambazo tumezitangaza leo asubuhi sisi kupewa pia, tumetenga fedha kwa ajili ya kununua mitambo ya ukaushaji wa mazao ya uvuvi kwa kila Mkoa ili kuongeza thamani na kupunguza upotevu wa mazao. Kwa ukanda wa bahari Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza namna ambavyo mradi wetu wa *IFAD* bado upo, tunazo zaidi ya Bilioni Thelathini na Sita kwa ajili ya kazi hiyo kwa upande wa ukanda wa bahari wote. Kwa hiyo, tutafanya kazi hii kwa upande wa dagaa ili kusudi tuweze kupunguza upotevu wa mazao ya samaki, hususan dagaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la leseni za Bahari Kuu kuwa ni kubwa. Suala hili lilianzishwa na

Mheshimiwa Simai. Kwa mujibu wa Kanuni ya Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu ya mwaka 2021 bei za leseni za uvuvi wa bahari kuu kwa meli za Kitanzania zilipunguzwa kati ya asilimia 70 hadi asilimia 86 ikilinganishwa na bei za leseni kwa meli za kigeni. Mfano, uvuvi wa mishipi ni Dola 8,000 tu kwa mwaka kwa wazawa, ikilinganishwa na dola 50,000 kwa wageni. Kwa hiyo, utaona zimepunguzwa kwa sehemu kubwa sana hizi bei za leseni ambazo Mheshimiwa Mbunge alikuwa akizitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya suala la mwani imeelezwa vizuri na Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kulikuwa na suala lililosemwa na Kamati kuhusu biashara ya mwani inakua kwa kasi na inatekelezwa na wanawake, Wizara iandae mpango wa kuwaelimisha na kuwawezesha wakulima wa mwani mbinu bora za kilimo hicho. Sasa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa 2021/2022 tumetoa mafunzo ya uzalishaji na uhifadhi wa zao la mwani kwa wakulima 4,569 katika Mikoa ya Tanga, Lindi na Mtwara, pia Wizara tumewezesha wakulima wa mwani katika Mikoa ya Tanga na Lindi kwa kuwapatia kamba zenye thamani ya shilingi milioni 20. Mwaka wa 2022/2023 Wizara tutaendelea kuhamasisha na kuwawezesha wakulima 2,000 ili waweze kutumia teknolojia bora za uzalishaji na uongezaji thamani wa zao la mwani katika Mikoa ya pwani. Vilevile kujenga vichanja 10 vya kukaushia mwani katika Halmashauri za Wilaya za Mtwara, Lindi, Lindi *DC,* Lindi *MC,* Kilwa, Mkuranga, Mafia, Bagamoyo, Pangani, Tanga, Mkinga na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda wangu unakimbia sana niende nigusie pia masuala machache yanayohusiana na mifugo. Kulikuwa na suala la udhibiti wa magonjwa ya mifugo ambalo Mheshimiwa Kenneth Nollo alilisema. Kwa mwaka wa 2021/2022 Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, sekta ya mifugo tumejenga majosho 192, na ninadhani kwenye taarifa yetu yapo, kwa gharama ya Shilingi

3,458,000,000 katika Halmashauri 45 kwenye Vijiji vyenye mifugo mingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa 2022/2023 Wizara tutajenga tena majosho mengine 406 yenye thamani ya shilingi 7,304,441,000 yakiwemo majosho 128 kwa gharama ya shilingi 2,304,441,000 kwa fedha za ndani na majosho 278 kwa kiasi cha shilingi 5,000,000,000 fedha za nje, majosho haya yatajengwa katika maeneo ya malisho kwa lengo la kupunguza magonjwa yaenezwayo na kupe. Kwa hiyo, kazi hii tunaendelea kuifanya na kwa mwaka huu unaokuja tutaifanya kwa sehemu kubwa sana. Waheshimiwa Wabunge kila mmoja angehitaji majosho mahali ambapo kuna ng'ombe kwenye Jimbo lake, nadhani safari hii tutajitahidi angalao kila Mbunge kupata josho moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala la ufugaji wa punda na kufungwa kwa kiwanda cha punda kule Shinyanga. Mheshimiwa Khadija Aboud alisema Serikali ihamasishe kufanya kazi hiyo. Kwa kifupi ni kwamba, nchi nyingi duniani zimepiga marufuku biashara hii ya nyama ya punda. Zimepiga marufuku kwa sababu ya uzalianaji wa punda, punda wanazaliana kwa nadra sana. Punda anaweza kuchukua miaka mitatu ili aweze kuzaa na baada ya kuzaa hapo anaweza akachukua miaka mingine sita au zaidi ili aweze kuzaa. Kwa hiyo, punda hawaongezeki kama ng'ombe wanavyoongezeka au kama wanyama wengine wanavyozaliana. Kwa hiyo, bila kuwa na tahadhari tunapowatumia kama kitoweo basi wanaweza wakatoweka kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, punda wanatumika pia kwa shughuli nyingine za uzalishaji. Siyo nyama tu na ngozi na vitu vingine, wanatumika pia kwa njia za uzalishaji. Kulikuwa na suala lingine la ufugaji katika *ranch* za Taifa. Hili suala limezungumzwa sana, lakini kwa uzito sana limezungumzwa

na Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Dkt. Kikoyo na Waheshimiwa wengine wamelizungumza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme pengine kwamba Kampuni yetu ya Ranchi za Taifa - *NARCO* inamiliki ranchi 14 na inazitumia. Inawezekana isiwe kwa uwezo wake uliopo, lakini nadhani ni vizuri tungeenda taratibu kwenye suala hili kwa sababu Serikali imeweka maeneo hayo kama *buffer areas* ili wakati Serikali itahitaji ardhi kwa jambo mahsusi ambalo linahusu maslahi ya nchi yetu inaweza wakati wowote ikaenda kwenye *ranch*. Sasa tukisema *ranch* hizi zipo tu halafu sasa tuzitumie kama tutakavyotaka, mimi naamini tunaweza kuonekana kama hatujatumia vizuri rasilimali hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya *Ranch* ya Mwisa na Kagoma, Mheshimiwa Dkt. Kikoyo na Mheshimiwa Mwijage nimewasikia na hoja yenu nimeichukua, lakini pia Mheshimiwa Mwijage alihitimisha vizuri sana baada ya kusema Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Ardhi, tukutane chini ya Waziri Mkuu ili tuweze kulizungumza suala hili. Nami naunga mkono hoja hiyo kwamba ni vizuri tuzungumze suala hili na mamlaka za nchi ili tuone tunalimalizaje, kwa sababu tukiendelea kuzungumza *NARCO* pamoja na Waheshimiwa Wabunge wawakilishi wa wananchi, tunaweza tusifikie muafaka ambao utakuwa mzuri sana kwa sababu ninaposikia Mheshimiwa Dkt. Kikoyo anasema hata *Ranch* ya Mwisa na Kagoma hazipo kwa mujibu wa sheria, basi nadhani linakuwa suala zito kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nadhani tutakutana ili tuweze kuzungumza, nami naamini tutafikia muafaka sawasawa, tutafikia muafaka mzuri ili kwamba rasilimali hizi *ranch,* pia wananchi wetu na wenyewe wakae kwa amani, wakae kwa starehe kwenye hayo maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya Kamati ya Bunge kutokana na umuhimu wa vitalu katika kuzalisha mifugo bora zoezi la kupanga vitalu lizingatie manufaa ya kufuga kisasa badala ya kuchunga. Tunauchukua ushauri huo na mimi wakati wote nimekuwa nikikutana na wafugaji na kuwaeleza kwamba, ndugu zangu lazima tuanze sasa kufikiria kufuga badala ya kuchunga. Kwa sababu, tumechunga miaka yote hii, lakini tija bado haijaonekana kwetu wafugaji wenyewe, pia hata kwa Taifa lenyewe. Sasa tunayo haja ya kufanya mabadiliko, kuna haja ya kuboresha ili tuingie kwenye kufuga mifugo. Wafugaji wetu siyo wagumu sana ndiyo maana kwenye hotuba yangu, kama mmesoma vizuri, hii mliyokuwa mnanisikiliza hapa ni *summary* lakini hotuba ndefu ilikuwa kwenye vishkwambi vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mmenisoma vizuri nimesema kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023 nitaanza kampeni kwa kukutana na wafugaji, hawa ambao tunawaita ni wachungaji, tuelimishane juu ya kufuga kwa tija, tuelimishane juu ya kufuga kibiashara, tuelimishane ni kwa namna gani tunaweza kutumia rasilimali hizi za mifugo zikanufaisha familia na zikanufaisha Taifa letu. Kwa hiyo, tutafanya kampeni kubwa, pia zaidi ya kampeni tutatumia viongozi walioko ngazi kuanzia ya Kijiji mpaka ngazi ya Mkoa ili tuweze kuelewana, mbali na hivyo tutaendelea pia kutenga maeneo ili kwamba, tuwe sasa na maeneo maalum ya kufugia mifugo yetu ikiwa ni pamoja na wafugaji wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu suala hili linataka kuachwa kwa Serikali kana kwamba, Serikali ina ardhi kibao imelala mahali, sasa ikipungua itaenda ichukue impe mtu aende aweze kufuga, Hapana! Wafugaji pia tuna ardhi na maeneo ambayo mifugo yetu ipo, maeneo hayo tunaweza kuanza kuyaboresha, tukiondoka hapo ndiyo tuende kwenye maeneo ya wazi. Na maeneo haya ya wazi pia yako chini ya

Halmashauri. Tumezungumza na Halmashauri nao wayaboreshe, siyo kuyaacha kama yalivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ziko Halmashauri nyingi ambazo zimetenga maeneo kwa ajili ya malisho, lakini bado maeneo hayo hayajaboreshwa, hayana miundombinu stahiki inayotakiwa, majosho, maji, na kadhalika. Sasa tuchukue hatua sisi wote wadau kwenye suala hili la mifugo, kuanzia wafugaji wenyewe. Ndiyo maana tunasema lazima tuanze sasa utaratibu wa kupanda malisho, suala la malisho haliepukiki kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi, lakini kutokana na tunavyoongezeka Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, binadamu tunapoongezeka shughuli zetu za kiuchumi zinaongezeka pia. Sasa zinapoongezeka lazima ardhi itapungua ile ambayo utachunga huria, sasa lazima tuanze kufikiria kuwa na mashamba ya malisho yanayomilikiwa na wafugaji wenyewe. Ndiyo maana kwenye mashamba yale 100 ambayo tutayaanzisha ambayo tumeita ni mashamba darasa, haya mashamba tutayakabidhi kwa mfugaji mmoja-mmoja na baadaye tutatathmini ni mfugaji yupi anaelekea kwenye kufuga kiuendelevu. Badala ya kuyaweka kwenye taasisi za Serikali tutawapa wafugaji na hawa wafugaji ndiko wafugaji wengine watakwenda kujifunza namna ya kulima na kutunza hayo mashamba ya malisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ni mengi, huduma za ugani, Mheshimiwa Nollo pia anasema Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo ni vya zamani. Nakubaliana na wazo hilo ni kweli…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa bado una dakika mbili.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ooh, nakushukuru sana. Ahsante sana kwa kunipa muda, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN *Ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Kitabu cha Pili, Matumizi ya Kawaida, Fungu Namba 99 Sekta ya Mifugo, Ukurasa wa 501.

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 99 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo)**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*.............Sh. 3,978,694,570

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuko katika mshahara na nimeshapewa orodha ya majina. Namuita Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata maelezo kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu hii hamahama holela ya wafugaji katika kutafuta mazao na malisho ya mifugo yao vilevile katika kudhibiti migogoro ya

wakulima na wafugaji, ambayo kwa sasa hivi imeendelea kuwa mikubwa kiasi cha kufanya kwamba wafugaji wanapoteza mifugo yao na mali zao, pia wakulima wanapoteza mazao yao na hatimaye wakati mwingine kutokea maafa hapa nchini. Kwa hiyo, nataka kujua mpango na mkakati wa Wizara katika kudhibiti hali hiyo na kama itashindikana kwa kweli nitachukua Shilingi ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ninamuomba tu Mheshimiwa Mbunge asituchukulie Shilingi yetu. Mkakati wetu wa kudhibiti migogoro hii ni:

Moja; mwaka 2021 Disemba, tuliona tuwe na mwongozo wa malisho, vyakula vya mifugo na kadhalika. Baada ya kuona kwamba suala la migogoro ya wakulima na wafugaji linasababishwa sana na malisho halafu inafuatia maji. Sasa kwenye mwongozo ule tumeeleza vizuri, Disemba 2021 tuliuzindua pale Mkoa wa Pwani na tumeusambaza kwenye Wilaya zote. Tulipokutana na Mabwana Mifugo wa Wilaya zote mwaka huu tuliwapitisha kwenye mwongozo huo. Sasa hatutegemei kuona wafugaji wakiendelea kulisha mashamba ya wakulima kwa sababu, kama mwongozo huo ukifuatwa unaeleza kabisa mifugo inachungwa wapi, maeneo ya machunga yanafanywa nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama kunaendelea na migogoro hii kwa sababu ya malisho na kwa sababu ya maji, basi itakuwa ni uvunjifu wa sheria kama ambavyo mkulima au mfugaji anavunja sheria kwa namna ya kuingiliana kati yao hawa wawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nadhani ni vizuri Sheria zetu pia huko kwenye maeneo yetu tuzisimamie vizuri, kwa

sababu kama mfugaji ameenda kwenye shamba la mkulima, amelisha mifugo yake, sheria na taratibu za nchi hii zipo. Kama mkulima ameenda kwenye eneo la malisho akalima shamba lake huko kama alivyofanya kule Kiteto mwaka 2021 amelima katikati ya eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya malisho. Mfugaji ameenda, akapeleka ng'ombe wake kule, wamekula. Sasa migogoro ya namna hiyo itatuliwe kwa kufuata sheria na taratibu za nchi yetu. Vinginevyo, kama tukiendelea kulealea hivi na kufumbafumba macho, tutakuwa na miongozo, sheria, kanuni na kila kitu, lakini bado matatizo haya yataendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sijaridhika na majibu ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa, kwa sababu migogoro bado imeendelea kuwepo na wananchi wanaendelea kupata shida. Hapa tunazungumzia siyo wakulima tu, hata wafugaji, wanapoteza mazao yao kwa sababu ya kukosa malisho, kukosa maji na Serikali haijaonyesha mpango thabiti wa kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa bado sijaridhika na kwa kweli naomba Wabunge wenzangu mniunge mkono katika hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa AG una hoja?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nalazimika kusimama kwa mujibu wa kifungu alichosimama nacho Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kinahusu suala la kisera. Mheshimiwa Waziri amejitahidi kueleza sera na mwongozo uliotolewa na baadaye yanayobaki ni uvunjifu wa sheria; na kama ni mambo ya uvunjifu wa sheria, nchi yetu inaongozwa kwa utaratibu wa

sheria. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hana kingine cha kufanya zaidi ya wahalifu kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa *AG,* lakini bado Mbunge kwa mujibu wa kanuni ana haki ya kuendeleza hoja yake. Mheshimiwa Innocent. *(Makofi)*

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niendelee. Kiuhalisia kesi ziko Mahakamani kama *AG* anavyosema, lakini watu hawapati haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja hili jambo lijadiliwe.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Babu Tale, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Ridhiwani, Mheshimiwa Kakoso, Mheshimiwa Bulaya, Mheshimiwa Mnzava, Mheshimiwa Halima, Mheshimiwa Ally na Mheshimiwa Dkt. Florence au! Mheshimiwa Ndulane, tuanze na hao kwanza. Mheshimiwa Innocent.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Serikali ina wajibu wa kuja na mpango mkakati wa kusaidia kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji na vile vile kusaidia wafugaji wetu ili ng'ombe zao na mifugo yao isife wakati wa kiangazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano halisi, sasa hivi tunakwenda katika kipindi kigumu sana. Mvua mwaka huu hazikunyesha, tunatarajia kabisa kwamba kutakuwa hakuna

majani na ng'ombe watapata wakati mgumu sana kama ilivyotokea katika kipindi kilichopita, ng'ombe walifika mpaka kwenye vyanzo vya maji na kusababisha ukosefu wa maji, hata Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa natarajia Wizara ingekuja na mpango na mikakati kama ilivyofanyika Loliondo. Kama Loliondo wameweza kupima ardhi na kupeleka huduma za msingi ambazo wafugaji wamepelekwa Handeni, nilikuwa natarajia katika kipindi hiki kinachokuja, Mheshimiwa Waziri angekuja atuambie tu kwamba katika hatua za muda mfupi tungeweza kuhakikisha kwamba kila Jimbo kama alivyosema, tungeona katika hotuba yake kunachimbwa mabwawa ili kusudi maji yaje, tunapeleka mashamba darasa ili wafugaji wetu wapate majani na kujifunza mbinu sahihi. Tukiweza katika hilo ni haki, lakini sasa tunafika mahali tunapelekewa juu juu tu; sisi kama Wabunge katika maeneo tunakotoka tunapata wakati mgumu kwa wananchi wetu; wafugaji na wakulima wanapohangaika na matatizo wanayopata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanauana. Juzi tu Morogoro tarehe 9 watu wameuana. Hiki kitu ni hatari; na Serikali imekaa kimya. Kwangu inanipa wakati mgumu kama mwakilishi wa wananchi, na wananchi wangu kule ninakotoka wanapata adha kubwa; wafugaji na wakulima wote na wote ni watu wangu, wanauana. Wanagombana katika kitu gani wakati nchi hii bado tuna maeneo makubwa, Serikali inaweza ikapima maeneo na kuwapeleka watu huko, lakini tumenyamaza kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, la kwangu lilikuwa hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Jafo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze mtoa hoja kwa maelezo yake na vile vile nampongeza kaka yangu Mheshimiwa Innocent, anachokisema nakielewa, lakini linakuja palepale suala la *good faith* ambayo imeonyeshwa na Waziri na hasa ukiangalia mikakati iliyoanza kuwekwa. Tumepitia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa kwamba mkakati uliokuwepo miongoni mwa changamoto kubwa ni majosho; takribani majosho 400 ambayo yatasaidia katika changamoto hiyo. Pia ukiangalia naye kuna mipango mbalimbali ya kufanya na mambo mengine mtambuka katika Wizara nyingine katika ujenzi wa malambo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili pia nimeliona pale Kiteto katika kazi kubwa iliyofanywa ya mradi wa maji na kutengeneza sehemu maalum za ng'ombe kunywea maji. Hili jambo alivyoeleza Mheshimiwa Waziri, tunajua kweli tatizo ni kubwa, lakini suala zima la kuzihusisha sheria zetu na mkakati wa Wizara, nadhani tumpe nafasi Mheshimiwa Waziri kuwa mkakati wake kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023 kama alivyopanga katika kuwasaidia Watanzania kwa ujumla wetu. Tunajua tatizo hili ni kubwa lakini tuipe nafasi Serikali na Wizara ikalitatue tatizo hili kwa maslahi mapana ya Watanzania, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bulaya

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Innocent.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanafikia hapa kwa Watanzania kugombana wenyewe kwa wenyewe kwa sababu Serikali imeshindwa kupanga matumizi bora ya ardhi. Wewe unajua miaka nenda rudi, ikifika Bajeti ya Maliasili kuna tatizo; Bajeti ya Ardhi, kuna tatizo; Bajeti ya Kilimo, kuna tatizo;

na Bajeti ya Mifugo kuna tatizo. Tukaambiwa kumeundwa kikosi kazi cha Mawaziri nane kushughulikia migogoro ya nchi hii, mpaka leo ripoti haijaletwa, bado wananchi wetu wanagombana. Haya mambo tutayasema mpaka lini? Watanzania wanauana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule kwetu Mara kulikuwa na migogoro hivi hivi upande wa Maliasili, ikaundwa sijui Operesheni Tokomeza watu wakafa. Morogoro kila siku watu wanauawa na maeneo mengine, Serikali mnajisikiaje wananchi wenu wanaowapigia kura, kila siku wanagombana kwa kitu kimoja, ardhi kupangwa ikatumika kwa mazingira sahihi kwa wafugaji, kwa wakulima na kwa maeneo ya hifadhi. Hivi hili nalo linatuhitaji zaidi ya miaka 60 ili kuwakomboa Watanzania na migogoro isiyokukwa na sababu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, Serikali ije na majibu leo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Innocent Kalogeris kwamba Serikali bado haijaja na majawabu ya kutatua migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Pamoja na kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 49 ameeleza hilo, lakini pia katika Mpango wa mwaka huu wa Wizara, ukurasa wa 88, anasema tutaendelea kutatua migogoro. Yaani hii ni tafsiri kabisa kwamba migogoro kumbe ni kitu ambacho Wizara inaitaka na mikakati yake ni kuendelea kutatua, kidogo inaleta shida. Tulichohitaji na tulichotegemea hapa ni *commitment* kwamba tunaendaje kumaliza migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilwa peke yake tumeshuhudia vifo vinne kutokana na migogoro hii, ambapo Jimbo la Kilwa Kusini tumepoteza wananchi watatu kwa migogoro ya wakulima na wafugaji, Jimbo la Kilwa Kaskazini tumepoteza mwananchi mmoja, ndani ya miezi mitatu tu iliyopita huko nyuma. Mheshimiwa Waziri hapa anatuambia ametoa mwongozo, huo ni mwongozo gani ambao mimi Mjumbe wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri yangu siujui?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kama kuna mwongozo huo, basi Afisa anayehusika na dhamana ya mifugo kwenye Halmashauri yangu awasilishe kwenye Baraza, tuusikie, tuuchangie tukausimamie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Hatubishani wala hatupingi kabisa hoja ya Mheshimiwa Mbunge aliyoitoa, ina mantiki kubwa kabisa, lakini nilichotaka nimwombe, arudishe Shilingi na atambue jitihada ambazo Mheshimiwa Rais amezichukua ndani ya mwaka mmoja katika kushughulikia sekta hii ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo huwa linawafanya wafugaji wahame, wala siyo mipango ya ardhi peke yake, ni malisho na maji. Hivyo ndiyo vitu vikubwa. Sasa katika kutambua hivyo, Mheshimiwa Rais ameweka fedha na manunuzi yameshafanyika ya kununua mitambo ya kuchimba mabwawa kwa ajili ya maji ya wafugaji ambapo kila ukanda wa nchi yetu hii utakuwa na mtambo wake. Maana yake nini? Taasisi yetu ambayo inahusika na kuchimba mabwawa, itakuwa na kazi hiyo ya kuchimba mabwawa, kwa hiyo, maji yatapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii ambayo Mheshimiwa Waziri ameisoma, tumetenga takribani Shilingi bilioni 40 ambazo zinakwenda kwenye *modernization* ya sekta hii ya mifugo. Maana yake ni nini? Baada ya kuwa tumeshaanza utaratibu wa wafugaji kufuga kisasa ambapo tunaunganisha mifugo pamoja na viwanda, kidogo kidogo wafugaji wataanza kutoka kwenye ufugaji ule tuliokuwa tumeuzoea kwenda kwenye ufugaji wa kisasa ambao utatoa jawabu la kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama tutapanga leo hii, lakini tusipowianisha idadi ya mifugo na *modernization* ya sekta nzima, hili tatizo bado litaendelea kwa sababu mifugo yenyewe haijui mipaka wala haijui kwamba haya ni majani na haya ni mazao. Kwa maana hiyo, hatua ambazo amezichukua Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Mbunge na Mwenyekiti wa Chama wa muda mrefu, aelewe jitihada hizi ambazo zinafanyika, arejeshe Shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwambia, tutakaporudi kwenye Bunge linalokuja, tutakuwa na *story* tofauti kuhusiana na jambo la aina hii. Mitambo kila ukanda haijawahi kutokea. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami nichukue nafasi hii kumwomba tu ndugu yangu Mheshimiwa Innocent; kwanza, napongeza juhudi zake kwa sababu yeye mwenyewe anayo mitambo ya maji. Sasa tukijumlisha na yale niliyoyasema, Mwongozo ule wa Malisho pamoja na vyakula vya mifugo; na yale tuliyosema, mashamba darasa 100 ya malisho tutakayoyaanzisha na pengine Mkoa wa Morogoro tunaweza kuwapendelea kidogo ili tuweze kupunguza kwa haraka migogoro aliyonayo, kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Innocent anirudishie

Shilingi ili tufanye kazi hii kwa pamoja mwaka unaokuja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent, funga hoja yako.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaishukuru Serikali, kwa namna moja au nyingine imeonesha kwamba inajali na nadhani itatia jitihada huko tunakokwenda. Nakurudishia Shilingi yako, lakini ombi langu, pamoja na suala la Mheshimiwa Waziri kusema kwamba kuna mitambo itakuja na kuchimba, na kdhalika, nami naomba vile vile kama alivyosema Mheshimiwa Mwijage, jambo hili tunakoendea ni janga kubwa katika Taifa. Ni wakati muafaka kwa Waziri Mkuu ambaye ndiye anasimamia majanga, lakini kama wewe ni Waziri wa Kilimo, kama Waziri wa Ardhi tuone jinsi gani ya kutatua tatizo hili kwa kuandaa maeneo ambayo tutapeleka wafugaji wetu wakakae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ambayo umeyatoa ambayo yameleta Imani. Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama ulivyosema, mabadiliko; *change is here.* Ahsante sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaingia kwenye *guillotine*.

**Fungu 99 – Sekta ya Mifugo**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……......................…Sh. 3,978,694,570
Kifungu 1002 – *Finance Accounts Unit*...............Sh. 939,159,000
Kifungu 1003 – *Policy & Planning Division*..........Sh.1,065,538,000

Kifungu 1004 – *Research Training and Extension Unit*..........................................Shs. 9,025,903,000
Kifungu 1005 – *Information Education & Communication Unit*...............................................Sh. 296,136,000
Kifungu 1007 – *Internal Audit Unit*........................Sh. 253,775,400
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*...............................................Sh.356,786,400
Kifungu 1009 – *Legal Services Unit*.......................Sh. 222,950,000
Kifungu 1010 – *ICT Unit*..........................................Sh. 305,070,000
Kifungu 1011 – *Environment Management Unit*..Sh. 100,958,500
Kifungu 7001 – *Veterinary Services*....................Sh. 8,444,762,930
Kifungu 7003 – *Livestock Infrastructure Development Unit*…............................................Sh. 351,820,000
Kifungu 7005 – *Veternary Council of Tanzania*....Sh. 312,088,000
Kifungu 8001 – *Livestock Production and Marketing*...................................Sh. 7,944,982,200
Kifungu 8002 – *Grazing Land and Animal Feed Resources*…...............................Sh.1,441,584,000
Kifungu 8003 – *Animal Breeders Rights Unit*..........................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 64 – Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Unit*.....................Sh. 2,041,516,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*......Sh. 1,009,653,441
Kifungu 1003 – *Policy & Planning Division*..........…Sh. 890,616,860
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*………..….….…Sh. 283,924,410
Kifungu 1005 – *Legal Unit* ……………………..………Sh. 361,686,940
Kifungu 1006 – *Procurement Unit*.........................Sh. 429,488,410
Kifungu 1007 – *ICT Unit* ..........................................Sh. 313,044,000
Kifungu 1008 – *Fisheries Laboratory* ..................Sh. 1,127,611,000
Kifungu 1009 – *Environment Management Unit*...............................................Sh. 152,980,000

Kifungu 1010 – *Government Communication Unit*......................................................Sh. 219,932,000
Kifungu 9001 – *Fisheries Development Division*........................................Sh. 7,529,768,683
Kifungu 9002 – *Aquaculture Development*......Sh. 1,606,587,589
Kifungu 9003 – *Fisheries Aquaculture Research, Training*......................................Sh. 7,082,836,667
Kifungu 9004 – *Fisheries & Aquaculture Infrastructure*..................................Sh. 300,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**MPANGO WA MAENDELEO**

**Fungu 64 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division*.....Sh. 1,171,826,530
Kifungu 1007 – *ICT Unit* ..........................................Sh. 655,353,930
Kifungu 1009 – *Environment Mgt Unit*...................Sh. 153,081,750
Kifungu 9001 – *Fisheries Development Division*........................................Sh.10,173,537,034
Kifungu 9002 – *Aquaculture Development*......Sh. 1,952,900,000
Kifungu 9003 – *Fisheries Aquaculture Research, Training*.........................................Sh. 5,635,195,563
Kifungu 9004 – *Fisheries & Aquaculture Infrastructure*............................Sh. 73,109,642,193

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 99 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division* ................................ Sh. 0
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*..............Sh. 400,000,000

Kifungu 1004 – *Research Training and Extension Unit*..............................................Sh. 3,400,000,000
Kifungu 7001 – *Veterinary Services*……………..Sh. 5,403,441,000
Kifungu 7003 – *Livestock Infrastructure Development Unit*..................................................Sh. 450,000,000
Kifungu 8001 – *Livestock Production and Marketing*....................................Sh. 5,081,075,000
Kifungu 8002 – *Grazing Land and Animal Feed Resources*…..............................Sh. 2,276,100,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi.

*(Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge ya 123(3)(a) na (b), naomba kutoa taarifa kuwa Bunge lililokaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Bajeti hii imepita vizuri sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, timu ya Wizara, Katibu Mkuu na wataalam, hongereni kwa kazi nzuri. Tumeona mabadiliko ya mwaka huu, boti 350 siyo kazi ndogo; boti ambazo zina *GPS*, boti ambazo zina *freezer,* boti zina *fish finder*. Boti zitakwenda Mtwara, Tanga, *Lake Victoria*, *Lake Tanganyika*, *Lake Nyasa* na watu watakula Samaki, watapata afya na watajiandaa na Uchaguzi wa 2025. *(Makofi/Kicheko)*

Mambo mazuri yanakuja. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, ana jeshi kamili akisaidiwa na Mwanasheria, Waziri wa Fedha, Mawaziri wote na Waziri Mkuu. Kwa kweli mabadiliko yanaonekana, *a change is here*. Kwa hiyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa leo kulikuwa na mabanda pale. Nampongeza sana Mheshimiwa Mama Sitta, kaenda pale kalalamika sana, na imefahamika katika nchi hii kumbe Urambo ndiyo sehemu kubwa ambayo umeme unatoka. Kwa hiyo, ameahidiwa mambo yake sasa mazuri. Mheshimiwa Rais ametoa Shilingi bilioni 500 *(five hundred billion)* za kufanya marekebisho ya maeneo yote ambayo umeme una matatizo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wananchi, nawazungumzia wananchi wa Dar es Salaam sasa na hasa Ilala kwangu, yale matatizo ya umeme Waziri ameahidi ikifika mwezi wa Saba, wa Nane yamekwisha. Kwa hiyo, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutoa pesa nyingi kama hizi kufanya marekebisho ya miundombinu ya umeme ambayo ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mengine kuhusu mabanda atayasemea Mheshimiwa Spika mwenyewe ana maneno mazuri makubwa na kwa vile yeye ndiye mwenye nyumba, ndio atakuwa na mamlaka ya kuyasemea, sio mimi.

Kwa hiyo, baada ya maneno haya, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 26 Mei, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*